

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 10 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Kikao cha Ishirini na Sita cha Mkutano wetu huu wa Kumi na Moja. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA - MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya

Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimwa Makamu Mwenyekiti. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Jimbo la Sumve, swali fupi tafadhali.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa idhini yako, naomba uniruhusu niungane na Watanzania wenzangu kwa kuipongeza sana Serengeti Boys baada ya kushinda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa, moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, Tanzania imepewa heshima kubwa ya kuandaa mashindano ya vijana chini ya umri wa miaka 17, *AFCON U17*. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imejipangaje kufanikisha mashindano hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Ndassa amezungumzia vijana ambao

wameshinda hivi karibuni Kombe la Afrika Mashariki lakini pia na hawa ambao tunawaandaa kwa mashindano ya Afrika. Kwanza, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana vijana wetu wa umri chini ya miaka 17 kwa ushindi mzuri, mkubwa walioupata kule Burundi na ambao pia wataendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, tunayo timu ya chini ya miaka 19 ambayo itatuwakilisha kwa kucheza Kombe la AFCON kama ambavyo ameeleza sambamba na heshima ambayo nchi yetu imepewa ya kuendesha mashindano ya chini ya umri wa miaka 19 ambayo yatafanyika 2019. Kwa ujumla wake, timu hizi zote ambazo tunazo kwa sasa ambazo zinacheza kwenye ngazi ya Kimataifa ni jukumu letu kama Serikali kuziandaa. Mimi nataka nitumie nafasi hii kulipongeza sana Shirikisho la Soka Tanzania kwa pamoja na Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwamba wamefikia hatua nzuri baada ya kupata heshima hii kufanya maandalizi na maandalizi yanaendelea. Maandalizi haya, kwanza timu zenyewe tunaziandaa na ninazo taarifa, moja kati ya maandalizi ambayo tunayafanya kwa timu hii ambayo itatuwakilisha tunaipeleka nchini Sweden kwa ajili ya kupata ufundi na maarifa zaidi ili kujihakikishia kwamba michezo yote itakayokuja mwakani tutaweza kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, tunajiandaa huku ndani kupata viwanja ambavyo vitatumika kuchezea Kombe lile, lakini pili, maeneo ambayo yatafikiwa na wageni wetu kwa sababu tutakuwa na wageni wengi na mambo yote ambayo yanahusiana na afya, usafiri wao ndani ya nchi, haya yote yanaendelea kufanyiwa maandalizi. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania maandalizi juu ya michezo yetu ya Kimataifa ambayo pia tumepata heshima ya kucheza hapa nchi yote yanaendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Watanzania, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara na Shirikisho la Soka Tanzania, nawasihi Watanzania tuendeleo kuziunga mkono timu zetu zote zinazofikia ngazi za Kimataifa ili ziweze

kufanya vizuri na nchi yetu iendelee kupata heshima. Pia kwa kufanya hilo, mashindano mengi mengine ambayo yatakuja, basi yaelekezwe nchini Tanzania ili tuweze kupata tija kwa uwepo wa michezo hiyo hapa kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndassa, swali fupi sana tafadhali.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, sawa nitauliza swali fupi sana. Kupitia mashindano haya na kwa sababu kutakuwa na wageni wengi kutoka nje na kwa sababu tunazo fursa za utalii, je, *TANAPA* na Ngorogoro watashirikishwa namna gani? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza heshima ambayo tumeipata ya kuendesha mashindano ya dunia hapa kwetu mwakani nayo pia ni fursa kwetu na ziko nyingi ikiwemo na hiyo ya kutangaza vivutio vyetu lakini kuwapeleka wageni wetu kwenye vivutio vile ili tuweze kujipatia fedha. Ni kweli tumeamua kutangaza na mipango ambayo Wizara ya Maliasili inayo sasa ni ya kuimarisha sekta ya utalii kikamilifu kwa kutangaza mapori na vivutio vyote vilivyopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutatumia fursa kama hii, kwanza, kwenye viwanja vyake. Pili, kwenye matangazo ya *radio* na *television*, lazima tuvionyeshe wakati wote wageni wakiwa hapa. Tatu, kutoa fursa kwao angalau timu moja, mbili, tatu kuwapeleka Kigoma huko wakaone sokwe mtu; tuwapeleke Serengeti na Selou wakaone utalii wa huko na tuwapeleke Kilwa wakaone majengo ya zamani yaliyokaliwa na Waarabu na maeneo mengine yote yenye vivutio vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba nafasi hii tutaitumia vizuri na kimsingi niliposema tunafanya maandalizi ni pamoja na kutangaza vivutio vya ndani. Kwa hiyo, nawasihi Watanzania sasa tutumie fursa hii, kila mmoja mwenye sekta ambayo anaona ujio wao utamletea faraja basi ajipange vizuri ili wakati ule wageni wanapoingia aweze kuitumia. Kama unaimarisha sekta ya usafirishaji, kama unaimarisha sekta ya vyakula, kama pia una sekta ambazo unadhani wanahitaji mavazi na kila kitu, ni fursa kwetu Watanzania kutumia matukio kama haya ambayo pia Serikali inaendelea kuyavutia nchini kwetu ili yafungue milango kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Twende *CUF*, Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa maelekezo kwamba katika msimu huu wa mwaka 2018/2019 zao la ufuta litanunuliwa katika mfumo wa stakabadhi ghalani. Mpaka sasa navyozungumza, ufuta uko tayari, wakulima wameshavuna na wengine wameshauza. Pia maelekezo ya Serikali pia yalisisitiza mikoa yote inayolima zao la ufuta ijijandae kwa mfumo wa stakabadhi ghalani. Je, ni nini tamko la Serikali maana iko kimya na mpaka sasa wafanyabiashara na wakulima hawajui nini kinachoendelea?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijubu swali la Mheshimiwa Vedasto Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumeweka utaratibu wa masoko ya mazao yetu yote nchini. Tumeanza

na mazao matano lakini pia tumeanza kuingia kwenye mazao haya ambayo yanaonekana yanazalishwa kwa wingi ambayo pia yanatuletea tija kwa wakulima lakini hata kwa Serikali kwa ujumla wake ikiwemo na zao la ufuta. Tumetoa maelekezo kwa Wizara ya Kilimo iratibu vizuri mikoa yote inayolima ufuta. Zao hili mwaka huu litauzwa kwa njia ya mnada ili kuzuia mfanyabiashara mmoja mmoja kwenda kuwarubuni wakulima na kusababisha kupata bei ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapotoa maelekezo maana yake kila mmoja anayewajibika kwenye eneo hili lazima afanye kazi yake. Tumetoa maelekezo maalum pia kwa Wakuu wa Mikoa wote wakutane na Wizara na *of course* Wizara inawajibu wa kuwaita iandae utaratibu na utaratibu huu uende sasa kwa wakulima waelimishwe, waeleweshwe namna nzuri ya kusimamia jambo hili na halmashauri zisimamie kwa karibu kuhakikisha kwamba wakulima ndani ya halmashauri zile hawadhulumiwi na hawauzi kwa bei ndogo ili iweze kuwapatia tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maelekezo haya na kwa swali lako sasa Wizara ya Kilimo wamesikia, Wakuu wa Mikoa wamesikia na wilaya zinazolima ufuta kwa sababu siyo nchi nzima wanalima ufuta, sasa wajipange wahakikishe wanaratibu vizuri kupitia Maafisa Ushirika na Maafisa Kilimo kuwatambua wakulima na maeneo watakayouza kama mnada ili wakusanye mazao, watangaze siku moja, wanunuzi waje, bei ipatikane wakulima wapate faida, ndiyo mkakati wa Serikali. Wizara ipo na itasimamia jambo hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Saed Kubenea, CHADEMA.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali ni kila mtu kuabudu dini anayoitaka na kutokuingilia dini ya mtu mwingine. Katiba

yetu, Ibara ya 3(1) inasema Serikali yetu haina dini isipokuwa watu wana dini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kibali kwa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kuratibu zoezi zima la hija kwa mwaka huu. Kwa msingi huo imeziacha taasisi nyingine ambazo zilikuwa zinapeleka Mahujaji Makkah zisifanye kazi hiyo ikiwemo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana - Zanzibar ambayo nayo inatakiwa iratibiwe na BAKWATA.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini msimamo wa Serikali sasa kwa kuwa suala hili limeleta sintofahamu na gharama za kupeleka Mahujaji Makkah kupitia BAKWATA zimekuwa kubwa zaidi kulinganisha na taasisi zingine, je, Serikali iko tayari kuziruhusu taasisi zingine zipeleke Mahujaji Makkah katika kipindi hiki kifupi kilichosalia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, mbona kila ukisimama unauliza maswali ya kidini? Yaani ukisimama una mambo ya kidini, ukisimama una mambo ya kidini. *(Makofi)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawakilisha Watanzania wakiwemo Waislam na mimi mwenyewe ni Muislam na nina *interest* na jambo hili la *Hijja*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, swali linalofuata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na ubishani baina ya *SUMATRA* pamoja na *TABOA* kuhusu upitishwaji wa kanuni bila kuwashirikisha wadau. Je, ni hatua gani Serikali inachukua ili kuweza kuinusuru sekta hii ya usafirishaji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mlata, Mbunge wa Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la *SUMATRA* na *TABOA* ni suala ambalo linaendelea kufanyiwa mazungumzo juu ya uandaji wa Kanuni za Usafirishaji kwa mujibu wa kumbukumbu ambazo sasa ninazo. Suala hili nimelifanyia kazi mimi mwenyewe hasa wakati ule *TABOA* walipokuwa wanalalamikia *SUMATRA*, *SUMATRA* ilipokuwa inatengeneza Kanuni za Usafirishaji na hasa zile kanuni ambazo zilikuwa zinagusa sana juu ya adhabu na tozo mbalimbali zinazotozwa kwa wamiliki wakati mwingine kwa watumishi wa shughuli za usafirishaji na zikaanza kuleta migongano miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, *TABOA* wamewahi kulalamikia uundaji wa Kanuni hizo na kwamba hawakushirikishwa Kanuni hizo zilipokuwa zinatengenezwa na *SUMATRA*. Walipoleta malalamiko, tuliitaka *SUMATRA* sasa irudie mchakato wake kwa kukutanisha wadau wote wa sekta ya usafirishaji. Tunajua kwenye sekta ya usafirishaji wako hao *TABOA* (wamiliki wa mabasi) lakini kuna *TATOA* (wasafirishaji wa malori) halafu wako pia hawa wenye mabasi ya daladala. Taasisi zote hizi zinashughulikia usafirishaji. Kanuni ambazo zilikuwa zinalalamikiwa kwenye eneo hili kwa mujibu wa kumbukumbu zangu ni pale ambapo madereva waliopewa dhamana ya kuendesha mabasi yao au malori yao wanapotenda kosa adhabu yake anatozwa mmiliki wa basi akiwa hayupo kwenye basi. Tozo hizi zimekuwa zikilalamikiwa na wamiliki na kwamba lazima zifafanuliwe vizuri ili kila mmoja atendewe haki yake pale ambapo anatenda kosa au la. Kama dereva anatenda kosa basi adhabu iende kwa dereva na siyo mmiliki na kama kosa litakuwa ni la basi lenyewe wataangalia vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mgongano ule tulilazimika kuwataka wakae pamoja ili wazungumze, watengeneze Kanuni zinazoweza kutosheleza mahitaji ya wote pamoja, *SUMATRA* pamoja na wamiliki wa vyombo



hivi vya usafirishaji. Kwa hiyo, jambo hilo limeendelea vizuri na wajibu wa Serikali sasa ni kusimamia kuwa *SUMATRA* kama mwakilishi wa Serikali anashiirikisha wadau ambao ni wamiliki wa vyombo vya usafirishaji ili kutengeneza Kanuni ambazo zitawezesha hawa wamiliki pamoja na Serikali kufanya kazi bila ya kuwa na mgongano usiokuwa na umuhimu. Kwa hiyo, kazi hiyo tumelifanya na nimetoa maelekezo wakutane na taarifa ninazo kwamba wanaendelea kukutana ili ku-*harmonize* zile Kanuni ili baadaye zitakapokamilika ziendeleo kutumika ili kila mmoja atendewe haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Busega, Dkt. Raphael Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakusanya fedha nyingi kutokana na tozo pamoja na kodi kutoka katika masoko yaliyo rasmi na yasiyokuwa rasmi. Licha ya makusanyo hayo, kumekuwepo na matatizo mengi ambayo yanasababisha kutokuwepo na uhalisia wa miundombinu mizuri kutokana na uchafu na pengine kuwa na hali hatarishi. Je, ni nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba halmashauri karibu zote ndiyo zinamiliki masoko na ndiyo wanaohusika hasa na utozaji wa kodi kwenye masoko haya. Kodi hii kwa kila halmashauri ni mapato ya ndani na mapato haya ni yale ambayo yanapangiwa matumizi yake na Baraza la Madiwani katika kila halmashauri. Kwa hiyo, ni wajibu wa kila halmashauri inapopata zile tozo kutenga mgao kwa ajili ya

usafi kwenye masoko yao. Siyo tu masoko bali maeneo yote yanayohitaji kufanyiwa usafi ndani ya halmashauri yao, ni wajibu wa kila halmashauri kupitia Baraza la Madiwani kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za usafi kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia usafi hatuzungumzii kufagia na kuzoa taka tu, ni pamoja na kuimarisha miundombinu ambayo umeisema. Ni lazima miundombinu iwe rafiki kwa ajili ya kuendesha shughuli za biashara kwenye maeneo hayo au maeneo mengine. Tunajua kuna maeneo ni muhimu sana kwa halmashauri pamoja na soko lakini pia kuna vituo vya mabasi, maeneo ya hospitali na maeneo kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, masoko mengi haya yanayomilikiwa na halmashauri lazima yaratibiwe vizuri. Tunajua yako masoko mengine kwenye mamlaka nyingine kama vile Soko la Kariakoo ambalo lina mamlaka yake, nao pia wanawajibika, wakipata mapato yao watenge fedha kwa ajili ya usafi na kuimarisha ubora wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, alizindua kampeni ya usafi wa ujumla. Kwa hiyo, mambo yote haya tukiyachanganya pamoja yanafanya Taifa hili kila eneo kuwa safi. Azimio lile limeeleza kila Jumamosi itumike vizuri kuanzia asubuhi hadi saa tatu, saa nne kwa ajili ya usafi. Kwa hiyo, halmashauri na viongozi wote wanajibika kusimamia ili nchi iweze kuwa safi katika maeneo yote yakiwemo ya kutolea huduma ikiwemo na eneo la soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako, naomba kutoa maagizo kwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Maafisa Afya wa Halmashauri za Wilaya, ni jukumu lao kusimamia suala hili. Nawasihi wahakikishe maeneo yote ya kutolewa huduma ikiwemo masoko yanaimarishwa kwa miundombinu na usafi wake kwa ujumla . Nasi tutawapima kwa kuhakikisha kwamba halmashauri zao na maeneo yote

ya utoaji huduma huduma yanakuwa safi, vinginevyo hatua nyingine zinaweza kuchukuliwa pale ambapo tunaona hakuna uratibu mzuri wa usafi kwenye maeneo hayo, hakuna uratibu mzuri wa uboreshaji wa miundombinu kwenye maeneo ya kutolewa huduma kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Bashe.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu Bure imewarahisishia wazazi kuweza kuwapeleka watoto shule lakini haisaidii watoto kubaki shuleni kwa sababu kubaki shuleni kunategemea na mazingira wezeshi kwa watoto kupenda shule. Kwa sasa bado tunaona watoto wengi wanatoroka shuleni tunakutana nao mitaani wakifanya kazi za ombaomba na wakisaidia watu kubeba mizigo sokoni ili wapate kitu cha kula. Je, ni lini Serikali itabadilisha sera hii ili sasa upatikanaji wa chakula shuleni uwe ni sehemu ya jambo la lazima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hizi programu za elimu nchini tunaziratibu kwa kadri ya mahitaji na wakati kwa maana ya utoaji wa huduma ulio bora. Tumeanza na elimu bure kwa kuondoa michango ambayo haikuwa

muhimu iliyokuwa inawakwaza sana wazazi ili watoto hawa sasa waweze kwenda shuleni.

Mheshimiwa Spika, nataka nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania tuna shule zaidi ya 17,000 na kila shule ina watoto wasiopungua 300 na kuendelea, hasa shule za msingi ambazo sasa tumeongeza hata usajili wa watoto wetu. Nachoweza kusema ni kwamba programu ya chakula ni muhimu sana kwa watoto wetu na Serikali hatuwezi kulibeba jambo lote hili kwa kulisha shule zote 17,000, tukiwa na sekondari zaidi ya 3,547 ambazo ni za *boarding* na *day*. Kwa hiyo, tumeanza na shule za bwani kwa upande wa sekondari na sasa tunaendelea kuratibu vizuri tuone namna nzuri ya kutoa chakula kwenye shule za sekondari za kutwa lakini pia na shule za misingi ili vijana wetu hawa wanapokuwa shuleni waweze kupata huduma ya chakula ambayo inasaidia kimsingi kumfanya kila mtoto aweze kupata masomo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini tumefanya? Tuliposema tutoe elimu bure kwa kuwapunguzia michango wazazi wetu, nafasi hiyo pia inamfanya mzazi sasa kuchukua jukumu lingine la kumhudumia mtoto huyu ikiwemo na kuhakikisha mtoto anapata chakula cha kutosha, anapata sare na vifaa muhimu vya kwenda shule ili imuwezeshe mtoto huyu kwenda shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaendelea kuratibu hili ndani ya Serikali na kwa kuwashirikisha wananchi, nitoe wito pale ambapo wazazi wamevuna vizuri mwaka huo na wanaweza kupata chakula cha kutosha, iko haja na umuhimu wa kutekeleza dhana ya kupeleka chakula shuleni na kuratibu. Tumeona baadhi ya halmashauri zilizokuwa na ubunifu mzuri lakini zilikuwa na fursa nzuri ya uzalishaji, vijana wake wanapata chakula shuleni. Siyo lazima kiwe chakula kama ugali au wali lakini angalau uji kwa saa nne wanaendelea kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwamba pamoja na jitihada za Serikali za kuimarisha elimu, bado

tunahitaji kushirikiana pamoja na wazazi na wadau kuhakikisha kwamba tunatafuta njia nzuri ya kuboresha elimu ikiwemo na utoaji wa huduma kwa vijana wetu ili waweze kusoma vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imechukua hatua kubwa na za kupongezwa katika usimamizi wa masoko ya mazao. Je, ni lini itatoa mwongozo kwenye zao la kahawa kama ilivyotoa kwenye pamba, chai na korosho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la kahawa ni miongoni mwa mazao yale ambayo tumeshaanza kuyasimamia na kutolea uratibu wake vizuri na sasa tunaenda kwenye msimu wake. Kwa bahati nzuri nimeshaita kikao cha viongozi wa Vyama vya Ushirika, Maafisa Ushirika, wakiongozwa na Mrajisi wa Ushirika ndani ya Wizara ya Kilimo, Wizara yenyewe ya Kilimo kwa mikoa yote inayolima kahawa tukutane hapa Dodoma tarehe 20, ili tuanze sasa kuzungumza kwa sababu bei dira kwa kila zao haitolewi tu na Serikali bali inatolewa kwa kuwashirikisha wadau wakiwemo wakulima, wanunuzi pamoja na Bodi ambayo inasimamia zao hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunajua sasa zao la kahawa tunaenda sokoni na maelekezo ya ununuzi kwa njia ya ushirika ni pamoja na zao la kahawa, baada ya vikao hivi ambavyo pia vitaangalia gharama za uzalishaji. Pia bei dira lazima iangalie na soko la dunia ili tuweze kutoa mwelekeo na bei dira ni ile ambayo inamfanya mnunuzi asinunue chini ya hapo. Kwa hiyo, bei dira hii tutajadili kwa pamoja kupitia vikao vyetu vya wadau baada ya kufanya

mapitio haya, gharama za uzalishaji na uendeshaji kwa wanunuzi wetu lakini pia bei ya soko ya dunia ili baadaye sasa tutaitangaza na kwa kuwa masoko yanaanza tutatangaza hivi karibu baada ya kikao chetu ili sasa wakulima na wanunuzi wa kahawa waweze kujua bei dira hiyo ni kiasi gani na kila mmoja ajipange vizuri kununua kwa mfumo ambao tumeuelekeza wa ununuzi wa njia ya ushirika. Jambo hili tutalisimamia kwa lengo la kumfanya mkulima aweze kupata tija kwenye mazao yote haya ikiwemo na zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni, Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia. (*Makofi*)

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa za kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga pesa nyingi sana katika kuboresha mfumo wetu wa usafiri hasa mabasi ya mwendo kasi katika Jiji la Dar es Salaam. Pamoja na fedha hizo nyingi bado suala la usafirishaji katika Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia mradi huu lina changamoto nyingi ikiwepo mgogoro kati ya mwendeshaji na *MaxMalipo* na hata miundombinu. Je, Serikali ina mpango gani kuboresha usafiri huu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtolea, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna Mradi wa Usafirishaji Jijini Dar es Salaam (*UDART*) ambao ni muunganisho wa *UDA* pamoja na *DART*. Kwa sasa mradi huu kwa sasa unaendelea pamoja na changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge

amezisema. Niseme tu kwamba Serikali tunazijua kwamba miundombinu yetu na hasa makao makuu ya yale mabasi sasa hivi yamekuwa ni mapito ya maji kutokana na mvua kuwa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini mbili mgogoro anaousema Mheshimiwa Mbunge wa uendeshaji, popote panapokuwa na taasisi mbili zimeunganishwa kuwa chombo kimoja ili kusimamia kunakuwa na migogoro ya ndani ambayo tutaisimamia. Kwa kuwa *DART* ni sehemu ya Serikali na *UDART* ni wawekezaji lakini pia Serikali ipo, jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwaambie kwamba mfumo huu wa usafirishaji Dar es Salaam *UDART* sasa hivi tunaingia kwenye awamu ya pili ya uendeshaji ambapo tutatafuta mbia mwingine aweze kuingiza mabasi yake tuweze kupata huduma bora na *competitive* kwa maana ya ushindani ili iweze kuwa na huduma bora zaidi. Sisi tunaamini mwendeshaji mmoja anapoleta matatizo kama kuna mwingine inakuwa ni changamoto kwake, hivyo anaweza kuimarisha. Kwa hiyo, tunaendelea na hatua hiyo ili kuondoa matatizo yote ya uendeshaji yaliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale ambapo itabainika kwamba mwendeshaji wa sasa ana matatizo yaliyokithiri hatuna shida tutamuondoa kwa sababu waendeshaji wako wengi. Wako Watanzania wanaweza kuendesha, lakini yako mataifa ya nje yanaweza kuendesha yakaleta mabasi lakini pia tuna umoja ule wa UWADA (Umoja wa Wasafirishaji wa Daladala) nao waliomba pia fursa ya kuweza kuendesha mabasi na usafirishaji Jijini Dar es Salaam nao pia tutawapa fursa ya kuona kama wanaweza kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi, tunaendelea kuondoa changamoto za mwendeshaji aliyepo sasa. Pia tumeshaanza utaratibu wa kupata mwendeshaji mwingine ili tupate kampuni nyingine ambayo itaingiza mabasi yake kuimarisha usafiri wa Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, suala la miundombinu, baada ya mvua hizi kuisha tutaimarisha. Naamini wote mmeona kwamba mvua hizi zimeharibu miundombinu mingi ikiwemo na eneo la *UDART*. Kwa hiyo, tutaimarisha na tutajipanga vizuri kuhakikisha huduma hii inaendelea na Watanzania wananufaika na usafirishaji pale Jijini Dar es Salaam. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Muda wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu umeisha. Tunakushuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, *at least* orodha ya wote walikuwa wameomba wamepata nafasi, wengine nimewanyima maswali ya nyongeza ili kuwapa na wengine nafasi. Kwa maana hiyo, wote mmepata nafasi angalau ya kuuliza maswali ya msingi. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 217

**Bei ya Gesi Inayotumika Majumbani**

**MHE. ZAINABU M. AMIRI** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itapunguza bei ya gesi kwa matumizi ya majumbani ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kutumia gesi kwa matumizi yao ya nyumbani na kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Mndolwa Amiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, gesi iliyogunduliwa nchini ni gesi asilia (*natural gas*) ambayo husafirishwa kutoka kwenye visima vya gesi hadi kwa watumiaji kupitia mabomba. Mpaka sasa watumiaji wakubwa wa gesi hapa nchini ni viwanda na mitambo ya kufua umeme. Mradi wa majaribio wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ulianza kupitia mradi wa mfano (*pilot project*) ambapo nyumba 70 zilizopo Mikocheni Jijini Dar es Salaam zimeunganishwa na gesi kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa gesi inayotumiwa na wananchi kupikia majumbani ni *Liquefied Petroleum Gas (LPG)* ambayo huagizwa na wafanyabiashara kutoka nje kama ilivyo katika mafuta ya *petrol*, *diesel* na mafuta ya taa au ndege. Gesi hii hujazwa katika mitungi kwa ujazo tofauti tofauti na gharama ya gesi hii inategemeana na soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji katika sekta ya gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani ili kuleta ushindani katika sekta hii. Mpaka sasa makampuni mengi yameanza kujenga miundombinu ya gesi katika sehemu mbalimbali za nchi na kuonesha nia ya kushirikiana na Serikali katika kusambaza gesi asilia nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPDC* imeanza matayarisho ya kutekeleza mradi wa kuunganisha gesi majumbani ambapo awamu ya kwanza ya mradi huo utapita katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na Mtwara na baadaye katika mikoa mingine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainabu, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kutokana na kugundulika kwa gesi nchini mwetu, je, ni lini Serikali itasitisha

uingizaji wa gesi ili tuweze kutumia gesi yetu hapa nchini?  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, *pilot project* iliyofanyika ni Mikocheni Dar es Salaam, je, ni vigezo gani vimezingatiwa katika *project* hiyo na isiwe kule ilikotoka gesi Mtwara?  
(Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainabu Mndolwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ameuliza ni lini Serikali itasitisha uagizaji wa gesi kutoka nje ya nchi. Ni kweli ugunduzi wa gesi asilia iliyogunduliwa hapa nchini ni gesi zaidi ya mita za ujazo trilioni 55,000. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge matumizi ya gesi yapo mengi kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi ikiwemo kwenye uzalishaji wa umeme, matumizi ya viwanda na matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna mipango mbalimbali ambayo inafanywa na Serikali ikiwemo pia ujenzi wa kiwanda cha kusindika gesi asilia Mkoani Lindi. Kwa hiyo, baada ya kiwanda hiki kukamilika na hizi fursa mbalimbali za usambazaji gesi na miundombinu mbalimbali ya kusambaza gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani na viwandani itakapokamilika, Serikali itatafakari kwa kina namna ambavyo inaweza kusitisha uagizaji wa gesi hiyo nchini. Kwa sasa bado tuna mahitaji na kwa kuwa mipango inaendelea, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatafakari na kuchukua hatua pale ambapo tutakuwa tumejiridhisha na soko na uhitaji wa gesi asilia ndani ya nchi na kwa matumizi ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili alikuwa anauliza kuhusu vigezo vilivyotumika kwa maeneo ya kusambaza gesi

kwa matumizi ya majumbani na ameuainisha Mkoa wa Mtwara. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuna miradi na tafiti zinazoendelea katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Dodoma, Mwanza na Tanga chini ya Mradi wa *JICA* ili kuona mahitaji ya matumizi ya gesi ya kupikia ili kuanza mradi wa usambazaji wa gesi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nimthibitishie katika Mkoa wa Mtwara kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha shilingi milioni 140 zimetengwa kuendelea na *study*hiyo na kwamba mkoa huo utapatiwa usambazaji wa gesi kwa matumizi ya nyumbani. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mashekhe mnamtia gesi majumbani? Hili swali lina wenyewe hili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Halima Mdee, nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kufuatia ugunduzi wa gesi, Serikali ya CCM iliwahakikishia Watanzania na wananchi wa Mtwara kwamba maisha yetu kwa kiwango kikubwa yatabadilika. Ikumbukwe kwamba bomba la gesi lilijengwa kwa mkopo usiopungua shilingi trilioni 1.5 kwenda shilingi trilioni 2. Hivi tunavyozungumza na kwa taarifa za Serikali inaonesha kwamba tunatumia asilimia 5 tu ya gesi katika bomba husika. Nataka tu Serikali ituambie, Deni la Taifa linakua, tulikopa tukajenga bomba tukajua kwamba tunapata suluhu lakini sasa hivi tunatumia bomba asilimia 5, ni nini kimetokea hapo katikati kilichopelekea kushindwa kulitumia kwa asilimia 95 ? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa tena kuna mpango *Stigler's Gorge* wa kuzalisha umeme. Sasa mtuambie bomba la gesi limekwamia wapi katika uzalishaji wa umeme na hii *Stiegler's Gorge* inaanzia wapi ili kama Taifa tuwe na taarifa, maana tunaona tunapelekwapeleka tu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilitekeleza mradi mkubwa huu wa ujenzi wa bomba la gesi la Mkoa wa Mtwara. Kama alivyoeleza kwenye swali lake, kwa sasa matumizi ya kusafirisha gesi kwa kupitia bomba hili kwa mwaka huu unaoendelea imefika lita za ujazo milioni 175 kutoka milioni 145 za mwaka 2016/2017, ni wazi ongezeko linatokana na mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimthibitishie tulipokuwa tunajenga bomba hili na ahadi tulizotoa kwa wana Mtwara, ahadi zile ni sahihi kwa sababu kuna miradi mbalimbali ambayo inayoendelea. Kwa mfano, Mtwara peke yake tunajega mradi wa kuzalisha umeme wa *megawatts* 300 kwa kutumia gesi asilia ya Mkoa wa Mtwara. Sambamba na hilo, pia kuna mpango wa kujenga mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia Somanga Fungu, kwa kuzalisha *megawatts* 330 kwa kutumia gesi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote lazima izalishe umeme kwa vyanzo mbalimbali, huwezi kutumia gesi asilia peke yake ukatosheleza mahitaji ya nchi nzima. Ndiyo maana tunazalisha umeme kwa kutumia maji na gesi. Sasa hivi zaidi ya asilimia ya 50 *megawatts* zinazozalishwa zinatumia gesi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba gesi ambayo iligundulika Mtwara imeleta tija katika uzalishaji wa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama tunavyofahamu umuhimu wa kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo vingine, Serikali imetafakari, kwa sababu lengo la Serikali ni kuzalisha umeme wa bei nafuu na kumfikia mtumiaji kwa bei nafuu. Ndiyo maana Serikali imekuja na mradi wa *Stiegler's Gorge* utakaozalisha *megawatts* 2,100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimewahi kusema ndani ya Bunge

Iako Tukufu kwamba uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji una unafuu zaidi, unatumia shilingi 36 ukilinganisha na gesi ambayo ni shilingi 147. Kwa nchi inayotarajiwa kujenga viwanda nchi nzima na kazi inayoendelea lazima tuzalishe umeme kwa wingi. Kwa kuwa lengo la Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ni kuzalisha *megawatts* 5,000 mradi wa *Stiegler's Gorge* ndiyo wakati wake muafaka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu ya uhakika. Haya ndiyo majibu tunayoyataka kutoka Serikalini namna hii. Maana Mheshimiwa Halima amejibiwa mpaka mwenyewe kakubali. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

Na. 218

**Fidia kwa Nyumba Zilizowekwa Alama ya "X"  
Kitongoji cha Sanzale-Bagamoyo**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Upanuzi wa barabara kutoka mita 22.5 hadi 30 kutoka katikati ya barabara umesababisha baadhi ya wananchi katika Kitongoji cha Sanzale, Kata ya Magomeni kufuatwa na barabara na nyumba zao kuwekwa X:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, tafadhali Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara ya mwaka 1932 ilifanyiwa mabadiliko mwaka 2007, ambapo eneo la hifadhi ya barabara lilibadilika kutoka mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande wa barabara kuu na barabara za Mikoa kuwa mita 30 na hivyo kufanya eneo la hifadhi ya barabara kuwa mita 60 badala ya mita 45 za awali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko hayo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilifanya zoezi la kuainisha maeneo yote yaliyoathirika na Sheria mpya ya Barabara ya mwaka 2007 kwa nchi nzima. Aidha, wananchi wote wenye mali zao katika eneo la kuanzia mita 22.5 hadi 30 kutoka katikati ya barabara kila upande ambao wamewekewa alama ya "X" ya kijani watalipwa fidia kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa pindi maeneo yatakapohitajika kwa ajili ya ujenzi au upanuzi wa barabara na hivyo mali zao kuathirika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, nilikuona.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na shukrani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ambayo amenipa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, eneo lile la Kitongoji cha Sanzale ni Bagamoyo Mjini na wananchi hawa wamewekewa alama za "X" miaka nane imepita, hawawezi kukarabati nyumba zao, hawawezi kujenga upya, hawawezi

kufanya chochote na majibu ni kwamba watafidiwa pale maeneo yatakapohitajika. Je, ni lini maeneo hayo yatahitajika kwa sababu wananchi hawa *psychologically* wameendelea kupata matatizo makubwa sana? Wafanye nini maana wanaishi na watoto wao katika nyumba ambazo zimewekewa "X" lakini hawajui lini watalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika barabara ya Makofia - Mlandizi ambayo imo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 pia katika Ilani ya mwaka 2015 kujengwa kwa kiwango cha lami. Wananchi hawa wanapenda kujua fidia zao zitalipwa lini?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASLIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kwa kufuatilia sana maendeleo ya Bagamoyo kwa ujumla wake. Natambua kwamba kutakuwa na ujenzi wa bandari ya Bagamoyo na hivyo hizi barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge anazitaja ni muhimu kweli. Yeye mwenyewe anatambua kwamba zipo harakati za awali ambazo zimefanyika ili kuhakikisha kwamba fidia kwa wananchi wake zinalipwa mapema.

Mheshimiwa Spika, swali lake anasema ni lini sasa tutalipa fidia hiyo. Niseme kwamba harakati za ujenzi wa barabara ya lami kwa barabara ambazo zinaingia Bagamoyo zinaendelea na hatua za tathmini zimeshafanyika na kwa vile zina hatua mbalimbali, kwa upande wa *TANROADS* tumeshafanya jukumu letu na tunaendelea

kuwasiliana ili kuweza kupata fedha ili wakati wowote tuweze kuwalipa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, najua kwa eneo hili amelitaja mahsusi Mheshimiwa Mbunge, wapo wakazi wasiozidi 20 ambao wanahitaji kufanyiwa malipo ya *compensation*. Kwa hiyo, nikuombe tu Mheshimiwa Mbunge na Ndugu zangu wananchi wa Bagamoyo eneo hili wavute subira wakati wowote tutafanya zoezi la kuweza kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anauliza juu ya *compesation* kwenye barabara hii inayotoka maeneo ya Mlandizi kuja Bagamoyo. Kama nilivyosema barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya kuja kutoa huduma katika Bandari ya Bagamoyo itakapojengwa hii ikiwa ni pamoja na eneo lingine kuja Bagamoyo ukitokea Kibaha, maeneo ya Vikawe kuja Mapinga na kwenyewe harakati zinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, natambua Ilani ya mwaka 2010 ya Chama cha Mapinduzi na Ilani ya mwaka 2015 imetaja kupanua barabara hii. Kwa hatua ambazo tumefikia wananchi wameshapata *valuation form* wazijaze, wazirudishe halafu Serikali tutasimamia kwa haraka ili wananchi hawa pia waweze kulipwa kulingana na sheria inavyotaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia, nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, majanga mengi sasa hivi yanasababishwa na binadamu zaidi ya asilimia 96 ikiwepo kwenda kinyume na uumbaji wa dunia ya Mwenyezi Mungu. Sheria hii ya tangu mwaka 1932 mpaka 2007 kwa kiasi kikubwa ni uharibifu mkubwa wa mazingira na hasa



barabara za vijijini. *International Standard* na vigezo vyake vya ujenzi wa barabara huwezi uka-*upgrade* barabara kutoka *stage* moja kwenda *stage* nyingine za vijijini ukafanya mita 60.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zinazoenda vijijini, kwa mfano barabara ya Kawawa - Pakula, Jimbo la Vunjo na barabara ya Himo na Himo - Mwika, kwa nini mnaamua kuchukua mashamba bila fidia na siyo *standard*? Barabara zinajengwa kwenda juu na siyo kupanua tu kwa *horizontally*?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kulipongeza Bunge kwa kutunga Sheria hii Na.13 ya mwaka 2007 ambayo kwa kweli ilizingatia sana mabadiliko, ukiisoma Sheria ya mwaka 1932 utaona namna ilivyokuwa. Kwanza ilikuwa ni ndogo sana, ilikuwa na kama *section* saba tu na ilikuwa inatoa mamlaka makubwa sana kwa wale watekelezaji wa ujenzi wa barabara wanaweza wakafanya maamuzi, sheria iliyowaruhusu. Mabadiliko haya yaliyokuja mwaka 1969 na baadaye kuja hii Sheria Na.13 imetoa nafasi kwa Mamlaka zetu za Barabara kuweza kuzingatia maeneo maalum na kuweza kufanya *declaration* ya ujenzi wa barabara. Hivyo, sheria ipo vizuri ni vema tu tuendeleo kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, nimueleze Mheshimiwa Mbatia niseme kwamba Serikali inalipa fidia kulingana na sheria zilizopo pia lazima tuangalie na mamlaka zetu katika halmashauri. Mamlaka za Barabara zipo kwenye Halmashauri

zetu, kwa mfano, sasa hivi tunayo *TARURA* na *TANROADS* kwa upande wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tu tukatazama sheria zote, Sheria za Barabara pamoja na sheria za kusimamia mamlaka zetu ili wananchi waweze kupata haki. Kama jambo hili linaweza kuwa mahsusi Mheshimiwa Mbunge alilete tulizungumze tuone namna nzuri ya kulishughulikia lakini Serikali ina nia thabiti ya kuwalipa wananchi fidia kulingana na sheria zilizopo.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa. Tuendeleo na Wizara ya Kilimo tafadhali, swali linaulizwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

*(Swali Na. 219 na Na.220 yalirukwa)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, samahani, swali langu Namba 219 umeliruka.

**SPIKA:** Tatalirudia.

Na. 221

**Agizo la Kahawa Kuuzwa Kwenye  
Vyama vya Msingi**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Serikali imezuia biashara ya BUTURA na wanunuzi wa kahawa kwa watu binafsi (moja kwa moja kwa wakulima) na kuagiza yote iuzwe kwa Vyama vya Msingi wakati vyama kama *KDCU* vilishindwa kuwapa bei nzuri wakulima:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inakuja na mbinu mpya ya kuwapa bei nzuri wakulima wa kahawa?

(b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa haraka ili kuhakikisha wale walioua Vyama vya Ushirika wanashtakiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imejipanga kuhakikisha kuwa biashara ya zao la kahawa itaendeshwa na kusimamiwa na Vyama vya Ushirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali chini ya mfumo wa stakabadhi za ghala. Aidha, kupitia mfumo huu, kahawa ya mkulima itakusanywa na kukobolewa na kisha kuuzwa mnadani chini ya usimamizi wa Vyama Vikuu vya Ushirika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Kahawa na Bodi ya Stabadhi za Ghala ambapo kahawa itanunuliwa kwa bei ya ushindani na yenye tija itakayowezesha mkulima kulipwa malipo ya pili na ziada.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), imeendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara na kaguzi za kiuchunguzi katika vyama vya ushirika na kuchukua hatua mbalimbali za kisheria pindi inapobainika kuwepo kwa ubadhirifu. Aidha, wahusika wa ubadhirifu wamekuwa wakichukuliwa hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na Bodi za Uongozi na Menejimenti zake kuondolewa madarakani na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola ambapo baada ya uchunguzi kukamilika watuhumiwa hushtakiwa Mahakamani na kuwataka kurejesha fedha walizoiba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate, tafadhali.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake kuhakikisha inaboresha zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, kwenye zao la kahawa kulikuwa na kodi nyingi na Serikali imejitahidi kuondoa kodi 17, lakini hizi kodi hazimnufaishi mkulima moja kwa moja zinawalenga wafanyabiasha. Je, Serikali imejipanga vipi kuondoa hizi kodi ambazo zinamgusa moja kwa moja mkulima ili aweze kupata bei nzuri ya kahawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mara nyingi mkulima anapoanza kulima, kupalilia mpaka kuvuna hasaidiwi kitu chochote, mwisho anaanza kukatwa kodi na mambo mengine. Je, Serikali imejipanga vipi kumsaidia huyu mkulima ili iweke miundombinu mizuri kuanzia anapolima akiwa shambani mpaka kwenye mnada? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa ukaribu sana zao hili la kahawa ambalo linalimwa pia kwa wingi katika Jimbo lake lile la Kyerwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye maswali yake mawili ya nyongeza, katika swali lake la kwanza, ni kweli kwamba Serikali tumeliona hili na ndiyo maana tumeanzisha ule utaratibu wa kuuza kahawa mnadani moja kwa moja kupitia Vyama vyetu vya Ushirika. Vilevile Serikali tumepunguza tozo ya mauzo ya mazao kupitia *cess* au *farm gate price* kutoka asilimia 5 hadi asilimia 3.

Mheshimiwa Spika, swali lake lile la pili ni kwamba zao la kahawa linategemea sana na muonjo ule wa kahawa. Kwa maana hiyo, katika kuweka ubora wa miundombinu pia na ubora wa zao lenyewe, ni kwamba kulekule shambani wakulima wanapaswa kutumia zile CPU kwa ajili ya kuchakata zile kahawa kwa sababu kahawa mbichi hairuhusiwi, hivyo iweze kuanikwa na kusafishwa vizuri, kabla haijapelekwa kukobolewa kule kwenye curing.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba.

Na. 219

### **Hitaji la Malambo – Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Jimbo la Mlimba lina mito mingi inayotiririka mwaka mzima ambayo inaweza kutumika kujenga malambo kwa ajili ya mifugo:-

Je, ni lini Serikali itajenga Malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Mlimba?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa

Mbunge kwamba uwepo wa mito mingi katika Jimbo la Mlimba ni fursa kwa ajili ya upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali ikiwemo mifugo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara yangu imepokea ombi la Mheshimiwa Susan Kiwanga na litazingatiwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019. Pia nitoe wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuhamasisha sekta binafsi, wafugaji pamoja na wadau wa maendeleo kuibua miradi ya ujenzi wa malambo, mabwawa, majosho na visima virefu kwa lengo la kuboresha shughuli za ufugaji ili kuleta tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimepokea majibu ya Naibu Waziri. Kwa kuwa ametoa ahadi na bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakuja tarehe 17 Mei, 2018 na tarehe 18 Mei, 2018, nitajiridhisha kwenye vitabu vyao kama kweli wametenga na wameingiza kuhusu ujenzi wa malambo ndani ya Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nampongeza Mkurugenzi na Halmashauri ya Kilombelo angalau tumetenga sisi kwa mapato ya ndani shilingi milioni 103 kwa ajili ya kuboresha na kujenga malambo ndani ya Halmashauri na Jimbo la Mlimba. Hizo ni jitihada tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu linakuja, kwa kuwa, Jimbo la Mlimba lina takribani vijiji 18 na kuna kilometa 606 eneo ambalo wafugaji wamekaa huko kwa wingi na vinaenda kufutwa, je, Wizara hii au Naibu Waziri yupo tayari sasa kwenda Jimbo la Mlimba kuangalia taharuki hii inayotokea kwa wafugaji hao na kuona umuhimu wa kuweka malambo ili wananchi hao na wafugaji wasiende kuingia kwenye haya maeneo ambayo yanachukuliwa na Serikali kwa ajili ya kupeleka maji kwenye *Stiegler's Gorge*? Kuna taharuki kubwa sana ndani ya Jimbo la Mlimba. Je,

yupo tayari sasa kwenda kuangalia na kupanga mipango sahihi? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Susan Kiwanga. Kwa ruhusa yako, naomba nimpongeze sana Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mlimba kwa kutenga pesa hizo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mifugo yetu inapata maji.

Mheshimiwa Spika, swali lake ni kutaka kujua kama niko tayari kwenda naye Mlimba kuangalia juu ya adha wanayopata wafugaji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tunafahamu ufugaji ni maisha yetu na maisha yetu ni ufugaji. Hivyo, nipo tayari kwenda Mlimba kuungana naye kwa ajili ya kwenda kuwaona wafugaji hawa.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na linaulizwa na Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, tafadhali.

Na. 220

### Hitaji la Chuo cha Ufundi Lushoto

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Wilaya ya Lushoto haina Chuo cha Ufundi (VETA) na kuna vijana wengi waliohitimu elimu ya msingi na sekondari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Chuo cha Ufundi (VETA) ili vijana hao waweze kupata elimu ya ufundi ya kuwasaidia katika kujajiri?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Olenasha, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya kuandaa rasilimali watu watakaotumika katika viwanda ili kufikia lengo la Serikali kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025. Vyuo hivi vitasaidia kuwaandaa vijana kwa kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kujijiri na kuajiriwa ikizingatiwa kuwa kundi kubwa la vijana wetu halipati fursa ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wake wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vya Mikoa na Wilaya ikiwemo Lushoto kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Lengo ni kila Mkoa na Wilaya kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na ujenzi wa vyuo hivyo, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi (*Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ*) ambapo katika mradi huu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vitakarabatiwa ili kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi sambamba na elimu ya wananchi. Hivyo, katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea na jitihada hizi, nashauri wananchi wa mikoa na wilaya zote ambazo hazijawa na vyuo vya *VETA* kutumia vyuo vya ufundi vilivyopo nchini hususan kwenye mikoa na wilaya jirani ili vijana wetu wapate



ujuzi na stadi hizi muhimu kwa maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Chuo cha *VETA* kiko mbali sana na Wilaya ya Lushoto na hii imesababisha vijana wengi wa Lushoto kukosa fursa ya kujajiri na kuajiriwa, je, Serikali haioni kwamba imefikia wakati sasa kuchukua hatua za haraka ili kuwajengea chuo hicho vijana wa Lushoto waweze kupata elimu hiyo ya ufundi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali pili, kwa kuwa kuna majengo ya *TBA* na majengo yale yana karakana ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Je, Serikali haioni sasa kuwa kuna haja ya kurudisha majengo hayo katika Wizara ya Elimu kwa nia ya kufungua Chuo cha *VETA* katika majengo hayo ili vijana wa Lushoto waliokosa elimu hiyo ya ufundi kwa muda mrefu waweze kupata sasa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa William Olenasha, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi Stadi Lushoto, naomba nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kwamba kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, Serikali itaendelea kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika wilaya na mikoa yote kadri fedha zitakavyopatikana. Kwa hiyo, kwa sasa nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zikipatikana Serikali itajenga Chuo cha Ufundi Lushoto kama itakavyofanya katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu majengo ya *TBA* kama ni wakati sasa wa kurudishwa Wizara ya Elimu ili yaweze kutumiwa kama Chuo cha *VETA*, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba hili linawezekana lakini wao waanzishe mchakato katika ngazi yao ya halmashauri, wawasiliane na *TBA*. Wakishapata yale majengo kwa maana ya wakiruhusiwa, sisi Wizara ya Elimu tuko tayari kuja kuyakagua na kuangalia kama yanafaa kuwa *VETA* na hatimaye tukiona yanafaa hatuna kipingamizi, tutahakikisha kwamba majengo yale yanageuzwa kuwa *VETA*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia muda mtaona muda wetu wa kipindi cha maswali unatakiwa uishie hapo. Kwa hiyo, tuendeleo na matangazo ya wageni.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza katika Jukwaa la Spika, nina wageni maalum kabisa, wageni wa Spika ambao wamenitembelea nao ni *mate* wenzangu wanne ambao tulisoma nao Kibaha Sekondari enzi hizo. Karibuni sana. Naomba nimtambulishe kwenu ndugu Jackson Kalikumtima, karibu sana Jackson; Ndugu David Nchaina, karibu sana David; Ndugu Hussein Mzara, karibu sana pamoja na Ndugu Sadik Shekimweri. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, unajua ukipata nafasi ya kukutana na wenzako mlisoma pamoja basi inatia moyo pia kuona tumezeeka kiasi gani sasa toka enzi zile. Tulipokuwa tukicheza ule mpira usiokuwa na refa wala usiokuwa na idadi ya wachezaji, kule Kibaha Sekondari unaitwa Mbugi, hata watu 100 mnacheza kwenye uwanja mmoja huo huo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia, nimtambulisha Ndugu Frank Kanyusi, Afisa Mtendaji Mkuu *BRELA*, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine tulionao katika Jukwaa la Spika ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambao wameongozana na Katibu Mkuu Prof. Elisante Ole Grabriel. Karibu sana Katibu Mkuu. Naibu Katibu Mkuu, Biashara na Uwekezaji, Ndugu Joseph Buchweishaja, karibu. Naibu Katibu Mkuu Viwanda, Ndugu Ludovick James Nduhiye, karibu. *(Makofi)*

Pia, tunao Wenyeviti wa Bodi, Mwenyekiti wa Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (*TEMDO*), Prof. Patrick Makungu; Mwenyekiti wa Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*), Profesa Makenya Maboko na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TANTRADE*), Eng. Christopher Chiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chiza alikuwa ni Mbunge mwenzetu huyu na alipata kushika nafasi mbalimbali katika Serikali ikiwemo ya kuwa Waziri wa Kilimo na masuala ya Umwagiliaji, Mbunge kutoka kule Kibondo, nadhani Jimbo la Muhambwe kama sikosei, wakati huo. Karibu sana Mheshimiwa Chiza Bungeni tena kwa mara nyingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Mwenyekiti wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*), Prof. Longinus Rutasitara, karibu; Mwenyekiti wa Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), Dkt. Samuel Nyantahe; Mwenyekiti wa Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*), Prof. Idris Mshoro; Mwenyekiti wa Bodi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (*CARMATEC*), Prof. Suleiman Chambo; Mwenyekiti wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (*TFC*), Prof. Egid Mubofu. Karibuni sana. Pia, wameambatana na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi mbalimbali, Idara, Vitengo vilivyo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni mwingine wa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara leo ambaye yuko kwenye Jukwaa ni Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo. Mhandisi Evarist Ndukilo ni Mkuu wa Mkoa ambaye amejipambanua katika masuala ya uwekezaji wa viwanda, mkoa wake ukiwa unaongoza kabisa katika kuvutia wawekezaji katika eneo la viwanda. Tunakushukuru sana, tunakupongeza sana Mhandisi Ndikilo kwa kazi nzuri unayoifannya. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Kamati ya Maudhui ya TCRA. Karibuni sana Kamati ya Maudhui. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 74 wa Mheshimiwa Emmanuel Papian ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Engusero iliyopo Kiteto Mkoani Manyara. Karibuni sana walimu na wanafunzi wa Engusero, majirani zetu wa Kongwa hawa. *(Makofi)*

Mgeni wa Bunge *Sports Club* kutoka Mkoani Morogoro ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Ngeleja ni Ndugu Francis Cheka. Kwa hatua hii niwatambulishe, kama mnavyojua Ndugu Francis Cheka ni *boxer*, siku ya Jumamosi tarehe 12 katika uwanja wa Jamhuri kutakuwa na pambani la mchezo wa ngumi wa Kimataifa kati ya Ndugu Francis Cheka ambaye atapambana na Ndugu Liben Masamba wa kutoka Malawi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tunakaribishwa Jumamosi Uwanja wa Jamhuri, *VIP* mtaingia kwa Sh.50,000 na mzunguko Sh.10,000. Mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambao ni viongozi wa CCM kutoka Ngara, Mkoani Kagera. Karibuni sana wageni kutoka Ngara. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa Silvestry Koka ambao ni wafanyabiashara kutoka Kibaha Mkoani Pwani. Karibuni sana wafanyabiashara kutoka Pwani. Mmekuja siku nzuri sana maana leo ni siku ya mambo yenu ya biashara. Kwa hiyo, kaeni hapa msikilize mambo ya biashara yatakavyoteremka hapa. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni viongozi wa CCM, Kata ya Sanjaranda - Itigi, Wilaya ya Manyoni, Mkoani Singida. Karibuni sana pale mlipo wageni wa kutoka kule Itigi. *(Makofi)*

Wageni 37 wa Mheshimiwa Elibariki Kingu ambao ni Wenyeviti na Makatibu wa CCM wa Kata za Jimbo la Singida Magharibi wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya na Katibu wa CCM wa Wilaya. Karibuni sana Wanyampaa. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaye ni mjomba wake Ndugu Hamdani Salum. *(Makofi)*

Wageni Sita wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ambao ni familia yake na wapiga kura wake kutoka Mufindi Mkoa wa Iringa. Karibuni sana wageni kutoka kule Mufindi. Mheshimiwa Mgimwa ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara na mtaona hapa akifanya mambo yake baadaye. Hapana, Mheshimiwa Mgimwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Samahani sana nimechanganya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wanne wa Mheshimiwa Edward Mwalongo ambao ni kaka zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mwisho ni wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya John Merlini iliyopo Miyuji Jijini Dodoma. Ooh! Karibuni sana watoto wazuri. Karibuni sana Bungeni na baadaye nina hakika mtapata maelezo yanayohusu Bunge na mtapata nafasi ya kuuliza maswali mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Mendrad Kigola, anawatangazieni Waheshimiwa Wabunge ambao mnapenda kushiriki katika zoezi la kulenga shabaha ambalo huwa linafanyika JKT Makutupora, muda wa mazoezi mtatangaziwa ila anachoomba ni kwamba mjiandikishe pale mapokezi. Kwa wale wanaopenda mchezo wa *range*, kulenga shabaha kwa silaha mbalimbali, msiokuwa na mishtuko ya moyo mjiandikishe Jengo la Utawala pale chini ili tukishapata idadi yenu basi ipangwe ratiba kwa ajili ya kwenda JKT Makutupora kwa ajili ya zoezi la kulenga shabaha.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho wa matangazo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Katibu, nisomee majina.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Simba Chawene, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Maftaha.

**SPIKA:** Tunaanza na Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), naomba nipate Mwongozo wako kwa Kanuni yenyewe hiihii ya 68(7) na naomba niisome, inasema kwamba:-

*“Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba “Mwongozo wa Spika” kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema...”.*

Mheshimiwa Spika, naomba nipate ufafanuzi tafsiri ya hili neno ‘Bungeni’, kwa maana ya kwamba Bungeni tunamaanisha kwenye viti hivi ndani ya Bunge au Bungeni

hata ukiingia getini pale *compound* hii ya eneo lote ni Bungeni? Nilikuwa naomba mwongozo wako juu ya tafsiri hii.

**SPIKA:** Eneo lote hili kama ulivyosema hilo la pili ni Bungeni.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Ni eneo lote?

**SPIKA:** Haimaanishi chumba hiki peke yake.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, jana niliomba mwongozo kutokana na mambo ambayo yalikuwa yanaendelea katika eneo hili la Bunge. Kulikuwa na watu wa Serikali wa Wizara ya Ardhi lakini pia TAMISEMI wakiwa wanagawa viwanja kwa Waheshimiwa Wabunge na kwamba vile viwanja tumepewa muda maalum ndani ya siku 30. Kwa hiyo, niliomba mwongozo kwamba kwa nini Bunge lisiweke utaratibu ili sisi Waheshimiwa Wabunge tuweze kuishi hapa *comfortably* tukiwa na viwanja na tumejenga nyumba kwa sababu hali ya kiuchumi sasa hivi ni mbaya kwa Waheshimiwa Wabunge, ukaongezwa muda hivi angalau miezi sita.

Mheshimiwa Spika, hivyo niliomba mwongozo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha, nimekusikia na nimekuelewa. Utaratibu uliowekwa na Manispaa au sasa Jiji la Dodoma ndiyo huo na ni kwa wananchi wote kwamba anayetaka kiwanja, viwanja vipo unachagua kiwanja, unalipia ndani ya mwezi mmoja, kwa wananchi wote. Sasa ukisema Waheshimiwa Wabunge peke yao wachukuliwe kama ni daraja la kipeke yake wao wapewe miezi sita, wakati mwananchi wa kawaida anapewa mwezi mmoja, sidhani kama jambo hilo linakubalika kwa kweli. Kwa hiyo, ukitaka kiwanja, kiwanja kipo ndani ya siku 30 uwe umemaliza

kulipa ili fedha zile zipime viwanja vingine. Kwa hiyo, Bunge hatuwezi kubadilisha maamuzi ya Manispaa lakini ni ombi ambalo Manispaa au Jiji sasa wamelisikia, tuwaachie waangalie uzito wake kadri watakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) juu ya jambo ambalo limetokea mapema Bungeni nalo ni swali Na.218 la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa kuhusu mita za barabara ambazo zimeongezeka kwa sheria ya mwaka 2007, mita nane kutoka zile 22.5 mpaka mita 30. Kila wakati Serikali imekuwa ikijibu kwamba haya maeneo ya wananchi yatatumika pale Serikali itakapokuwa inahitaji na hata leo Mheshimiwa Dkt. Shukuru amejibiwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sisi ni watu ambao tumeathirika sana na hizi mita, ni miaka 11 sasa wananchi wengi wa Jimbo langu wameathirika kwa sababu Babati Mjini tuna barabara tatu za lami tumeunganishwa Singida kilometa 163, Arusha kutoka Babati kilometa 167, Babati – Dodoma kilometa 258, mita nane kila upande wananchi wana nyumba zao, Serikali haijui ni lini itawafidia, inasema siku ikihitaji itawafidia.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wamejenga nyumba zao, hawaruhusiwi kukarabati wala hata kujenga choo kama kimebomoka. Naomba mwongozo wako, ni kwa nini Serikali iendeleo kutujibu hivi wakati sheria hii mwaka 2007 wakati inatungwa, hii sheria iliwakuta na wana nyumba zao na wanategemea miaka 50 ijayo bado hatutapanua barabara zetu na sitegemei kama upanuzi utafanyika mapema. Kwa nini wananchi hawa wasifidiwe na Serikali inaendelea kutujibu hivyo wakati wananchi wanahangaika na nyumba zao zimedondoka?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.  
*(Makofi)*



**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Gekul, si ni sheria ilipitishwa na Bunge hili hili. Hebu tuendelee kwanza tuone, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo ambao unaenda kuzingatia majadiliano ambayo tunaendelea nayo ya bajeti hasa wakati wa Kamati ya Matumizi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua na iweze kueleweka ni Kanuni ipi hasa ambayo inatumika kipindi kile ambapo unakuta umesimama ili kuweza kum-*support* Mbunge ambaye amekuwa ameshika shilingi. Tumeona wakati wa Kamati ya Matumizi, Wenyeviti wamekuwa wakitumia Kanuni mbili, kuna mwingine anatumia ya Kanuni ya 56 ambayo inataka watu 10 waunge mkono hoja ndiyo iweze kujadiliwa lakini *at a time* unakuta kuna Mwenyekiti amekaa hapo anarejea Kanuni ya 103 ambayo mimi nahisi ndiyo *right one* kwa sababu inazungumzia hoja ya kuondoa shilingi kwenye majadiliano wakati wa Kamati ya Matumizi na haiweki *specifically* ni idadi ya watu wangapi ambao watasimama ili waweze kupewa nafasi kuweza kuunga mkono au ku-*support* kwa kuchangia hoja hiyo. Hii imeleta sintofahamu na inapoka haki ya kuweza kujadili kwa kina kuhusiana na hoja ambayo inakuwa Mezani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nijue, ni kwamba inatumika Kanuni ya 56 ambapo unakuta kama Mbunge ana hoja na imetaja kabisa kwamba Spika atamtaja Mbunge atoe hoja yake na baaaye ataendelea kuelezea kwa dakika tano na baadaye kuomba aungwe mkono kama itakubaliwa au kukataliwa au tunatumia hii Kanuni ya 103 ambayo imeweka bayana ni wakati wa Kamati ya Matumizi ambapo kama mimi nimeshika shilingi nasema naendelea kushika shilingi hata wakisimama wanne au watatu

wanachangia? Ningeomba ufafanuzi wa kina ili iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Hili litatolewa ufafanuzi wake kesho baada ya Katibu wa Bunge kuchambua na kuona njia ipi bora zaidi. Japo la kuungwa mkono linakuwa na uzito lakini tutaona hiyo kesho kwa sababu watu wengine wanatucheleweshā na hoja ambayo haina hata uzito, yuko nayo yeye peke yake, ndiyo maana ya kusema kwamba uwe na hoja inayoungwa mkono lakini kesho tutapata maelekezo ambayo ndiyo tutayafuata wote. Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nami nasimama kuomba mwongozo kwa Kanuni hiyohiyo ya 68(7). Tunaendelea na kipindi cha bajeti na najua kwamba bajeti inachukua mchakato mrefu kuanzia Serikali za Mitaa, wadau, kwenye Kamati zako za Bunge na baadaye inakuja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni wiki iliyopita tu tumepitisha bajeti ya Wizara ya Elimu na katika bajeti hiyo zilikuwa zimetengwa shilingi bilioni 2 kwa ajili ya upanuzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hata hivyo, ni juzi tu Mheshimiwa Rais ameamua fedha hizo zihamishwe kupelekwa Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, ni sahihi Bunge lako Tukufu liwe limepitisha mafungu haya halafu Mheshimiwa Rais aweze kuhamisha? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan una uhakika na jambo hilo? Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa kupitia Kanuni ya 68(7). Kimsingi mwongozo naouomba unahusu suala la utaratibu wa uendeshaji wa Bunge letu kupitia msingi wa Katiba, mila na desturi za Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kumetokea mazoea ya kukiuka Kanuni ya 64 na naomba nisome eneo ambalo nataka kupata mwongozo wako. Kanuni hii pamoja na kutambua haki ya Wabunge ya mjadala, haki ya Wabunge kusema jambo lolote inayotajwa na Katiba katika Ibara ya 100 lakini ikatengenezwa Kanuni ya 64 ambayo inakataza mambo fulani fulani katika Bunge hili. Inasema:-

*"(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-*

*(d) hatatumia jina la Rais kwa dhuhaka katika mjadala, au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.*

*(e) hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika wa Bunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahususi kuhusu jambo husika". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni hii imekuwa ikivunjwa mara kwa mara na *Chief Whip* wetu mara nyingi sana amekuwa akisimama kwa ajili ya eneo hili na mara nyingi sana Meza imekuwa ikikubaliana na *Chief Whip*. Je, utaratibu huu unapozidi kuendelea kila siku wakati Katiba yetu katika Ibara ya 33(2) inamtaja Rais kama Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Katiba hii imewaweka watu ndani ya Bunge hili na Ibara ya 52 inamtaja Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti na usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaani yuko humu ndani Bungeni na pia kuna Mawaziri wako humu ndani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapochangia wanawaacha hawa wote hawa wanataka kuzungumza kuhusu Rais. Mazoea haya ni kinyume kabisa na mila na desturi zetu za Kitanzania za kuheshimiana. Hivi katika nchi hii ni nani anayestahili

kuheshimiwa zaidi ya Rais? Ndiyo maana hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kukutana na Rais uso kwa uso wanazungumza hata yale ambayo hawakutaka kuzungumza kwa sababu ndiye anayestahili kuheshimiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini mazoea yaliyoko humu ni kwamba utani wa baadhi ya Wabunge ni Rais, wanaacha Waziri Mkuu yuko hapa, Mawaziri wako hapa na ndiyo maana tumepewa katika Kanuni zetu siku ya kumuuliza maswali yoyote yale Mheshimiwa Waziri Mkuu maana ndiye anaweza kuwajibishwa. Pia Bunge limewekewa utaratibu wa kuweza kumtoa Waziri Mkuu kama kuna jambo la Kiserikali kutokana na majukumu ya Waziri Mkuu halijaenda sawa. Hivi hawa wote Waziri Mkuu na Mawaziri waliopo wanashindwaje kuzungumza nao tukazungumza ndani ya Bunge lakini mpaka wamtaje mtu ambaye yuko nje ya Bunge na ni Kiongozi Mkuu wa Nchi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba mwongozo wako kuhusu jambo hili. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene uliyoyasema sidhani kama nahitaji kuongeza hata sentensi moja kwa sababu ndiyo ukweli wenyewe. (Makofi)

Ulichokifanya ni kutukumbusha tu wote kuzingatia Kanuni zetu na kuheshimu taratibu zetu na kama ulivyosema Kiti kimekuwa kikisisitiza mara kwa mara na Mheshimiwa *Chief Whip* amesimamia jambo hili mara kwa mara. Kwa hiyo, umetusaidia kutukumbusha zaidi na zaidi katika jambo hilo na sisi tunaendelea kusimamia kuona kwamba halijirudiirudii jambo hilo, nakushukuru sana sana.

Kwa wengine ambao sijatoa miongozo yao tutaifanyia kazi kadiri tunavyoenda, kama meza tumeichukua. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Viwanda,  
Biashara na Uwekezaji**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosoma Katibu, tunaingia katika kuangalia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, siku mbili leo na kesho. Kwa hiyo, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa hotuba yake na baada ya hapo ajiandae Mwenyekiti wa Kamati. Bado hatuna hotuba ya Upinzani kwa upande huo, tunapata nusu saa ya nyongeza angalau, Mheshimiwa Waziri tafadhali, karibu sana. *(Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuskilizane, nafikiri mmeliona hilo buku. Kwa hiyo, tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri, tumuazime masikio yetu ili tuweze kumsikia. Mheshimiwa Waziri, karibu sana tafadhali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hotuba yangu, naomba nikuahidi muda si mrefu nitaleta *addendum* inayoonyesha marekebisho ya maandiko katika hotuba yangu. Nitaomba mabadiliko hayo yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Ukurasa wa 13 aya 33 kuna mabadiliko ya takwimu katika sentensi ya kwanza, takwimu ya jumla ya thamani ya miradi mipya ya viwanda iliyosajiliwa kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018 isomeke Dola za Kimarekani milioni 3,667 badala ya Dola za Kimarekani milioni 4,161. Vilevile jumla ya ajira 36,025 badala ya 44,798. Ukurasa wa 29, aya ya 68, tarakimu 500 isomeke mita za luku 500,000. Ukurasa wa 349 iongezwe aya ya 350 itakayosemeka Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa rususa yako, naomba uniruhusu niwatambulisha wanaviwanda waliokuja kushuhudia bajeti hii na wengi wao wakitoka Mkoa wa Pwani. Wanaviwanda wote naomba msimame juu hadhara hii iwaone. Ahsanteni mnaweza kukaa, lakini kabla ya kuendelea ningeomba utulivu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea, naomba niombe samahani hiki kilichopo hapa mbele yenu nimekipata kwenye takwimu za Taifa ndivyo viwanda vilivyotengenezwa kijiji kwa kijiji, vyote vimeandikwa hapa kurasa 900. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuweka Mezani taarifa iliyochambua bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka 2018/2019.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sauti zenu ziko juu sana, tafadhilini sana, hasa upande wangu wa kulia huku, endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge lako Tukufu kujadili utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018, vilevile kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza kwa busara na hekima na hivyo kuendelea

kuifanya nchi yetu kuwa na amani, utulivu na maendeleo. Kwa namna ya pekee, nawapongeza kwa kusimamia kwa vitendo agenda ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa na imani nami na kuendelea kunipa dhamana ya kuiongoza na kuisimamia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kusimamia kwa umakini mkubwa masuala muhimu ya ushirikiano wa kisekta na ya Muungano kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni kuongoza Wizara mbalimbali. Kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya kuwa Naibu Waziri Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Namshukuru kwa ushirikiano anaonipa kama Naibu Waziri katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kupitia chaguzi ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imeweka msingi na mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka 2018/2019, ambayo baadhi yake yanahusu majukumu ya Wizara yangu. Pia, napenda kuungana na wenzangu kuwapongeza watoa hoja walionitangulia kuwasilisha bajeti zao na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Ahmed Sadiq Suleiman, Mbunge wa Mvomero kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia Viwanda, Biashara na

Mazingira. Pia, nampongeza Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati hiyo. Ninaishukuru Kamati nzima kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa inayoendelea kutupa katika kutekeleza majukumu yetu ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Bajeti hii. Napenda kuliihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itazingatia ushauri, mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwa uongozi thabiti kabla ya kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Ni imani yangu kuwa, mtaendeleza hekima na weledi mlionao kuisimamia na kuishauri Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuniombea, kunivumilia na kunipa moyo kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi. Pia nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Muleba Kaskazini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo langu la Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara yangu wakiongozwa na Profesa Elisante Ole Gabriel Laizer, Katibu Mkuu; Profesa Joseph Rwegasira Buchweishaija, Naibu Katibu Mkuu (Biashara na Uwekezaji) na Ndugu Ludovick James Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu (Viwanda), kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba dhana ya uchumi wa viwanda inafanikiwa.



Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kipekee kuwashukuru pia wahisani mbalimbali ambao wamekuwa wakishirikiana nasi katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Naupongeza uongozi wa Sekta Binafsi na taasisi zake chini ya uongozi wa Dkt. Reginald Abraham Mengi, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF) na Mkurugenzi Mtendaji wake Ndugu Godfrey Simbeye. Napongeza pia uongozi wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) chini ya Mhandisi Raymond Mbilinyi na Katibu Mtendaji wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge na familia za wafiwa kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Leonidas Gama wa Jimbo la Songea Mjini. Vilevile, napenda kutoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia ya majanga mbalimbali kama mafuriko, ajali za moto viwandani, ajali za barabarani na majanga mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa viwanda katika uchumi wa Taifa. Kutokana na matakwa ya wakati, leo hii ninapowasilisha bajeti yangu ya tatu nikiwa Waziri mwenye dhamana ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda tena kurejea tafsiri ya kiwanda. Kiwanda ni eneo ambalo malighafi huchakatwa kwa muktadha wa uongezaji wa thamani. Hivyo, shughuli yoyote, ndogo au kubwa, ya uongezaji thamani kwenye malighafi kwa lengo la kuzalisha bidhaa nyingine ni kiwanda.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kimataifa vya kugawa viwanda katika makundi ya viwanda vimeelezwa na nitaendelea kuvieleza zaidi. Napenda niwaeleze kuwa kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), hadi kufikia mwezi Machi 2018, nchi yetu ilikuwa na jumla ya viwanda 53,876. Kati ya hivyo, viwanda vikubwa ni 251, vya kati ni 173, vidogo ni 6,957 na vidogo sana ni 46,495. Kwa kipindi ambacho Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, chini ya uongozi mahiri wa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hadi Machi 2018, viwanda vipya 3,306 vimejengwa.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uchumi wa viwanda tunamaanisha shughuli zinazolenga maendeleo ya watu na vitu wakati maendeleo ya watu yakipewa kipaumbele na sekta ya viwanda ikiwa kiungo muhimu cha kuhamasisha maendeleo ya sekta nyingine. Sekta hizo wezeshi na tegemezi katika uchumi wa viwanda ni pamoja na kilimo, uvuvi, mifugo, misitu na madini kwa upande wa uzalishaji malighafi za viwanda. Kwa upande mwingine, ustawi wa viwanda hutegemea miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa anga, nishati, mawasiliano na maji. Aidha, uchumi wa viwanda unahitaji rasilimali watu wenye afya thabiti ambao ni muhimu katika mnyororo mzima kuanzia uzalishaji malighafi, uzalishaji wa bidhaa viwandani na usambazaji wa bidhaa hadi mikononi mwa mlaji.

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa uchumi wa viwanda utakaoleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo ni muhimu sana. Umuhimu wa sekta hiyo unatokana na ukweli kwamba inahitaji ujuzi na mitaji ambayo Watanzania walio wengi wanaimudu. Sekta hiyo ni shule kwani kwa kupitia viwanda vidogo na biashara ndogo, wajasiriamali hupata ujuzi na uzoefu wa shughuli za uzalishaji na kuweza kuhitimu kuwa wawekezaji na wafanyabiashara wa kati na wafanyabiashara wakubwa. Ili kuweza kuakisi vyema mchango wa sekta hiyo hatuna budi kuelekeza nguvu kubwa katika kubuni mikakati ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo.

Mheshimiwa Spika, ustawi wa shughuli za viwanda unategemea ushiriki wa wadau mbalimbali. Ujenzi wa viwanda unaanza kwa kutambua eneo la kujenga kiwanda ambalo hubainishwa na kuwekewa miundombinu wezeshi na saidizi na mamlaka mbalimbali. Vilevile, ili kujenga sekta ya viwanda iliyo endelevu, suala la mazingira ni muhimu. Ujenzi wa viwanda unahitaji Serikali lakini unahitaji sekta binafsi pia.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango na maendeleo ya bajeti kwa mwaka 2017/2018. Kufikia mwezi

Machi 2018, Wizara ilikusanya maduhuli ya Sh.9,728,635,810.84 sawa na asilimia 48.64 ya malengo. Vilevile, hadi kufikia tarehe 9 Aprili 2018, Wizara ilikuwa imepokea Sh.47,267,949,999.91 kwa ajili ya Fungu 44 na Fungu 60, sawa na asilimia 38.68 ya bajeti kwa ajili ya Wizara na taasisi zake. Kati ya fedha hizo, Sh.32,641,257,816.33 ni za Matumizi ya Kawaida na Sh.14,626,688,183.58 ni za Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda. Ukurasa wa 11 mpaka wa 42 katika Kitabu cha Hotuba nimezungumzia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu suala la ubinafsishaji. Kufuatia zoezi la ubinafsishaji nchini, kati ya taasisi za umma 341 zilizobinafsishwa, 156 zilikuwa na sifa ya kuwa viwanda. Kufikia mwezi Mei 2017, kati ya viwanda hivyo, 62 vilikuwa vinafanya kazi vizuri, 28 vilikuwa vinafanya kazi chini ya uwezo, 56 vilikuwa havifanyi kazi kabisa na 10 vilikuwa vimeuzwa kwa mali moja moja (*asset stripping*). Kuanzia mwezi Agosti 2017 hadi Machi 2018, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina na Wizara za Kisekta ilifanya tathmini ya viwanda vilivyobinafsishwa ili kubaini hali ya viwanda hivyo baada ya kufanya zoezi la kuhamasisha ufufuaji wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, hali ilivyo hadi mwezi Machi, 2018. Kati ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa, 61 vinafanya kazi vizuri, 22 vinafanya kazi chini ya kiwango, viwanda 18 vimefanyiwa maboresho na wamiliki wake, viwanda 35 viko chini ya uangalizi wa Serikali, viwanda 10 visivyofanya kazi vinafanyiwa tathmini kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria kulingana na mikataba ya ubinafsishwaji na viwanda 10 vilivyouzwa mali moja moja na kupoteza sifa ya kuendelea kuwa na shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, miradi mipya ya viwanda. Kuanzia Julai 2017 mpaka Machi 2018, jumla ya miradi mipya 243 yenye thamani ya Dola za Kimarekani shilingi milioni 3,667 na inayotarajiwa kuajiri watu 36,025 ilikuwa imesajiliwa. Kati ya

hiyo, miradi 99 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,317 itakayoajiri watu 12,995 ilisajiliwa na *TIC*, miradi 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 368.92 iliyoajiri watu 4,881 ilisajiliwa na *EPZA* na miradi 122 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 981 na itakayoajiri watu 18,149 ilisajiliwa na *BRELA*. Rejeba kiambatanisho changu 4, 5 na 6.

Mheshimiwa Spika, viwanda mama na miradi ya kielelezo. Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga, Serikali iliunda Timu ya Wataalam wa Serikali ikiwa na jukumu la kutambua vivutio vilivyoombwa na mwekezaji. Uchambuzi huu ulifanyika kwa kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na mabadiliko ya Sheria ya mwaka 2017 katika kusimamia rasilimali zetu. Timu hiyo imekamilisha taarifa ya awali ambayo inasubiri kutolewa maamuzi na mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Matairi Arusha. Msimamo wa Serikali ni kuhakikisha Kiwanda cha Matairi Arusha kinafanya kazi. Jukumu la kuboresha na kuendesha kiwanda hicho litakuwa mikononi mwa sekta binafsi huku Serikali ikibaki na hisa kulingana na rasilimali zilizopo bila kuwekeza mtaji zaidi. Mpaka sasa, Kamati Maalum ya Serikali inaendelea kupitia mpango wa kiwanda hicho ili kuamua utaratibu utakaofaa katika kuwekeza na kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha Magadi Engaruka Soda. Wizara kupitia *NDC* na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli imekamilisha zoezi la upimaji ardhi ya mradi pamoja na uthaminishaji wa mali ya wananchi ili kubainisha kiasi cha fidia kitakacholipwa. Michoro na matumizi ya ardhi iko kwenye hatua ya kukamilishwa. Aidha, *NDC* inaendelea kutangaza mradi huo kwa wawekezaji mbalimbali ili kumpata mbia wa kushirikiana naye kuanzia hatua ya utafiti kwa kuzingatia teknolojia bora ya kuvuna magadi hayo.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Maeneo ya Uwekezaji. Maeneo Maalum ya Serikali ya Uwekezaji (*EPZ*). Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imeendelea kuhamasisha wawekezaji ndani ya maeneo yote ya *EPZ* na *SEZ*. Hadi mwezi Machi 2018, kuna jumla ya viwanda 111 katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ*. Tathmini ya uwekezaji na matokeo ya viwanda chini ya programu za *EPZ* na *SEZ* tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya *EPZ*, imeonesha mafanikio. Hadi Machi 2018 jumla ya mtaji wa Dola za Kimarekani bilioni 1.86 uliwekezwa na mauzo ya bidhaa nje ya nchi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,359.94 yalifanyika na ajira 52,698 zimeweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, viwanda vyenye hadhi ya *EPZ* nje ya Maeneo Maalum ya Serikali. Hadi sasa, kuna viwanda 72 ambavyo vinamilikiwa na kuendeshwa na sekta binafsi chini ya utaratibu wa *EPZ* nje ya maeneo maalum ya Serikali. Viwanda hivyo vimewekeza jumla ya Dola za Kimarekani milioni 315 na kutoa ajira 13,930. Kwa mwaka 2017/2018 pekee, viwanda hivyo vimeweza kuuza nje ya nchi bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 115.12. Rejea Kiambatisho Na. 8.

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika sekta ndogo na viwanda vidogo. Mradi wa kuunganisha matrika aina ya URSUS unaendelea katika eneo la *TAMCO* Kibaha chini ya usimamizi wa *NDC*. Hadi mwezi Disemba 2017, *Semi Knocked Down (SKD)* matrika 727 yamewasili nchini ikiwa ni sehemu ya matrika 2,400 yaliyoanishwa katika mkataba na uunganishaji unaendelea. Kati ya *SKD* za matrika yaliyowasili, 148 yameunganishwa na yako tayari kwa mauzo.

Mheshimiwa Spika, uunganishaji wa magari. Kampuni ya *Jiefang Motors* simeunganisha magari 803 yanayojumuisha *SKD assembled* 354, *CBU* 449. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaandaa sera ya kuunganisha magari, ili kuhamasisha uendelezaji wa sekta hiyo nchini.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, kulikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma ikiwa ni ongezeko la viwanda vitatu kwa kipindi cha mwaka mmoja. Uwezo uliosimikwa ni wa kuzalisha tani 577,600 kwa mwaka. Kwa sasa uwezo wa uzalishaji (*capacity utilization*) ni asilimia 42.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *Kiluwa Steel* kilichoko Mlandizi Mkoani Pwani kinaendelea na uzalishaji ambapo mwaka 2017 kilizalisha tani 12,000 za vyuma. Kiwanda cha *Lodhia Steel Industry* kimeanza uzalishaji ambapo wanazalisha takriban tani 3,700 za nondo na mabomba mbalimbali. Kiwanda cha *Lake Steel Allied Products* kipo katika hatua za mwisho za kuweka mitambo na Kampuni ya ALAFimetengeneza tawi lake hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya saruji. Mpaka sasa kuna viwanda vya saruji 14 vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani milioni 10.98 kwa mwaka na uwezo unaotumika ni takriban tani milioni 7.4 kwa mwaka wakati mahitaji ya nchi ni takriban tani milioni 4.8. Aidha, uwekezaji katika kiwanda cha saruji unaendelea kukua ambapo katika kipindi cha mwaka 2017/2018, kiwanda kipya cha saruji cha *Kilimanjaro Cement* kilichoko Mkoa wa Tanga kilianza kazi.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya vigae. Nchi yetu ina viwanda viwili vikubwa vya uzalishaji wa vigae vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mita za mraba 130,000 kwa siku. Kiwanda cha *Vigae cha Goodwill Ceramic* kimekamilika na kinaendelea na uzalishaji. Kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha mita za mraba 80,000 kwa siku, kinaajiri watu 2,200 kikihusisha ajira 700 za kudumu na vibarua 1,500. Asilimia 30 – 40 ya vigae vinavyozalishwa na kiwanda hiki vinauzwa hapa nchini, wakati asilimia 60 – 70 vinauzwa nje ya nchi. Vilevile, Kiwanda cha *Twxford* kilichoko Chalinze chenye uwezo wa kuzalisha mita za mraba 50,000 za vigae kwa siku kimekamilika na kimeanza uzalishaji mwezi Novemba 2017. Kiwanda hiki kinasubiri mamlaka kuweza kukifungua.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya vioo. Tanzania ina kiwanda kimoja cha vioo na juhudi zinafanyika na tumepata wawekezaji watatu kuja kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kutengeneza chokaa. Kiwanda cha *Neelkanth Lime Ltd* kilichopo katika eneo la Amboni Mkoani Tanga kinazalisha tani 15,000 za chokaa kwa mwezi na kuajiri wafanyakazi 430. Kiwanda kipo katika hatua za awali za upanuzi ambapo Dola za Kimarekani milioni 18.4 zinatarajiwa kutumika. Upanuzi huo unaotarajiwa kukamilika mwaka 2019 utaongeza uwezo wa uzalishaji hadi tani 35,000 kwa mwezi na kuongeza ajira za moja kwa moja mpaka 1,500 na zisizokuwa za moja kwa moja 2,500. Soko kuu la bidhaa hii ni Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Zambia pamoja na migodi ya madini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya dawa. Hivi sasa nchi ina jumla ya viwanda 15 vya kuzalisha dawa na vifaa tiba. Viwanda hivyo vinazalisha asilimia 12 ya mahitaji ya dawa nchini. Ili kutatua changamoto ya uwezo mdogo wa uzalishaji nchini, juhudi za kuhamasisha uwekezaji zimeendelea kufanyika ambapo Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilifanya mkutano na wadau tarehe 4 Aprili, 2018, ambapo wawekezaji 38 walionesha nia ya kuwekeza katika sekta ya dawa na vifaa tiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya dawa na vifaa tiba, Bohari Kuu ya Tanzania (*MSD*) imetoa kipaumbele na kuingia mikataba ya kununua dawa kutoka viwanda vya ndani vinavyozalisha dawa zinazokidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya nguo. Tanzania ina viwanda 11 vya nguo na mavazi vinavyofanya kazi ambavyo kwa sasa hutumia asilimia 50 ya uwezo wake uliosimikwa. Hali hiyo imetokana na ushindani wa nguo kutoka nje ya nchi na baadhi ya viwanda kutumia teknolojia zilizopitwa na wakati na hivyo kutumia asilimia 30 tu ya

pamba inayozalishwa nchini. Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kundeleva sekta ya pamba mpaka mavazi ikiwa ni pamoja na kushirikisha Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika nyama. Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani jumla ya viwanda 7 vyenye uwezo wa kuchakata ng'ombe 2,260 na mbuzi na kondoo 9,200 kwa siku vinaendelea kujengwa. Kukamilika kwa viwanda hivyo kutaifanya Tanzania kuwa na jumla ya viwanda 25 vyenye uwezo wa kuchakata jumla ya ng'ombe 3,800, mbuzi na kondoo 10,090, nguruwe 300 na kuku 44,000 kwa siku. Aidha, Serikali itaendelea na juhudi za kuhakikisha kiwanda cha *Triple S* kilichobinafsishwa na Kiwanda cha Nyama cha Mbeya ambacho utaratibu wa ubinafsishaji wake haukukamilika vinafanya kazi. Rejea Kiambatisho Na. 10.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya vinywaji. Tanzania ina viwanda vingi vya kuchakata maji, juisi, maziwa, mvinyo, bia na vinywaji vikali na idadi ya viwanda hivyo inaongezeka. Moja ya viwanda vipya vya maji ni kiwanda cha Kampuni cha *Dodoma Innovation & Production Ltd* kilichoko Ntyuka katika Jiji la Dodoma. Kiwanda hicho kiko katika hatua za mwisho za ujenzi na kitakuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha maji na kuajiri watu 80 kwa siku wa moja kwa moja na 120 wasiokuwa wa moja kwa moja. Pamoja na kiwanda hicho, viwanda vya vinywaji baridi vya Sayona na Lakairo vya Jijini Mwanza vilimezinduliwa mwaka 2017 na vinaendelea na uzalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina viwanda saba vya kusindika zabibu vilivyopo katika Mkoa wa Dodoma. Kati ya hivyo, viwili hutengeneza mvinyo na vitano vinatengeneza michuzi ya zabibu na kuiza kwa viwanda vya mvinyo. Kiwanda cha mvinyo cha *CETAWICO* kina uwezo wa kuzalisha tani milioni 2 hadi 3 za mvinyo kwa mwaka. Kiwanda hicho kinatoa ajira 35 za moja kwa moja na hupata malighafi kutoka kwa wakulima zaidi ya 600. Kiwanda cha *ALKO-VINTAGE Ltd* cha Jijini Dodoma kina uwezo wa kuzalisha lita



milioni 1.5 za mvinyo na kutoa ajira 50 za moja kwa moja na hupata zabibu kutoka kwa wakulima zaidi ya 500.

Mheshimiwa Spika, pamoja na viwanda hivyo viwili, viwanda vitano vilivyosalia ni vidogo na vinatengeneza michuzi ya zabibu ambayo inauzwa kwa wenye viwanda vikubwa vya mvinyo. Aidha, kiwanda cha *DOWICO* ambacho kilibinafsishwa kinakarabatiwa ili kianze uzalishaji. Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuhakikisha wakulima wa zabibu nchini wanapata soko la uhakika na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina viwanda 82 vya maziwa vyenye uwezo usiosimikwa wa kusindika jumla ya lita 757,550 kwa siku. Kwa sasa usindikaji ni lita 154,100 kwa siku, sawa na asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya vifaa vya umeme. Kufuatia Serikali ya Awamu ya Tano kutoa kipaumbele kwa viwanda vya ndani, hatua hiyo imechochea kwa kiasi kikubwa viwanda vya ndani kuongeza uwezo wa uzalishaji. Mfano, Kiwanda cha *TANELEC Limited* kina uwezo sasa wa *transformer* 14,000 kwa mwaka na kitaongeza ajira kutoka 120 hadi 300 ifikapo mwisho wa mwaka 2018. Kampuni ya *Euro* imewekeza Dola za Kimarekani 38 milioni kwa ajili ya kutengeneza vifaa mbalimbali vya umeme ikiwemo *transformer*. Kiwanda hicho kitakapokamilika kitaajiri wafanyakazi 800. Vilevile, kuna viwanda viwili vya kutengeza Luku za umeme ambavyo ni *INHEMETER* kilichowekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 2 na kiwanda kingine *Baobab Energy Systems Tanzania* kilichowekeza Dola milioni 1.7. Viwanda hivi vitakapokamilika tutaweza kuwa na mita za kutosha na kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uhamasishaji mkubwa katika uwekezaji wa sekta ya sukari, Kampuni ya *Kigoma Sugar* imeonesha nia ya kuwekeza, *Green Field Plantations* nayo inategemea kuwekeza Mkoani Kigoma, *Nkusu Theo Sugar Company* itawekeza Mkoani Ruvuma. Napenda nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba hawa wawekezaji

ambao walipewa fursa hii watakapozembea Serikali itachukua hatua mara moja, hasa Kampuni ya *Kigoma Sugar*.

Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha wenye viwanda vya sukari kuongeza uzalishaji, utaratibu wa uagizaji wa upungufu wa sukari (*gap sugar*) uliwekwa chini ya kampuni zinazozalisha sukari kwa kupeana kiwango maalum (*quota*) na siyo wafanyabiashara wengine. Kupitia utaratibu huo, makampuni manne yanayozalisha sukari yamepewa jukumu la kuagiza sukari kwa masharti kuwa hakutakuwepo na upungufu wa sukari nchini na lazima wapanue mashamba ya miwa ili ifikapo mwaka 2020, Tanzania ijitosheleze kwa sukari. Kwa kuzingatia masharti hayo, viwanda vya sukari vya Kilombero, *TPC*, *Kagera Sugar*, Mtibwa, vimeonesha nia ya kupanua uwekezaji katika mashamba ya miwa na uwezo wa usindikaji wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika vyakula, mbogamboga na matunda. Jitihada zilizokwishaanza za kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusindika matunda zinaendelea vizuri na hivyo kuwa suluhisho la uharibifu wa matunda. Kiwanda cha kusindika matunda cha *Elven Agri Company Limited* kilianzisha uzalishaji mwezi Februari 2017, kinasindika tani 4 za matunda kwa siku. Kiwanda cha *Sayona Fruits* kilichoko katika eneo la Mboga, Chalinze kimekamilisha ujenzi wa majengo na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2018. Ujenzi wa kiwanda cha kusindika nyanya cha *DABAGA* kilichoko Mkoani Iringa eneo la Ikokoto, Ilula umekamilika. Kiwanda hicho kina uwezo wa kusindika tani 1,200 kwa mwezi na kutoa ajira za moja kwa moja 100.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Mahashree Agroprocessing Tanzania Limited* imewekeza katika kiwanda cha kusindika mazao jamii ya kunde husasan mbaazi. Kiwanda hicho kinajengwa katika Kijiji cha Mtego wa Simba, Halmashauri ya Morogoro Vijijini ambapo Dola za Kimarekani milioni 220 zitawekezwa. Ujenzi huo unategemea kukamilika na kuanza uzalishaji mapema mwaka 2019 na kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kusindika tani 2,000 mpaka 6,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika chai na kahawa. Ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Chai cha *UNILEVER* kilichoko Mkoani Njombe umekamilika. Kiwanda hicho kilichojengwa kwa gharama ya *EURO* milioni 7.5, kitakapokamilika kitaweza kusindika majani ya chai tani 50 kwa siku na kuongeza uzalishaji hadi kufikia tani 150 kwa siku na kuajiri wafanyakazi 300 ikiwemo na kusaidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza kanda na kongano za viwanda. Wizara iliingia Makubaliano ya Awali (*Memorand of Understanding*) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda tarehe 08 Machi, 2018 kwa ajili ya kutekeleza Programu ijulikanayo kama *Partnership for Country Programme*. Programu hiyo inayosimamiwa na *UNIDO* inajielekeza katika ujenzi wa maendeleo endelevu na jumuishi ya viwanda na inalenga kutekeleza mipango na programu za nchi na kuleta maendeleo ya viwanda kulingana na programu za kipaumbele tutakazojiweka.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *NDC* imetenga eneo la ekari 95 kati ya ekari 230 za Eneo la Viwanda la *TAMCO* – Kibaha kwa ajili ya ujenzi wa Kongano maalum la viwanda vya nguo na mavazi. Mpango Kabambe (*Master Plan*) kwa kuendeleza eneo hilo na michoro ya eneo hilo imetayarishwa na kuingizwa katika ramani ya Mji wa Kibaha.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kukusanya takwimu za viwanda vidogo, vya kati na vikubwa itakayowezesha kuandaa Taarifa ya Mwaka ya Utafiti wa Uzalishaji Viwandani (*Annual Survey of Industrial Production*) inayotarajiwa kukamilika mwezi Juni 2018. Taarifa hizo zitatumika kufanya chambuzi mbalimbali zitakazosaidia Serikali kufanya maamuzi ya kisera na kuweka mikakati ya kuendeleza sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makuu ya sekta ya viwanda. Hivi sasa, nchi yetu inajitosheleza kwa mahitaji ya saruji tukiwa na viwanda 14. Kwa hivi sasa tunavyo viwanda

25 vya kuzalisha chuma. Hali hiyo imetuwzesha kujitosheleza kwa mahitaji ya mabati, nondo, *angle bars, hollow section*, kwa kutaja baadhi. Vilevile tuna viwanda 15 vya kuzalisha bidhaa za plastiki ikiwemo mabomba ya maji. Hali hiyo imetufanya tuwe na uwezo wa kuzalisha mabomba ya kutosha kwa mahitaji ya soko la ndani na ziada kuuza nje. Tunao uwezo wa kuzalisha vigae vyenye uwezo wa kuzalisha mita za mraba 130,000 kwa siku na imekuwa kichocheo cha kujenga nyumba nzuri na safi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia inajitosheleza kwa mahitaji ya vinywaji mbalimbali hususan maji ya chupa, soda, vileo kwa kutaja baadhi. Maendeleo katika ujenzi wa viwanda yanaonekana pia katika usindikaji wa vyakula kwa kutumia mitambo ya kisasa na ujuzi katika ufungashaji. Hali hiyo imesaidia kuongeza thamani ya mazao na kuwzesha wananchi mpaka ngazi ya vijiji kupata vyakula vyenye viwango na ubora wa hali ya juu. Tumefanikiwa kuvutia ujenzi wa viwanda viwili vya kutengeneza mita za umeme, kama nilivyoeleza awali *Europe* pamoja na *Africables* wameongeza uwezo katika kutengeneza Transfoma. Tanzania hatupaswi kuagiza transfoma kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, nimeieleza ukurasa wa 42 - 48 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, viwanda vidogo ni muhimu katika ustawi wa Taifa letu kwani vinachochea ujenzi wa uchumi jumishi. Sekta hiyo inaajiri takribani Watanzania milioni 6 kwa sasa na huchangia Pato la Taifa kwa takribani asilimia 35. Viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vimechukua zaidi ya asilimia 98 ya idadi ya viwanda nchini na wawekezaji wa viwanda katika kundi hilo ni Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nitaomba nirudie hapo, viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vimechukua zaidi ya asilimia 98 ya idadi ya viwanda nchini na wawekezaji wa viwanda katika kundi hilo ni Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanda vidogo na biashara ndogo. Wizara imekamilisha Mwongozo wa Kusimamia Maendeleo na Ujenzi wa Viwanda nchini utakaowezesha mikoa na wilaya kusimamia jukumu hilo kwa ufanisi na tija. Mwongozo uko tayari.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na TAMISEMI. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imetembelea baadhi ya mikoa ili kutathmini zoezi la utengaji wa maeneo ya uwekezaji wa viwanda na biashara ndogo nchini. Maeneo yaliyotembelewa ni Mikoa ya Kigoma, Mbeya, Singida na Tanga.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Ujasiriamali (*NEDF*). Hadi kufikia Machi 2018, mtaji wa *NEDF* umeweza kufikia shilingi bilioni 7.8. Ukuaji kwa shilingi bilioni 2.7 umetokana na kuzungusha mtaji wa shilingi bilioni 5.05 uliotolewa na Serikali tangu Mfuko ulipoanzishwa mwaka 1994. Pamoja na ongezeko la pesa hizo, tumeweza kutoa ajira 4,438 mwaka 2017/2018, kati yao wanawake ni 2,308.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uwekezaji, nimeielezea ukurasa wa 48 – 53. Ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini unahitaji ushiriki mpana na shirikishi wa sekta ya umma na binafsi. Moja ya kazi muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda ni kuhamasisha na kuvutia mitaji na wawekezaji; kuweka mazingira wezeshi na rafiki; kutangaza fursa zilizopo katika miradi na maeneo mbalimbali; kuboresha na kutangaza vivutio katika maeneo mbalimbali ya uchumi, kwa kutaja machache. Wizara kupitia *TIC* na kwa kushirikiana na Taasisi za Sekta Binafsi imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje, napenda kuchomokea kwamba imefanya kazi hii vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuratibu uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji. Wizara iliendelea kuandaa na kushiriki vikao vya pamoja vya mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa lengo la kupata maoni ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Katika mwaka 2017/2018,

mikutano miwili ya ngazi ya juu iliyohusisha Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na viongozi wakuu wa taasisi za Serikali na binafsi ilifanyika Oktoba na Januari 2018 Mjini Dodoma. Serikali na Sekta Binafsi wamekubaliana kuendelea kuwa na mikutano kama hiyo ya majadiliano kwa kuwa ina umuhimu sana katika kupata ufumbuzi wa changamoto zilizopo na kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya biashara nimeielezea ukurasa wa 53 – 67 katika Kitabu changu. Wizara ina jukumu la kujenga na kuendesha mfumo wa kibiashara unaosimamiwa kisheria, unaotabirika na wenye uwazi ili kuwezesha ufanyaji biashara kwa urahisi na tija kubwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kufungua fursa mbalimbali za biashara kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza majadiliano ya biashara ili kupanua fursa za masoko na uwekezaji, majadiliano baina ya nchi na nchi. Wizara iliratibu Mkutano wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (*JPC*) kati ya Tanzania na India; Mkutano wa Tatu wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (*JPC*) kati ya Tanzania na Misri; na Mkutano wa Pamoja kati ya Tanzania na Kenya. Aidha, Wizara ilipitia Mkataba wa Biashara na Uchumi baina ya Tanzania na Urusi na Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Tanzania na Mauritius.

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya Kikanda. Mwaka 2017/2018, Tanzania iliendelea kushiriki katika Mikutano ya Kikanda yenye lengo la kurahisisha ufanyaji biashara baina ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania imeendelea kuwa na msimamo wa kutokusaini Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya nchi za Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya. Msimamo huo umezingatia Azimio la Bunge kuishauri

Serikali kutosaini mkataba huo hadi hapo utakapokidhi maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa 29 wa Kamati ya Mawaziri wa Biashara wa *SADC*, Tanzania ilifanikiwa kutetea na kukubaliwa kuendelea kutoza ushuru sukari ya viwandani asilimia 10 na ya majumbani asilimia 25. Hivyo, sukari hiyo inayoingizwa nchini kutoka nchi za *SADC* itaendelea kutozwa ushuru kwa kipindi cha miaka mitatu (3) mpaka 2020 tutakapokuwa tunazalisha sukari ya kutosha kama nilivyoeleza awali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilishiriki Mkutano wa Nne wa Mawaziri wa Biashara wa Umoja wa Afrika ambapo Tanzania iliweza kutetea na kupendekeza maboresho kwenye vipengele vyenye kuleta unafuu kwa nchi katika Mkataba wa *Africa Continental Free Trade Area (AfCFTA)* hususan Itifaki ya Masuala ya Biashara ya Bidhaa na Biashara ya Huduma.

Mheshimiwa Spika, sekta ya masoko nimeieleza kwenye ukurasa wa 67 -77 katika Kitabu changu inahusu kutoa tozo zenye kero, ada zinazojirudia na kurahisisha majukumu ya taasisi mbalimbali. Vilevile, inahusu kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kuanzisha Vituo Maalum vya Kuuzia Mazao. Katika sehemu hiyo tunahamasisha ushindani katika ununuzi na uzaji wa mazao. Pia tunahamasisha kuimarisha biashara ya masoko mipakani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa taasisi zilizoko chini ya Wizara nimeieleza ukurasa wa 85 – 135 katika kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*). Majukumu yaliyotekelezwa na taasisi hii yameanishwa na utekelezaji wa miradi ya viwanda mama na miradi ya kielelezo chini ya utekelezaji wa Sekta ya Viwanda, aya ya 34 hadi 36 na aya ya 39 mpaka 92 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kuna Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje. Hapa

tunaelezea kuendeleza Eneo Maalum la Uwekezaji la Kurasini; uendelezaji wa Mradi wa *Bagamoyo Special Economic Zone*; na tunaelezea shughuli za Kitengo Maalum cha Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imefikia hatua nzuri katika kutekeleza mpango wa maboresho ya Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji (*One Stop Service Centre*) na mifumo mbalimbali ya taasisi. Taasisi ya *TradeMark East Africa* imeidhinisha pendekezo kuhusu msaada wa kitaalam na fedha katika kuboresha mifumo mbalimbali ya taasisi kwa kutumia TEHAMA. Pia, Mamlaka ya *EPZ* inashirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*) katika kuandaa Programu ya Usalama wa Maji (*Water Security Program*) ambayo itawahakikishia wawekezaji uwepo wa maji muda wote na katika ubora unaokubalika.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*) litashughulika na kutoa huduma za kitaalam viwandani; kuanzisha na kuhakiki Maabara ya Makaa ya Mawe na Mafuta na Gesi; na inashughulikia pia shughuli za kushauri viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (*CAMARTEC*) inashughulikia kutafiti mahitaji na kuendeleza na kutengeneza teknolojia mbalimbali, nimeielezea. Kwa kina nimeelezea kutafiti na kuendeleza usambazaji wa teknolojia kwa matumizi bora ya nishati, hiyo ni kazi ya *CAMARTEC* na kuhamasisha usambazaji wa teknolojia zinazobuniwa nchini na hiyo ni kazi ya *CAMARTEC*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (*TEMDO*) wanaboresha, kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji na utumiaji wa kibiashara wa mitambo na wamebuni na kuendeleza teknolojia jadidifu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mbolea Tanzania. Katika mwaka 2017/2018, Kampuni ya Mbolea Tanzania (*TFC*), imesimamia uingizaji na usambazaji wa mbolea za aina mbalimbali hapa nchini. Katika kipindi hicho, *TFC* imefanikiwa kusambaza mbolea tani 5,720 katika mikoa yote ya Tanzania.



Mheshimiwa Spika, Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) limejenga maeneo ya viwanda katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara na Simiyu. Pia linaimarisha uwezo wa uhawilishaji wa teknolojia na uanzishwaji wa viwanda vidogo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*), kinahamasisha kwa kuwalenga wawekezaji wa nje na uwekezaji wa ndani; kusajili miradi ya uwekezaji; kusimamia changamoto za uwekezaji; kunaratibu miradi ya uwekezaji mahiri kama nilivyoeleza hapo mwanzoni na wanaboresha utoaji wa huduma mahiri kwa kutumia *One Stop Centre* na kuwezesha usajili kwa njia ya mtandao kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuzungumza hili katika *TIC*. Katika kipindi cha Julai, 2017/2018, taasisi imeendelea na maboresho katika kuhudumia wawekezaji ili kuwasaidia kupata vibali na leseni mbalimbali wanazozihitaji kuanzisha miradi yao. Katika juhudi hizo, Kituo kimeongeza idadi ya taasisi zilizopo katika Huduma za Mahali Pamoja kwa kuweka pamoja Maafisa wa *TANESCO*, *TFDA*, *TBS* pamoja na *OSHA* wote wanapokutana *TIC*. *TIC* wanasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kuibua fursa za uwekezaji na kuwaunganisha na wafanyabiashara wakubwa (*Business Linkages*).

*Mheshimiwa Spika*, Shirika la Viwango Tanzania wanakagua ubora na bidhaa zitokazo nje kabla ya kuingia nchini (*Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards-PVoC*) ili kulinda bidhaa na viwanda vya Tanzania. Pia wanatoa leseni ya ubora kwa bidhaa mbalimbali; wanatoa mafunzo kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (*quality assurance*); wametayarisha viwango vya kitaifa katika sekta ndogo za uhandisi na usindikaji wa kufanya ugezi kwa vifaa na mashine mbalimbali na wanapima sampuli na bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili wa Biashara (*BRELA*) wanaboresha mifumo na taratibu za utoaji huduma kwa kutumia teknolojia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani wanaainisha na kufanya ukaguzi wa ghala zinazosajiliwa na zinazotarajiwa kusajiliwa nchini na wanatoa elimu ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Hakimiliki (*COSOTA*) wanaongeza makusanyo ya mirabaha; wametoa elimu na wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa sanaa kuhusiana na mambo ya haki miliki na haki shiriki; wanafanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki (*Anti-Piracy Raids*) na kushughulikia migongano ya kikesi na wanaendelea kusajili wanachama wapya na wasanii katika kuratibu kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (*TANTRADE*) wanaboresha na wanaendelea kuboresha upatikanaji wa soko la bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; wanaratibu na kudhibiti uendeshaji wa maonyesho ya kimataifa nchini; wanaendelea kuandaa mikutano ya wafanyabiashara; wanashiriki katika maonyesho ya kimataifa ndani na nje ya nchi; na kuboresha na kuimarisha mfumo wa Taifa wa Taarifa za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Vipimo wanakagua na kusimamia matumizi sahihi ya vipimo na wanakagua bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo mbalimbali ya mipakani bandarini na viwandani.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Ushindani (*TFC*) shughuli zao, wanaendelea na kudhibiti na kupambana na uingizaji wa uzalishaji wa bidhaa bandia; wanachunguza mashauri yanayohusu migongano ya kimakampuni na wanamlinda na kumuelimisha mlaji.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Ushindani wanasikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za rufaa pale inapokuwa imetoka *TFCC*.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Elimu ya Biashara wanashughulika na ujenzi wa maktaba mpya; madarasa na

kumbi za mihadhara katika Kampasi ya Dar es Salaam na wanaimarisha uwezo wa watumishi (*capacity building*) ili chuo chetu kiweze kutoa elimu ya biashara.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji kwa mwaka 2018/2019. Ujenzi wa uchumi wa viwanda unatazamwa kuwa kiini cha mageuzi yenye kuleta mafanikio na mwelekeo wa maisha bora na yenye furaha kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya ujenzi wa uchumi wa viwanda imefafanuliwa zaidi na kuwekewa mikakati katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021. Msisitizo mkuu wa maendeleo ya viwanda vinavyotumia malighafi zinazozalishwa nchini hususan mazao ya kilimo (mafuta ya kula, sukari, vyakula na vinywaji), madini na chuma na kemikali. Aidha, Serikali imeahidi kusimamia kutekeleza mipango hiyo kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 - 2020.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze vipaumbele na malengo ya sekta kwa mwaka 2018/2019. Vipaumbele kwa mwaka 2018/19 nirejee hotuba yangu ukurasa wa 138 – 139 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2018/2019, vipaumbele vya Wizara kwa kushirikiana na taasisi zake ni kutunisha mtaji wa *NEDF*; kuendeleza miradi ya kielelezo: Mchuchuma na Liganga kwa kulipia fidia, Magadi Soda Engaruka na Kiwanda cha Matairi Arusha; uendelezaji wa Eneo la Viwanda *TAMCO* Kibaha; Mradi wa kuunganisha Mtrekta ya *URSUS*; uendelezaji wa mitaa/maeneo ya viwanda vya *SIDO*; kuendeleza Kanda Kuu za Uchumi (Ruvuma, Tanga, Kigoma na Manyoni), Bagamoyo *Special Economic Zone*, Kurasini *Logistic Centre*, Kigamboni *Industrial Park*; kuendeleza utafiti kwa ajili ya *TIRDO*, *CAMARTEC* na *TEMDO*, Dodoma *Leather and Dodoma Special Economic Zone* na ujenzi wa *industrial parks*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo, Wizara itaweka msukumo wa kipekee katika kuhamasisha ujenzi wa sekta binafsi ya Kitanzania iliyo imara ili iweze kushiriki na kuchangia ipasavyo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nirudie, pamoja na vipaumbele hivyo, Wizara itaweka msukumo wa kipekee katika kuhamasisha ujenzi wa sekta binafsi ya Kitanzania iliyo imara ili iweze kushiriki na kuchangia ipasavyo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, malengo ya 2018/2019 yameandikwa kwenye ukurasa wa 139 -159 katika kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda. Katika mwaka 2018/2019, sekta ya viwanda ina malengo yafuatayo: kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji viwandani pamoja na mahitaji ya bidhaa za viwandani; kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996 – 2020 (*Sustainable Industrial Development Policy - SIDP*) na kuandaa mkakati wa utekelezaji; kujenga uwezo wa taasisi za utafiti za Wizara; kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya viwanda mama na Miradi ya Kimkakati; kuendelea na utekelezaji wa mikakati mikuu ya kuendeleza sekta za alizeti, ngozi na bidhaa za ngozi, pamba mpaka mavazi, viwanda vya dawa; na kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda vidogo. Katika mwaka 2018/2019, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo itatekeleza malengo yafuatayo: Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo na biashara ndogo nchini; kuwezesha uanzishwaji wa kongano la karanga; kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003; kuendelea kusimamia Mfuko wa *NEDF* na kutumia *SIDO* kama nyenzo ya kujenga viwanda vidogo na vya kati nchini.

Tutaitumia *SIDO* kama nyenzo ya kujenga viwanda vidogo na vya kati nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uwekezaji. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia sekta ya uwekezaji itatekeleza malengo yafuatayo: Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996; kukamilisha mapitio ya Sera, Mkakati na Sheria ya Uwekezaji; kufuatilia miradi ya uwekezaji nchini na kuratibu kwa karibu uwekezaji katika sekta maalum.

Mheshimiwa Spika, sekta ya biashara. Katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Wizara yangu tutasimamia sekta ya biashara na itatekeleza mambo yafuatayo: Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi (*Bilateral*), Kikanda (*Regional*) na Kimataifa (*Multilateral*) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini; kuhamasisha jumuiya za wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatokanayo na majadiliano ya nchi na nchi, kikanda na kikanda na kimataifa; na kukamilisha mapitio ya Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measures*.

Mheshimiwa Spika, sekta ya masoko kwa mwaka 2018/2019. Wizara kupitia sekta ya masoko itatekeleza malengo yafuatayo: Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuwaunganisha wazalishaji na masoko; kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala; kutafiti na kutafuta masoko mapya ndani na nje ya nchi hususan katika nchi za Afrika Mashariki, *DRC* Congo, China, Mashariki ya Kati, Mashariki ya Mbali, Ulaya na nchi nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya taasisi chini ya Wizara. Malengo haya nimeyaeleza ukurasa wa 151 -152. Taasisi za kisekta zitajielekeza katika kuendeleza uwekezaji katika miradi ya vielelezo na kimkakati; usimamizi wa viwango na ubora; kuendeleza biashara ya ndani na nje; utafiti katika

teknolojia na viwanda; kumtetea na kumlinda mlaji; ulinzi na kusimamia haki za wabunifu; usajili wa makampuni na leseni za biashara; kuendeleza maeneo ya uwekezaji wa viwanda; kuendeleza na kuvilinda viwanda vidogo sana hadi vikubwa nchini; kutoa elimu ya biashara; kusimamia mfumo wa kumlinda mzalishaji na muuzaji; kusimamia haki za biashara; kuhamasisha uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi na kuendeleza teknolojia za kutumika vijijini. Malengo ya kina taasisi za kisekta katika mwaka 2018/2019, yameanishwa vizuri ukurasa 151 mpaka 172 kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2018 mpaka 2019 ambayo nimeyaandika vizuri katika hotuba yangu ukurasa wa 175 - 177. Kwa mwaka 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Taasisi zake inaomba kutengewa jumla ya Sh.143,334,153,648, kati ya hizo, Sh.43,309,628,648 ni Matumizi ya Kawaida na Sh.100,024,525,000/= ni za Matumizi ya Maendeleo. Katika fedha za matumizi ya kawaida, Sh.19,193,110,000 ni za mishahara na Sh.5,069,373,000 ni za matumizi mengineyo. Aidha, katika fedha za maendeleo Sh.90,500,000,000 ni fedha za ndani na Sh.2,524,525,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, katika Fungu 44 (Viwanda) fedha zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo, fedha za ndani ni Shilingi bilioni 90.5 ambazo zimeelekezwa katika miradi mikubwa ya kielelezo; miradi ya ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; uanzishwaji wa kanda maalum za kiuchumi; uendelezaji wa eneo la viwanda la TAMCO Kibaha; kuendeleza Kongano za viwanda; kuendeleza tafiti za maendeleo viwandani; kuendeleza viwanda vidogo, biashara ndogo, ujasiriamali na kuongeza Mfuko wa NEDF.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji) imetengwa Shilingi Bilioni 7 fedha za ndani kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo katika miradi ya kuendeleza ujenzi wa maabara ya kisasa; kuboresha mfumo wa usajili wa kazi za wanachama wanaojishughulisha na kazi za

ubunifu kwa njia ya mtandao; Bodi ya Stakabadhi Maghala (*WRRB*); kuimarisha uhakiki wa vipimo na miradi mingine chini ya *ASDP II*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Maamuzi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ni msimamo makini wa Serikali yetu unaozingatia uzoefu kutoka nchi nyingine ulimwenguni zilizopata mafanikio na maendeleo kupitia viwanda. Kuthubutu kutumia fursa, kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano kutumia rasilimali kwa nidhamu ni masuala muhimu ya kuzingatiwa ili kufikia malengo. Wakati Serikali inaendelea na jitihada za kuweka mazingira rafiki na wezeshi, sekta binafsi ina jukumu la kutumia fursa zilizopo na zilizojitokeza kuanzisha viwanda na kufanya biashara. Matokeo ya jitihada zilizofanyika yameanza kuzaa matunda.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunahitaji kuendelea kuunganisha nguvu kwa dhamira njema bila kuchoka katika vita ya kujenga uchumi wa viwanda ulimwenguni kuhakikisha ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali unaendelezwa. Inawezekana endapo tukiweka nguvu ya pamoja katika kuendeleza sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa shabaha ya kumbukumbu ya *Hansard*, naomba tena niombe kitabu changu chote cha bajeti kwa mwaka 2018/2019 na marekebisho niliyotoa na nitakayoleta *addendum* yawekwe kwenye kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara, [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, naafiki.

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA  
UWEKEZAJI MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE (MB.),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWAMWAKA 2018/2019  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuweka mezani taarifa iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka 2018/2019.

**2. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge lako Tukufu kujadili utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018, vilevile kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2018/2019.

**3. Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza kwa busara na hekima na hivyo kuendelea kuifanya nchi yetu kuwa na amani, utulivu na maendeleo. Kwa namna ya pekee, nawapongeza kwa kusimamia kwa vitendo agenda ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa na imani nami na kuendelea kunipa dhamana ya kuiongoza na kuisimamia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**4. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya



Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kusimamia kwa umakini mkubwa masuala muhimu ya ushirikiano wa kisekta na ya Muungano kwa ujumla.

**5. Mheshimiwa Spika**, pia nawapongeza waheshimiwa mawaziri na naibu mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni kuongoza wizara mbalimbali. Kwa namna ya pekee, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya (Mb.), kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Namshukuru kwa ushirikiano anaonipa kama Naibu Waziri katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, nawapongeza waheshimiwa wabunge wapya waliochaguliwa kupitia chaguzi ndogo ambao ni Mheshimiwa Wakili Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.), Jimbo la Songea Mjini; Mheshimiwa Justin Joseph Monko (Mb.), Jimbo la Singida Kaskazini; Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.), Jimbo la Siha; Mheshimiwa Stephen Lemomo Kiruswa (Mb), Jimbo la Longido; na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia (Mb.), Jimbo la Kinondoni. Pia, nampongeza Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Mbunge.

**6. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imeweka msingi na mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka 2018/2019, ambayo baadhi yake yanahusu majukumu ya Wizara yangu. Pia, napenda kuungana na wenzangu kuwapongeza watoa hoja walionitangulia kuwasilisha bajeti zao na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

**7. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Ahmed Sadiq Suleiman, Mbunge wa Mvomero kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia Viwanda, Biashara na Mazingira. Pia, nampongeza Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe kwa kuchaguliwa

kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Nawapongeza waheshimiwa wabunge wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati hiyo. Ninaishukuru Kamati nzima kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa inayoendelea kutupa katika kutekeleza majukumu yetu ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itazingatia ushauri, mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Stanslaus Nyongo (Mb.), aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwa uongozi thabiti kabla ya kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini. Nampongeza kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa huo.

**8. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Ni imani yangu kuwa, mtaendeleza hekima na weledi mlionao kuisimamia na kuishauri Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

**9. Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuniombea, kunivumilia na kunipa moyo kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi.

**10. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Muleba Kaskazini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo. Nawapongeza kwa kazi na juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo. Aidha, ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yao hapa bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha kuwa maendeleo yao yanazidi kushamiri.

**11. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Prof. Elisante Ole Gabriel Laizer, Katibu Mkuu; Prof. Joseph Rwegasira Buchweishaija,

Naibu Katibu Mkuu (Biashara na Uwekezaji) na Ndugu Ludovick James Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu (Viwanda) kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba dhana ya uchumi wa viwanda inafanikiwa kwa vitendo.

**12. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru pia wahisani mbalimbali ambao wamekuwa wakishirikiana nasi katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Baadhi yao ni: Benki ya Dunia, JICA, KOICA, GIZ, Serikali ya Uswisi na taasisi za Umoja wa Mataifa (UNIDO, UNDP, UNCTAD, UNWOMEN na ILO). Taasisi nyingine ni EIF, EU, TMEA na USAID. Naupongeza uongozi wa Sekta Binafsi na taasisi zake chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Reginald Abraham Mengi, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Godfrey Simbeye. Napongeza pia uongozi wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) na watumishi wote wa TNBC chini ya uongozi wa Mhandisi Raymond Mbilinyi, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo kwa ushirikiano wanaoutoa katika juhudi za kuboresha mazingira ya biashara hapa nchini.

**13. Mheshimiwa Spika,** natoa pole kwako, waheshimiwa wabunge na familia za wafiwa kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Leonidas Gama wa Jimbo la Songea Mjini. Vilevile, napenda kutoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia ya majanga mbalimbali kama mafuriko, ajali za moto viwandani, ajali za barabarani na majanga mengine yanayofanana na hayo.

**14. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze umuhimu wa viwanda katika uchumi wa nchi yetu.

## 2.0 UMUHIMU WA VIWANDA KATIKA UCHUMI WA TAIFA

**15. Mheshimiwa Spika,** kutokana na matakwa ya wakati, leo hii ninapowasilisha Bajeti yangu ya tatu nikiwa

Waziri mwenye dhamana ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda tena kurejea tafsiri ya kiwanda. Kiwanda ni eneo ambalo malighafi huchakatwa kwa muktadha wa uongezaji wa thamani. Hivyo, shughuli yoyote, ndogo au kubwa, ya uongezaji thamani kwenye malighafi kwa lengo la kutoa bidhaa ni shughuli za kiwanda.

**16. Mheshimiwa Spika,** vigezo vya kimataifa vya kugawa makundi ya viwanda vinavyotumika mara nyingi ni ajira, mtaji na mapato. Vigezo vinavyotumika kwa Tanzania ni mtaji na ajira zinazotokana na shughuli husika za uongezaji thamani. Hivyo, kiwanda kidogo sana, kinatakiwa kuwa na mtaji wa hadi Shilingi 5,000,000 na ajira ya hadi watu wanne (4); kiwanda kidogo kinatakiwa kuwa na mtaji wa kati ya Shilingi 5,000,000 hadi milioni 200 na ajira ya watu watano (5) hadi 49; na kiwanda cha kati kinatakiwa kuwa na mtaji wa kati ya Shilingi milioni 200 hadi 800 na ajira ya watu 50 hadi 99. Kiwanda kikubwa kinatakiwa kuwa na mtaji wa zaidi ya Shilingi milioni 800 na ajira ya kuanzia watu 100 na kuendelea. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, hadi kufikia mwezi Machi 2018, nchi yetu ilikuwa na jumla ya viwanda 53,876. Kati ya hivyo, viwanda vikubwa ni 251 vya kati ni 173, vidogo ni 6,957 na vidogo sana ni 46,495. Kwa kipindi ambacho Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, chini ya uongozi mahiri wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hadi Machi 2018, viwanda vipya 3,306 vimejengwa.

**17. Mheshimiwa Spika,** tunapozungumzia uchumi wa viwanda tunamaanisha shughuli zinazolenga maendeleo ya watu na vitu wakati maendeleo ya watu yakipewa kipaumbele. Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda Sekta ya Viwanda inakuwa kiungo muhimu cha kuhamasisha maendeleo ya sekta nyingine. Sekta hizo wezeshi na tegemezi katika uchumi wa viwanda ni pamoja na kilimo; uvuvi na mifugo; misitu; na madini kwa upande wa uzalishaji malighafi za viwanda. Kwa upande mwingine, ustawi wa viwanda hutegemea miundombinu ya barabara, reli, usafiri

wa anga, nishati, mawasiliano na maji. Aidha, uchumi wa viwanda unahitaji rasilimali watu ambao ni muhimu katika mnyororo mzima kuanzia uzalishaji malighafi, uzalishaji wa bidhaa viwandani na usambazaji wa bidhaa hadi mikononi mwa mlaji.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika kujenga uchumi wa viwanda, ambao lengo lake kubwa ni kufanya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ni muhimu sana. Umuhimu wa sekta hiyo unatokana na ukweli kwamba inahitaji ujuzi na mitaji ambayo Watanzania walio wengi wanaweza kuimudu. Sekta hiyo ni shule kwani kupitia viwanda vidogo na biashara ndogo, wajasiriamali hupata ujuzi na uzoefu wa shughuli za uzalishaji na kuweza kuhitimu kuwa wawekezaji na wafanyabiashara wa kati na wakubwa. Katika jitihada za kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa msambao wa nchi nzima, ni viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vinavyoweza kujengwa na kuendeshwa kwa tija nchi nzima. Ni dhahiri kuwa Sekta hiyo ni muhimu sana katika kushiriki na kuchochea ujenzi wa uchumi jumuishi kutokana na kutegemea malighafi inayozalishwa na wakulima walio wengi na hutumia teknolojia rahisi.

**19. Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kuakisi vyema mchango wa Sekta hiyo ambao ni muhimu katika kufikia azma ya uchumi wa kati, hatuna budi kuelekeza nguvu kubwa katika kubuni mikakati ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo. Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi pamoja na kubuni mikakati mbalimbali ili kuziwezesha shughuli za ujasiriamali mdogo na wa kati kukua na kuwa wenye tija.

**20. Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu huo wa viwanda vidogo, viwanda vikubwa ni vya msingi katika kutoa chachu kwa ujenzi na uendeleo wa viwanda vidogo, vidogo sana na vya kati. Kwa upande mmoja, viwanda hivyo huzalisha bidhaa ambazo ndiyo msingi wa viwanda vingine na kuzalisha bidhaa za kati ambazo hutumiwa na viwanda

vya kati, vidogo na vidogo sana katika kuzalisha bidhaa. Kwa upande mwingine, viwanda hivyo hupokea bidhaa kutoka viwanda vidogo au malighafi kutoka kwa wazalishaji kuzalisha bidhaa nyingine. Hivyo, Wizara itafanya jitihada za kuunganisha nguvu na viwanda vikubwa kwa kuwa uwepo wa viwanda vya aina hizo zote ni muhimu ili kukamilisha mnyororo wa uzalishaji wa viwanda ambao ni endelevu na unganishi kwa sekta za uzalishaji malighafi hususan zitokanazo na kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.

**21. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa ustawi wa shughuli za viwanda unategemea kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wadau mbalimbali. Ujenzi wa viwanda unaanza kwa kutambua eneo la kujenga viwanda ambalo ubainishwaji wake na uwekaji wa miundombinu wezeshi na saidizi unahusisha mamlaka mbalimbali. Vilevile, ili kujenga Sekta ya Viwanda iliyo endelevu, suala la mazingira ni muhimu sana. Kama ilivyoelezwa awali, uendeshaji wa viwanda na sekta wezeshi na saidizi zinahitaji nguvu kazi zenye ujuzi na weledi. Kwa misingi hiyo, mafanikio ya dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ni matokeo ya ushirikiano na jitihada za Wizara zote na Serikali kwa upande mmoja na Sekta Binafsi kwa upande mwingine.

### **3.0 VIPAUMBELE NA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MALENGO YA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018**

#### **3.1 VIPAUMBELE KWA MWAKA 2017/2018**

**22. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, vipaumbele vya Wizara vilikuwa ni kuvutia wawekezaji na kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini; kufufua viwanda vilivyobinafsishwa; kuendeleza viwanda mama na miradi ya kimkakati (flagship projects) kwa kushirikisha Sekta Binafsi; kuendelea kubainisha maeneo ya viwanda katika mikoa yote na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ & SEZ) pamoja na kongano za viwanda (industrial clusters) nchini; kujenga uwezo wa taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; kuhamasisha uanzishaji na

maendeleo ya viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati; na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Utekelezaji wa mipango hiyo unalenga kuhakikisha kuwa Sekta ya Viwanda nchini inakua na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa, inazalisha bidhaa zinazotumiwa na Watanzania walio wengi na kuzalisha ajira kwa wingi.

**23. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa vipaumbele hivyo umezingatia mipango iliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/2017 – 2020/2021, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Mipango hiyo imefafanuliwa kisekta katika Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano na Mpango Kazi wa mwaka 2017/2018. Pia, Wizara imezingatia ahadi na maagizo ya viongozi wakuu wa Serikali, sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, kitaifa na kimataifa. Aidha, Wizara imeendelea kuzingatia ushauri mzuri ambao umekuwa ukitolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Viwanda Biashara na Mazingira na kamati nyingine za Bunge ambazo zimehusika katika kuishauri Wizara yetu.

### 3.2 MWENENDO WA BAJETI

#### 3.2.1 Maduhuli

**24. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilitarajia kukusanya Shilingi 20,000,000,000 kutokana na ada za leseni za biashara, uuzaji wa nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Shilingi 9,728,635,810.84 zilikuwa zimekusanywa, sawa na asilimia 48.64 ya malengo. Mwelekeo wa makusanyo hadi mwezi Juni 2018, inategemewa kufikia asilimia 65 ya lengo.

#### 3.2.2 Bajeti Iliyoidhinishwa na Kupokelewa

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilitengewa Shilingi 122,215,109,750. Kati ya fedha hizo, Fungu 44 (Viwanda) lilitengewa Shilingi 98,012,870,000

zinazojumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 24,172,493,000 na fedha za Maendeleo Shilingi 73,840,377,000. Aidha, Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji) lilitengewa Shilingi 24,202,239,750 zinazojumuisha Shilingi 17,852,239,750 fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 6,350,000,000 fedha za Maendeleo.

**26. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 9 Aprili 2018, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 47,267,945,999.91 kwa ajili ya Fungu 44 na Fungu 60, sawa na asilimia 38.68 ya Bajeti kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha hizo, Shilingi 32,641,257,816.33 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 14,626,688,183.58 ni za Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Wizara ilipokea fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 8,066,718,730.33 na Taasisi zilipokea Shilingi 24,503,739,886. Aidha, kwa upande wa fedha za Maendeleo, Wizara ilipokea Shilingi 3,026,341,089.58 na Taasisi zilipokea Shilingi 11,600,347,094.

### 3.3 UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MALENGO

#### 3.3.1 Sekta ya Viwanda

**27. Mheshimiwa Spika**, mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 5.5, ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 0.6 (*Kiambatisho Na. 1*). Kasi ya ukuaji wa Sekta ya Viwanda ilikuwa asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2016 (*Kiambatisho Na. 2*). Aidha, ajira katika Sekta ya Viwanda imeongezeka kwa asilimia 5 kutoka ajira 267,524 mwaka 2016 hadi 280,899 mwaka 2017 (*Kiambatisho Na. 3*).

#### a) Uendelezaji wa Viwanda Vilivyobinafsishwa

**28. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala - CCM (2015- 2020), Wizara yangu, pamoja na mambo mengine, inatakiwa kuhakikisha utekelezaji wa mambo makubwa matatu yafuatayo: Kwanza, ni kuhakikisha kwamba viwanda vilivyopo bila kujali umiliki wake vinazalisha kwa uwezo wa



juu uliosimikwa (maximum installed capacity); Pili, kuhakikisha kuwa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi vinafanya kazi; na Tatu, kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vipya.

**29. Mheshimiwa Spika**, kufuatia zoezi la ubinafsishaji nchini, kati ya taasisi za umma 341 zilizobinafsishwa, ni taasisi 156 zilizokuwa na sifa ya kuwa viwanda. Kufikia mwezi Mei 2017, kati ya viwanda hivyo, viwanda 62 vilikuwa vinafanya kazi vizuri; 28 vilikuwa vinafanya kazi chini ya kiwango; 56 vilikuwa havifanyi kazi kabisa na 10 vilikuwa vimeuzwa kwa mali moja moja (Asset Stripping). Kuanzia mwezi Agosti 2017 hadi Machi 2018, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina na wizara za kisekta ilifanya tena tathmini ya viwanda vilivyobinafsishwa, ili kubaini hali ya viwanda hivyo baada ya kufanya zoezi la kuhamasisha ufufuaji wake.

**30. Mheshimiwa Spika**, kutokana na uhamasishaji huo, baadhi ya wamiliki ambao viwanda vyao vilikuwa havifanyi kazi walioonesha utayari wa kuvifufua na hivyo walipewa muda maalum wa kutekeleza mipango ya ufufuaji. Mpaka Machi 2018, viwanda 18 vilikuwa vimefikia hatua mbalimbali za ufufuaji. Vipo viwanda ambavyo vimekamilisha ukarabati na kuanza uzalishaji wa majaribio; vipo viwanda ambavyo wamiliki wamewekeza mitaji mikubwa kukarabati mitambo iliyokuwepo na hata kununua mitambo mipya. Pia, vipo viwanda ambavyo wamiliki wamewekeza katika kupanua majengo yaliyopo na kujenga majengo mapya.

**31. Mheshimiwa Spika**, kati ya viwanda 56 ambavyo vilikuwa havifanyi kazi kabisa, viwanda 35 vimewekwa chini ya uangelizi wa Serikali. Katika kundi hilo, kuna viwanda ambavyo uboreshaji wake umekwama kutokana na kuwa na mashauri mahakamani. Vipo viwanda ambavyo kutokana na hali yake, havina sifa ya kuendelea kuitwa viwanda. Taratibu zinafanywa ili kuviondoa katika orodha ya viwanda. Pia, kuna viwanda ambavyo ni mali ya Serikali au taasisi zake ambavyo mamlaka husika ziko katika hatua mbalimbali za kuviendeleza. Viwanda vitatu (3) katika kundi la viwanda 56, pamoja na viwanda vingine saba (7)

vimeunganishwa katika kundi la viwanda 10 ambavyo hatua mbalimbali za kiutawala zinachukuliwa ikiwemo kutafuta wawekezaji wengine.

**32. Mheshimiwa Spika**, kwa muhtasari, baada ya zoezi la uhamasishaji, hadi mwezi Machi 2018, kati ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa, 61 vinafanya kazi vizuri; 22 vinafanya kazi chini ya kiwango; viwanda 18 vinafanyiwa maboresho na wamiliki; viwanda 35 viko chini ya uangalizi wa Serikali; viwanda 10 visivyofanya kazi vinafanyiwa tathmini kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria kulingana na mikataba ya ubinafsishwaji; na 10 ni vilivyouzwa mali moja moja na kupoteza sifa ya kuendelea na shughuli za uzalishaji.

**b) Miradi Mipya ya Viwanda**

**33. Mheshimiwa Spika**, kuanzia Julai 2017 mpaka Machi 2018, jumla ya miradi 243 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 3,667 na inayotarajiwa kuajiri watu 36,025 ilikuwa imesajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 99 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,317 na itakayoajiri watu 12,995 ilisajiliwa na TIC (*Kiambatisho Na. 4*); miradi 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 368.92 na itakayoajiri watu 4,881 ilisajiliwa na EPZA (*Kiambatisho Na. 5*); na miradi 122 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 981 na itakayoajiri watu 18,149 ilisajiliwa na BRELA (*Kiambatisho Na. 6*).

**c) Viwanda Mama na Miradi ya Kielelezo**

**i) Mradi wa Mchuchuma na Liganga**

**34. Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga, Serikali iliunda timu ya wataalam wa Serikali ikiwa na jukumu la kuchambua vivutio vilivyoombwa na mwekezaji. Vilevile, uchambuzi ulikuwa ufanyike kwa kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Madini, 2010; Sheria ya *Natural Wealth and Resources*

*Permanent Sovereignty Act, 2017; na The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms), 2017* na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na Serikali. Timu hiyo imekamiliisha taarifa ya awali ambayo inasubiri kutolewa maamuzi na mamlaka husika.

**ii) *Kiwanda cha Matairi Arusha***

**35. *Mheshimiwa Spika***, msimamo wa Serikali ni kuhakikisha Kiwanda cha Matairi Arusha kinafanya kazi. Jukumu la kuboresha na kuendesha kiwanda hicho litakuwa mikononi mwa Sekta Binafsi huku Serikali ikibaki na hisa kulingana na rasilimali zilizopo bila kuwekeza mtaji zaidi. Mpaka sasa, Kamati Maalum ya Serikali inaendelea kupitia mpango wa kiwanda hicho ili kuamua utaratibu utakaofaa katika uwekezaji kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa.

**iii) *Mradi wa Kuzalisha Magadi wa Engaruka***

**36. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia NDC na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli imekamiliisha zoezi la upimaji ardhi ya mradi pamoja na uthaminishaji wa mali za wananchi, ili kubainisha kiasi cha fidia kitakachohitajika. Michoro ya matumizi ya ardhi hiyo iko kwenye hatua ya mwisho ya kukamilishwa. Aidha, NDC inaendelea kutangaza mradi huo kwa wawekezaji mbalimbali ili kumpata mwekezaji wa kushirikiana naye kuanzia hatua ya utafiti kwa kuzingatia teknolojia bora ya kuvuna magadi hayo.

**d) *Uendelezaji wa Maeneo ya Uwekezaji***

**i) *Maeneo Maalum ya Serikali ya Uwekezaji (Government EPZ/SEZ)***

**37. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea kuhamasisha uwekezaji ndani ya maeneo yote ya EPZ na SEZ. Hadi mwezi Machi 2018, kuna jumla ya viwanda 111 katika maeneo ya EPZ na SEZ (*Kiambatisho Na. 7*). Tathmini

ya uwekezaji na matokeo yake kwa viwanda chini ya programu za EPZ na SEZ tangu Mamlaka ya EPZ kuanzishwa, imeonesha mafanikio. Hadi mwezi Machi 2018, jumla ya mtaji (cummulative) wa Dola za Kimarekani bilioni 1.86 uliwekezwa na mauzo ya bidhaa nje ya nchi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,359.94 (cummulative) yalifanyika na ajira 52,698 za moja kwa moja zimepatikana. Aidha, kwa mwaka 2017/2018 pekee, jumla ya mtaji uliowekezwa ni Dola za Kimarekani milioni 368.92, ajira zilizopatikana ni 4,881 na mauzo ya nje ni Dola za Kimarekani milioni 159.89.

***ii) Viwanda vyenye hadhi ya EPZ/SEZ nje ya Maeneo Maalum ya SEZ/EPZ (Stand Alone EPZ/SEZ)***

**38. Mheshimiwa Spika**, pamoja na maeneo ya EPZ yaliyoko chini ya umiliki na usimamizi wa Serikali, yako maeneo yenye hadhi hiyo ya EPZ yanayomilikiwa na kuendeshwa na Sekta Binafsi. Hadi sasa, kuna viwanda 72 ambavyo vinamilikiwa na kuendeshwa na Sekta Binafsi chini ya utaratibu wa EPZ (*Kiambatisho Na.8*). Viwanda hivyo vimewekeza jumla ya Dola za Kimarekani milioni 315.01 na kutoa ajira 13,930. Kwa mwaka 2017/2018 pekee, viwanda hivyo vimeweza kuuza nje bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 115.12.

**e) Maendeleo katika Sekta Ndogo za Viwanda (Industrial Sub-Sectors)**

***i) Viwanda vya Kuunganisha Magari na Mtreka - SKD***

**39. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuunganisha mtrekta aina ya *URSUS* unaendelea katika eneo la TAMCO Kibaha chini ya usimamizi wa NDC. Hadi mwezi Desemba 2017 *Semi Knocked Down* (SKD) za mtrekta 727 yamewasili nchini ikiwa ni sehemu ya mtrekta 2,400 yaliyoanishwa katika mkataba na uunganishaji unaendelea. Kati ya SKD za mtrekta yaliyowasili, 148 yameunganishwa na yapo tayari kwa mauzo. Uunganishaji wa mtrekta katika Kituo cha

TAMCO ni hatua ya muda ikisubiri shughuli hizo kuhamishiwa katika kiwanda kipya kinachojengwa katika eneo hilo la Kibaha. Pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matreka, vituo nane (8) vya kuhudumia wateja vitajengwa katika mikoa nane (8) nchi nzima. Kufuatia maelekezo ya Waziri Mkuu, matrekta hayo ni kwa ajili ya matumizi ya kilimo vijijini.

**40. Mheshimiwa Spika**, pamoja na viwanda vya kuunganisha matrekta, hivi sasa kuna kampuni zinazojishughulisha na kuunganisha magari na kutengeneza matrela hapa nchini. Kampuni ya *Superdoll Co.Ltd* ni kati ya kampuni ya muda mrefu nchini katika utengenezaji wa matrela ya magari makubwa. Vilevile, kumejitokeza kampuni nyingine za kuunganisha magari kwa kuagiza SKD na CBU (Complete Build Up) kutoka nje. Kwa mfano, kati ya mwaka 2015 hadi 2017, Kampuni ya *Jiefang Motors (T) Ltd* imeunganisha magari 803 yanayojumuisha *SKD assembled* (tipper, light cargo truck rigid trailers) 354 na CBU (tractor head truck) 449. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaandaa Sera ya Kuunganisha Magari, ili kuhamasisha uendelezaji wa sekta hiyo nchini.

#### ***ii) Viwanda vya Kuzalisha Chuma na Bidhaa za Chuma***

**41. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2018, kulikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma ikiwa ni ongezeko la viwanda vitatu (3) kwa kipindi cha mwaka mmoja. Uwezo uliosimikwa ni wa kuzalisha tani 577,600 kwa mwaka. Baadhi ya bidhaa za chuma kama vile mabati kwa sasa viwanda vyetu vinatosheleza mahitaji ya ndani. Kwa sasa, uwezo wa uzalishaji (capacity utilization) ni wastani wa asilimia 42. Hali hiyo ya uzalishaji chini ya uwezo imesababishwa na kupanda kwa bei ya malighafi kutoka nje (billets) na kuadimika kwa vyuma chakavu nchini.

**42. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha *Kiluwa Steel Ltd* kilichopo Mlandizi Mkoa wa Pwani kinaendelea na uzalishaji

ambapo mwaka 2017 kilizalisha tani 12,000. Kiwanda cha *Lodhia Steel Industry Ltd* kimeanza uzalishaji ambapo wanazalisha tani takriban 3,700 za nondo na mabomba kwa mwezi na kinaajiri wafanyakazi 231. Aidha, Kiwanda cha *Lake Steel and Allied Products Ltd* kipo katika hatua ya kumaliza usimikaji wa mashine na kinatarajia kuanza uzalishaji katikati ya mwezi Juni, 2018. Katika kuleta huduma karibu na wajenzi wa makao makuu ya nchi, Kiwanda cha ALAF kimefungua tawi lake mjini Dodoma na kilizinduliwa na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

### **iii) Viwanda vya Saruji**

**43. Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa kuna viwanda 14 vya saruji ambavyo ni *Tanzania Portland Cement Co. Ltd* (TPCC), *Mbeya Cement Co. Ltd* (MCC), *Tanga Cement Co. Ltd* (TCCL), *Dangote Industry (T) Ltd* (DIL), *Lake Cement Co. Ltd* (LCC), *Maweni Limestone Ltd* (ARM), *Kilimanjaro Cement Co. Ltd* (KCC), *Kisarawe Cement Co. Ltd* (KCCL), *Camel Cement Co. Ltd Ltd* (CCC), *Fortune Cement Co. Ltd* (FCC), *Lee Building Material Ltd* (LBM), *Changjiang Cement Co. Ltd*, *Arusha Cement Co. Ltd* na *Moshi Cement Co. Ltd*. Viwanda vyote kwa ujumla vina uwezo uliosimikwa (Installed Capacity) wa kuzalisha takriban tani milioni 10.98 kwa mwaka na uwezo unaotumika (Utilized Capacity) ni takriban tani milioni 7.4 kwa mwaka wakati mahitaji ya nchi ni takriban tani milioni 4.8.

**44. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, kiwanda kipya cha saruji cha *Kilimanjaro Cement Co. Ltd* kilichopo mkoani Tanga kilianza uzalishaji. Pamoja na hayo kuna miradi mipya ya viwanda vya saruji vyenye uwezo wa kuzalisha saruji takribani tani milioni 8 kwa mwaka vitakapokamilika. Viwanda hivyo ni *Mamba Cement Co. Ltd* (tani milioni 1.0) kitakachojengwa Mkoa wa Pwani na Mradi wa Kiwanda cha *Hengya Cement Co. Ltd* kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni saba (7,000,000) za saruji. Mradi wa Kiwanda cha *Hengya Cement*

*Co. Ltd* umehamishiwa katika eneo jipya la Mtimbwani katika Wilaya ya Mkinga kutokana na eneo la Amboni kutofaa kwa uwekezaji mkubwa kama huo.

#### ***iv) Viwanda vya Vigae (Tiles)***

**45. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina viwanda viwili (2) vikubwa vya uzalishaji wa vigae (tiles) vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mita za mraba 130,000 kwa siku. Kiwanda cha Vigae cha *Goodwill Ceramic Ltd* kilichopo Kijiji cha Mkiu Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani kimekamilika na kinaendelea na uzalishaji. Kiwanda hicho kinachozalisha mita za mraba 80,000 kwa siku, kimeajiri watu 2,200 kikihusisha ajira 700 za kudumu na vibarua 1,500. Asilimia 30 hadi 40 ya vigae vinavyozalishwa vinauzwa hapa nchini, wakati asilimia 60 hadi 70 vinauzwa nje ya nchi. Vilevile, Kiwanda cha *Twylford Ltd* kilichopo Chalinze chenye uwezo wa kuzalisha mita za mraba 50,000 za vigae kwa siku kimekamilika na kimeanza uzalishaji mwezi Novemba 2017. Kiwanda hicho kimeajiri wafanyakazi 860. Bidhaa hizo huuzwa katika soko la ndani na nje ya nchi hususan Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Zambia.

#### ***v) Viwanda vya Vioo***

**46. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina kiwanda kimoja (1) cha *Kioo Ltd* ambacho kinazalisha chupa kwa ajili ya ufungashaji wa bidhaa hususan vinywaji na dawa. Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza vioo ambapo jumla ya miradi mitatu (3) ya viwanda imesajiliwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Miradi hiyo ni *Java Glass Limited* kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 2 na kuajiri watu 38; *Zion Glass (T) Ltd* utakaowekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 3 na kuajiri watu 12; na *EA Glass Investment Limited* utakaowekeza Dola za Kimarekani milioni 1.2 na kuajiri watu 163. Miradi hiyo iko katika hatua za awali za uanzishaji wa viwanda husika.

**vi) Viwanda vya Kutengeneza Chokaa**

**47. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha *Neelkanth Lime Ltd* kilichopo katika eneo la Amboni Mkoa wa Tanga kinazalisha tani 15,000 za chokaa kwa mwezi na kuajiri wafanyakazi 430. Kiwanda kipo katika hatua za awali za upanuzi ambapo Dola za Kimarekani milioni 18.4 zinatarajiwa kutumika. Upanuzi huo unaotarajiwa kukamilika mwaka 2019, utaongeza uwezo wa uzalishaji hadi tani 35,000 kwa mwezi na kuongeza ajira za moja kwa moja 1,500 na zisizo za moja kwa moja 2,500. Soko kuu la bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho ni nchi za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Zambia pamoja na migodi ya *Barrick Gold Mines Ltd* ya hapa nchini.

**vii) Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba**

**48. Mheshimiwa Spika**, hivi sasa nchi ina jumla ya viwanda 15 vya kuzalisha dawa na vifaa tiba. Katika kuendeleza viwanda vya dawa na vifaa tiba, Bohari Kuu ya Dawa (MSD) imetoa kipaumbele na kuingia mikataba ya kununua dawa kutoka viwanda vya ndani vinavyozalisha dawa zinazokidhi viwango. Viwanda hivyo vinazalisha asilimia 12 tu ya mahitaji ya dawa nchini. Ili kutatua changamoto hiyo, juhudi za kuhamasisha uwekezaji zimeendelea kufanyika ambapo Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilifanya mkutano na wadau tarehe 4 Aprili 2018, ambapo wawekezaji 38 walionesha nia ya kuwekeza katika Sekta ya Dawa na Vifaa Tiba. Baadhi ya wawekezaji hao ni *Kairuki Pharmaceutical Industry Ltd*, *SUMA JKT* watakaozalisha *Intravenous Infusion*, *Biotech Ltd* na *Novabi Ltd* watakaozalisha dawa na chanjo za mifugo (vaccines, oral solid and liquids). Wizara inaendelea kufuatilia wawekezaji waliojitokeza.

**49. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kuandaa Mkakati wa Taifa wa Sekta ya Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba. Mkakati huo



unafadhiliwa na Shirika la UNDP kupitia Mradi wa *Access of Medicine and Delivery*. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeshiriki kuandaa Taratibu za Uzalishaji Bora wa Dawa katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Community Good Manufacturing Practice-EACGMP Roadmap), ili kuhakikisha kuwa viwango stahiki vinazingatiwa.

**50. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kutengeneza vifaa tiba vitokanavyo na pamba (medical textile) katika Mkoa wa Simiyu unaojengwa na NHIF, upo katika hatua ya kufungua kampuni itakayoendesha mradi huo. Aidha, hatua za awali za kuanzisha kiwanda cha kuzalisha dawa cha *Zinga Pharmaceutical Ltd*, Bagamoyo zimefanyika ikiwemo kufanya upembuzi yakinifu, kuandaa michoro pamoja na kuainisha teknolojia itakayotumika. Aidha, katika uendelezaji wa viwanda vya kemikali nchini, kiwanda kikubwa cha kuzalisha kemikali aina ya *Chlorine* kwa ajili ya kusafisha maji kiliwekewa jiwe la msingi tarehe 24 Aprili 2018. Mradi huo utakaojengwa Mlandizi Mkoa wa Pwani utagarimu Shilingi bilioni 246 na utatoa ajira 700 za moja kwa moja kitakapoanza uzalishaji na wakati wa ujenzi utajiri watu 300. Malighafi ya Kiwanda hicho ni chumvi ghafi kiasi cha tani 2,500 kwa mwezi.

**viii) Viwanda vya Nguo na Mavazi**

**51. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina viwanda 11 vya nguo na mavazi vinavyofanya kazi. Viwanda hivyo vinatumia wastani wa asilimia 50 ya uwezo uliosimikwa. Hali hiyo imetokana na ushindani usio wa haki kutokana na nguo zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na baadhi ya viwanda kuendelea kutumia teknolojia zilizopitwa na wakati. Aidha, kuzalisha chini ya kiwango kumesababisha matumizi madogo ya pamba inayozalishwa nchini ambayo ni asilimia 30 tu na hivyo asilimia 70 inayobaki huuzwa nje ya nchi ikiwa ghafi. Serikali inaendelea kuhamasisha uendelezaji wa Sekta ya Pamba mpaka mavazi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha sekta inaendeshwa kwa haki na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

**52. Mheshimiwa Spika**, katika kuhamasisha uwekezaji nchini, Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (Tanzania Social Security Association-TSSA) linashiriki katika juhudi za kuwekeza katika viwanda vya kuchambua pamba na kuzalisha nguo. Shirikisho hilo lina mpango wa kuwekeza katika vinu 10 vya kuchambulia pamba ambapo uchambuzi kwa vinu vitatu (3) vya awali umekamilika. Uchambuzi unaonesha kuwa vinu vya Ngasamo, Nyambiti na Kasamwa ni miradi itakayoanza kutekelezwa. Aidha, Shirikisho hilo limekamilisha maandalizi yote muhimu kwa ajili ya kuwekeza katika Kiwanda cha *Morogoro Canvas Mill Ltd* ambapo ukarabati unatarajiwa kuanza mwezi Mei 2018, na uzalishaji kuanza mwezi Juni 2018. Vilevile, Shirikisho limepokea maandiko ya miradi ya viwanda vya *MWATEX* na *URAFIKI* kwa ajili ya kuipitia kwa lengo la kuwekeza.

#### **ix) Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi**

**53. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina jumla ya viwanda sita (6) vya kusindika ngozi vinavyofanya kazi. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kusindika futi za mraba 71,520,000 za ngozi kwa mwaka. Viwanda hivyo ni *Lake Trading Co. Ltd* kilichopo Kibaha, *Himo Tanners and Planters Ltd* na *Moshi Leather Industries Ltd* (Moshi), *SAK International Ltd* na *Meru Tannery Ltd.* (Salex) (Arusha) na *ACE Leather (T) Ltd* (Morogoro) (*Kiambatisho Na. 9*).

**54. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza wapo katika hatua za uboreshaji wa majengo ya kiwanda na ukarabati na mfumo wa umeme kwa lengo la kuboresha Kiwanda cha Kutengeneza Viatu cha Karanga (Karanga Leather Industries Co. Limited). Upanuzi wa kiwanda hicho utaongeza uwezo wa uzalishaji kutoka jozi 150 hadi 400 za viatu kwa siku. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni atakayekiuzia kiwanda mitambo mipya kwa ajili ya upanuzi amepatikana na taratibu za manunuzi zinaendelea.

**55. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kiwanda cha Viatu cha Karanga unahusisha pia ujenzi wa kiwanda kipya

kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha jozi 4,000 za viatu kwa siku pamoja bidhaa nyingine zinazotokana na ngozi. Mradi huo mpya umetengewa ekari 20 na kupewa Hati Miliki tofauti na kiwanda cha zamani. Tafiti mbalimbali zikiwemo *Geotechnical & Topographical Surveys, Environmental Impact and Social Assessment - EIA* zimefanyika na michoro ya majengo imeandaliwa. Aidha, taratibu za ununuzi wa mitambo zimeanza na ujenzi wa majengo unategemea kuanza katika robo ya kwanza ya mwaka 2018/2019.

**56. Mheshimiwa Spika**, juhudi za kuendeleza viwanda vya ngozi zimewezesha kiwanda cha viatu cha Bora kilichoanza uzalishaji mwanzoni mwa mwaka 2017 kuendelea kuzalisha viatu vya ngozi, ambapo kwa sasa kinazalisha jozi 1,000 za viatu kwa siku. Vilevile, Kiwanda cha *Woisso Shoes Company Ltd* kimeagiza mashine za kutengeneza soli za viatu zenye uwezo wa kuzalisha jozi 100 hadi 300 kwa siku. Juhudi hizo za kufufua na kupanua wigo wa bidhaa zinategemewa kuongeza uzalishaji wa viatu na bidhaa za ngozi. Mkakati huo wa kuzalisha zaidi kutumia viwanda vya ndani utaongeza makusanyo ya kodi, kuokoa matumizi ya fedha za kigeni na kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje. Kiwanda cha Mwanza *Tennaries Ltd* kilichokuwa kimebinafsishwa kimewekwa chini ya uangalizi wa Serikali na Mthamini wa Serikali amekamilisha tathmini kama hatua ya kuelekea kutangazwa, ili kupata mwekezaji mwingine.

**57. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Biashara na Uwekezaji kati ya Afrika na India (Supporting Indian Trade and Investment for Africa - SITA) iliwezesha wadau wa ngozi kukutana na wawekezaji kutoka India na Italia mwezi Desemba 2017, Jijini Dar es Salaam. Matokeo ya mkutano huo ni kwamba Kiwanda cha Viatu cha Bora kilipata ushauri wa kitaalam wa namna ya kuzalisha bidhaa za ngozi zenye ubora wa kimataifa. Pia, baadhi ya wataalam wao wamewezeshwa kupata mafunzo nchini Ethiopia.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Maonesho ya DTIF, Wizara ilitenga siku na banda maalum la maonesho ya viatu na bidhaa za ngozi. Lengo lilikuwa kuzitangaza bidhaa hizo kwa umma na kuhamasisha matumizi ya bidhaa za Tanzania. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za TANTRADE, TBS, DIT, VETA, SIDO, BRELA na OSHA walitoa mafunzo kwa watengenezaji 20 wa viatu na bidhaa za ngozi kuhusu elimu ya urasimishaji wa biashara, misingi ya ujasiriamali na utunzaji wa kumbukumbu; mbinu mbalimbali za kuingia kwenye masoko na uzalishaji kwa kulenga masoko.

**x) Viwanda vya Kusindika Nyama**

**59. Mheshimiwa Spika**, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya mifugo vimeendelea kuongezeka ambapo tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, jumla ya viwanda 7 vimejengwa katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Pwani na Shinyanga. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuchakata ng'ombe 2,260 na mbuzi na kondoo 9,200 kwa siku. Viwanda hivyo vitakapokamilika na kuanza uzalishaji vitaifanya Tanzania kuwa na jumla ya viwanda 25 vyenye uwezo wa kuchakata ng'ombe 3,800, mbuzi na kondoo 10,090, nguruwe 300 na kuku 44,000 kwa siku (*Kiambatisho Na. 10*).

**60. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha Nyama cha *Nguru Hills Ranch Ltd* kilichopo Wilaya ya Mvomero Mkoa wa Morogoro ambacho nilitoa taarifa zake katika Hotuba yangu ya mwaka 2017/2018, kipo katika hatua za awali za ujenzi. Kazi ya kusimika mitambo imeanza kwa ushirikiano na LAPF ambao wameingia ubia na kukubali kuwekeza Shilingi bilioni 3.89. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchakata ng'ombe 300 na mbuzi 2,000 kwa siku na kutoa ajira zisizopungua 500. Aidha, Kiwanda kitajihusisha na mnyororo wa thamani kwa kushirikiana na wafugaji wadogo wadogo, kurutubisha mifugo na kusindika nyama.

**61. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha *Triple Skilichopo* katika mkoa wa Shinyanga ambacho kilikuwa

kimebinafisishwa na sasa kimewekwa chini ya uangalizi wa Serikali. Mthamini wa Serikali amekamilisha tathmini yake ikiwa ni hatua ya mwisho kabla ya kukitangaza kwa mwekezaji mwingine. Aidha, Kiwanda cha Nyama cha Mbeya ambacho utaratibu wa ubinafsishaji wake haukukamilika hapo awali, kinafanyiwa tathmini upya ili nacho kitangazwe kwa lengo la kutafuta mwekezaji mahiri.

***i) Viwanda vya Vinywaji***

**62. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Maji katika eneo la Ntyuka kilichopo katika Jiji la Dodoma kinachomilikiwa na Kampuni ya *Dodoma Innovation & Production Ltd* kipo katika hatua za mwisho za ujenzi. Kiwanda hicho kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha chupa za maji 150,000 kwa siku, kinategemea kutoa ajira 80 za moja kwa moja na 120 zisizo za moja kwa moja na kinategemea kuanza uzalishaji mwezi Mei 2018. Pamoja na kiwanda hicho, viwanda vya vinywaji baridi vya Sayona na Lakairo vya jijini Mwanza vilizinduliwa mwaka 2017 na vinaendelea na uzalishaji.

**63. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina viwanda saba (7) vya kusindika zabibu vilivyopo katika Mkoa wa Dodoma. Kati ya hivyo, viwili (2) hutengeneza mvinyo na vitano (5) vinatengeneza michuzi ya zabibu na kuiuza kwa viwanda vya mvinyo. Kiwanda cha Mvinyo cha CETAWICO Ltd kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 2 hadi 3 za mvinyo kwa mwaka. Kiwanda hicho kinatoa ajira 35 za moja kwa moja na hupata malighafi kutoka kwa wakulima zaidi ya 600. Kiwanda cha *ALKO-VINTAGE Ltd* cha jijini Dodoma kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 1.5 za mvinyo na kutoa ajira 50 za moja kwa moja na hupata zabibu kutoka kwa wakulima zaidi ya 500. Pamoja na viwanda hivyo viwili (2), viwanda vitano (5) vilivyosalia ni vidogo na vinatengeneza michuzi ya zabibu ambayo inauzwa kwa wenye viwanda vikubwa vya mvinyo. Viwanda hivyo ni muhimu katika kukamilisha mnyororo wa thamani wa zao la zabibu ambalo ni dhahabu ya Mkoa wa Dodoma. Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, ili kuhakikisha wakulima wa

zabibu nchini wanapata soko la uhakika na hivyo kuwaongezea kipato.

**64. Mheshimiwa Spika**, mmiliki wa Kiwanda cha kutengeneza mvinyo cha DOWICO cha mkoani Dodoma kilichobinafashwa ameanza kukifanyia ukarabati. Ukarabati huo unategemea kukamilika mwezi Desemba, 2018 na kukiwezesha kuanza uzalishaji. Kukamilika kwa ukarabati huo utaongeza fursa kwa wakulima kupata soko la zabibu zao. Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuhakikisha wakulima wa zabibu nchini wanapata soko la uhakika na kuongeza kipato.

**65. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina viwanda 82 vya maziwa vyenye uwezo uliosimikwa wa kusindika jumla ya lita 757,550 kwa siku. Kati ya hivyo, viwanda sita (6) havifanyi kazi. Viwanda vinavyofanya kazi vinasindika jumla ya lita 154,100 kwa siku, sawa na asilimia 20 ya uwezo uliosimikwa (*Kiambatisho Na. 11*). Uzalishaji wa chini ya uwezo uliosimikwa unatokana na kiasi kidogo cha maziwa kinachozalishwa na wafugaji. Kampuni ya *Watercom Ltd* yenye Kiwanda cha Kusindika Maziwa kwa teknolojia ya *Ultra-Heat Treatment* (UHT) kilichopo Kigamboni, Mkoa wa Dar-es-Salaam kimeanza uzalishaji mwezi Novemba 2017. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 67.5 za maziwa kwa mwaka ambapo kwa sasa kinazalisha lita milioni 3 kwa mwaka na kuajiri wafanyakazi 500. Aidha, mitambo ya kuzalisha juisi na soda imesimikwa na kiwanda kimeanza uzalishaji.

**66. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha Maziwa cha Tanga (Tanga Fresh Ltd) chenye uwezo wa kusindika lita 50,000 kwa siku na kutoa ajira za moja kwa moja 150 kinafanya upanuzi ili kuongeza uzalishaji. Upanuzi huo utakaogharimu Shilingi bilioni 12 unategemea kuongeza uwezo uliosimikwa kutoka lita 50,000 za sasa hadi lita 120,000 kwa siku. Upanuzi huo ambao uko katika hatua ya majaribio ya mashine utawezesha kuongezeka kwa ajira za moja kwa moja kutoka 150 za sasa hadi 200 wakati ikitegemewa kuongezeka mara

mbili kwa wafugaji wanaokiuza maziwa kutoka 6,000 kwa sasa.

**ii) Viwanda vya Vifaa vya Umeme**

**67. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha *TANELEC Limited* kinachozalisha transfoma za umeme kimeongeza uwezo wa kuzalisha kutoka transfoma 10,000 hadi 14,000 kwa mwaka. Upanuzi huo umegharimu Dola za Kimarekani milioni 1.4 na kimeweza kuongeza ajira kutoka wafanyakazi 120 hadi 180 na inatarajia kuongeza ajira hadi kufikia 300 ifikapo mwisho wa mwaka 2018. Viwanda hivyo ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwani vinatekeleza azma ya Serikali ya kufikisha umeme nchi nzima na hivyo kuchochea ujenzi wa viwanda nchi nzima. Kampuni ya *Europe Inc Industries Ltd* iliyoko Dar es Salaam nayo imewekeza Dola za Kimarekani milioni 38 kwa ajili ya kutengeneza vifaa mbalimbali vya umeme vikiwemo transfoma. Kiwanda hicho kitakapokamilika kitaajiri wafanyakazi takriban 800.

**68. Mheshimiwa Spika,** kama inavyojulikana, Tanzania imekuwa ikitumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya kuagiza mita za LUKU kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na viwandani. Changamoto hiyo imepata ufumbuzi baada ya wawekezaji *INHEMETER (T) Ltd* kuwekeza nchini. Kiwanda hicho kimewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani 2,000,000 na kinatarajiwa kuzalisha mita 1,000,000 kwa mwaka. Kiwanda cha *Baobab Energy Systems Tanzania Ltd* (BEST) kimewekeza Dola za Kimarekani 1,700,000 kinachotarajiwa kuzalisha mita za LUKU 500,000 kwa mwaka na inatarajiwa kuuzwa katika soko la ndani na nje ya nchi. Jumla ya ajira 200 zinataraajiwa kupatikana katika viwanda hivyo viwili (2). Viwanda hivyo ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwani vitawezesha upatikanaji wa mita za kutosha ambazo zilikuwa zinaagizwa na TANESCO kutoka nje. Aidha, uzalishaji huo utatosheleza mahitaji ambayo ni wastani wa mita 483,000 kwa ajili ya uunganishaji mpya unaofanywa na TANESCO na Wakala wa Nishati Vijiji. Upatikanaji wa mita za umeme nchini utawezesha utekelezaji wa azma ya Serikali

ya kufikisha umeme nchi nzima na hivyo kuchochea ujenzi wa viwanda nchini.

**iii) Viwanda vya Mafuta ya Kula**

**69. Mheshimiwa Spika**, mafuta ya kula ni moja ya bidhaa zinazoagizwa kwa wingi kutoka nje ya nchi ambapo huigharimu nchi fedha nyingi za kigeni. Takwimu za mwaka 2013 zinaonesha kuwa uagizaji mafuta ya kula uligharimu Dola za Kimarekani bilioni 44.83, ikiwa ni namba mbili baada ya mafuta ya petroli. Kwa sasa kuna viwanda 21 vya kati na vikubwa na vidogo vipatavyo 750 vyenye uwezo wa uzalishaji wa tani 210,000, kati ya hizo alizeti ni tani 180,000. Mahitaji ya mafuta ya kula ni tani 700,000, hivyo uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula unatosheleza kwa asilimia 30 tu wakati asilimia 70 ikiagizwa kutoka nje. Kwa umuhimu huo, nchi haina chaguo jingine zaidi ya kutoa msukumo wa kipekee wa kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta na kufanya usindikaji kwa kutumia viwanda vya ndani na kutumia kwa teknolojia ya kisasa. Jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika, ili kupata suluhu ya kudumu kuhusu uzalishaji wa mafuta ya kula nchini. Mkakati wa Kuendeleza Mafuta ya Alizeti umeandaliwa ili kuelekeza hatua za kuendeleza zao la alizeti nchini.

**70. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na asasi ya *Global Community Tanzania* imewezesha kukutanisha wadau wa Sekta ya Mafuta ya Kula wapatao 300 na wanunuzi wakubwa wa hapa nchini. Mikutano hiyo ya ana kwa ana ya biashara (*Business to Business –B2B*) iliyofanyika sambamba na Maonesho ya 41 ya DTIF. Wadau walipata fursa ya kupata maelezo kuhusu Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Alizeti pamoja na matarajio ya Serikali kuona Sekta ya Alizeti inakua na kulinufaisha Taifa.

**71. Mheshimiwa Spika**, kutokana na jitihada za kuhamasisha ujenzi na upanuzi wa viwanda, usindikaji wa mbegu za mafuta umeendelea kuongezeka. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Kiwanda cha Kusindika



Mafuta cha *Mount Meru Millers Ltd* kilichopo mkoani Singida. Kiwanda hicho kina uwezo wa kusindika mbegu za alizeti tani 300,000 kwa mwaka na kuzalisha mafuta tani 90,000 hadi 150,000 kwa mwaka kitakapofikia uwezo wake wa juu wa uzalishaji na kuongeza ajira za moja kwa moja kufikia 300 na zisizo moja kwa moja 900.

#### ***iv) Viwanda vya Sukari***

**72. *Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya sukari nchini ni takriban tani 630,000 kwa mwaka. Kati ya hizo, tani 485,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na tani 145,000 ni kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Sukari kwa matumizi ya viwandani haizalishwi hapa nchini. Uwezo wa uzalishaji wa ndani kwa sasa ni wastani wa tani 320,000 kwa mwaka. Pengo la mahitaji ya takriban tani 165,000 za sukari ya kawaida na tani 145,000 za viwandani huzibwa kwa kuagizwa kutoka nje.

**73. *Mheshimiwa Spika***, katika msimu wa 2017/2018, hadi kufikia tarehe 20 Aprili, 2018 tani 303,899 za sukari zilikuwa zimezalishwa, wakati matarajio yalikuwa kuzalisha tani 314,000. Lengo halikufikiwa kutokana hali ya ukame mkubwa uliozikumba nchi za ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika. Kwa kutambua ongezeko la mahitaji ya sukari lisiloendana na uzalishaji sukari nchini, Serikali inahamasisha uwekezaji katika miradi mipya na upanuzi ya uzalishaji miwa na sukari kwa viwanda vikubwa na vidogo vilivyopo nchini, ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje ya nchi.

**74. *Mheshimiwa Spika***, kufuatia uhamasishaji huo miradi mipya mikubwa mitatu (3) ya kilimo cha miwa na uzalishaji sukari imeanza. Miradi hiyo ni:- Mradi wa Kilimo cha Miwa na Uzalishaji wa Sukari Mbigiri uliopo Dakawa katika Mkoa wa Morogoro; Mradi wa Kilimo cha Miwa na Uzalishaji Sukari Mkulazi ulio katika Wilaya ya Morogoro Vijijini; na Mradi wa Kilimo cha Miwa na Uzalishaji wa Sukari Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Miradi hiyo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kampuni ya *Morogoro Sugar Co. Ltd* inaendelea

na taratibu za uhaulishaji wa ardhi ngazi ya wilaya. Kiwanda cha Sukari cha Mbigiri kinatarajia kuzalisha tani 48,000 za sukari kwa mwaka. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2022. Mradi wa Sukari wa Mkulazi unategemea kuzalisha tani 200,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2025; na Mradi wa Sukari Bagamoyo unatarajiwa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka ifikapo 2020.

**75. Mheshimiwa Spika**, katika Mradi wa *Bagamoyo Sugar Co. Ltd*, kampuni imekamilisha upembuzi wa kina mwezi Desemba 2017. Tayari Kampuni hiyo imeanzisha kitalu cha mbegu za miwa (seedcane nursery) chenye ukubwa wa ekari 20 katika Kijiji cha Nambari Nne wilayani Bagamoyo. Hii ni sehemu ya matayarisho ya kuanzisha shamba kuu la mradi huo linalotegemewa kuanza mwezi Juni 2019. Ujenzi wa Kiwanda umeanza na unatarajia kukamilika na kuanza uzalishaji katika msimu wa 2019/2020. Vilevile, makampuni mengine yanayojishughulisha na uzalishaji wa sukari ni pamoja na *Kigoma Sugar Co. Ltd* na *Green Field Plantations Co. Ltd* ya Kigoma na *Nkusu Theo Sugar Company Ltd* ya Ruvuma. Katika Mkoa wa Ruvuma, kampuni ya *Nkusu Theo Sugar Company Ltd* imetengewa hekta 40,000 na inaendelea na mchakato wa kuhaulisha ardhi katika vijiji husika kwa ajili ya kilimo cha miwa. Kwa miradi iliyopo katika Mkoa wa Kigoma, Serikali inapitia upya miradi hiyo, ili kuona namna bora ya uwekezaji.

**76. Mheshimiwa Spika**, ili kuhamasisha wenye viwanda vya sukari kuongeza uzalishaji, utaratibu wa uagizaji wa pengo la mahitaji ya sukari (gap sugar) uliwekwa chini ya kampuni zinazozalisha sukari kwa kupeana kiwango maalum (quota) na siyo wafanyabiashara wengine. Kupitia utaratibu huo, makampuni manne (4) yanayozalisha sukari yamepewa jukumu la kuagiza sukari kwa masharti kuwa hakutakuwepo na upungufu wa sukari nchini na lazima wapanue mashamba ya miwa, ili ifikapo mwaka 2020, Tanzania ijitosheleze kwa sukari.

**77. Mheshimiwa Spika**, kutokana na uamuzi huo wa Serikali, Kampuni ya *Kilombero Sugar Ltd* imeonesha nia ya

kuwekeza kiasi cha Shilingi bilioni 500 kupanua uzalishaji. Kampuni hiyo itaboresha mifumo ya kilimo cha umwagiliaji kwenye hekta 1,500 na kupanua mashamba ya miwa ili kuongeza mavuno kwa hekta. Pia, itatoa mbegu bora na huduma za ugani kwa wakulima wa miwa wapatao 8,000, ili waongeze uzalishaji wa miwa. Ongezeko la uzalishaji wa miwa litaendana na upanuzi wa usindikaji miwa kutoka tani 270 za miwa kwa saa (Tons Cane per Hour -TCH) kwa sasa hadi tani 380 ifikapo Juni 2021.

**78. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha Sukari cha TPC nacho kinafanya upanuzi wa uwezo wa usindikaji wa miwa kutoka tani 190 za miwa kwa saa hadi kufikia tani 220. Vilevile, Kiwanda kitaboresha miundombinu ya umwagiliaji, ili kuongeza mavuno ya miwa na uzalishaji wa sukari. Katika Kiwanda hicho, ongezeko la uzalishaji wa sukari umejikita zaidi kwenye mavuno ya miwa na usindikaji miwa (vertical expansion).

**79. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha Sukari cha Kagera kinaendelea kufanya upanuzi wa kiwanda na kilimo cha miwa. Ufungaji wa miundombinu ya umwagiliaji ya kisasa ya *center pivot* unaendelea sambamba na kuongezwa hekta 3,800 za miwa kwa awamu hii na hekta 4,000 kuanzia mwaka 2020. Pia, Kiwanda kinafunga mitambo ambayo itaongeza uwezo wa usindikaji wa sukari kutoka tani 180 za miwa kwa saa awamu ya sasa hadi tani 220 mwaka 2022.

**80. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa kinafanya upanuzi wa kilimo cha miwa na pia kuweka miundombinu mikubwa ya kisasa ya umwagiliaji. Vimejengwa vituo vikubwa vya kusukuma maji (pump stations) kwa ajili ya umwagiliaji mashambani na usambazaji mabomba makubwa chini ya ardhi umefanywa. Uwekezaji katika mitambo ya kisasa ya umwagiliaji maji mashambani (Center Pivot Irrigation System) unaohusisha hekta 5,000 kwa awamu ya kwanza unaendelea. Ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa kuvuta umeme wa 33KV kutoka Morogoro hadi Mtibwa na kuusambaza eneo lote la mradi, ili kuwezesha umwagiliaji umefanyika.

**81. Mheshimiwa Spika**, uwekezaji katika upanuzi wa mashamba, miundombinu ya umwagiliaji na mitambo ya usindikaji miwa unaoendelea utawezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa sukari ya matumizi ya kawaida kutoka tani 320,000 hadi kufikia tani 482,000 kwa mwaka katika msimu wa 2021/2022. Serikali inaendelea kujadiliana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuweka mazingira wezeshi, hususan ushuru wa forodha stahiki utakaochochea uzalishaji sukari kwa matumizi ya viwandani hapa nchini.

**v) Viwanda vya Kusindika Vyakula, Mbogamboga na Matunda**

**82. Mheshimiwa Spika**, jitihada zilizokwishaanza za kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kusindika matunda zinaendelea vizuri na hivyo kuwa suluhisho la uharibifu wa matunda. Kiwanda cha kusindika matunda cha *Elven AgriCo. Limited* kilichoanza uzalishaji mwezi Februari 2017, kinasindika tani 4 za matunda aina ya maembe, papai, ndizi na mananasi kwa siku. Aidha, asilimia 80 ya bidhaa inazozalishwa na kiwanda hicho huuzwa katika nchi za Botswana, Italia, Ufaransa, Uingereza na Zambia na asilimia 20 huuzwa katika soko la ndani. Aidha, Kiwanda kimefanya juhudi ya kutumia mabaki yanayotokana na uzalishaji kutengeneza nishati ya umeme na mbolea hivyo asilimia 50 ya nishati hutokana na mabaki matunda. Kiwanda cha *Sayona Fruits Limited* kilichopo katika eneo la Mboga, Chalinze kimekamilisha ujenzi wa majengo na uzalishaji wa majaribio unaendelea na uzalishaji wa kibiashara unatarajiwa kuanza Julai 2018.

**83. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa kiwanda cha kusindika nyanya cha DABAGA kilichopo mkoani Iringa eneo la Ikokoto Ilula umekamilika. Kiwanda hicho kimewekeza mtaji wa Shilingi bilioni 5 na kina uwezo wa kusindika tani 1,200 kwa mwezi na kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 100. Kukamilika kwa kiwanda hicho kutatoa fursa kwa wakulima kupata soko la uhakika la mazao ya nyanya, piilipili,

tangawizi, vitunguu saumu, karoti, maembe, nanasi na mazao mengine ya mbogamboga. Uzalishaji unategemewa kuanza mwezi Mei 2018.

**84. Mheshimiwa Spika**, Serikali imehamasisha uwekezaji katika usindikaji wa nafaka na kufanikiwa kumpata mwekezaji *Mahashree Agroprocessing Tanzania Limited* anayewekeza katika kiwanda cha kufungasha mazao jamii ya kunde husasan mbaazi. Kiwanda hicho kinajengwa katika Kijiji cha Mtego wa Simba, Halmashauri ya Morogoro Vijijini ambapo Dola za Kimarekani milioni 220 zitawekezwa. Ujenzi huo unategemea kukamilika na kuanza uzalishaji mapema mwaka 2019. Kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kusindika tani 2000 hadi 6,000 kwa mwezi. Kiwanda hicho kitakuwa mkombozi kwa mkulima kwani mbali na kununua mazao yanayozalishwa na wakulima kitapunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na hivyo kuwaongezea kipato. Aidha, mwekezaji *Murzah Wilmar Rice Millers* ameanza ujenzi wa kiwanda cha kisasa kitakacho sindika mpunga katika eneo la viwanda la Kihonda mkoani Morogoro.

**vi) Viwanda vya Kusindika Chai**

**85. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Chai cha *UNILEVER Ltd* kilichopo katika Mkoa wa Njombe kilichojengwa kwa gharama ya EURO milioni 7.5 umekamilika ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya barabara na umeme. Hatua inayoendelea ni usimikaji wa mitambo. Wakulima wa chai karibu na eneo hilo wameendelea kuhamasishwa kuendeleza na kilimo cha chai ili kurahisisha upatikanaji wa malighafi. Kiwanda kitakapoanza uzalishaji kitakuwa na uwezo wa kusindika majani ya chai tani 50 kwa siku na kuongeza uzalishaji hadi kufikia tani 150 kwa siku na kuajiri wafanyakazi wapatao 300.

**vii) Viwanda vya Kusindika Kahawa**

**86. Mheshimiwa Spika**, zao la kahawa ni moja ya chanzo kikuu cha fedha za kigeni hapa nchini. Ili kuhakikisha

kuwa nchi inaendelea kupata fedha za kigeni, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika kahawa. Kiwanda cha *GDM Co. Ltd* kilichopo eneo la Mlowo Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe, kilianza kujengwa mwanzoni mwa mwaka 2017 kwa mtaji wa Shilingi bilioni 5.2. Kiwanda hicho kitakacho jishughulisha na ukoboaji na usindikaji wa kahawa kipo katika hatua za mwisho za usimikaji wa mitambo na kinatarajiwa kutoa ajira 450.

**viii) Viwanda vya Sabuni**

**87. Mheshimiwa Spika**, Kiwanda cha *KEDS Tanzania Ltd* chenye uwezo wa kuzalisha sabuni za unga kiasi cha tani 50,000 kwa mwaka, ujenzi wake umekamilika na kimeanza uzalishaji. Vilevile, Kiwanda cha *Sabuni Industries Ltd* cha Tanga kilichobinafsishwa ambacho sasa kinaitwa *Murzah Wilmar Soap Industry*, kimefanyiwa ukarabati na kuanza uzalishaji mwezi Machi 2018.

**ix) Viwanda vya Kutengeneza Sigara**

**88. Mheshimiwa Spika**, viwanda vya sigara ni kichocheo kikubwa cha uongezaji thamani wa zao la tumbaku nchini. Hadi kufikia mwaka 2017, Tanzania ilikuwa na viwanda viwili (2) vya kutengeneza sigara vya *Tanzania Cigarette Company* (TCC) na kiwanda cha *Tobacco Mastermind* vilivyopo mkoani Dar es Salaam. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha sigara milioni 7,412 kwa mwaka. Kutokana na mchango wake katika uchumi, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani zao la tumbaku ambapo mwekezaji wa Kampuni ya *Philip Morris Tanzania Ltd* alipatikana na kuwekeza kwa ajili ya kuzalisha sigara katika eneo la Kingolwira mkoani Morogoro. Uzinduzi wa kiwanda umefanyika mwezi Machi 2018. Kiwanda hicho kina uwezo wa kutengeneza sigara milioni 400 kwa mwaka na kuajiri wafanyakazi 224.

f) ***Viwanda Vinginevyo***

**89. Mheshimiwa Spika**, uwekezaji wa viwanda umeendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini kwa kulenga makundi manne ya viwanda:- (i) ujenzi wa viwanda vya vifungashio maalum kwa ajili ya kutunzia na kuhifadhi mazao; (ii) viwanda vya kusindika mazao ikiwemo usindikaji wa nafaka; (iii) viwanda vya vinywaji vikali; na (iv) viwanda vya vipodozi.

g) ***Kuendeleza Kanda na Kongano za Viwanda***

**90. Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa kuharakisha kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, Wizara iliingia Makubaliano ya Awali (Memorandum of Understanding) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) tarehe 8 Machi, 2018. Makubaliano hayo yataiwezesha Tanzania kutekeleza Programu ya Nchi ya Ushirikiano (Partnership Country Programme-PCP) inayosimamiwa na UNIDO na inayojielekeza katika ujenzi wa maendeleo endelevu na jumishi ya viwanda. Utekelezaji wa PCP unatarajiwa kuanza baada ya Bodi ya UNIDO kuridhia Tanzania kutekeleza mwezi Juni 2018. Mfumo wa utekelezaji wa PCP hushirikisha wadau mbalimbali chini ya udhamini wa UNIDO wakiwepo wadau wa maendeleo, taasisi za fedha za kimataifa na UNIDO kama mtaalam na Mshauri Mkuu wa Programu ya PCP. Aidha, Programu huwezesha vijana kupata mafunzo maalum ya taaluma muhimu za viwanda na huwahamasisha wawekezaji wakubwa wanaoaminika kuwekeza katika uendelezaji wa viwanda vinavyotekelezwa na Programu hiyo.

**91. Mheshimiwa Spika**, Programu ya PCP italenga kutekeleza mipango na programu za nchi yetu za kuleta maendeleo ya viwanda kulingana na vipaumbele tulivyojiwekea. Maeneo makubwa ambayo Programu ya PCP itajihusisha ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji kama vile kanda na kongano za uzalishaji ili kuiwezesha Sekta Binafsi ya ndani na nje kuwekeza na kuzalisha bidhaa bora za viwandani kwa maendeleo ya nchi yetu. Programu hii

itaiwezesha nchi yetu kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo kwa kasi zaidi.

**92. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) imetenga eneo la ekari 95 kati ya ekari 230 za eneo la viwanda la TAMCO - Kibaha kwa ajili ya ujenzi wa kongano maalum la viwanda vya nguo na mavazi. Mpango Kabambe (*Master Plan*) wa kuendeleza eneo hilo umeandaliwa kwa msaada wa Shirika la *Gatsby Africa* na michoro ya eneo hilo imetayarishwa na kuingizwa katika ramani ya Mji wa Kibaha. Aidha, Serikali imekubaliana na SUMA JKT kutekeleza kazi ya kusawazisha eneo hilo ili kurahisisha ujenzi wa miundombinu.

**h) Kujenga na Kuimarisha Mifumo ya Taarifa za Viwanda**

**93. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaendelea kukusanya takwimu za viwanda vidogo, vya kati na vikubwa itakayowezesha kuandaa Taarifa ya Mwaka ya Utafiti wa Uzalishaji Viwandani (Annual Survey of Industrial Production - ASIP) inayotarajiwa kukamilika mwezi Juni 2018. Taarifa hizo zitatumika kufanya chambuzi mbalimbali zitakazosaidia Serikali kufanya maamuzi ya kiseru na kuweka mikakati ya kuendeleza Sekta ya Viwanda.

**i) Tathmini na Uendelezaji wa Mahitaji ya Ujuzi Maalum wa Viwanda katika Sekta ya Nguo na Mavazi**

**94. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa *Supporting Indian Trade and Investment for Africa (SITA)*, imetafiti hali ya ujuzi katika Sekta ya Nguo na Mavazi. Utafiti huo ulibaini upungufu mkubwa wa ujuzi (technical and soft skills) hasa kwa waendesha mitambo. Juhudi za kupunguza tatizo la ujuzi (technical skills) zimefanyika kwa kutoa mafunzo maalum yaliyofanyika nchini Ethiopia na kufadhiliwa na mradi wa SITA. Mafunzo hayo yalikusishwa baadhi ya wafanyakazi kutoka viwanda vya *21<sup>st</sup> Century, A-Z na MWATEX*. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu ilidhamini mafunzo



kwa kushirikiana na Mamlaka ya EPZ, viwanda vya *Mazava Fabrics Ltd* na TOUKU. Mafunzo hayo yalikusisha kutoa stadi za uzalishaji viwandani kwenye Sekta ya Nguo na Mavazi kwa vijana wa kitanzania hususan katika maeneo ya usanifu, ukataji na ushonaji wa mavazi. Lengo la mafunzo hayo ni kufanya uzalishaji wa nguo na mavazi nchini kufikia viwango vinavyokidhi mahitaji ya masoko ya nje ya nchi kupitia fursa mbalimbali zikiwemo za AGOA na EBA (*Everything But Arms*) na pia soko la ndani .

j) **Mafanikio Makuu ya Sekta ya Viwanda**

**95. Mheshimiwa Spika**, katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali imejielekeza katika ujenzi wa viwanda ambavyo vinatumia kwa wingi malighafi zinazozalishwa nchini hususan kutoka sekta za kilimo, mifugo, madini na misitu. Vilevile, tunalenga kuendeleza viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika na wananchi walio wengi ili kuboresha ustawi wa jamii na kuokoa matumizi ya fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Aidha, eneo jingine linalopewa msukumo ni viwanda vinavyojiri watu wengi.

**96. Mheshimiwa Spika**, hivi sasa, nchi yetu inajitosheleza kwa mahitaji ya saruji tukiwa na viwanda 14 vyenye uwezo uliosimikwa wa tani milioni 10.98. Uzalishaji uliowahi kufikiwa ni tani milioni 7.4 kwa mwaka wakati mahitaji ya soko la ndani kwa sasa ni tani milioni 4.8. Hivyo, nchi yetu ina ziada ya uwezo wa kuzalisha wa tani milioni 2.6 kwa kuzingatia uzalishaji halisi inayoweza kuuzwa nje ya nchi (*Kiambatisho Na.12*).

**97. Mheshimiwa Spika**, kwa hivi sasa tunavyo viwanda 25 vya kuzalisha bidhaa za chuma. Hali hiyo imetuwzesha kujitosheleza kwa mahitaji ya mabati, nondo, *angle bars, hollow section*, kwa kutaja baadhi. Vilevile, tunavyo viwanda 15 vya kuzalisha bidhaa za plastiki zikiwemo mabomba ya maji. Hali hiyo imetufanya tuwe na uwezo wa kuzalisha mabomba ya kutosha kwa mahitaji ya soko la ndani na ziada kuuza nje ya nchi. Pia, ujenzi wa

viwanda viwili vya vigae vyenye uwezo wa kuzalisha mita za mraba 130,000 kwa siku imetufanya tujitosheleze kwa mahitaji ya vigae nchini. Hivyo, ongezeko hilo limekuwa kichocheo cha kujenga nyumba imara na za kisasa mpaka maeneo ya vijijini.

**98. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu pia inajitosheleza kwa mahitaji ya vinywaji mbalimbali hususan maji ya chupa, soda, vileo kwa kutaja baadhi. Maendeleo katika ujenzi wa viwanda yanaonekana pia katika usindikaji wa vyakula kwa kutumia mitambo ya kisasa na ujuzi katika ufungashaji. Hali hiyo imesaidia kuongeza thamani ya mazao na kuwezesha wananchi mpaka ngazi ya vijiji kupata vyakula vyenye viwango na ubora wa hali ya juu.

**99. Mheshimiwa Spika**, tumefanikiwa kuvutia ujenzi wa viwanda viwili vya kutengeneza mita za umeme, hali itakayotwezesha kupunguza gharama za kuagiza mita hizo kutoka nje ya nchi. Vilevile, Tanzania sasa tuna uwezo mkubwa wa kutengeneza transfoma kufuatia upanuzi wa Kiwanda cha TANELEC, ujenzi wa kiwanda kipya cha *Europe Inc Industries Ltd*, na uanzishaji wa kitengo cha kutengeneza transfoma katika Kiwanda cha *Africables Ltd*. Pamoja na viwanda hivyo, miradi mingi iko katika hatua za awali ikilenga sekta ya kutengeneza vifaa vya umeme ikiwemo nguzo za zege.

### **3.3.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

**100. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, viwanda vidogo ni muhimu katika ustawi wa Taifa letu kwani vinachochea ujenzi wa uchumi jumuishi. Sekta hiyo inaajiri takribani Watanzania milioni 6 kwa sasa. Viwanda hivyo huchangia Pato la Taifa takriban asilimia 35. Viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vimechukua zaidi ya asilimia 98 ya idadi ya viwanda nchini na wawekezaji wa viwanda katika kundi hilo ni Watanzania wenyewe.

(a) **Kuendelea Kuhamasisha Ujenzi wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

(i) ***Kutoa Mwongozo wa Usimamizi wa Ujenzi wa Viwanda kwa Mamlaka za Wilaya na Mikoa***

**101. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua kuwa ujenzi wa viwanda hufanyika chini ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, Wizara imeandaa na kukamilisha Mwongozo wa Kusimamia Maendeleo na Ujenzi wa Viwanda Nchini utakaowezesha mikoa na wilaya kusimamia ujenzi wa viwanda kwa ufanisi na tija. Lengo kuu la Mwongozo huo ni kujenga uelewa wa pamoja kwa watendaji wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Mwongozo pia utatoa maelekezo kwa watendaji, ili kurahisha usimamizi, utekelezaji na uendelezaji wa ujenzi wa viwanda. Hatua hiyo itasaidia na kuharakisha mafanikio ya ujenzi wa viwanda ambao ni endelevu na jumuishii. Mwongozo huo pia umeainisha wadau muhimu katika ujenzi wa viwanda ambao mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zitapaswa kushirikiana nao ili kuharakisha maendeleo ya viwanda nchini.

(ii) ***Kushirikiana na TAMISEMI katika Kuhamasisha Utengaji wa Maeneo ya Ujenzi wa Viwanda na Biashara Ndogo***

**102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilitembelea baadhi ya mikoa ili kutathmini zoezi la utengaji wa maeneo ya uwekezaji wa viwanda na biashara ndogo nchini. Maeneo yaliyotembelewa ni mikoa ya Kigoma, Mbeya, Singida na Tanga. Katika ufuatiliaji huo, imebainika kuwa mikoa inaendelea vyema katika kutenga maeneo. Mkoa wa Tanga umetenga maeneo yafuatayo: Halmashauri ya Jiji la Tanga, hekta 27.8 (Kange); hekta 68 (Pongwe); na hekta 3.9 (Masiwani). Vilevile, viwanja 101 (Pongwe) na viwanja 324 (Amboni) vimetengwa. Pia, jumla ya mita za mraba 23,671 zimetengwa katika maeneo ya Tangasisi, Mnyanjari na Mzingani. Halmashauri ya Muheza imetenga ekari 2,829 katika eneo la Chaturi; ekari 5,730 (Shambamombwera); ekari 12,255 (Azimio Kilapua); ekari 2,148 (Shamba Kibaranga); na ekari 2,829 (Sigimiembeni). Halmashauri ya Mji wa Korogwe imetenga mita za mraba

21,600 katika eneo la Makorakanga na hekta 114.68 katika eneo la Kalalani. Aidha, hekta 2,043 zimetengwa kwa ajili ya EPZ.

**103. Mheshimiwa Spika**, Mkoa wa Mbeya umetenga maeneo yafuatayo: Halmashauri ya Kyela ekari 39.5 katika eneo la Ipyana; ekari 50 katika eneo la Kajujumle; na ekari 60 katika eneo la Busele. Halmashauri ya Jiji la Mbeya imetenga ekari 54 kwa ajili ya viwanda vya kati na ekari 36 kwa ajili ya viwanda vidogo katika eneo la Inyala na ekari 7 katika eneo la Iwindi. Halmashauri ya Rungwe imetenga ekari 17 kwa ajili ya viwanda vidogo na ekari 10.67 kwa ajili ya biashara ndogo katika eneo la Ilinge.

**104. Mheshimiwa Spika**, Mkoa wa Singida umetenga maeneo katika Halmashuri zake kama ifuatavyo: Iramba (ekari 20); Mkalama (ekari 10); Itigi (ekari 10); Manyoni (ekari 11); na Ikungi (ekari 4). Aidha, Mkoa wa Kigoma umetenga maeneo katika Halmashauri za Kasulu Vijijini (ekari 25); Kasulu Mji (ekari 20); Uvinza (ekari 20); Kakonko (ekari 20); Buhigwe (ekari 20); na Kibondo (ekari 20). Wizara itaendelea kushirikiana na mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inatenga na kulinda maeneo kwa ajili ya viwanda na biashara na kuweka mikakati ya kuyaendeleza.

(iii) **Kitabu cha Taarifa Muhimu kwa Wajasiriamali**

**105. Mheshimiwa Spika**, katika kuhamasisha uendelezaji wa biashara kwa wajasiriamali, Wizara imeandaa Kitabu cha Taarifa Muhimu kwa Wajasiriamali kilichoweka pamoja taarifa zilizo chini ya usimamizi wa mamlaka mbalimbali zinazohusika katika kuanzisha na kuendesha biashara. Taarifa hizo zitawarahisishia wananchi kufahamu aina ya vibali au leseni zinazotakiwa wakati wa kuanzisha aina tofauti za biashara. Kitabu hicho kinaainisha taasisi na mahali huduma zinapopatikana tofauti na hali ya sasa ambapo mjasiriamali analazimika kufuatilia mwenyewe na wakati mwingine anakuwa hafahamu mahali na aina ya huduma husika zilipo. Hatua inayofuata

ni kuchapisha, kufanya uzinduzi, kusambaza na kutoa elimu kwa umma.

(iv) ***Kuwezesha Uanzishwaji wa Kongano za Samani***

**106. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Mzumbe chini ya ufadhili wa taasisi ya *International Growth Centre* ya Uingereza imekamilisha utafiti ulioangalia namna ya kuendeleza Sekta ya Samani nchini. Lengo la utafiti huo ni kubaini fursa katika sekta hiyo na kupanga mikakati ya kuendeleza na namna nzuri ya kushirikisha wadau. Utafiti huo umekamilika na una mapendekezo mbalimbali ya kuboresha sekta ikiwemo kuanzisha kongano kwa ajili ya kuwaweka pamoja wajasiriamali wa Sekta ya Samani. Mapendekezo mengine ni kuboresha teknolojia na nyenzo zinazotumika kutengenezea samani na kuwapa wajasiriamali mafunzo muafaka ya kutengeneza samani bora na shindani katika soko. Aidha, utafiti huo utawezesha kujua stadi zinazohitajika, vifaa na mashine zinazohitajika. Maeneo lengwa yatakayotumika kuanzisha kongano hizo ni yale yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za viwanda.

(v) ***Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya Mwaka 2003***

**107. *Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendelea na mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya Mwaka 2003. Tathmini ya utekelezaji wa sera imekamilika na hivi sasa Wizara inaendelea na tafiti katika maeneo yaliyobainishwa kuhitaji utafiti wa kina. Maeneo hayo ni sanaa za mikono; sekta zinazoibuka hasa mafuta, gesi na madini; na ukuaji wa jasiriamali. Maeneo mengine ni mfumo wa sheria na usimamizi wa biashara; upatikanaji wa masoko; uratibu wa sekta; na upatikanaji wa fedha. Aidha, maandalizi ya kufanya utafiti katika maeneo ya ubunifu na teknolojia; maswala mtambuka; huduma za kuendeleza biashara; na miundombinu ya msingi na uendelezaji viwanda vijijini yanaendelea.

(vi) ***Kuendelea Kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Ujasiriamali (NEDF)***

**108. *Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi 2018, mtaji wa NEDF umekua na kufikia Shilingi 7,819,422,990. Ukuaji huo umetokana na kuzungusha mtaji wa Shilingi 5,051,000,000 uliotolewa na Serikali tangu Mfuko uanzishwe mwaka 1994. Ongezeko la Shilingi 2,768,422,990 katika mtaji huo limetokana na juhudi za Wizara na SIDO kufuatilia kwa umakini maendeleo ya shughuli za wajasiriamali wanufaika na kuimarisha mifumo ya marejesho ya mikopo inayotolewa.

**109. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mfuko wa NEDF katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Singida na Tabora. Ufuatiliaji huo ulibaini kuwepo kwa maombi mengi ya mikopo ikilinganishwa na uwezo wa Mfuko. Maombi yaliyowasilishwa yalikuwa Shilingi bilioni 6.398 ikilinganishwa na uwezo wa Mfuko wa kutoa mikopo ya Shilingi bilioni 3.344. Licha ya kuwepo kwa changamoto hizo, Mfuko huo umefanikisha kupatikana ajira 4,438 mwaka 2017/2018, kati yao wanawake ni 2,308. Mafanikio mengine ni kuimarika kwa biashara na viwanda vidogo vilivyopata mikopo ya NEDF, wajasiriamali kumudu kusomesha watoto, kujenga nyumba za kisasa, kununua vyombo vya usafiri na kukuza vipato vya familia.

(b) ***Kutumia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kama Nyenzo ya Kujenga Viwanda***

***(i)Kulifanyia Mageuzi Shirika la SIDO***

**110. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuliwezesha Shirika la SIDO ili liweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa viwanda. Kwa mwaka 2017/2018, SIDO imepokea Shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya kuongeza maeneo ya kufanyia kazi wajasiriamali na kuendelea kujenga ofisi katika mikoa mipya ya Geita, Katavi na Simiyu ili kufikisha huduma za SIDO katika mikoa hiyo. Aidha, Wizara imeendelea kuongeza miundombinu ya majengo ili kuongeza idadi ya

wajasiriamali wa viwanda katika mitaa ya viwanda ya SIDO. Kwa kuanzia, majengo ya kufanyia shughuli za viwanda kwa wajasiriamali wadogo (industrial sheds) yanajengwa katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Manyara, Mtwara na Njombe.

**(ii) Kuhamasisha Wananchi Kushiriki katika Ujenzi wa Viwanda**

**111. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia SIDO iliandaa maonesho ya kanda katika mikoa ya Iringa, Kigoma, Kilimanjaro na Lindi. Maonesho hayo yalishirikisha wajasiriamali 520 kati ya hao wanawake ni 390. Wizara ilitumia fursa ya maonesho hayo kuhamasisha wajasiriamali kuwekeza katika viwanda; kutoa ushauri wa kuboresha bidhaa; na kuelezea sera na mikakati ya kisekta inayolenga kuendeleza viwanda kupitia vipeperushi. Vilevile, wananchi walihamasishwa kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ili kutanua soko la ndani na hivyo kuchochea viwanda hivyo kuzalisha zaidi.

**(c) Ushirikiano na Wadau**

**112. Mheshimiwa Spika**, Wizara inashirikiana na Serikali ya Canada kutekeleza mradi wa *Strengthen Small Business Value Chain*. Taasisi isiyo ya Kiserikali ya MEDA inatekeleza mradi huo kwa kushirikiana na SIDO, TCCIA na *Tanzania Women Chamber of Commerce*. Mradi huo unaohusisha ujenzi wa uwezo wa kuziwezesha jasiriamali kukua kupitia huduma za mafunzo, mitaji na teknolojia. Jasiriamali hizo ni zile zinazojihusisha na sekta za uongezaji thamani mazao, ujenzi, usambazaji (logistics), uchimbaji madini na uzalishaji viwandani. Mradi huo unatekelezwa katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Singida, Songwe na Tanga. Aidha, Mradi huo unaotekelezwa kuanzia mwaka 2015 hadi 2021, una thamani ya Dola za Canada milioni 30 na utanufaisha jasiriamali 10,000 katika mikoa husika. Hadi kufikia Machi 2018, Mradi huo umetoa huduma za kuendesha na kukuza biashara kwa jasiriamali 6,213; jasiriamali 1,428 zimewezeshwa kupata mitaji midogo

midogo na teknolojia na jasiriamali 500 zimepata ruzuku ya mbegu bora kwa zao la vanilla ili kuboresha uzalishaji.

### **3.3.3 Sekta ya Uwekezaji**

**113. Mheshimiwa Spika**, jitihada za ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini, pamoja na mambo mengine, zinahitaji ushiriki mpana na shirikishi wa sekta ya umma na binafsi. Jitihada hizo zinajumuisha uhamasishaji na uvutiaji mitaji na wawekezaji, kuweka mazingira wezeshi na rafiki, kutangaza fursa zilizopo katika miradi na maeneo mbalimbali, kuboresha na kutangaza vivutio katika maeneo mbalimbali ya uchumi kwa kutaja machache. Wizara kupitia TIC na kwa kushirikiana na Taasisi za Sekta Binafsi zinajishughulisha na uhamasishaji wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

#### **a) Kuhamasisha Wawekezaji wa Ndani na Nje**

**114. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ilihamasisha wawekezaji kupitia makongamano yaliyofanyika katika mikoa ya Tanga (Agosti 2017) na Kagera (Desemba 2017). Vilevile, Wizara ilishiriki katika Kongamano la uwekezaji kati ya Tanzania na China lililofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Novemba 2017; Tanzania na Jordan mwezi Desemba, 2017; Tanzania na Ufaransa, tarehe 18 Aprili 2018, Dar es Salaam; na Tanzania na Israel lililofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 23 hadi 24 Aprili 2018. Vilevile, kupitia programu ya kuimarisha uwekezaji na biashara kati ya India na Tanzania (SITA) iliwakutanisha wawekezaji wa ngozi na bidhaa zake mwezi Desemba, 2017. Makongamano yalihusisha wafanyabiashara wa ndani na nje zaidi ya 1,000 na fursa mbalimbali zilizopo Tanzania ziliainishwa. Aidha, Wizara ilishiriki Mkutano wa Pili wa Afrika Mashariki wa Biashara na Wajasiriamali ulioenda sambamba na maonesho ya biashara za wajasiriamali yaliyofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 14 hadi 16 Novemba, 2017.

**115. Mheshimiwa Spika**, kufuatia makongamano na mikutano hiyo pamoja na ushirikiano wa karibu wa Ofisi zetu za Ubalizi, ujumbe wa wawekezaji mbalimbali wameweza



kufika nchini na kutembelea Kituo cha TIC, Wizara na taasisi nyingine za umma na Sekta Binafsi. Baadhi ya kampuni zilizotembelea nchini ni: Ujumbe wa taasisi ya *CRG Group of Institutions* ya India inayotaka kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa chuo cha ufundi stadi; Ujumbe wa kampuni ya *Artech Fze Group* kutoka Misri wameonesha nia ya kuwekeza kwa ubia na taasisi au shirika la Serikali kwa ubia katika mradi wa uchimbaji makaa ya mawe na uzalishaji wa saruji kwa ajili ya kuuza nje ya nchi; na ujumbe wa kampuni ya *A & T Agricultural Ltd* ya Vietnam kwa ajili ya kufanya biashara ya korosho ghafi na kuwekeza katika viwanda vya kubangua korosho.

**116. Mheshimiwa Spika**, wengine ni makampuni tisa (9) ya China yakiongozwa na taasisi ya Kongamano na Viwanda Kati ya China na Afrika yaani *China Africa Industrial Forum* (CAIF) wakilenga Sekta ya Nishati, viwanda na miundombinu; ujumbe wa kampuni ya *TVS Global Automotive* kutoka India ukiwa na nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa pikipiki hapa nchini; na ujumbe wa wafanyabiashara na wawekezaji kutoka China wakiongozwa na wawakilishi wa *China WTO Africa Affairs Committee on Trade Promotion Centre* (CWTO) ulioonesha nia ya kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo na Biashara.

**117. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha jitihada za kuvutia wawekezaji kutoka nje, Wizara imeandaa rasimu ya mwongozo kwa balozi za Tanzania nje ya nchi. Mwongozo huo unaelekeza ofisi hizo kutumika kuvutia mitaji na uwekezaji nchini. Pia, unasisitiza jukumu la kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania zikiwemo zinazozalishwa na viwanda vidogo na vya kati; na kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko nchini. Mwongozo huo unaelekeza kuanzishwa kwa madawati maalum ya kushughulikia masuala ya biashara na uwekezaji. Rasimu hiyo itawasilishwa kwa wadau na Wizara za kissekta ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo ndiyo mtekelezaji mkuu. Aidha, ili kuimarisha diplomasia ya uchumi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara na taasisi nyingine ilifanya maonesho

ya bidhaa za Tanzania katika nchi za Kenya na Dubai tarehe 26 Aprili, 2018.

**118. Mheshimiwa Spika,** maamuzi ya Serikali ya kuhamia makao makuu Dodoma yameambatana na kuhamasika kwa sekta binafsi kujenga viwanda Dodoma. Kampuni ya Bia ya *Tanzania Breweries Ltd* (TBL) imeazimia kuwekeza katika ujenzi wa kiwanda kipya cha kuzalisha bia mkoani Dodoma kama mkakati wake wa kuongeza uzalishaji nchini. Kampuni hiyo inatarajia kuwekeza Shilingi bilioni 225. Kiwanda hicho kipya kinatarajia kuzalisha lita milioni 100 za bia kwa mwaka na kutoa ajira kwa watu 600. Kiwanda hicho kitahitaji malighafi kiasi cha tani milioni 5.6 na hivyo kutoa fursa nzuri ya soko kwa wakulima wa mtama, mahindi, shayiri na mihogo.

**b) Kuratibu Uwepo wa Mazingira Bora ya Uwekezaji**

**119. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kuandaa na kushiriki vikao vya pamoja vya mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa lengo la kupata maoni ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Katika mwaka 2017/2018, mikutano miwili (2) ya ngazi ya juu iliyohusisha Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, na viongozi wakuu wa taasisi ya Sekta Binafsi ilifanyika mwezi Oktoba 2017 jijini Dar es Salaam na Januari 2018 mjini Dodoma. Serikali na Sekta Binafsi wamekubaliana kuendelea kuwa na mikutano kama hiyo ya majadiliano kwa kuwa ina umuhimu sana katika kupata ufumbuzi wa changamoto zilizopo na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

**120. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza maazimio ya mikutano hiyo iliyopendekeza kuitishwa kwa mikutano midogo ya sekta maalum, Wizara za Serikali kwa kushirikiana na vyama vya kisekta zimefanikisha kuitishwa mikutano ya mashauriano ya kisekta kati ya Wizara husika na wadau. Mikutano hiyo ni pamoja na mikutano kati ya

Sekta Binafsi na Wizara ya Fedha na Mipango kujadili masuala ya kikodi; Wizara ya Nishati kujadili masuala ya nishati; na Wizara ya Maliasili na Utalii kujadili masuala ya utalii. Vilevile yalifanyika majadiliano na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo na TAMISEMI kujadili changamoto za uongezaji thamani kwenye mnyororo wa uzalishaji wa pamba. Pia, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilijadiliana na Sekta Binafsi kuhusu changamoto mbalimbali kwenye Sekta ya Chuma na Mabati ikiwemo kupanda kwa bei ya chuma. Kimsingi, mikutano hiyo imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi, na Serikali imeahidi kuendelea kushauriana na wafanyabiashara na wawekezaji ili kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji na hivyo kukuza uchumi.

**c) Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996**

**121. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara imefanya mapitio na kukamilisha rasimu ya Sera ya Uwekezaji ili iendane na matakwa ya mipango ya kitaifa. Rasimu hiyo itapelekwa kwa wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kupata maoni yao kabla ya kuandaa mkakati wa utekelezaji. Vilevile, Wizara inaendelea kuratibu maandalizi ya Sera ya Uwekezaji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Investment Policy) ambayo inalenga kuhamasisha matumizi ya fursa za uwekezaji kwa nchi wanachama kwa pamoja.

**d) Kukamilisha Mapitio ya Sheria ya Uwekezaji ya 1997**

**122. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imefanya uchambuzi wa Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 na Sheria nyingine za kodi na kupendekeza maboresho ili kubadili sifa na vigezo vya aina ya uwekezaji unaotambulika na Sheria ya Uwekezaji. Aidha, hatua hiyo inalenga kuzifanya sheria za kodi kuitambua misamaha ya kodi inayotolewa chini ya Sheria ya Uwekezaji ili kuwezesha utekelezaji wa

maamuzi ya Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (National Investment Steering Committee-NISC). Hatua hiyo ni muhimu katika kukabiliana na changamoto zilizopo hususan katika utekelezaji wa sheria za kodi katika kutoa misamaha kwa wawekezaji mahiri (Strategic Investors) ambayo imeidhinishwa na NISC. Mapendekezo hayo yamewasilishwa katika hatua za mwisho za majadiliano na maamuzi.

#### **3.3.4 Sekta ya Biashara**

**123. Mheshimiwa Spika**, Wizara ina jukumu la kujenga na kuendesha mfumo wa kibiashara unaosimamiwa kisheria, unaotabirika na wenye uwazi ili kuwezesha ufanyaji biashara kwa urahisi na tija. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kufungua fursa mbalimbali za biashara kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini. Jitihada hizo zimeshirikisha kwa ukaribu wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Matokeo ya jitihada hizo yamechochea katika kukuza mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa ambapo kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 11.0 ikilinganishwa na asilimia 10.8 mwaka 2016.

#### **a) Mwenendo wa Biashara ya Kimataifa**

**124. Mheshimiwa Spika**, mauzo ya bidhaa kwenye masoko ya upendeleo yalikuwa kama ifuatavyo: soko la China yalipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 355.9 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani milioni 142.3 mwaka 2017. Upungufu huo ulitokana kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa mauzo ya vito vya thamani. Manunuzi ya Tanzania kutoka China yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 1,630.2 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 1,408.1 mwaka 2017 (*Kiambatisho Na. 13*). Mauzo katika Soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 706.4 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani milioni 977.6 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na uuzaji wa bidhaa mbalimbali kama karafuu, korosho, ngozi za wanyama, nazi, mazao ya jamii ya kunde, samaki, pamba na nyuzi za katani. Manunuzi ya Tanzania kutoka India yalipungua kutoka

Dola za Kimarekani milioni 1,421.6 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,077.6 mwaka 2017 (*Kiambatisho Na. 14*). Hali hiyo ilisababishwa na kupungua kwa kiwango cha uingizaji wa bidhaa kama vile chuma, chai, tumbaku (Tobacco, partly or wholly stemmed/stripped), nafaka, bidhaa za plastiki na kemikali.

**125. Mheshimiwa Spika,** mauzo katika soko la Japan yalipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 139.2 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani milioni 75.7 mwaka 2017. Upungufu huo unatokana na kupungua kwa mauzo ya vito vya thamani (precious metal ores), chai, kahawa na pamba. Mwaka 2016, manunuzi ya bidhaa kutoka Japan yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 369.2 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 365.2 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 1.2 (*Kiambatisho Na. 15*). Upungufu huo unatokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za chuma (Flat rolled products of iron), magari kuanzia cc 1500 hadi 2000 (of cylinder capacity exceeding 1500cc but not exceeding 2000cc), magari yasiyozidi cc 1500 (of a cylinder capacity not exceeding 1500cc)

**126. Mheshimiwa Spika,** bidhaa zilionunuliwa na Tanzania kutoka Jumuiya ya Ulaya zilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 557.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 936.1 kwa mwaka 2017, ikiwa ni ongezeko la asilimia 67.9. Pia mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 236.5 kwa mwaka 2016 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 441.4 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 86.7. Kutokana na hali hiyo urari wa biashara umeonesha nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 494.7 (*Kiambatisho Na. 16*), ikimaanisha thamani ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ni kubwa ikilinganishwa na thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko hilo. Hii inatokana na Tanzania kuuza zaidi malighafi katika soko la Jumuiya ya Ulaya wakati Tanzania inaagiza bidhaa za viwandani (finished products).

**127. Mheshimiwa Spika**, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia Mpango wa AGOA kwa mwaka 2017 yaliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 40.545 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 37.476 kwa mwaka 2016 (*Kiambatisho Na. 17*). Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na Sekta ya Nguo na Mavazi kwa asilimia 99.2. Aidha, ili kuongeza mauzo zaidi katika soko hilo, Wizara imeanza kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Mauzo ya Tanzania katika soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA.

**128. Mheshimiwa Spika**, katika kutumia fursa za masoko ya kikanda, mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2017 yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 349.6 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 437.7 mwaka 2016. Upungufu huo umetokana na uzalishaji wa bidhaa zinazofanana kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, bidhaa za Tanzania zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni pamoja na mbogamboga, chai, matunda, magunia, mifuko ya plastiki, wanyama hai, viazi, samaki, udongo asilia, kahawa, mahindi, mchele, unga wa nafaka, karanga, mawese, ufuta, pamba na makaa ya mawe. Kwa upande mwingine, ununuzi wa Tanzania kutoka nchi za Jumuiya hiyo ulipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 220.4 mwaka 2017 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 298.9 mwaka 2016 (*Kiambatisho Na. 18*). Hali hiyo imechangiwa na kuimarika kwa uzalishaji bidhaa ndani hivyo kupunguza kasi ya uagizaji wa bidhaa kama vile madawa (medicaments), *Chewing gum, whether or not sugar-coated*, chumvi, sabuni, vifaa vya plastiki, mafuta ya kupikia, sukari, nyama, wanyama hai, vinywaji na bidhaa za mifugo.

**129. Mheshimiwa Spika**, mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), mwaka 2017 yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 877.8 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 1,017.9 mwaka 2016. Upungufu huo umetokana kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa uuzaji wa dhahabu katika soko la Afrika ya Kusini. Aidha, bidhaa zilizouzwa katika soko la SADC

ni pamoja na dhahabu, chai, mazao jamii ya kunde, tumbaku, ngano, ngozi, pamba, matunda ya kutengeneza juisi, mawese, mbolea, vipuri vya magari na samaki. Ununuzi wa Tanzania kutoka katika soko hilo uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 612.4 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,7781.4 mwaka 2017 (*Kiambatisho Na.19*). Ongezeko hilo limetokana na uagizaji kwa wingi bidhaa za chuma, petroli [Motor Spirit (gasoline) premium], dawa za binadamu (medicaments), *gas oil*, mafuta ghafi (crude oil), mafuta ya taa (Kerosene type Jet Fuel), *Turbojets*, *turbo-propellers*

**b) Kuendeleza Majadiliano ya Kibiashara ili Kupanua Fursa za Masoko na Uwekezaji**

**i) Majadiliano Baina ya Nchi na Nchi**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara iliratibu mikutano mbalimbali kati ya Tanzania na nchi nyingine ili kuendelea kutafuta fursa nafuu za biashara na uwekezaji. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (JTC) kati ya Tanzania na India uliofanyika New Delhi, India tarehe 28 – 29 Agosti, 2017. Mkutano huo ulifikia makubaliano ya kukamilisha Mkataba wa Kuhamasisha na Kulinda Uwekezaji; Mkataba wa Ushirikiano kwenye Usimamizi wa Forodha; na mkopo wa kutekeleza mradi wa maji kwa ajili ya miji 17 nchini.

**131. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Tatu wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) kati ya Tanzania na Misri uliofanyika Cairo, tarehe 10 Januari, 2018. Makubaliano yaliyofikiwa kwenye Sekta ya Viwanda na Biashara ni pamoja na kukamilisha Makubaliano ya Ushirikiano wa Kibiashara ambapo kwa upande wa Tanzania rasimu ya makubaliano hayo imekamilika na imepitia taratibu zote za ndani na kuwasilishwa upande wa Misri kwa ajili ya kuridhiwa na kusainiwa. Pia, makubaliano ya kushirikiana katika maonesho ya kibiashara; kuanzisha kiwanda cha uzalishaji wa nyama nchini; kituo kwa ajili ya

maonesho ya bidhaa za Misri; na kiwanda cha bidhaa za ngozi yalifikwa.

**132. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha mapitio ya Mkataba wa Biashara na Uchumi baina ya Tanzania na Urusi ambao umewasilishwa Urusi mwezi Januari 2018 kwa ajili ya kuridhiwa na kusainiwa. Aidha, Wizara inaendelea kukamilisha Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Biashara baina ya Tanzania na Mauritius na taratibu zote za ndani zimekamilika na utasainiwa baada ya upande wa Mauritius kukamilisha taratibu zao.

**133. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliandaa mkutano wa pamoja kati ya Tanzania na Kenya uliofanyika Namanga tarehe 3 Agosti, 2017 na jijini Dar es Salaam tarehe 6 hadi 8 Septemba, 2017. Mikutano hiyo ililenga kuondoa Vikwazo vya Kibiashara Visivyo vya Kiushuru (NTBs) baina ya nchi hizo mbili. Katika mikutano hiyo, Kenya iliridhia uingizaji wa gesi ya kupikia majumbani (LPG) na unga wa ngano kutoka kwa wafanyabiashara na wazalishaji wa Tanzania ambapo hapo awali zilizuiliwa kuingia nchini Kenya. Vilevile, Wizara ilishiriki katika mkutano wa pamoja baina ya Tanzania na Kenya uliofanyika Mombasa, Kenya tarehe 24-31 Januari, 2018. Mkutano huo ulilenga kuondoa Vikwazo vya NTBs baina ya pande hizo mbili ambapo Kenya imeruhusu unga wa mahindi, mafuta ya kupikia na bidhaa za Azam (Azam ice cream, juice na soda) kuingia nchini humo bila vikwazo vyovyote.

## ii) *Majadiliano ya Kikanda*

**134. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kurahisisha biashara baina ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki, Wizara kupitia mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji uliofanyika jijini Arusha tarehe 9 Februari 2018, Tanzania iliridhia kuondoa tozo ya Dola za Kimarekani 40 kwa ajili ya stika za kubandika kwenye magari yanayobeba bidhaa kutoka Bandari ya Dar es Salaam kupeleka nchi za Burundi, Rwanda na Uganda. Tanzania iliondoa tozo hiyo kwa kuwa imekuwa



ikilalamikiwa na wadau wa usafirishaji na hata kusababisha baadhi ya waagizaji wa mizigo kutoka nchi hizo kuanza kutumia bandari za nchi jirani.

**135. Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Dharura wa 35 wa Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki uliofanyika mjini Kampala, Uganda tarehe 15 hadi 20 Februari 2018, Wizara ilifanikiwa kuomba na kukubaliwa kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 ya thamani ya bidhaa za mitumba ya nguo na ngozi inayotoka nje ya Afrika Mashariki. Hii inatokana na kusudio la Marekani la kutaka kuziondoa nchi za Tanzania, Rwanda na Uganda kwenye Mpango wa AGOA. Uamuzi wa Marekani ulitokana na nchi za Afrika Mashariki kuongeza kodi kwa bidhaa za mitumba ikiwemo nguo na viatu kutoka Dola senti 20 hadi Dola senti 40 kwa kilo na kutoza kodi ya asilimia 35 ya thamani ya bidhaa. Hatua hiyo itawezesha Tanzania kuendelea kunufaika na fursa za soko la AGOA.

**136. Mheshimiwa Spika**, kupitia Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mjini Kampala, Uganda tarehe 23 Februari, 2018 Tanzania imeendelea kuwa na msimamo wa kutokusaini Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya nchi za Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC-EU EPA). Msimamo huo umezingatia Azimio la Bunge kuishauri Serikali kutosaini Mkataba huo hadi hapo utakapokidhi maslahi ya Taifa.

**137. Mheshimiwa Spika**, katika kuhamasisha jumuiya za wafanyabiashara kuhusu fursa nafuu za upendeleo za biashara zinazotokana na majadiliano ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya EAC iliandaa mafunzo ya kutoa taarifa kwa mfumo wa kielekroniki kwa Sekta Binafsi na wataalam wa taasisi za uhibitaji jijini Dar es Salaam tarehe 13 Desemba, 2017. Mafunzo hayo yalilenga kuwezesha walengwa kutumia vyema fursa za miradi mbalimbali zilizopo kwenye mikataba ya urahisishaji biashara; ulinzi wa afya za binadamu, wanyama na mimea (SPS); na vikwazo vya kiufundi vya kibiashara (TBT). Pia, mafunzo yalilenga kuwajengea uwezo na uelewa zaidi wadau kutoka Sekta

Binafsi na Umma kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Ushirikiano baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani, hususan kwenye eneo la urahisishaji biashara na utatuzi wa vikwazo vya biashara vinavyohusiana na masuala ya viwango na ubora wa bidhaa.

**138. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki katika mkutano wa tatu wa wataalam wa EAC kwa ajili ya kupitia Mpango Kazi wa Vikwazo vya TBT wa mwaka 2016/2017 na kuandaa Mpango Kazi wa mwaka 2017/2018. Mkutano huo ulifanyika Kampala, Uganda tarehe 4 hadi 6 Oktoba, 2017. Pia, Wizara ilishiriki katika mkutano wa uwezeshaji Jukwaa la Kikanda la Vikwazo vya Kiufundi vya Kibiashara (EAC TBT Forum) uliofanyika Dar es Salaam tarehe 12 hadi 14 Desemba, 2017. Washiriki waliweza kupata taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya TBT na kubadilishana uzoefu, hali inayotarajiwa kusaidia uboreshaji wa matumizi ya TBT kama sehemu ya kurahisisha ufanyaji wa biashara.

**139. Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa 29 wa Kamati ya Mawaziri wa Biashara wa SADC uliofanyika Pretoria, Afrika Kusini tarehe 14 Agosti, 2017 Tanzania ilifanikiwa kutetea na kukubaliwa kuendelea kutoza ushuru sukari ya viwandani asilimia 10 na ya majumbani asilimia 25. Hivyo, sukari hiyo inayoingizwa nchini kutoka nchi za SADC itaendelea kutozwa ushuru kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2019/2020. Vilevile, Mkutano huo uliridhia, maombi ya Tanzania ya kutoza ushuru wa asilimia 25 kwa bidhaa za karatasi za vifungashio (Pulp and Paper) zinazoingizwa nchini kutoka nchi za SADC kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2019/2020. Hatua hizo zinalenga kulinda na kutoa fursa kwa viwanda vyetu vya sukari na karatasi kuweza kujipanga vyema kuhimili ushindani katika bidhaa hizo kutoka kwa wazalishaji wa soko la SADC.

**140. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha tunatekeleza ipasavyo Itifaki ya Biashara ya SADC, Wizara imefanikiwa kupata ufadhili wa EUR 1,400,000 kupitia mradi wa *SADC Trade Related Facility* (SADC-TRF) unaofadhiliwa na

Umoja wa Ulaya. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Wizara imepokea EUR 420,000 kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi. Mradi huo unalenga kusaidia uendelezaji wa mnyororo wa uongezaji thamani hususan katika mazao ya kilimo; kuboresha usimamizi wa viwango; uwezeshaji biashara, na ukuzaji wa masoko. Aidha, ulilenga kurejea Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996 – 2020.

**141. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki Mkutano wa Nne wa Mawaziri wa Biashara wa Umoja wa Afrika uliofanyika Niamey, Niger tarehe 1-2 Desemba, 2017 kwa lengo la kukamilisha majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (African Continental Free Trade Area-AfCFTA). Kupitia Mkutano huo, Wizara iliweza kutetea na kupendekeza maboresho kwenye vipengele vyenye kuleta unafuu kwa nchi katika Mkataba wa AfCFTA hususan Itifaki ya Masuala ya Biashara ya Bidhaa na Biashara ya Huduma. Rasimu ya Mkataba na itafiki hizo ziliwasilishwa katika ngazi ya Wakuu wa Nchi na Serikali kwa uamuzi.

**142. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali kwa ajili ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) uliofanyika mjini Kigali, Rwanda tarehe 21 Machi, 2018. Mkutano huo ulitanguliwa na mikutano iliyofanyika mjini Kigali kuanzia tarehe 26 Februari, 2018 katika ngazi za wataalam, mabalozi, makatibu wakuu na mawaziri wanaohusika na masuala ya biashara, sheria na mambo ya nje. Mkutano huo ulikamilika kwa Wakuu wa nchi na Serikali kutia saina makubaliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Afrika. Kupitia Mkutano huo, Tanzania imetia saina Azimio la Kuunga Mkono Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Afrika (The Kigali Declaration on the Establishment of the African Continental Free Trade Area). Azimio hilo linaunga mkono na kubainisha nia na dhamira ya Tanzania na nchi nyingine wanachama katika kukamilisha baadhi ya maeneo ya majadiliano yaliyobaki katika hatua ya kwanza ya majadiliano kuwezesha nchi zote za Umoja huo kutia saina na kisha kuridhia Mkataba wa uanzishwaji wa AfCFTA. Maeneo yatakayojadiliwa katika

hatua ya pili yanahusu Uwekezaji, Sera ya Ushindani, Haki Miliki na Ubunifu (Intellectual Property Rights-IPR). Kwa ujumla, Mkataba huo utatoa fursa za upendeleo kupitia ushirikiano wa biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Afrika. Makubaliano hayo yanatoa fursa kwa Tanzania kuuza na kununua bidhaa kwa upendeleo kutoka nchi 55 za Afrika zenye soko lenye watu bilioni 1.2.

**143. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki katika mkutano wa majadiliano ya biashara ya huduma katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Lengo la ushiriki huo ni nchi wanachama kufunguliana masoko ya biashara ya sekta za kipaumbele za huduma kwa kuondoa vikwazo vya kisera, kisheria, kanuni na taratibu mbalimbali. Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wanachama zinatumia mfumo maalum kwa ajili ya kuhimiza mashirikiano ya kuondoa vikwazo vinavyoathiri biashara ya huduma miongoni mwao. Aidha, kwa upande wa SADC, nchi wanachama wamekubaliana kuendelea kukamilisha majadiliano ya kufunguliana milango katika baadhi ya sekta zikiwemo usafirishaji, utalii, fedha, mawasiliano, ujenzi na nishati. Majadiliano hayo yatakapokamilika yatasaidia wazalishaji, wafanyabiashara na watoa huduma wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika kutumia fursa za utoaji huduma zinazopatikana katika Jumuiya hizo.

**144. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki Mkutano wa kikosi kazi cha kikanda cha mapitio ya ushuru wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common External Tariff-CET review) uliofanyika mjini Kampala, Uganda kuanzia tarehe 20 hadi 23 Machi, 2018. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili na kukubaliana makundi ya viwango vipya vya pamoja vya kodi (tariff bands) vitakavyotumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, Mkutano huo haukuweza kukubaliana kuhusu makundi mapya ya viwango vya pamoja vya kodi. Imekubalika kuwa suala hilo lisogezwe mbele ili kutoa muda zaidi kwa kila nchi mwanachama kujitathmini.

iii) *Majadiliano ya Biashara za Kimataifa*

**145. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza majadiliano ya biashara ya kimataifa (Multilateral negotiations) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na biashara, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Mawaziri wa Biashara wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO 11<sup>th</sup> Ministerial Conference-MC11) uliofanyika mjini Buenos Aires, Argentina tarehe 10 hadi 13 Desemba, 2017. Baadhi ya mafanikio ya mkutano huo ni kukubaliana kuendelea na kazi ya kuandaa mkataba (legal text) wa uondoaji wa ruzuku kwenye Sekta ya Uvuvi; kuongeza muda (moratorium) wa miaka miwili kwa ajili ya kukamilisha mkataba wa kusimamia biashara kwa njia ya mtandao (e-commerce) hususan kwenye utozaji kodi kwenye miamala ya kibiashara inayofanyika kwa njia ya mtandao; kuongeza muda wa miaka miwili (2) kwa ajili ya kukamilisha makubaliano ya kimkataba yanayozifunga nchi changa ikiwemo Tanzania kwenye suala la Haki Miliki na Ubunifu (Trade Related Intellectual Property Rights-TRIPS); na Sudani ya Kusini kukubaliwa fursa ya *observer status* wakati mchakato wa kuwa mwanachama kamili ukiendelea.

**146. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza juhudi za usimamizi na ujenzi wa uwezo katika masuala ya viwango vya bidhaa, na kwa kuzingatia matakwa ya mkataba wa WTO wa masuala ya SPS, Wizara imeunda Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Masuala ya Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea. Kamati hiyo inayojumuisha wajumbe wapatao 36 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ina jukumu la kusimamia na kushauri Serikali kuhusu masuala ya SPS. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wataalam kutoka Umoja wa Afrika (African Union Inter-Bureau for Animal Resources AU-IBAR) iliendesha mafunzo ya siku tatu jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 23 hadi 25 Oktoba, 2017. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo na uelewa wa Kamati ili kusimamia ipasavyo masuala ya SPS nchini.

**147. Mheshimiwa Spika**, Wizara ina wajibu, kama nchi mwanachama wa WTO, kuweka wazi sera, sheria, mikakati na kanuni zinazolenga kusimamia biashara ili kufanya soko letu kuwa lenye kutabirika. Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara imewasilisha taarifa za viwango vipya 28 vya ubora (notifications of technical standards) kwenye Shirika la Biashara la Dunia (WTO) kwa bidhaa za mayai, nyama, nafaka, vileo, karatasi, vifaa vya huduma ya kwanza, nyaya za umeme, vifaa vya usafi na matairi ya magari kwa ajili ya maoni ya wajumbe wa WTO kabla ya kuanza kwa matumizi.

**148. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu kikao cha tatu cha Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara kilichofanyika tarehe 16-19 Januari, 2018 Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kamati hiyo yenye wajumbe 53 kutoka sekta za umma na binafsi za Tanzania Bara na Zanzibar. Kikao kilipitia na kupitisha maeneo muhimu ya utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation Agreement - TFA). Maeneo hayo yaliwasilishwa katika Shirika la WTO mwezi Machi 2018. Pia, kikao kilijadili mapendekezo ya miradi inayotarajiwa kutekelezwa nchini ili kukidhi matakwa ya TFA. Wadau mbalimbali wa maendeleo wamejitokeza na kuonesha nia ya kutaka kusaidia Tanzania katika kutekeleza mkataba huo.

**c) Kuratibu zoezi la kuridhiwa kwa Mkataba wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO) wa Uwezeshaji wa Biashara (Trade Facilitation Agreement-TF)**

**149. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, Wizara imekamilisha kuandaa na kuwasilisha Serikalini rasimu ya Waraka kwa ajili ya kuishauri Serikali kuridhia Mkataba wa WTO wa Uwezeshaji wa Biashara. Ni matarajio yetu kuwa mara baada ya Serikali kujiridhisha, mapendekezo kuhusu uridhiwaji wa Mkataba huo wa uwezeshaji biashara utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kufanya maamuzi. Licha ya kwamba Tanzania haijaridhia, Mkataba huo umeanza kufanya kazi

rasmi tarehe 22 Februari, 2017 baada ya theluthi mbili ya nchi wanachama wa WTO kuridhia mkataba huo.

**d) Kufanya Mapitio ya Sera za Biashara kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya Shirika la Biashara la Dunia**

**150. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki kwenye kikao cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kama sehemu ya maandalizi ya mapitio ya sera za biashara kwa nchi za Jumuiya hiyo. Warsha ya kikanda ilifanyika tarehe 30 Oktoba hadi 3 Novemba, 2017 mjini Arusha na iliandaliwa kwa ushirikiano wa Sekretariati ya WTO na Sekretariati ya EAC. Kikao hicho kililenga kufanya majumuisho ya taarifa zilizokusanywa na kila nchi mwanachama kwa ajili ya kukamilisha zoezi la mapitio ya sera za biashara kwa nchi husika. Taarifa hizo zinatarajiwa kutumika katika mapitio ya sera za biashara za nchi wanachama wa EAC chini ya WTO ambayo yamepangwa kufanyika Novemba, 2018. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta za Umma na Binafsi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar waliweza kukusanya majibu kwenye masuala yaliyoulizwa na WTO kwa kutegemea hali na mazingira ya nchi wanachama. Hatua inayofuata ni WTO kufanyia kazi taarifa hizo na kufanya vikao vingine na wadau kuanzia mwezi Mei 2018. Zoezi hilo la mapitio ya sera za biashara linalenga kujenga uelewa zaidi kwa nchi nyingine wanachama wa WTO kuhusu soko na namna ya ufanyaji wa biashara nchini Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, zoezi hilo linalofanywa na WTO kila baada ya miaka minne (4) linatusaidia kujitathmini na kujipanga vema zaidi katika kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini na namna tunavyokidhi matakwani ya uanachama wetu katika Shirika la Biashara la Dunia.

**3.3.5 Sekta ya Masoko**

**a) Mwenendo wa Biashara ya Ndani**

**151. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukusanya na kusambaza taarifa za mwenendo wa bei ya mazao na ule wa mifugo pamoja na bidhaa za mifugo

(Livestock Information Network and Knowledge System - LINKS) kwa lengo la kuongeza uwazi na ushindani wa haki katika biashara nchini. Aidha, taarifa za baadhi ya bidhaa za viwandani hususan vifaa vya ujenzi (nondo, mabati na saruji) na sukari zimeendelea kukusanywa.

**152. Mheshimiwa Spika,** taarifa hizo za masoko husambazwa kwa wadau kwa njia ya radio za kijamii, ujumbe wa simu za kiganjani, barua pepe, tovuti na magazeti. Taarifa zinazokusanywa ni bei za jumla za mazao makuu ya chakula kutoka katika masoko 26 ya miji ya mikoa. Pia bei za rejareja kwa bidhaa zote muhimu kutoka masoko 114 yaliyo katika Halmashauri zote nchini hukusanywa. Aidha, Wizara imeendelea kukusanya taarifa za mwenendo wa bei za mifugo (ng'ombe, mbuzi na kondoo) kutoka katika minada 58 nchini. Taarifa zinazokusanywa zinahusu idadi ya mifugo iliyouzwa kwa kila mnada, bei za wastani kwa madaraja kwa dume, na wastani kwa madaraja kwa jike. Taarifa hizo zimeongeza uwazi katika biashara na hivyo kuwasaidia wafugaji kupata bei nzuri ya mifugo yao wanapopeleka katika minada.

**153. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, bei ya mazao makuu ya chakula hususan mahindi, maharage na mchele zimeshuka na baadhi yake kupanda kwa viwango tofauti ikilinganishwa na msimu wa 2016/2017. Kwa mfano, wastani wa bei ya jumla ya mahindi kwa gunia la kilo 100 ilipungua kutoka Shilingi 98,077 msimu wa 2016/2017 hadi kufikia Shilingi 49,386 msimu wa 2017/2018, sawa na upungufu wa asilimia 49.65. Bei ya jumla ya maharage kwa gunia la kilo 100 ilishuka kutoka Shilingi 178,070 mwaka 2016/2017 hadi kufikia Shilingi 169,771 mwaka 2017/2018, sawa na upungufu wa asilimia 4.66. Kushuka kwa bei za mahindi na maharage kumechangiwa na kuongezeka kwa ugavi kulikotokana na hali ya hewa nzuri iliyosababisha uzalishaji mzuri wa mazao hayo msimu wa 2017/2018. Aidha, bei ya jumla ya mchele kwa gunia la kilo 100 iliongezeka kutoka wastani wa Shilingi 174,316 msimu wa 2016/2017 hadi Shilingi 195,201 msimu wa 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 11.98 (*Kiambatisho Na.20*). Ongezeko hilo la bei ya



mchele linatokana na ongezeko la mahitaji kwa zao hilo ikilinganishwa na uzalishaji wake.

**154. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, bei ya jumla ya ng'ombe wa daraja la pili iliongezeka kutoka wastani wa Shilingi 1,074,431 mwaka 2017 hadi Shilingi 1,080,975 mwezi Februari 2018, sawa na ongezeko la asilimia 0.6. Bei ya ng'ombe wa daraja la tatu (3) iliongezeka kutoka Shilingi 806,490 mwaka 2017 hadi Shilingi 823,978 mwezi Februari 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.2 (*Kiambatisho Na. 21*). Katika mwaka 2018, ugavi wa mifugo iliyopelekwa katika minada umepungua ukilinganishwa na mwaka 2017. Hali hiyo imesababisha bei ya ng'ombe karibu kwa madaraja yote (isipokuwa madume daraja la II) kupanda. Kupungua kwa ugavi kumesababishwa na hali nzuri ya malisho ambayo imefanya wafugaji wengi kubaki na mifugo yao badala ya kuiuza. Aidha, malisho mazuri yamechangia katika kuongeza ubora na bei ya ng'ombe katika minada.

**b) Kuondoa Tozo zenye Kero, Ada Zinazojirudia na Kurazinisha Majukumu ya Taasisi za Udhibiti**

**155. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa andiko maalum la Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini linaloitwa *Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment for Tanzania*. Andiko hilo limeainisha sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazojirudia au kukinzana na hivyo kuongeza gharama za kufanya biashara nchini. Andiko hilo liko katika hatua ya maamuzi Serikalini na mapendekezo yake yataanza kutekelezwa mwaka 2018/2019.

**156. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini kupitia taasisi husika chini ya Wizara ambazo ni BRELA, FCC, TBS, TIC na WMA kwa kuongeza muda wa kufanya kazi hadi saa 24, siku 7 kwa wiki. Vilevile, taasisi hizo zimeendelea kutoa elimu kwa umma na kufanya vikao vya mara kwa mara na wadau ili kujadili utekelezaji wa majukumu yao.

**c) Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kuanzisha Vituo Maalum vya Kuuzia Mazao**

**157. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi Stakabadhi za Ghala na Halmashauri za maeneo yanayotekeleza Mfumo stakabadhi katika mwaka 2017/2018, imefikia makubaliano ya kuanzisha matumizi ya vituo maalum vya kuuzia mazao. Vituo hivyo vina lengo la kuwasaidia wakulima kudhibiti ubora wa mazao yao, kupata taarifa za masoko na kuimarisha ushindani wa bei.

**d) Kuhamasisha Ushindani Katika Ununuzi na Uuzaji wa Mazao**

**158. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha ushindani kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ambao umefanikisha uuzaji wa mazao kwa uwazi na hivyo kumpatia mkulima bei shindani. Kwa mfano, Mfumo umewezesha bei ya korosho kupanda na kufikia wastani wa Shilingi 3,880 kwa kilo msimu wa 2017/2018 ikilinganishwa na Shilingi 3,346 kwa kilo msimu wa 2016/2017. Aidha, mauzo ya korosho kupitia Mfumo huo yameongezeka kutoka tani 249,912 msimu wa 2016/2017 hadi tani 291,614 msimu wa 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 16.7.

**e) Kusimamia na Kuhimiza Matumizi ya Vipimo Rasmi**

**159. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhimiza matumizi ya vipimo rasmi katika biashara ikiwemo kwenye vituo vya kuuzia mazao vilivyopo katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuanzisha na kusimamia vituo vya kuuzia na kununulia mazao katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI ipo katika hatua za maandalizi ya Sheria Ndogo ya kusimamia matumizi ya vipimo rasmi katika biashara kwa lengo la kumlinda mlaji.

**f ) Kuimarisha Biashara na Masoko ya Mipakani**

**160. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika kuboresha utendaji wa Vituo vya Pamoja Mipakani (OSBP). Hadi sasa, vituo vimejengwa katika mipaka ya Holili/Taveta, Sirari/Isebania, Namanga/Namanga, Kabanga/Kobero, Rusumo/Rusumo, Mutukula/Mutukula na Horohoro/Lungalunga. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Pamoja Mipakani cha Tunduma/Nakonde upande wa Tanzania ulioanza mwezi Novemba 2016, unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2018. Hadi kufikia mwezi Februari 2018 ujenzi wa kituo hicho umefikia asilimia 75.

**g) Kutoa Elimu kwa Jamii ya Wafanyabiashara Kuhusu Fursa na Taratibu za Kufanya Biashara ya Mipakani (Cross Border Trade)**

**161. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na TanTrade, BRELA, WMA, SIDO, na OR - TAMISEMI imetoa mafunzo katika mikoa ya Kagera, Mara na Mbeya yaliyolenga kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi na kuvisajili kwa ajili ya kurasimisha biashara mipakani. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu ujasiriamali na vipimo, urasimishaji wa biashara na umuhimu wa wafanyabiashara kuungana katika vikundi. Mafunzo hayo yalifanyika kati ya mwezi Septemba na Disemba 2017. Jumla ya vikundi 44 vilianzishwa na kusajiliwa rasmi katika mikoa hiyo. Kazi hiyo itaendelezwa katika mikoa mingine ya mipakani.

**h) Kuhamasisha na Kuwezesha Wananchi Kutangaza Bidhaa na Huduma za Tanzania**

**162. Mheshimiwa Spika,** Wizara na Taasisi zake 14 zilishiriki Maonesho ya Wakulima (Nane Nane) mwezi Agosti 2017 mkoani Lindi kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu kazi na huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara na Taasisi zake. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa wajasiriamali katika kutoa ajira, kuhamasisha viwanda vidogo vidogo na kuongeza kipato, Wizara katika Maonesho

hayo ilidhamini vikundi 15 vya wajasiriamali. Wajasiriamali hao walikuwa ni wasindikaji wa mazao ya kilimo kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani ambao walipata fursa ya kutangaza bidhaa zao na kujifunza kutoka kwa washiriki wengine.

**163. Mheshimiwa Spika**, katika maonesho hayo, Wizara kupitia Bodi ya WRRB iliendesha mafunzo kuhusu Mfumo wa Stakabadhi kwa wakulima wapatao 198 na kwa viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika wa Masoko (AMCOS) zipatazo 85 kutoka katika Mikoa mbalimbali nchini. Mafunzo hayo yalilenga kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei nzuri ya mazao kwa kuuza katika mfumo rasmi; kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno; na kuwa na biashara ya mazao inayozingatia ubora na vipimo sahihi.

**i) Ushirikiano katika Masuala ya Biashara kati ya SMT na SMZ**

**164. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (SMT) na Wizara ya Viwanda na Biashara (SMZ) zimefanya vikao vya ushirikiano kujadili masuala ya kisekta ili kutafuta suluhu ya changamoto mbalimbali za ushirikiano. Vikao hivyo viliwezesha kupatikana kwa ufumbuzi wa masuala mbalimbali. Hivi sasa taasisi za TBS na ZBS zinatekeleza Mkataba wa Makubaliano ya kufanya kazi kwa pamoja katika kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuuzwa katika pande zote mbili. Aidha, TFDA na ZFDA zinafanya kazi kwa pamoja katika uthibiti wa bidhaa za chakula na dawa ili kulinda afya ya mlaji.

**j) Kuandaa na Kupitia Sera, Mikakati, Sheria na Kanuni Mbalimbali**

**i) Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji**

**165. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Taifa linakuwa na mfumo mahiri wa kumtetea na kumlinda mlaji,

Wizara imeanza maandalizi ya kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji. Mwezi Septemba 2017, wataalam walikutana na kuandaa mpango kazi wa kutekeleza kazi hiyo. Aidha, katika hatua za kutekeleza mpango kazi huo mwezi Februari 2018, timu imeanza kukusanya taarifa mbalimbali zitakazosaidia katika kuandika Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji na Mkakati wake.

***ii) Sera ya Taifa ya Viwango***

**166. Mheshimiwa Spika**, bidhaa za wazalishaji wengi nchini zimekuwa zikutana na vikwazo na hivyo kushindwa kukidhi matakwa ya soko la ndani na nje ya nchi. Katika jitihada za kukabiliana na changamoto hizo, Wizara kupitia TBS kwa kushirikiana na wadau wengine, imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ubora na Mkakati wake. Kukamilika kwa Sera hiyo itasaidia kutoa mwongozo wa usimamizi wa ubora na viwango vya bidhaa na huduma zinazotolewa kwa walaji. Vivyo hivyo, Sera hiyo itasaidia kuandaa mkakati na mipango mbalimbali ya mafunzo juu ya ubora kwa wazalishaji wadogo na wa kati. Katika kufanikisha jukumu hilo, Wizara imeunda kikosi kazi cha kuandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Ubora ambacho kimekusanya maoni yatakatotumika katika kuandaa Rasimu ya Sera hiyo.

***iii) Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu***

**167. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu na hivi sasa iko katika hatua za kujumuisha maboresho zaidi kufuatia maoni yaliyowasilishwa kutoka kwa wadau.

***iv) Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009***

**168. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekusanya maoni ya wadau kuwezesha marekebisha ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009. Hivi sasa, Wizara inafanya uchambuzi wa maoni hayo ili kukamilisha mapendekezo ya Sheria hiyo kwa kushirikisha taasisi husika.

v) ***Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999***

**169. Mheshimiwa Spika**, katika kuiwezesha COSOTA kutekeleza majukumu yake wakati ikisubiri marekebisho ya Sheria mama, Wizara imeandaa *Miscellaneous Amendments* katika baadhi ya vifungu vitakavyorahisha utendaji wa Taasisi hiyo katika kipindi cha mpito. Aidha, Wizara kupitia COSOTA na kwa kushirikiana na *Rulu Arts Promoters* kwa ufadhili wa *Best AC* ilikusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999. Mapendekezo hayo yapo katika hatua ya maamuzi.

vi) ***Kanuni za Sheria ya Vipimo ya Mwaka 2016***

**170. Mheshimiwa Spika** katika mwaka 2017/2018, Wizara iliunda timu ya wataalam kutoka Wizarani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakala wa Vipimo ili kupitia Kanuni za jumla za Vipimo (Weight & Measure General Regulation) za mwaka 2016. Lengo ni kuhakikisha kuwa Kanuni za Vipimo zinazingatia marekebisho ya Sheria mbalimbali yaliyofanyika na kugusa Sheria ya Vipimo. Marekebisho hayo yanalenga kuipa uzito Sheria hiyo kwa kuongeza adhabu ili iweze kuendana na wakati na uzito wa makosa husika. Pia iliangalia dosari nyingine za kisheria ili kuongeza ufanisi wa Wakala wa Vipimo.

vii) ***Kuandaa Sheria Ndogo ya Kusimamia Matumizi ya Vipimo Rasmi katika Biashara Ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Wilaya***

**171. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeandaa kikao cha wataalam kutoka Wizarani, Wakala wa Vipimo, TAMISEMI na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kitakachofanyika mwezi Mei 2018, ili kuandaa rasimu ya sheria ndogo kufuatia marekebisho yaliyofanywa katika Sheria ya Vipimo ya mwaka 2016. Lengo la sheria hizo ndogo ni kuimarisha usimamizi wa vipimo sahihi ili kumlinda mlaji. Aidha, baada ya kukamilisha

rasimu na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kingereza, vitafanyika vikao vya wadau kujadili rasimu ya Sheria hizo ndogo.

### **k) Kuelimisha Umma kuhusu Masuala ya Kibiashara**

**172. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya mikutano ya kazi kwa njia ya mtandao (Video Conference) na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa tarehe 18 hadi 20 Desemba, 2017. Mikutano hiyo iliandaliwa ili kuwafikia kwa pamoja na kwa gharama nafuu wadau muhimu wa ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini wakiwemo Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya na Maafisa Biashara. Nia ya mikutano hiyo ni kujenga uelewa wa pamoja wa utekelezaji wa sera na mikakati ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mikoa 19 ya Tanzania Bara kati ya Mikoa 25 ilifikiwa. Jumla ya wadau 530 walishiriki kwa mchanganuo ufuatao: Arusha (19), Dar es Salaam (19), Dodoma (18), Geita (6), Iringa (14), Kagera (31), Katavi (30), Kigoma(42), Kilimanjaro (64), Lindi (31), Manyara (29), Mbeya na Songwe (46), Morogoro (20), Mtwara (33), Mwanza (5), Pwani (15), Singida (58), Tabora (34) na Tanga (16).

#### **3.3.6 Huduma za Sheria**

**173. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imesimamia na kufuatilia mashauri ambayo Wizara na Taasisi zake zimeshitaki au kushitakiwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia imesimamia marekebisho ya Sheria na Kanuni za Wizara na Taasisi zake ikiwemo; marekebisho ya Sheria ya Leseni Tanzania ili kuhamisha jukumu la utoaji leseni Daraja "A" kutoka Wizarani kwenda BRELA; na Kanuni za Wakala wa Vipimo kuhusu gesi asilia na umeme. Aidha, imesimamia Mikatiba na Hati za Maelewano (MoU) mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara na Taasisi husika.

### 3.3.7 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

174. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kusimamia matumizi bora na sahihi ya miundombinu ya TEHAMA katika kutoa huduma kwa wateja wa ndani na nje. Miundombinu ya TEHAMA imeboreshwa na mafunzo mbalimbali yametolewa kwa watumishi kuhusu matumizi bora na sahihi ya miundombinu na rasilimali za TEHAMA. Aidha, Tovuti ya Wizara imehuishwa ili kuwapatia wananchi taarifa sahihi na kwa wakati na kuwawezesha kutoa na kupata mrejesho wa maoni au malalamiko juu ya huduma zinazotolewa na Wizara. Maboresho hayo yamehusisha uzinduzi wa barua pepe mahususi kwa ajili ya kuwapatia msaada wananchi/wawekezaji juu ya masuala yote yanayohusiana na Wizara, ambayo ni: [dawatilamsaaada@mit.go.tz](mailto:dawatilamsaaada@mit.go.tz) na [feedback@mit.go.tz](mailto:feedback@mit.go.tz).

### 3.3.8 Mawasiliano Serikalini

175. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2017/2018, Wizara iliendelea kuelimisha umma kuhusu majukumu na kazi zinazofanywa na Wizara. Aidha, Wizara iliweza kutoa taarifa mbalimbali za kisekta kwa wadau ikiwemo fursa mbalimbali zinazojitokeza ili wananchi waweze kuzichangamkia.

### 3.3.9 Udhhibiti wa Matumizi

176. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na sheria, miongozo na kanuni zilizowekwa na kuwezesha kupata hati safi ya hesabu za mwaka 2016/2017. Pia, Wizara iliendesha mafunzo ya usimamizi wa vihatarishi (risk management) kwa watumishi wake pamoja na kuanzisha daftari la kusajili vihatarishi (risk Register) na hivyo kuweza kupanga mipango yake kwa kuzingatia maeneo yenye vihatarishi. Aidha, Wizara imefanikisha kuhakiki na kutoa ushauri katika taasisi zilizoko chini yake zikiwemo SIDO, FCT na WRRB na kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kulingana na taratibu, kanuni na miongozo waliyojiwekea na hivyo kuweza kupata hati safi za ukaguzi.



### 3.3.10 Usimamizi wa Ununuzi

**177. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali za ununuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011(iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016) na kanuni zake za mwaka 2013, GN 446. Katika mwaka 2017/2018, Wizara iliandaa Mpango wa Ununuzi na kusimamia utekelezaji wake. Pia iliandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi na kila robo ya mwaka na kuwasilishwa kwa Taasisi ya kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA). Aidha, Wizara ilihakiki mali zake na kufanikisha uhuishaji wa daftari la Mali za Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

### 3.3.11 Maendeleo ya Rasilimali Watu na Utoaji wa Huduma

#### a) Ajira za Watumishi

**18. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ikama iliyoidhinishwa mwaka 2017/2018, Wizara inapaswa kuwa na watumishi 249. Hadi kufikia Machi 2018, Wizara ina Watumishi 233, kati ya hao Viongozi ni 5, Wachumi 49, Watakwimu 14, Wahandisi 4, Maafisa Tawala 6, Maafisa Utumishi 3, Maafisa Sheria 4, Maafisa TEHAMA 6, Maafisa Ugavi 6, Maafisa Biashara 67, Maafisa Habari 2, Wakaguzi wa Ndani 5, Wahasibu 15, Wasaidizi wa Maktaba 2, Wasaidizi wa Kumbukumbu 11, Fundi Sanifu 2, Makatibu Mahsus 17, Wasaidizi wa Ofisi 5, Opereta wa Kompyuta 1 pamoja na Madereva 9.

**179. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2017/2018, Wizara imeajiri madereva 2, Katibu Mahsus 2, Afisa TEHAMA 1 na Opereta wa Kompyuta 1 na kuwapandisha vyeo watumishi 16 ambao tayari walikuwa wamekasimiwa kwa mwaka 2016/2017. Aidha, zoezi la upandishaji vyeo limefanyika baada ya Serikali kuruhusu utekelezaji wa utoaji ajira mpya, ajira mbadala pamoja na masuala yote yanayohusisha marekebisho ya mishahara yanayotokana na upandishwaji vyeo kwa watumishi.

**b) Mafunzo**

**180. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara iliandaa Mpango wa Mafunzo wa muda wa mwaka mmoja ili kuwajengea watumishi uwezo na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Mpango huo ullenga kuwapeleka watumishi 15 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 50 katika mafunzo ya muda mfupi. Hadi kufikia Aprili 2018, Wizara imepeleka watumishi 14 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 16 katika mafunzo ya muda mfupi, ndani na nje ya nchi.

**c) Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi**

**181. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, watumishi 222 kati ya 241 wamesaini mikataba yao ya kazi kwa wakati na kufanya mapitio ya nusu mwaka mwezi Desemba 2017. Watumishi 14 hawakuweza kusaini mikataba yao kwa kuwa wapo masomoni. Aidha, kufikia mwisho wa mwezi Juni 2018 kila mtumishi wizarani atafanyiwa tathmini ya utendaji wake wa kazi kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kutumia utaratibu wa MWAMTUKA.

**d) Michezo na Afya za Watumishi**

**182. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018 katika kutekeleza dhana ya michezo kwa afya, furaha na ufanisi kazini, Wizara imeshiriki katika bonanza lililohusisha washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi. Lengo la kushiriki michezo hiyo ilikuwa ni kujenga afya za watumishi kupitia mazoezi na michezo na kujenga uhusiano mzuri miongoni mwa watumishi na wadau wa sekta binafsi. Aidha, Wizara imeendelea kuwahimiza watumishi kujenga tabia ya kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao na kujikinga na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) yanayoweza kuepukika kama vile, uzito uliopitiliza, shinikizo la damu na kisukari.

**e) Baraza la Wafanyakazi**

**183. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuwashirikisha watumishi katika vikao

vya maamuzi kupitia Baraza la Wafanyakazi ili waweze kutetea maslahi yao na kuwasilisha mawazo yao. Wizara imefanya kikao kimoja cha Baraza la Wafanyakazi tarehe 6 Aprili, 2018 ambapo lilipitia, kushauri na kuridhia mapendekezo ya Mipango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na kupokea hoja za watumishi na kuzifanyia maazimio ya utekelezaji.

**f) Kuhamia Makao Makuu Dodoma**

**184. Mheshimiwa Spika**, kufuatia agizo la Serikali la kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Nchi Dodoma, Wizara ilipanga kuhamisha watumishi katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ilipanga kuhamisha Watumishi 94, awamu ya pili 69, na awamu ya tatu 70. Aidha, kila awamu inahusisha kuhamisha vifaa na mifumo ya utendaji ikiwemo Mifumo ya Mitandao ya Kompyuta. Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, Wizara imewahamisha watumishi 163. Wizara inatarajia kuwahamisha watumishi 70 waliosalia ifikapo mwezi Agosti 2018.

**3.3.12 Masuala Mtambuka**

**a) Kupambana na Rushwa**

**185. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara imeendeleza jitihada za mapambano na udhibiti wa rushwa kwa kuwaelimisha na kutoa maelekezo kwa watumishi wake kutoa huduma bora kwa wateja wa ndani na nje bila kupokea rushwa. Aidha, wizara imeongeza msisitizo kwa watumishi kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais za kupinga vitendo vya rushwa kwa kutekeleza wajibu wao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

**186. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliitisha kikao cha wadau wa ndani tarehe 28 Septemba, 2017 kwa ajili ya kupokea maoni na maandalizi ya Mpango Mkakati wa Wizara katika kupambana na kuzuia rushwa. Aidha, Wizara ilifanya kikao tarehe 28 na 29 Novemba, 2017 ili kuandaa mpango kazi wa kutekeleza Mkakati wa Taifa Awamu ya

Tatu wa Kupambana na Kuzuia Rushwa. Mpango kazi huo umekamilika.

**b) Usimamizi wa Mazingira**

**187. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara imeshiriki katika shughuli mbalimbali za utunzaji mazingira na kuzuia uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli za viwanda hasa viwanda vya saruji na chuma. Aidha, Wizara imeshiriki katika tathmini ya athari za mazingira kwa viwanda vipya vinavyoanzishwa nchini kwa kushirikiana na NEMC.

**c) Mapambano ya UKIMWI**

**188. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi watatu (3) wenye maambukizi ya VVU na waliojitokeza kwa kuwapa posho ya lishe, usafiri na virutubisho ili kuwaweka katika hali ya afya bora na kudumu zaidi kwenye utumishi wa umma. Aidha, kupitia michezo Wizara imetoa fursa kwa watumishi wake wote kuimarisha afya zao kwa njia ya kufanya mazoezi na pia kutoa ujumbe wa umuhimu wa mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na magonjwa sugu yasiyoambukiza.

**d) Masuala ya Jinsia**

**189. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara ilishiriki warsha ya mapitio ya utekelezaji wa sheria ya uondoaji wa vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru pamoja na kutoa maoni katika sheria hiyo ambayo ipo katika rasimu ya awali. Warsha hiyo iliandaliwa na TGNP mtandao kupitia Mfuko wa AWDF kwa kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Usimamiaji na Uondoaji Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru tarehe 8-9 Februari, 2018 Dar es Salaam. Lengo la warsha lilikuwa kuhakikisha sheria zinazoandaliwa zinajumuisha masuala ya jinsia na urahisishaji biashara ndani na nje ya nchi.

**190. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki mkutano wa kikanda uliofanyika nchini Uganda tarehe 24 Januari, 2018. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni ushirikishwaji wa wanawake wafanyabiashara mipakani katika uandaaji wa sera mbalimbali za masuala ya biashara. Aidha, Wizara ilishiriki kwenye kikao tarehe 23 Februari, 2018 cha uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa Itifaki ya Maendeleo ya Jinsia ya mwaka 2008 na kutoa mchango wake katika kipengele cha 17 (Economic Empowerment) na 18 (Access to property and resources) cha Itifaki hiyo.

**191. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki mafunzo ya kuzingatia masuala ya kijinsia katika biashara za mipakani kuanzia tarehe 6-7 Februari, 2018. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo washiriki namna ya kuwasaidia wanawake wafanyabiashara mipakani kufanya biashara zao kwa ufanisi na kufuata utaratibu wa biashara. Mafunzo hayo yaliandaliwa na TGNP Mtandao kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake wa Afrika (AWDF).

**192. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeshiriki katika kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA- VAWC 2017/2018 – 2021/2022) uliofanyika tarehe 16-17 Februari, 2018. Mpango huo utasaidia ufuatiliaji wa matokeo ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kupata taarifa za kimkakati zitakazotumika katika kufanya uamuzi kuanzia ngazi ya Taifa. Aidha, viashiria vimeandaliwa katika kila eneo la utekelezaji na *baseline survey* inatarajiwa kufanyika ili kukusanya takwimu ambazo zinakosekana kwenye baadhi ya viashiria.

### 3.4 UTEKELEZAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

#### 3.4.1 Shirika la Maendeleo la Taifa

##### a) Kuanzisha Mgodini wa Mawe wa Kuzalisha Kokoto

**193. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kwa kushirikiana na TRC inafanya juhudi za kumpata mwekezaji katika mradi wa mgodi wa mawe katika Kijiji cha

Muhamba, Wilaya ya Muheza ambapo kampuni kadhaa zimeonesha nia ya kuwekeza. Aidha, NDC na TRC zimeendelea kuhakikisha kwamba leseni za kumiliki eneo la Mgodini wa Mawe lililoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza zinalipiwa wakati taratibu za kupata Hati ya Umiliki zinaendelea. Vilevile, NDC na TRC kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji cha Muhamba zinaendelea kuhifadhi eneo la mgodi ili lisivamiwe.

**194. Mheshimiwa Spika**, Majukumu mengine yaliyotekelezwa na taasisi hii yameanishwa katika utekelezaji wa miradi mama na ya kielelezo chini ya utekelezaji wa Sekta ya Viwanda.

### **3.4.2 Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi**

#### **a) Kuendeleza Eneo Maalum la Uwekezaji la Kurasini**

**195. Mheshimiwa Spika**, katika eneo la *Kurasini Trade Logistic Centre* hatua iliyofikiwa ni kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekamilisha uthamini wa nyumba tatu ambazo hazikuthaminiwa awali ambapo Shilingi 441,295,000 zitahitajika kwa fidia hiyo. Malipo hayo yatafanyika mara baada ya kupokea fedha kutoka Serikalini. Kazi za upimaji wa maeneo imefanyika na ukamilishaji wa ramani ya mipango miji sambamba na taratibu za upatikanaji wa hati ya eneo hilo uko hatua za mwisho. Aidha, timu ya wataalam ya kushauri njia bora za kutekeleza mradi imekamilisha kazi yake na imeshauri uendelezaji wa eneo hilo kwa kuhusisha ujenzi wa viwanda (light industries) utakaoambatana na maghala ya kutunzia mizigo.

#### **b) Uendelezaji wa Mradi wa Bagamoyo SEZ**

**196. Mheshimiwa Spika**, majadiliano kuhusu uendelezaji wa Eneo la Uwekezaji la Bagamoyo (Bagamoyo SEZ) linalohusu ujenzi wa bandari na eneo la viwanda (*Portside Industrial Zone*) yanaendelea. Majadiliano hayo

yanatumia andiko lililoandaliwa na wawekezaji (CMPort na SGRF) na kuridhiwa na Serikali mwezi Oktoba 2017 kama msingi wa majadiliano. Lengo la majadiliano hayo ni kupata namna nzuri zaidi ya kushirikiana katika kutekeleza mradi huo kwa manufaa ya pande zote (Serikali ya Tanzania na Wawekezaji). Makubaliano ya awali yamefikwa na hatua inayofuata ni majadiliano ya kina ya mikataba yanayotegemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2018. Mbali na wawekezaji waliotajwa hapo juu, makampuni mengine 12 yamepewa leseni kwa ajili ya kujenga viwanda katika eneo la Bagamoyo SEZ lililokwisha lipiwa fidia nje ya eneo lililotolewa kwa CMPort na SGRF.

**197. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya EPZ inashirikiana na Serikali ya Korea Kusini kupitia programu ya *Knowledge Sharing Program* (KSP) na *Korea Exim Bank* kuendeleza kituo cha teknolojia ya juu kitakachojengwa katika eneo la mradi wa Bagamoyo SEZ. Mshauri mwelekezi kutoka chuo cha *Science and Technology Policy Institute* (STEPI) amefanya sehemu ya kwanza ya Stadi ya mradi kwa lengo la kupata uelewa mpana wa mradi na kuishauri Mamlaka ya EPZ kuhusu *Masterplan* ya Mradi iliyoandaliwa na Kampuni ya *Voyant Solutions Pvt* kutoka India. Aidha, STEPI kitaishauri *Korea Exim Bank* kuhusu gharama za ujenzi wa miundombinu wezeshi katika eneo la mradi. Benki hiyo imeonesha nia ya kusaidia kiasi cha Shilingi Bilioni 40.

**198. Mheshimiwa Spika;** Mamlaka ya EPZ inaendelea na maandalizi ya kutekeleza Makubaliano ya Awali (MoU) yaliyofikiwa baina yake na SNTL GROUP (SNTL) ya Morocco kuhusu uendelezaji wa maeneo ya maalum ya uwekezaji. Makubaliano hayo yalifikiwa mwezi Oktoba, 2016 wakati wa ziara ya Mfalme wa Morocco nchini Tanzania. Mamlaka ya EPZ inakamilisha *Project Portfolio* itakayokuwa msingi wa mazungumzo yatakayofikia hatua ya kuingia mkataba wa kushirikiana kuendeleza maeneo kadhaa ya SEZ kama *Industrial Parks* na *Trade and Logistics Centre*.

**199. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefikia hatua nzuri katika kutekeleza Mpango wa Maboresho ya Kituo cha

Huduma kwa Wawekezaji, *One Stop Services Centre* na mifumo mbalimbali ya taasisi. Taasisi ya *TradeMark East Africa* (TMEA) imeidhinisha pendekezo la taasisi kuhusu msaada wa kitaalam na fedha katika kuboresha mifumo mbalimbali ya taasisi kwa kutumia TEHAMA. Pia, Mamlaka ya EPZ inashirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) katika kuandaa Programu ya Usalama wa Maji (Water Security Program) ambayo itawahakikishia wawekezaji uwepo wa maji muda wote na katika ubora unaokubalika kimataifa. Utekelezaji wa Programu hiyo unatarajiwa kuwavutia wawekezaji wengi katika maeneo ya EPZ na SEZ.

**200. Mheshimiwa Spika;** Mamlaka ya EPZ imeendelea kuwashirikisha waandishi wa habari wa TV na magazeti katika kutembelea viwanda na maeneo maalum ya uwekezaji ili kutangaza kwa usahihi shughuli za uwekezaji zilizopo chini yake. Kupitia utaratibu huo, habari, vipindi na makala maalum zipatazo 42 zilitolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari vya *TBC1, ITV, Azam TV, Clouds TV, Channel Ten, Mwananchi, Citizen, The Guardian, Daily News* na kwenye tovuti ya Idara ya Habari Maelezo. Vile vile, maafisa waandamizi wa EPZA wamekuwa wakishiriki mijadala katika vipindi vya televisheni na radio ili kuelezea dhana ya viwanda na maeneo maalum ya uwekezaji. Juhudi hizo zitaendelea kadri miradi mipya itakapokuwa inaanzishwa ili kufikisha elimu na taarifa kwa umma kuhusu miradi hiyo na fursa ambazo watazania na wawekezaji kutoka nje ya nchi wataweza kunufaika nazo.

**201. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha utoaji wa taarifa sahihi kuhusu miradi, EPZA imekuwa ikifuatilia habari za kisekta na kitaasisi zinazotolewa na vyombo mbalimbali. Lengo ni kuitumia vizuri fursa ya uwepo wa waandishi ambao kwa juhudi zao wenyewe wamekuwa wakiandika habari mbalimbali kuhusu viwanda ama miradi iliyo chini ya Mamlaka ya EPZ. Mbinu hiyo imewezesha kuchapishwa kwa makala maalum saba (7) kuhusu bidhaa na viwanda vilivyo chini ya maeneo maalum ya uwekezaji. Pia, juhudi za kutangaza shughuli zote zilizo chini ya Mamlaka zimeendelea kutangazwa kupitia tovuti yake [www.epza.go.tz](http://www.epza.go.tz) ambayo



imekuwa msaada mkubwa kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi

### **3.4.3 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania**

#### **a) Kutoa Huduma za Kitaalam Viwandani**

**202. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) limeendelea kushirikiana na *TIB Development Bank* katika kazi mbalimbali ikiwemo uanzishwaji wa kiwanda cha bidhaa za pamba za mahospitali (Cotton based medical products) na kiwanda cha kuzalisha maji ya dripu za mahospitali (IV fluid Industry) katika Mkoa wa Simiyu. Miradi hiyo iko chini ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF). Vilevile, Shirika limefanya kazi na Benki ya CRDB katika kutoa ushauri wa kitaalam na kiufundi inayohusu mikopo ya wanaoanzisha na kuendeleza viwanda ikiwemo Kiwanda cha Mabomba kilichopo Vingunguti Dar es Salaam, Kiwanda cha Nyama Sumbawanga, Kiwanda cha *Ceramics* kilichopo Same na Kiwanda cha *Kahama Oil Mills* kilichopo Shinyanga. Pia TIRDO ni mshauri kiongozi (lead consultant) katika Mradi wa Kuboresha Kiwanda cha Viatu cha Gereza la Karanga lililoko mjini Moshi Kilimanjaro.

**203. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kufufua viwanda vilivyoacha uzalishaji, Shirika limefanya ukaguzi wa kitaalam (technical audit) katika Kiwanda cha SAAFI, Kiwanda cha Magunia cha Canvas Morogoro, na Kiwanda cha Nguo Ibadakuli – Shinyanga na kushauri namna bora ya ufufuaji wa viwanda hivyo. Pamoja na shughuli hizo, Shirika limeendelea kutoa huduma za upimaji wa uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za uzalishaji viwandani na kutoa ushauri. Viwanda vilivyopatiwa huduma ni pamoja na *Tanzania Cigarette Company*-Dar es salaam, *Tanzania Tobacco Processors Ltd*-Morogoro, *Premium Active Tanzania Ltd*- Mbeya, na *Tanga Cement Company* -Tanga. Pia maabara imeendelea kutoa huduma za mazingira kwa taasisi mbalimbali zikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Shirika la Viwango Tanzania.

b) **Kuanzisha na Kuhakiki Maabara ya Makaa ya Mawe, Mafuta na Gesi**

**204. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kuimarisha maabara zake kwa kuhakiki maabara za makaa ya mawe na uanzishwaji na uhakiki wa maabara ya mafuta na gesi ili kufikia viwango vya kimataifa. Maabara ya makaa ya mawe imekwishaanza kufanya kazi mbalimbali za upimaji wa ubora wa makaa ya mawe kwa wateja mbalimbali kama vile STAMICO, *Magamba Coal Ltd*, na *Tancoal Energy Ltd*. Hata hivyo, jitihada zinaendelea kufanyika ili maabara hiyo ipate vifaa vya kutosha ili kuweza kuhakiki na kukidhi vigezo vya kimataifa. Aidha, jitihada zinaendelea kufanyika za kuanzisha maabara ya mafuta na gesi.

c) **Kuanzisha na Kuboresha Maabara**

**205. Mheshimiwa Spika**, katika maabara ya mazingira, Shirika limewasilisha maombi ya usajili kwa Mamlaka ya Uhakiki (SADCAS). Shirika linaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya upimaji stadi (proficiency testing). Kwa upande wa maabara ya vifaa vya kihandisi (NDT), Shirika limeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua vifaa na kuendelea na uhakiki wa maabara hiyo. Aidha, Shirika limeandaa na kuwasilisha kwa wafadhili mbalimbali andiko kwa ajili ya kutafuta fedha za kuanzishia Maabara ya Vipimo vya Chuma Kigumu (Iron and Steel).

**3.4.4 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini**

a) **Kujenga Uelewa na Kuhamasisha Jamii kuhusu Umuhimu wa Kununua Zana za Kilimo zilizofanyiwa Majaribio Nchini**

**206. Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) kimeandaa Kanuni za Majaribio ya Zana za Kilimo ambazo zimechapishwa kwenye Gazeti la Serikali Tarehe 23 Februari 2018. Kupitia vyombo mbalimbali vya habari vya Televisheni, Radio, Magazeti na Mikutano, Kituo kimewaelimisha wadau kuhusu umuhimu wa vifaa vyao kufanyiwa majaribio kabla ya kuviuza kwa wateja. Aidha, Kituo kimetenga bajeti kwa ajili ya kuanzisha vituo vya ukaguzi na majaribio katika maeneo muhimu na pia

kuwasaidia wazalishaji wa ndani kuzifanyia majaribio na kukagua zana za kilimo wanazozialisha. Hatua hiyo ni sehemu ya kufanikisha mpango wa kujenga uelewa na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kufanyia majaribio zana za kilimo.

**b) Kutafiti Mahitaji, Kuendeleza na Kutengeneza Teknolojia mbalimbali za Kilimo**

**207. Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), kimefanya utafiti wa mahitaji na hali ya matumizi ya teknolojia za kilimo katika mikoa 12 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Njombe, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora. Matokeo yanaonesha kuwa, asilimia kubwa ya wakulima katika mikoa hiyo wanahitaji teknolojia za kupandia mazao mbalimbali ikifuatiwa na teknolojia za kupalilia, kupura na kupepetua mazao ya nafaka. Vile vile imebainika kuwa, wakulima wengi katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti bado wanatumia teknolojia duni kufanya shughuli za kilimo. Hali hiyo inatokana na ukosefu wa taarifa za uwepo wa teknolojia zinazoweza kuwasaidia kurahisisha shughuli za kilimo, ugumu wa upatikanaji wa teknolojia za kilimo katika maeneo yao na pia uwezo mdogo wa kifedha wa kumudu kununua teknolojia hizo.

**208. Mheshimiwa Spika,** Kituo kimeendelea na ukamilishaji wa trekta 5 na uboreshaji wa trekta 4 aina ya CFT 221 (CAMARTEFastrucktor-221). Maboresho yanafanyika kwenye mfumo wa kuinua jembe, mfumo wa kuongoza na kushikilia jembe lisiyumbe wakati wa kulima. Trekta tatu (3) kati ya nne (4) zimeboreshwa na kutumika kulima mashamba ya wakulima kwa majaribio katika eneo la Lake Tatu, USARIVER katika Wilaya ya Arumeru. Katika msimu huu wa kilimo, trekta hizo zimelima jumla ya ekari 120, ambapo ufanisi wake ni wastani wa ekari 3-4 kwa siku, kutegemea aina ya udongo.

**209. Mheshimiwa Spika,** ili kurahisisha upandaji wa zao la pamba kwa mstari na kwa nafasi sawa, CAMARTEC

imefanya utafiti wa kipandio cha mbegu za pamba kinachokokotwa na ng'ombe na kufanikiwa kuunda vipandio 50 kwa ajili ya wakulima wa Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu ambao wanafadhiliwa na Kampuni ya *bioRE Tanzania Ltd*. Vile vile, kwa kushirikiana na mjasiriamali anayemiliki Kampuni ya *Elmi Farm Implement Manufacturer* iliyoko mjini Kateshi, CAMARTEC imeweza kufanya majaribio na kuboresha Kipandio kinachovutwa na trekta kilichobuniwa na kutengenezwa na mjasiriamali huyo baada ya kubaini mapungufu katika mfumo wake wa kudondosha mbegu (Seed metering system). *Seed metering systems* 100 ziliagizwa kutoka China kwa ajili ya kuzifunga kwenye kipandio hicho na nyingine kuendelea kutumika kufanya utafiti wa vipandio vingine. Kituo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, kimeendelea kufanya utafiti wa *Solar Dryer* isiyoathiri virutubisho na rangi ya vitu vinavyokaushwa. Vilevile, CAMARTEC inaendelea kufanya utafiti wa teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na zinazohusiana na matumizi ya nishati ya *biogas*, kupalilia mpunga, kuandaa malisho ya wanyama, kupura na kupepete mazao ya nafaka.

**c) Kutafiti na Kuendeleza Usambazaji wa Teknolojia za Matumizi Bora ya Nishati**

**210. Mheshimiwa Spika**, CAMARTEC imeshirikiana na *Tanzania Breweries Ltd*-Arusha (TBL) kufanya utafiti wa matumizi ya chachu (yeast extract) katika uzalishaji wa *biogas*. Matokeo ya awali yameonesha kuwa, kiwango cha *biogas* kinachozalishwa kimeongezeka na pia kiwango cha joto kwenye *biogas* inayowaka kimeongezeka kutokana na kupungua kwa kiwango cha gesi zisizohitajika. Hivyo, wastani wa tani 2 za chachu ambazo huzalishwa kwa siku zitaweza kutumika moja kwa moja kulisha mitambo midogo ( $6m^3$ ) kati ya 32 hadi 48 na kuwanufaisha wananchi wanaozunguka maeneo hayo kuzalisha *biogas* au zitatumika na wafugaji kwa kuchanganya chachu hiyo na kinyesi cha ng'ombe ili kuharakisha na kuongeza uzalishaji wa *biogas*. Vilevile, Kituo kwa kushirikiana na *University of Nottingham* (UoN), ECHO (Arusha) na *Creative Energy* kutoka Uingereza kimeendelea kufanya utafiti unaohusisha matumizi ya kifaa

maalum (sensor) katika kutambua utendaji wa mtambo wa *biogas* hata bila kufika kwenye mtambo husika. Aidha, taarifa zitakazopatikana kupitia kifaa hicho zitatumika kuwashauri wakulima njia bora ya kurekebisha mtambo bila kufika huko na hivyo kupunguza gharama ambazo zingetumika kuitembelea mitambo hiyo ili kukagua utendaji wake.

**211. Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC kwa miaka zaidi ya 35, imekuwa mstari wa mbele kwenye utafiti na usambazaji wa teknolojia ya nishati mbadala ya kupikia na majiko banifu. Katika mwaka 2017, CAMARTEC kupitia mafundi iliyowafundisha sehemu mbalimbali hapa Tanzania, imefanikisha ujenzi wa mitambo ya *biogas* (biogas plants) ngazi ya kaya 198 yenye thamani ya Shilingi milioni 336. Kwa wastani, asilimia 14 ya fedha hizo ni ruzuku kutoka Serikali ya Tanzania kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na asilimia 86 ni fedha zilizowekezwa na wananchi wenyewe na wadau wengine wa maendeleo. Kwa mfano, *HEIFER International* imejenga jumla ya mitambo ya *biogas* 32 ya ngazi ya kaya. Kati ya hiyo, mitambo 22 imejengwa kupitia miradi yake ya *Igunga Eco Village* iliyoko katika Kata za Mbutu na Igunga, Wilayani Igunga, Mkoa wa Tabora na mitambo 10 imejengwa kupitia mradi wake wa *Mbozi Farmers Livelihood Improvement* ulioko katika Kata za Igamba na Isansa, wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe.

**212. Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mitambo ya *biogas* kwa mikoa ni kama ifuatavyo: Arusha (21), Dar-es-Salaam (5), Geita (1), Kilimanjaro (45), Manyara (7), Mara (5), Mbeya (20), Njombe (3), Pwani (3), Shinyanga (1), Simiyu (9), Singida (1), Songwe (10), Tabora (56) na Tanga (10). Ujenzi wa mitambo hiyo umetoa ajira za moja kwa moja za kudumu na za muda kwa Kampuni za *biogas* 22, mafundi 44 na vibarua zaidi ya 200.

**213. Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC kupitia Mradi wake wa *Tanzania Domestic Biogas Programme* (TDBP) unaofadhiliwa na *Africa Biogas Partnership Programme* (ABPP) imeshirikiana na Shirika la SNV kupitia Mradi wake wa *SNV Sustain* ulioko Sumbawanga kutoa mafunzo ya ujenzi

wa mitambo ya *biogas* kwa vijana 32. Kwa upande wa majiko banifu, Kampuni zilizozalisha kutokana na teknolojia ya CAMARTEC zimeendelea kusambaza majiko na sufuria katika sehemu mbalimbali za Tanzania. Kwa mwaka 2017, majiko na sufuria takriban 700 yenye thamani inayokadiriwa kufikia Shilingi bilioni 1 yalitengenezwa na kusambazwa. Majiko na sufuria hayo yanatumika zaidi kwenye shule za sekondari, vyuo, magereza na hospitali na yamesaidia kupunguza matumizi ya kuni kutoka malori 1,300 mpaka 450 kwa mwaka. Biashara hiyo kwa mwaka 2017 imeweza kutoa ajira za moja kwa moja za muda na za kudumu kwa zaidi ya wajasiriamali na wafanyabiashara 42 na vibarua zaidi ya 150. Hii ina maana kwamba, biashara ya majiko banifu ni kubwa zaidi kwani kuna wajasiriamali wengine walioko nje ya eneo la Kanda ya Kaskazini wanaofanya biashara kama hiyo, ingawa kwa asilimia kubwa majiko hayo yanatengenezwa na kusambazwa kutokea Arusha.

#### **d) Kuhamasisha Usambazaji wa Teknolojia Zinzobuniwa na Taasisi**

**214. Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC imeendelea kutafiti na kusambaza teknolojia za matumizi bora ya nishati ya kuni, mkaa na *biogas* kwa kushirikiana na wajasiriamali, makampuni binafsi, mafundi, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na wadau wetu wa maendeleo ambao ni *Africa Biogas Partnership Programme* (ABPP). Kuhusu ujenzi wa mitambo ya *biogas*, Kituo kilijenga mitambo 52 midogo ngazi ya kaya na mitambo 3 ya ngazi ya jumuiya katika maeneo ya Shule ya Msingi Emboreti katika Mkoa wa Manyara na Shamba la Nyabirezi katika Mkoa wa Geita. Ukarabati wa mitambo miwili ulifanyika katika Shule ya Sekondari Inyonga, Masasi na Shule ya Sekondari ya Wasichana, Tabora. Aidha, mafunzo ya utumiaji na utunzaji wa mitambo ya *biogas* yalifanyika maeneo ya Arusha, Shule ya Sekondari Inyonga, Masasi na Shule ya Sekondari ya Wasichana, Tabora ambapo zaidi ya watu 51 walipata mafunzo hayo.

### 3.4.5 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania

#### a) Kujenga Uwezo wa Taasisi katika Kubuni, Kuendeleza na Kusambaza Teknolojia

215. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) limefanikiwa kutoa mafunzo ili kuongeza ujuzi katika utendaji kazi kwa wafanyakazi zaidi ya kumi katika nyanja za ubora wa bidhaa, uzalishaji, CAD/CAM, usimamizi wa biashara ya kimataifa na ubunifu. Mafunzo hayo yalienda sambamba na maboresho ya karakana ya Taasisi kwa kupata na kusimika mashine mpya tano kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Uendelezaji wa Viwanda (UNIDO). Mashine hizo ni: *computerized plasma cutting machine; computerized tensile testing machine; computerized hardness tester; computerized material analyzer na semi-automatic spot welding machine.*

#### b) Kuboresha, Kuendeleza na Kuhamasisha Utengenezaji na Utumiaji Kibiashara wa Mitambo

216. *Mheshimiwa Spika*, usanifu, uendelezaji na utengenezaji wa mashine tatu za kuchakata bidhaa za marumaru umekamilika. Mashine hizo ni za kufyatua matofali ya kuhifadhi joto (refractory bricks), mashine ya kusaga udongo na mashine ya kuchekecha. Majaribio ya mashine hizo yanaendelea kwa kutumia malighafi za udongo unaopatikana nchini. Baada ya majaribio hayo na uhakiki wa ubora wake Shirika litaitangaza kupitia SIDO au kampuni binafsi zitakazojitokeza ili zikalishwe kibiashara. Kuhusu mafuta yatokanayo na mbegu za alizeti, wataalam wa TEMDO wametembelea na kushauriana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuwahamasisha kutumia teknolojia zilizobuniwa. Mwitikio ni mzuri na kwa sasa mipango inafanyika ili kufunga mitambo hiyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondo na mtaa wa viwanda, SIDO mkoani Singida.

#### c) Kubuni na Kuendeleza Teknolojia Jadidifu

217. *Mheshimiwa Spika*, uendelezaji na utengenezaji wa chasili cha mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na

nguvu za maji uitwao *Crossflow Turbine* na usanifu wa mtambo wa kuzalisha umeme unaotokana na nguvu za maji uitwao *Reverse Pump Turbine* umekamilika. Aidha, taarifa muhimu kuhusu aina ya makaa ya mawe yapatikanayo nchini na teknolojia zitakazotumika kutengeneza brikwiti za makaa ya mawe (*Coal dust briquettes*) zitakazotumika kupikia zimekusanywa. Taarifa muhimu za usanifu na utengenezaji wa mtambo huo zimekusanywa na usanifu umeanza. Inategemewa kuwa tafiti hizo zikikamilika na kutumika vizuri zitasaidia zaidi kupata nishati mbadala itakayosaidia kupunguza matumizi ya kuni na hivyo kutunza mazingira.

#### **3.4.6 Kampuni ya Mbolea Tanzania**

**218. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), imesimamia uingizaji na usambazaji wa mbolea za aina mbalimbali hapa nchini. Katika kipindi hicho, TFC imefanikiwa kusambaza mbolea tani 5,720 katika mikoa yote ya Tanzania Bara inayojumuisha aina ya DAP tani 1,800, UREA tani 3,000, SA tani 670 na CAN tani 250. Katika mtandao wa usambazaji wa mbolea nchini, Kampuni ya TFC ina maghala katika mikoa saba na imekodi maghala mengine saba katika mikoa mingine na hivyo kuwa na maghala katika mikoa 14 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 95,500 za mbolea kwa wakati mmoja.

#### **3.4.7 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo**

**a) Kujenga Maeneo ya Viwanda katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara na Simiyu**

**219. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limeendelea na ujenzi wa miundombinu ya ofisi na majengo (industrial sheds) ya kuendeshea miradi ya ujasiriamali. Ujenzi umeanza katika mikoa ya Geita, Kagera na Simiyu chini ya Mkandarasi - SUMA JKT. Aidha, mikataba ya ujenzi katika mikoa ya Dodoma, Katavi, Manyara na Mtwara imekwisha sainiwa na kazi ya ujenzi itaanza wakati wowote.

**b) Kusajili Viwanda Vidogo Nchini**

**220. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Shirika limehamasisha na kufanikisha kusajiliwa viwanda



vidogo 429 katika mikoa yote nchini kupitia BRELA na kupewa leseni na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo vilikoanzishwa.

**c) Kuimarisha Uwezo wa Uhawilishaji wa Teknolojia**

**221. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, teknolojia mpya 59 zilitambuliwa na kusambazwa. Mashine na zana za teknolojia hizo ziliwezesha kuanzishwa na kuimarisha shughuli za miradi 260 ya uzalishaji kote nchini. Teknolojia hizo zinahusu ubanguaji wa korosho; usindikaji wa mihogo; ukamuaji wa mafuta ya mawese; usindikaji wa vyakula; upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kama nishati; ufungashaji wa vyakula vilivyosindikwa; utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali; utengenezaji wa chokaa na chaki; utengenezaji wa sabuni; na usindikaji ngozi kwa njia za asili. Aidha, Shirika limewezesha utengenezaji wa mashine na zana 174 kwa ajili ya matumizi ya wajasiriamali wadogo mijini na vijijini. Teknolojia hizo zimesaidia kuimarisha na kuongeza ubora wa bidhaa za wajasiriamali.

**d) Kuwezesha Uanzishwaji wa Viwanda Vidogo**

**222. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Shirika limefanikisha uanzishwaji wa viwanda vipya vidogo vya aina mbalimbali 429 na kuzalisha ajira 1,287. Mafanikio hayo yametokana na huduma za kiufundi, ushauri, mafunzo, masoko na mikopo ilizozitoa kwa wajasiriamali. Aidha, maandiko 15 yaliandaliwa kwa ajili ya kuandaa miradi ya kuanzisha viwanda vidogo na vya kati chini ya Mkakati wa ODOP.

**e) Upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali kupitia NEDF**

**223. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, mikopo 1,948 yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.344 ilitolewa kupitia Mfuko wa NEDF ambapo asilimia 51 ya mikopo hiyo ilitolewa kwa wajasiriamali wanawake. Aidha, asilimia 42 ya mikopo ilitolewa kwa miradi ya vijijini. Mikopo hiyo

iliwezesha kupatikana ajira 4,438 zinazojumuisha wanaume 2,130 na wanawake 2,308.

### 3.4.8 Kituo cha Uwekezaji Tanzania

#### a) Uhamasishaji kwa Kuwalenga Wawekezaji wa Nje na Ndani

**224. Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilishiriki katika makongamano manne ya biashara na uwekezaji na kunadi fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Pia Kituo kiliwaalika wafanyabiashara mbalimbali na kushirikisha taasisi za umma katika makongamano mbalimbali yakiwemo yaliyofanyika katika nchi za Vietnam, India, China na Korea ya Kusini. Kutokana na mikutano hiyo, Kituo kimepokea Kampuni mbili (2) ambazo zimeonesha nia ya kuwekeza nchini. Kampuni hizo ni *MECEN IPC Limited* ambayo inatafuta mbia wa kuwekeza katika mradi wa kuzalisha chupa za plastiki na Kampuni ya Hyundai ambayo imemtuma wakilishi wake kuja Tanzania kuangalia fursa na kuwekeza katika miradi ya ujenzi wa miundombinu kupitia Mfumo wa PPP.

**225. Mheshimiwa Spika**, Kituo kiliratibu ziara za wawekezaji toka China, Czechoslovakia, Japan, Marekani, Mauritius, Misri na Thailand kuja nchini. Matokeo ya ziara hizo ni ujio wa Kampuni ya *Gullin Pharmaceuticals (Tanzania) Ltd* ambayo inaendelea na majadiliano ya ubia na kampuni ya dawa kutoka China ili kuwekeza katika kiwanda cha dawa Dar es Salaam. Pia majadiliano yanaendelea kati ya Kampuni ya *Argenta Capital Partners Ltd* ya Mauritius na SUMA JKT kuhusu mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Dawa za Binadamu eneo la Ruvu. Vilevile, Kampuni ya *Saisan Co. Ltd* kutoka Japan ilikuja na kuonesha nia ya kuwekeza katika usambazaji wa nishati ya gesi (LPG Bulk Distribution) kwenye taasisi za umma kama vile shule, jeshi, na vyuo. Kampuni hiyo imenuia kushirikiana na *Commercial Petroleum Company of Tanzania (COPEC)* ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Mafuta ya Petroli Tanzania (TPDC). Taratibu za kuja kuwekeza zinaendelea.

**b) Kupeleka Taarifa kwenye Balozi za Tanzania Nje ya Nchi**

**226.** *Mheshimiwa Spika*, TIC imeshiriki katika kutoa na kusambaza taarifa kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi zinazosaidia kuvutia uwekezaji nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kituo kimepeleka machapisho ya uhamasishaji uwekezaji katika Balozi hizo na kutoa mafunzo ya namna ya kuhamasisha wawekezaji wa nje ili waje kuwekeza nchini.

**c) Uhamasishaji Uwekezaji wa Ndani**

**227.** *Mheshimiwa Spika*, TIC ilishiriki kwenye Maonesho ya DITF yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam mwezi Julai hadi Agosti, 2017. Maonesho hayo yalitoa fursa kwa Kituo kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na TIC kwa wawekezaji wa ndani na wa nje. Vilevile TIC ilishiriki kwenye Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika katika Kanda za Kusini (Lindi), Kaskazini (Arusha) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) mwezi Julai na Agosti, 2017. Katika Maonesho hayo, TIC ilifanikiwa kupata Cheti cha Ushindi wa pili kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Cheti cha Ushindi wa tatu kwenye Kanda ya Kaskazini katika kundi la taasisi. Vile vile, TIC ilishiriki katika Maonesho ya *Mwanza East Africa Trade Fair* ambapo ilitunukiwa kikombe cha ushindi kwa kushika nafasi ya kwanza kwa kundi la Taasisi na Idara za Serikali. Ushiriki katika maonesho hayo ulitoa fursa kwa Kituo kujitangaza na kuufahamisha umma juu ya kazi na majukumu yake katika kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini.

**d) Kusajili Miradi ya Uwekezaji**

**228.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Februari 2018, TIC imefanikiwa kuandikisha miradi 169 ambayo inatarajia kuwekeza mtaji wa Dola za Kimarekani 107,855,688 na kuajiri wafanyakazi wapatao 19,799 ikiwa ni ajira mpya. Miradi yote iliyosajiliwa katika kipindi hicho ilikuwa ni miradi mipya.

**e) Kutatua Changamoto za Uwekezaji Nchini**

**229.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Februari 2018, Kituo cha Uwekezaji kimeanzisha

Kamati ya Wakuu wa Taasisi zinazohusika katika Kutoa Huduma zinazofanikisha Uwekezaji (National Investment Facilitation Committee-NIFC). Kamati hiyo ipo chini ya uenyekiti wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji na hukutana mara moja kila mwezi na kujadili namna taasisi husika zinavyoweza kuondoa changamoto wanazokutana nazo wawekezaji wakati wa kuomba vibali na leseni mbalimbali.

**f) Kuanzisha Mkutano wa Wawekezaji na Wakuu wa Taasisi**

**230. Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Uwekezaji kimefanikisha mkutano unaowakutanisha wawekezaji na wakuu wa taasisi zinazohusika katika kutoa leseni na vibali mbalimbali (Investors Dialogue Meeting). Lengo la mkutano huo ni kuwawezesha wakuu wa taasisi kusikiliza changamoto wanazokutana nazo wawekezaji wakati wanapoomba leseni na vibali mbalimbali kwenye taasisi zao ili waweze kuzifanyia kazi. Mkutano huo hufanyika mara moja kwa mwaka na mkutano wa kwanza ulifanyika tarehe 31 Oktoba, 2017 ambapo masuala yaliyoibuliwa na wawekezaji yanafanywa kazi kupitia NIFC.

**g) Kuwasaidia Wawekezaji Kupata Vibali na Hati mbalimbali za Kisheria**

**231. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwezi Julai 2017 mpaka Februari 2018, maombi ya vibali mbalimbali yaliyoshughulikwa katika taasisi yalikuwa 9,127.

**h) Kuratibu Miradi ya Uwekezaji Mahiri**

**232. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, TIC iliratibu mkutano mmoja wa Kamati ya Wataalam wa NISC ili kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na wawekezaji mahiri. Katika mkutano huo, NISC ilichambua na kutoa ushauri kuhusu namna ya kutatua changamoto za wawekezaji mahiri. Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu, na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo kilitembelea miradi sita (6) iliyoomba

hadhi ya uwekezaji mahiri ili kujionea hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ilipofikia. Katika kikao chake cha mwisho, NISC ilifanikisha kupitisha miradi mikubwa sita na kuipatia hadhi ya miradi mahiri yaani *strategic investment status*.

**i) Kufanya Tafiti zitakazotumika Kuishauri Serikali kuhusu Sera ya Uwekezaji**

**233. Mheshimiwa Spika**, Kituo kimeweza kushiriki na kuendesha tafiti mbalimbali kwa kushirikiana na wadau zikihusisha tafiti za kiseru na za masoko (*Policy and Market Research*). Kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi ya Takwimu ya Taifa, Kituo kimeweza kukamilisha utafiti wa mitaji kutoka nje (FDI) kwa mwaka 2016 na taarifa hiyo inasubiri maoni ili kuwasilishwa katika Kamati ya Utendaji. Pia utafiti kama huo kwa mwaka 2017 unaendelea ambapo taarifa za makampuni kwa mwaka 2016/17 kwa Mkoa wa Dar es Salaam zimeshakusanywa. Kwa kushirikiana na *International Growth Centre (IGC)*, Kituo kimekamilisha utafiti ya muundo wa kisheria wa Sekta ya Vipodozi na kushirikisha wadau wa sekta hiyo kwa ajili ya uhakiki na kikao cha wadau kujadili taarifa ya utafiti huo kinatarajia kufanyika nusu ya mwaka ya pili ya 2017/2018. Utafiti huo utawezesha kuona changamoto zinazoikabili sekta hiyo katika kuanzisha na kuendesha miradi yao. Vilevile, Kituo kimeweza kushirikiana na Mradi wa *Supporting India Investment and Trade with Africa (SITA)* kwa udhamini wa *International Trade Centre (ITC)* kukamilisha utafiti wa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Ngozi na utafiti katika fursa ya alizeti upo katika hatua za awali.

**j) Kuboresha Utoaji Huduma Mahali Pamoja (One Stop Shop) na Kuwezesha Usajili kwa Njia ya Mtandao kwa Wawekezaji**

**234. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai 2017 mpaka Februari 2018, Taasisi imeendelea na maboresho katika kuhudumia wawekezaji ili kuwasaidia kupata vibali na leseni mbalimbali wanazohitaji ili kuweza kuanzisha miradi yao. Katika juhudi hizo Kituo kimeongeza idadi ya taasisi zilizopo katika Huduma za Mahali Pamoja kwa kuweka pamoja maafisa wa TANESCO, TFDA, TBS pamoja na OSHA.

**k) Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo na wa Kati Kuibua Fursa za Uwekezaji na Kuwaunganisha na wafanyabiashara Wakubwa (Business Linkages)**

**235. Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kimeendelea kuwaunganisha wawekezaji wakubwa na wadogo, ili wawekezaji wadogo waweze kuwauzia (kuwasambazia) bidhaa wale wawekezaji wakubwa kulingana na ubora na mahitaji ya wawekezaji wakubwa. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Disemba 2018, wawekezaji wadogo wapatao 63 wameshiriki mafunzo hayo. Kazi hiyo hufanyika kupitia mafunzo maalum ambayo wawekezaji wadogo wadogo wa ndani wanapewa ili waweze kuendana na mahitaji ya wawekezaji wakubwa.

**l) Kutangaza Kazi za Kituo na Vivutio vya Uwekezaji**

**236. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, TIC ilishiriki katika vipindi maalum vya televisheni na radio ikiwamo *Radio One, Clouds FM, City Radio*, na *TBC* ili kutoa elimu kwa umma kuhusiana na majukumu yake. TIC ilitumia fursa hizo kutoa taarifa za uwekezaji na kuelezea malengo makuu ya Kituo katika shughuli za kuhamasisha uwekezaji, kuhudumia wawekezaji na kutoa huduma za mahala pamoja yaani *One Stop Facilitation Centre*. TIC iliweza kushiriki vipindi mbalimbali ikiwemo vipindi vya 'tunatekeleza' kupitia TBC, 'kumekucha na kipima joto' kupitia ITV. Vile vile, Taasisi imefanya mahojiano maalum na waandishi wa TBC, Channel Ten na ITV.

**3.4.9 Shirika la Viwango Tanzania**

**a) Kukagua Ubora wa Bidhaa zitokazo Nchi za Nje kabla ya Kuingia Nchini (Pre-shipment Verification of Conformity to Standards- PVoC ) ili Kulinda Viwanda vya Ndani**

**237. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Zanzibar

(ZBS), SIDO, TRA, GCLA, EWURA, SUMATRA, TFDA, FCC, NEMC, NIT, TPA na Jeshi la Polisi imeendelea kusimamia ubora wa bidhaa zikiwemo zinazotoka nje kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Lengo ni kuhakiki na kuthibitisha ubora ili kuwalinda walaji na viwanda vya ndani. Hadi kufikia Machi 2018, vyeti vya ubora wa bidhaa zitokazo nje ya nchi (*Certificate of Conformity - CoCs*) 25,055 vimetolewa, sawa na asilimia 73.7 ya lengo ya kutoa vyeti 34,000 vya ubora mwaka 2017/2018.

**238. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kudhibiti ubora wa bidhaa, ambapo bidhaa ambazo hazikukidhi viwango ziliteteketewa au kurudishwa nchi zilikutoka. Baadhi ya bidhaa zilizoteketewa ni pamoja na nondo tani 126, vilainishi vya mitambo (*engine oil*) lita 1,000, betri za *solar* vipande 91 na nyaya za umeme (*flat twin cables*) rola 208. Bidhaa zilizoteketewa zilikuwa na thamani ya Shilingi 217,301,000. Vilevile, bidhaa zilizorejeshwa nchi zilikutoka ni pamoja na shehena za mafuta ya petroli ya tani 74,968.95, nyaya za kuzuia radi (*earth rod*) vipande 4,950, mafuta ya breki za magari (*brake fluid DOT 3*) lita 9,880, malighafi ya kutengenezea bati tani 60.3 na nyaya za umeme (*PVC insulated cables*) katonni 53. Bidhaa zilizorejeshwa zilikuwa na thamani ya Shilingi 9,464,967,232.

**b) Kutoa Leseni ya Ubora kwa Bidhaa Mbalimbali**

**239. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2018, leseni 225 za ubora za TBS zimetolewa sawa na asilimia 93.8 ya lengo la kutoa leseni 240. Miongoni mwa leseni hizo, 41 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo kwa bidhaa za mvinyo, iliki, unga wa soya, unga wa mahindi, mafuta ya kujipaka, pilipili manga, maji ya chupa, chumvi, jemu, karafuu, tangawizi ya kusaga, chaki, sabuni za maji, mikate, sabuni za kuogea, maziwa, mtindi, mafuta ya alizeti, asali, vigae, grisi, chokaa, sharubati ya nanasi na mchele. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo bora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

**c) Kutoa Mafunzo kuhusu Viwango na Udhibiti wa Ubora (Quality Assurance Training)**

**240. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2018, semina 37 za mafunzo zilitolewa, sawa na asilimia 123.3 ya lengo la kutoa semina 30. Mafunzo na semina hizo zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali wapatao 3,201 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Katavi, Kigoma, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Ruvuma, Singida, Shinyanga, Songwe na Tabora.

**d) Kufanya Ugezi kwa Vifaa na Mashine mbalimbali**

**241. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2018 mitambo 4,211 ilifanyiwa ugezi, sawa na asilimia 52.9 ya lengo la kufanya ugezi wa mitambo 8,000.

**e) Kutayarisha Viwango vya Kitaifa katika Sekta Ndogo za Uhandisi na Usindikaji**

**242. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2018, Shirika limekamilisha viwango muhimu 267 katika sekta za uhandisi na usindikaji sawa na asilimia 76.3 ya lengo la kutayarisha viwango 350 kwa mwaka. Shirika pia liliendelea kusimamia viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora (*Certification Schemes*).

**f) Kupima Sampuli za Bidhaa Mbalimbali**

**243. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2018, sampuli 15,120 zilikuwa zimepimwa katika maabara mbalimbali za Shirika kwa lengo la kuhakiki ubora wake. Hiyo ni sawa na asilimia 122.9 ya lengo la kupima sampuli 12,300 kwa mwaka. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa nchini hali iliyosababisha kuongezeka kwa sampuli zinazohakikiwa ubora hapa nchini (*Destination Inspection*).

**g) Kufanya Ukaguzi na kutoa Leseni za Ubora wa Magari Yaliyotumika yanayoingizwa Nchini**

**244. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2018, vyeti 26,706 vya ukaguzi wa magari vimetolewa, sawa na asilimia 63.6 ya malengo ya vyeti 42,000. Kati ya magari



hayo yaliyokaguliwa, magari 31 yalikataliwa baada ya kushindwa kukidhi viwango vya ubora. Aidha, Shirika linatekeleza mradi unaofadhiliwa na *Trade Mark East Africa* (TMEA) wenye lengo la kuboresha miundombinu ya ubora ya Shirika. Kwa kupitia mradi huo, miundombinu ya TEHAMA ya TBS imeboreshwa hivyo imerahisisha utoaji wa huduma na kufupisha muda wa kuwahudumia wateja wa Shirika (*Turn Around Time*).

**h) Kuanzisha Ofisi Mpya za Mipakani na Kufungua Ofisi Mpya za Kanda**

**245. Mheshimiwa Spika;** katika kupanua wigo wa utoaji huduma na kudhibiti mianya ya uingizwaji wa bidhaa zisizokidhi ubora, Shirika limeomba ofisi kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na majadiliano yanaendelea ili kupata ofisi katika mipaka ya Itungi, Bukoba na Mtwara. Vilevile, Shirika linaendelea na jitihada za kutafuta ofisi katika mipaka ya Mtambaswala na Tarakea sambamba na kufuatilia vibali vya ajira ili kuwezesha ukaguzi wa bidhaa katika mipaka hiyo. Shirika limefungua ofisi za kanda zilizopo Arusha (Kanda ya Kaskazini) Mbeya (Kanda ya Nyanda za Juu Kusini), Mwanza (Kanda ya Ziwa) Dodoma (Kanda ya Kati) na Mtwara (Kanda ya Kusini).

**3.4.10 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni**

**a) Kuboresha Mifumo na Taratibu za Utoaji Huduma kwa Kutumia Njia za Kiteknolojia**

**246. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni imejenga Mfumo Mpana wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (Online Registration System - ORS) ambapo huduma zote zitolewazo na BRELA ambazo ni usajili wa makampuni, majina ya biashara, alama za biashara na huduma, hataza, leseni za biashara na viwanda zinatolewa kwa njia ya mtandao. Mfumo wa ORS umeunganishwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa ajili ya namba ya uraia na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) wa Kampuni ambayo pia huwa ni namba ya usajili wa Kampuni. Aidha, mfumo huo umekwishauganishwa na Mfumo wa Serikali wa

Ukusanyaji wa Maduhuli (Government Electronic Payment Gateway - GePG), pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa ajili ya utambuzi wa maeneo na anuani za makazi. Mfumo huo wa ORS unaweza kuunganishwa na taasisi nyingine za Serikali kwa lengo la kutoa huduma kwa pamoja (Electronic One Stop Shop).

**247. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza kutoa huduma kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 4 Januari, 2018, BRELA ilitoa mafunzo kwa wanasheria, wahasibu na wakaguzi, wawakilishi wa Sekta Binafsi na benki. Aidha, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa kutumia mifumo ya TEHAMA na kufanya usajili, Wakala imeanzisha dawati la kuelimisha na kusaidia wadau kusajili kwa njia ya mtandao katika jengo jipya la Ushirika. Mfumo huo unategemewa kufungwa katika Ofisi za Maafisa Biashara nchini ili kurahisisha utoaji wa huduma na elimu kwa wananchi katika Halmashauri zote nchini. Aidha, Wakala imetoa mafunzo kwa Maafisa Biashara wote wa Halmashauri za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani yaliyofanyika tarehe 5 na 6 Machi, 2018.

**b) Kuboresha Mifumo ya Uwajibikaji, Weledi na Uadilifu kwa Watumishi**

**248. Mheshimiwa Spika**, Wakala imeendelea kuboresha mifumo ya uwajibikaji kwa watumishi kwa kusimamia ujazaji wa fomu za MWAMTUKA (OPRAS). Wakala imekuwa na utamaduni kwa watumishi wake kutoa taarifa za utendaji za siku na wiki. Pia, katika kuhakikisha suala la maadili na uadilifu linafanyiwa kazi, Wakala ina kamati ya maadili ambayo pamoja na majukumu mengine inaratibu malalamiko ya wateja na kushughulikia masuala ya maadili ya wafanyakazi. Utaratibu huo umeweza kubaini maeneo yenye viashiria vya rushwa na pia kudhibiti na hata kuongeza usimamizi zaidi.

**c) Kutoa Elimu na Uhamasishaji wa Usajili na Urasimishaji wa Biashara kwa Wananchi**

**249. Mheshimiwa Spika**, Wakala imeendelea kutoa elimu kuhusu taratibu za usajili kwa njia ya mtandao

kwa kutumia vyombo vya habari, semina na warsha mbalimbali kwenye maeneo ya wafanyabishara wadogo wadogo mikoani na wilayani kwa kuanzia na ofisi za kanda za Mbeya, Mtwara na Mwanza. Aidha, Wakala unahamasisha urasimishaji wa biashara kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa vipeperushi vilivyoandaliwa kwa Kiswahili vikielezea taratibu za usajili na ada. Hadi kufikia Januari 2018, vipeperushi 22,480 vimetolewa kwa wajasiriamali mbalimbali mikoani na wilayani. Vilevile, Wakala inalenga kuwaelimisha na kuwapa huduma za usajili popote walipo kwa njia ya mtandao. Aidha, wafanyakazi wameelimishwa kuhusu mbinu na kuwahudumia wateja na kutekeleza mkataba kwa wateja.

### **3.4.11 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala**

#### **a) Kuainisha na Kufanya Ukaguzi wa Ghala zilizosajiliwa na zinazotarajiwa Kusajiliwa chini ya Mfumo**

**250. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imetoa leseni 23 kwa waendeshaji wa ghala kwenye mazao ya korosho, kahawa (1), mpunga (2), na mahindi (1) na kufikia jumla ya leseni 27. Aidha, Bodi imefanya kaguzi zote zinazotakiwa kisheria ambazo ni ukaguzi kabla ya mfumo kuanza (Pre-Inspection), na ukaguzi wakati Mfumo unaendelea (Surveillance Inspections). Leseni za kuendesha ghala hutolewa baada ya Bodi kutangaza kwenye tovuti yake na waombaji wenye sifa kukidhi matakwa ya kisheria ya uendeshaji wa ghala.

#### **b) Kutoa Elimu ya Mfumo wa Stakabadhi kwa Wadau**

**251. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala imeendelea kutoa elimu ya Mfumo kwa wadau wote ili kuongeza uelewa. Katika kipindi cha Julai hadi Oktoba 2017, wafanyakazi wa makampuni yanayoendesha ghala wapatao 52 walipewa mafunzo ya jinsi ya kupokea na kutoa mazao ghalani, Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, Kanuni na Miongozo ya mazao yanayotumia Mfumo wa Stakabadhi. Bodi kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, NMB PLC, CRDB PLC, NHIF, TIGO

Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na Mashirika ya Hifadhi ya Jamii walitoa mafunzo kwa wakulima wa Mtwara na Lindi mwezi Agosti 2017.

**252. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Bodi kwa kushirikiana na FSDT ilihamasisha wakulima wa korosho kutumia huduma za kibenki ikiwa ni pamoja na kufungua akaunti kwa ajili ya malipo wanapouza korosho. Zaidi ya wakulima 420,000 walifungua akaunti na kutumia huduma za kibenki kama ifuatavyo: NMB 224,000, CRDB 196,000, na POSTAL BANK 2,033. Aidha, wakulima wanaelimishwa na kuhamasishwa kutumia mitandao ya simu kupata taarifa za kila siku za masoko ya bidhaa na mazao.

**253. Mheshimiwa Spika**, Bodi imeendelea kufuatilia utendaji wa ghala zilizosajiliwa kuhifadhi mazao na kutoa elimu kuhusu uingizaji wa taarifa kwenye kanzidata na kurekebisha makosa mapema. Bodi kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania imetoa mafunzo kwa wakulima wapatao 200 wa mahindi katika Mkoa wa Rukwa katika wilaya za Sumbawanga, Kalambo na Nkasi kuhusu matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na jinsi ya kuuza mazao kupitia Soko la Bidhaa Tanzania.

### 3.4.12 Chama cha Hakimiliki Tanzania

#### a) Kuongeza Makusanyo ya Mirabaha

**254. Mheshimiwa Spika**, Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) imeendelea kuboresha ukusanyaji wa mirabaha, kwa kuongeza maafisa leseni wawili (2) na matumizi ya mfumo wa kielektroniki. Kwa sasa kuna jumla ya maafisa leseni watano (5) na maafisa ugani watatu (3) ambao wanafanya kazi ya ukusanyaji mirabaha kwa usimamizi wa COSOTA. Hadi Februari 2018, Shilingi 90,164,820 zilikusanywa na zoezi la kugawa mirabaha kwa wasanii litaendelea baada ya kukamilika kwa maboresho ya mfumo yanayofanywa na wataalam kutoka WIPO. Maboresho hayo yanayotarajiwa kukamilika tarehe 17 Mei, 2018 yatawezesha mirabaha kugawanywa kutokana na matumizi ya kazi za wasanii. Aidha, COSOTA imejiunga na Mfumo wa

Kielektroniki wa *Government e-Payment Gateway* ili kuongeza mapato.

**b) Kutoa Elimu kwa Wananchi na Wadau wa Sanaa Kuhusiana na Mambo ya Hakimiliki na Hakishiriki**

**255. *Mheshimiwa Spika***, COSOTA kwa kushirikiana na wadau wengine imetoa elimu katika mikoa ya Arusha (195), Dar es Salaam (54), Dodoma (190), Mbeya (220), Mwanza (188), Morogoro na Tanga kuhusu masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa watunzi na wabunifu wa kazi za sanaa zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 na umuhimu wa kusajili na kulinda kazi zao na masuala ya uharamia.

**c) Kufanya Ukaguzi wa Kazi Zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (Anti-Piracy Raids)**

**256. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari 2018, COSOTA ilifanya ukaguzi wa matumizi ya kazi za wasanii kupitia mfumo wa televisheni wa *cable* katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Mara, Morogoro, Mtwara, Singida na maeneo ya Namanga na Karatu. Kufuatia ukaguzi huo, kesi mbili zimefunguliwa kwa kukiuka Sheria moja ikiwa mkoani Singida na kesi nyingine katika mkoa wa Arusha wilayani Karatu. Aidha, kesi moja iliyofunguliwa mkoani Dodoma mwaka 2017 bado inaelendea kusikilizwa.

**d) Kushughulikia Migogoro na Kesi za Hakimiliki na Hakishiriki**

**257. *Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Februari 2018, COSOTA imepokea jumla ya migogoro 27. Kati ya hiyo, miwili (2) imeshughulikiwa na kumalizika, iliyobaki inaendelea na usuluhishi.

**e) Kuendelea Kusajili Wanachama Wasanii na Kazi Zao**

**258. *Mheshimiwa Spika***, COSOTA imeendelea kusajili wasanii na kazi zao. Katika kipindi cha 2017/2018, jumla ya wanachama 348 walisajiliwa. Kati ya hao, 77 walikuwa wa fani ya muziki, 125 fani ya filamu na 146 wa kazi za maandishi.

Kazi zilizosajiliwa ni 1,432 inayojumuisha kazi 908 za muziki, 276 za filamu na 248 za maandishi.

### **3.4.13 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania**

#### **a) Kuboresha Upatikanaji wa Soko la Bidhaa na Huduma Zinzazalishwa Nchini**

**259. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ilifanya tathmini ya mahitaji ya malighafi ya viwanda 70 vya matunda, viungo na nafaka ili kuunganisha wazalishaji wa mazao na viwanda. Hatua hiyo ililenga kusaidia upatikanaji wa masoko ya uhakika. Jitihada hizo zinajumuisha kutafuta soko kwa bidhaa zitokanazo na shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, ubunifu, utamaduni na huduma mbalimbali zitolewazo nchini.

#### **b) Kuratibu na Kudhibiti Uendeshaji wa Maonesho ya Kimataifa Nchini**

**260. Mheshimiwa Spika**, TanTrade iliandaa Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Juni hadi 13 Julai, 2017. Kupitia Maonesho hayo, Watanzania walipata muda wa kutembelea, kujifunza teknolojia, ujuzi na mbinu mbalimbali za kibiashara. Makampuni ya ndani 1,999 yalishiriki ikilinganishwa na makampuni 1,811 yaliyoshiriki maonesho ya 40 ya DITF ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.4. Aidha, kampuni 501 kutoka nje ya nchi yalishiriki ikilinganisha na kampuni 491 katika Maonesho ya 40 ya DTIF, sawa na ongezeko la asilimia 2.03. Vilevile, nchi 31, Wizara 6 na taasisi 37 za Serikali zilishiriki.

**261. Mheshimiwa Spika**, kupitia Maonesho hayo, wafanyabiashara wallingia mikataba mbalimbali yenye thamani ya Shilingi bilioni 15 na mauzo ya papo kwa papo ya Shilingi bilioni 10. Maonesho hayo yameendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuwa na siku maalum za kutangaza bidhaa za Tanzania. Aidha, mabanda maalum

kama vile Banda la Tanzania mahsusi kwa ajili ya kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini na Banda la Asali kwa ajili ya kutangaza bidhaa za asali yalitengwa. Mabanda hayo yameendelea kuwavutia watembeleaji wengi wakati wa maonesho.

c) **Kuandaa Mikutano ya Wafanyabiashara**

**262. Mheshimiwa Spika,** TanTrade kwa kushirikiana na shirika binafsi la *Global Community* iliratibu mikutano ya ana kwa ana ya biashara ili kuwaunganisha wazalishaji na masoko. Katika mikutano hiyo, mikataba mbalimbali isiyofungamana yenye thamani ya Shilingi bilioni 7, ikiwahusisha wanunuzi na wazalishaji wa alizeti, matunda na choroko kutoka mikoa ya Mtwara, Njombe na Singida ilisainiwa. Kadhalika, viwanda vya usindikaji wa maziwa vilionesha uhitaji mkubwa ikilinganishwa na uzalishaji wa maziwa unaofanywa kwa sasa. Mathalan, viwanda vya *Tanga Fresh* na *Milk Com* vilionesha utayari wa kutuma gari la kukusanya maziwa popote wafugaji watakapoweza kuzalisha zaidi ya lita 10,000 kwa siku. Vilevile, wakulima wa viungo na matunda waliunganishwa na viwanda vya *Elven Agri* na *Vegeta* vilivyopo wilayani Bagamoyo.

d) **Kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa Nje ya Nchi**

**263. Mheshimiwa Spika,** ili kutangaza na kukuza mahusiano ya kibiashara na nchi za nje, TanTrade iliratibu ushiriki wa kampuni za kitanzania katika maonesho mbalimbali nje ya nchi. Kampuni 72 zilishiriki katika maonesho ya nje ya nchi ikijumuisha Rwanda (18), Swaziland (11), Uganda (10) na Kenya (23). Mafanikio yaliyopatikana katika ushiriki huo ni pamoja na; mauzo ya papo kwa papo ya takribani Shilingi milioni 197; Kampuni tatu (3) ikijumuisha Kiwanda cha Mvinyo (Alko Vintage Co. Ltd), Urafiki, *21<sup>st</sup> Century* na Kampuni ya Waasili Asilia ziliingia makubaliano ya kuuza bidhaa za mvinyo, khanga, vitambaa na bidhaa za ngozi nchini Swaziland. Makubaliano ya kufanya biashara

ikiwa ni pamoja na oda ya kuuza tani 50 za kahawa, jozi 300 za viatu vya ngozi vya wazi (Sandals), tani 200 za mchele, tani 10 asali mbichi na tani 40 za nafaka.

e) **Kushiriki katika Mikutano na Makongamano**

**264. Mheshimiwa Spika**, TanTrade ilishiriki katika Kongamano la Tatu (3) la Watanzania Waishio Nje ya Nchi (Diaspora) lililofanyika Zanzibar kwa lengo la kutangaza fursa za biashara nchini. Kongamano hilo pia lililenga kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Utalii nchini kupitia *Diaspora*, kutambua mchango wa *Diaspora* katika kuleta muonekano mpya wa uchumi wa kati na kuweka mazingira ya kuandaa makongamano ya biashara na uwekezaji nje ya nchi kwa kushirikiana na *Diaspora*.

f) **Kuimarisha na Kujengea Uwezo Sekta Ndogo na ya Kati ya Biashara (SMEs)**

**265. Mheshimiwa Spika**, TanTrade inatambua mchango mkubwa wa kukuza uchumi, ajira na maendeleo kwa ujumla unaotolewa na Sekta Katiti, Ndogo na ya Kati ya Biashara (MSMEs). Kwa kutambua jukumu hilo, Mamlaka imeendelea kuwajengea wafanyabiashara uwezo kwa njia ya mafunzo na kuwapatia taarifa za biashara na masoko. Vilevile, Tantrade kwa kushirikiana na wadau wengine imesaidia kutatua changamoto na vikwazo vya kiutendaji na kushiriki kuweka mazingira rafiki ya kibiashara ili wafanyabiashara hao waweze kufikia vigezo vya ushindani na kuongeza tija na ufanisi katika biashara.

g) **Kuboresha na Kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Biashara**

**266. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa taarifa za kibiashara zilizo sahihi na kwa muda muafaka kutoka vyanzo vya kuaminika, TanTrade inatumia Mfumo wa Serikali wa Taarifa kwa Njia ya



Ujumbe Mfupi kwa Simu ya Mkononi (E-Government Mobile Platfom) kwa lengo la kukusanya na kusambaza taarifa za masoko ya bidhaa na huduma mbalimbali kwa umma. Hali kadhalika, katika kipindi cha 2017/2018, TanTrade ilifanikiwa kuziingiza kampuni 1,046 kwenye kanzidata ya mfumo huo ambao utawezesha kampuni hizo kupata wateja wa bidhaa zao na kuongeza mauzo hususan kwenye sekta za chai, kahawa, pamba, nguo, katani na korosho.

**h) Kutoa Ushauri wa Kibiashara kwa Wajasiriamali Wadogo**

**267. Mheshimiwa Spika**, TanTrade ilitoa ushauri kwa kampuni ndogo 20,036 na kuziwezesha kubuni, kuanzisha na kuendesha biashara kwa njia ya vikundi; kuandaa maandiko ya miradi; kutengeneza rajamu za bidhaa; kutoa ushauri wa kitaalam wa masuala ya kibiashara; kutengeneza nembo za kampuni; machapisho mbalimbali yanayotumika kutangaza bidhaa pamoja na huduma nyingine za kibiashara kupitia Kitengo cha BSB. Lengo la ushauri huo lilikuwa ni kuimarisha uwezo wa kampuni hizo kufanya biashara yenye tija. Vilevile, kampuni hizo ziliweza kuunganishwa na Taasisi za SIDO, TBS na TFDA kwa ajili ya kupata huduma nyingine za kibiashara. Huduma hiyo imekuwa kiunganishi muhimu kati ya taasisi na wadau mbalimbali kwenye masuala ya biashara nchini.

**i) Kuwaunganisha Wazalishaji wa Ndani na Masoko**

**268. Mheshimiwa Spika**, TanTrade ilifanikiwa kuwaunganisha wazalishaji 529 wa bidhaa za viungo, asali, maharage, mbaazi, soya, samaki, mboga na matunda, mikundekunde, chai, kahawa, miwa, chakula cha mifugo, ufugaji wa samaki, bidhaa za ngozi na usindikaji wa samaki na vyakula na bidhaa nyingine katika soko la ndani na la nje.

j) **Kuratibu Programu za Mafunzo**

**269. Mheshimiwa Spika**, TanTrade iliratibu programu mbili (2) za mafunzo ya kujenga uwezo kwa wazalishaji na wafanyabiashara wapatao 307 ili waweze kufanya biashara kiushindani, kwa kuzingatia ubora katika mnyororo wa thamani ya bidhaa na namna ya kutafuta masoko. Mafunzo hayo yalitolewa kwa kada mbalimbali za wazalishaji na wafanyabiashara nchini katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Lindi, Mtwara na Shinyanga Programu hiyo iliratibiwa kwa ushirikiano na wadau kutoka taasisi za umma na binafsi zikiwemo TBS, TFDA na *Agha Khan Foundation*. Walengwa wa mafunzo hayo walikuwa ni vikundi vya wasindikaji wa mafuta ya alizeti, wafugaji nyuki na wasindikaji asali na bidhaa zake ili waweze kuongeza uzalishaji na kufahamu mbinu za kutafuta masoko.

k) **Kuongeza Ushindani katika Sekta ya Biashara**

**270. Mheshimiwa Spika**, TanTrade imeendelea kufanya tafiti za kibiashara ili kuimarisha na kukuza biashara katika mikoa na nchi zinazoizunguka Tanzania; kufanya tathmini na upembuzi yakinifu wa bidhaa na mazao mbalimbali ili kubaini mifumo ya masoko; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo ili kuendeleza fursa za viwanda nchini.

**3.4.14 Wakala wa Vipimo**

a) **Kukagua na Kusimamia Matumizi Sahihi ya Vipimo**

**271. Mheshimiwa Spika**, vipimo 455,962 vimekaguliwa na kuhakikiwa, sawa na asilimia 95.6 ya vipimo 477,159 vilivyopangwa kukaguliwa kuanzia Julai, 2017 hadi Januari, 2018. Wakala imeendelea kufanya zoezi la kuzuia ufungashaji batili maarufu kwa jina la LUMBESA ambapo mikoa yote imeanzisha vituo maalum vya ukaguzi (Barriers). Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Januari 2018,

wafanyabiashara 2,501 walikaguliwa na 768 ambao ni asilimia 31 kati ya hao walipatikana na makosa na hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa ikiwemo kufilisiwa na kupelekwa mahakamani.

**272. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wakala iliendesha zoezi la ukaguzi wa mizani katika zao la korosho, sambamba na utoaji wa elimu katika mkoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Katika zoezi hilo, mizani 2,023 ilikaguliwa ambapo mizani 2,005 sawa na asilimia 99.1 ilikuwa sahihi kwa matumizi na mizani 18 (asilimia 0.9) ilihitaji marekebisho kabla ya kutumika. Aidha, Wakala ilifanya uhakiki wa mizani mikubwa (weigh bridges) katika maghala makuu matano (5) mkoani Lindi (Mtama, Nachingwea na Buko) na Mtwara (MCC na OLAM) ambako vyama vya msingi (AMCOS) hupeleka na kuuza korosho zao.

**273. Mheshimiwa Spika,** Wakala imeendelea kufanya uhakiki wa mizani inayotumika kununulia ufuta mkoani Lindi katika wilaya za Lindi Vijijini, Kilwa, na Ruangwa ambako vijiji 30 na vyama vya msingi sita (6) vilipitiwa. Katika ukaguzi huo mizani 65 ilihakikiwa na mizani 47 ilipitishwa, wakati mizani 18 ilifanyiwa marekebisho kabla ya kutumika. Wakati ukaguzi wa mizani ukiendelea, elimu ilitolewa kwa wakulima na wanaushirika kuhusu matumizi sahihi ya vipimo wakati wa uuzaji wa ufuta.

**274. Mheshimiwa Spika,** Wakala ilikagua mizani ishirini na tano (25) iliyotumika kwa ununuzi wa zao la tumbaku na kuhakikisha usahihi wake. Aidha, zoezi hilo la uhakiki wa mizani hiyo kwa msimu wa 2017/2018 lilifanyika katika vituo vya mauzo ili kuondokana na wasiwasi uliopo miongoni mwa wadau kuwa mizani huharibiwa wakati wa kusafirishwa inapohakikiwa nje ya vituo. Wakulima waliuza tumbaku yao kupitia mizani iliyohakikiwa na kupata stahiki kulingana na uzito sahihi na kuwaongezea hamasa ya kuzalisha zaidi.

**275. Mheshimiwa Spika**, Wakala iliendelea kufanya uhakiki wa mizani ya kupimia madini na vito katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ambapo hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka 2017/2018, ukaguzi ulifanyika katika vituo vya mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Ruvuma na Shinyanga ambapo mizani 89 ilikaguliwa. Kati ya hizo, mizani 64 ilipitishwa kuwa ni sahihi na mizani 25 ilielekezwa ifanyiwe marekebisho.

**276. Mheshimiwa Spika**, kutokana na uhakiki huo wa mizani za madini na vito, Serikali imeweza kubaini udanganyifu uliokuwa ukifanywa na wauzaji na wasafirishaji wa madini ndani na nje ya nchi na kusaidia kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, Serikali imetoa fedha za maendeleo kwa ajili ya kununulia vifaa vya kitaalam (Precision weighing scales and standard weights) vitakavyosaidia kuongeza kasi na ufanisi wa ukaguzi huo. Ununuzi wa vifaa hivyo uko katika hatua mbalimbali za manunuzi.

**277. Mheshimiwa Spika**, Wakala iliendelea kuhakiki *flow meter* zinazopokea mafuta, hususan mafuta mazito (diesel) yanayoingia nchini kupitia Bandari ya Dar es Salam. Hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka 2017/2018, mita hiyo iliweza kupitisha kwa usahihi lita za ujazo 4,326,179,690 za mafuta ya dizeli. Aidha, Wakala iliendelea kuhakiki mita zilizopo kwenye pampu za kuuzia mafuta na pia matenki yanayobeba mafuta ili kumlinda mtumiaji na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki. Katika kuhakikisha magari na matenki yanayobeba mafuta yana ujazo sahihi, Wakala inakamilisha ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Kupimia Matenki ya Mafuta (Calibration Bay) katika eneo la Misugusugu, Kibaha – Mkoani Pwani. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhakiki matenki nane (8) kwa wakati mmoja badala ya kituo cha sasa kilichopo Ilala chenye uwezo wa kuhakiki matenki mawili (2) kwa wakati mmoja. Kituo hicho kipyua kinatarajiwa kuanza kazi mapema mwezi Juni 2018 ambapo kasi na ufanisi katika ukaguzi wa magari yabebayo mafuta itaongezeka.

**278. Mheshimiwa Spika**, Wakala iliendelea kufanya ukaguzi wa vituo vya kuuzia gesi itumikayo majumbani (LPG). Ukaguzi umefanyika katika vituo vinavyopokea na kufungasha gesi (Gas Plants) na pia katika vituo vya kuuzia gesi vya jumla na reja reja ili kuwalinda watumiaji. Pamoja na ukaguzi huo, Wakala wa Vipimo imeendelea kutoa elimu hususan kwa watumiaji kupitia luinga, radio, vipeperushi na kwenye maonesho mbalimbali namna ya kutambua mitungi ya gesi iliyo na kipimo sahihi. Aidha, Wakala imefanya kaguzi za kushitukiza katika vituo vya kuuzia gesi ili kuhakikisha kuwa kila muuzaji wa gesi anayo mizani iliyohakikiwa na mitungi imewekwa alama stahiki za kuonesha uzito sahihi wa mtungi na gesi. Hadi kufikia robo ya tatu ya 2017/2018, Wakala imefanya ukaguzi kwa wauzaji wa jumla na reja reja kwa vituo 1,358 ambapo vituo 1,158 (asilimia 85.3) vilikuwa na mizani na vituo 200 (asilimia 14.7) havikuwa na mizani.

**279. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha dira za maji (water meters) zinahakikiwa, Wakala imeanza kuhakiki dira za maji zinazolingia nchini kabla ya kufungwa kwa ajili ya matumizi, pamoja na zile zilizoko kwenye matumizi. Katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Januari 2018, Wakala imehakiki dira za maji 682 ambapo dira za maji 670 zilipitishwa na dira za maji 12 zilikataliwa. Uhakiki umefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga na Tanga.

**Jedwali Na. 1: Uhakiki wa Dira za Maji (Julai 2017 hadi Machi 2018)**

Mkoa	Mita zilizohaki- kiwa	Mita zilizopit- ishwa kwa ma- tumizi (Passed)	Mita zilizokata- liwa (Rejected)
Dar es Salaam	61	5	1
Shinyanga	6	6	-
Tanga	3	3	-
<b>Jumla</b>	<b>68</b>	<b>6</b>	<b>1</b>

**b) Kutoa Elimu Kwa Umma**

**280. Mheshimiwa Spika**, taarifa na maandiko 38 yalitolewa kwenye magazeti mbalimbali katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Januari 2018. Vipindi 22 vya redio, vipindi 20 vya luninga, matangazo mawili (2) ya redio na matatu (3) ya luninga yalitolewa. Mikutano mitatu ya waandishi wa habari (3) na semina nne (4) kwa wajasirimali (TASWE, TWCC, MOWE na Lindi) zimefanyika. Aidha, Wakala imeshiriki katika maonesho mbalimbali (DITF, NaneNane, SIDO-Kigoma na Iringa; MOWE na wadau wa maji -Tanga).

**281. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka 2017/2018, Wakala wa Vipimo imeweza kutoa elimu na mafunzo maalum kwa wajasiriamali walio katika vikundi vipatavyo tisa (9) katika mikoa ya Kilimanjaro (Nandra Scales Enginnering, Moshi Common Facility, Hang Scales, Hagu Scales, IJM Scales na Paramount Scales); Arusha (Uruto Weighing Scales); Dar es Salaam (Hasat Inspiration Co. Ltd); na Mwanza (Msunga Bench Products) ambapo tayari wameanza kuunda mizani na kuingiza kwenye soko hapa nchini. Mizani inayoundwa na wajasiriamali wazalendo, imeonesha ubora mkubwa ambao umethibitishwa na Wakala ikilinganishwa na mizani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Viwanda hivyo vidogo vya uundaji wa mizani vimetoa ajira kwa vijana takriban 150 na kuwaongezea kipato.

**c) Kuiboresha Kanzidata ya Vipimo**

**282. Mheshimiwa Spika**, Wakala imeendelea na ukusanyaji wa takwimu za vipimo katika mikoa ili kupata idadi sahihi (Kanzidata) ya vipimo kwa nchi nzima. Kwa mujibu wa kanzidata iliyofanyika hadi mwezi Januari 2018 imeonesha kuwa kuna vipimo 830,000 kwa nchi nzima na kazi hiyo ni endelevu.

**d) Kununua Vitendea Kazi**

**283. Mheshimiwa Spika**, magari sita (6) kati ya magari 10 yaliyopangwa kununuliwa mwaka 2017/2018 yamelipiwa GPSA. Aidha, vifaa vya kitaalam vya kuhakiki dira za maji

(Water Meter Test Bench) na mizani ya kupimia uzito wa madini na vito (Weighing instrument) viko katika hatua mbalimbali za manunuzi.

**e) Kuanzisha na Kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E)**

**284.** *Mheshimiwa Spika*, Wakala imeendelea kuimarisha mfumo wake wa ufuatiliaji na tathmini kwa kuhuisha mifumo ya ICT ili kuharakisha ufuatiliaji katika mikoa yote ya Tanzania ambako Wakala ina ofisi.

**f) Kuongeza Idadi ya Watumishi na Kuwaongezea Uwezo wa Kitaalam**

**285.** *Mheshimiwa Spika*, Watumishi 21 katika ajira mbadala wameajiriwa, kati yao 10 ni Maafisa Vipimo na 11 ni Madereva. Aidha, watumishi 24 wamepata mafunzo mbalimbali ya kitaalam ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo.

**g) Kufanya Maboresho ya Ofisi za Wakala na Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Upimaji Matenki ya Mafuta Misugusugu Kibaha**

**286.** *Mheshimiwa Spika*, Ofisi nne (4) za Wakala katika Mikoa ya Mwanza, Mtwara, Temeke na Kitengo cha Bandari (Dar es Salaam) zimefanywa maboresho. Aidha, Kituo cha upimaji wa manteki ya mafuta cha Misugusugu kinatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018.

**h) Kuhamasisha Matumizi ya TEHAMA katika Kutekeleza Majukumu ya Wakala**

**287.** *Mheshimiwa Spika*, Wakala imendelea na matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utendaji kazi. Aidha, mifumo mbalimbali inatumika ikiwemo; *Shakira*, *EPICOR*, *Asset Management System*, pamoja na mfumo wa ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa (pre-packed goods).

**i) Ukaguzi wa Bidhaa Zilizofungashwa kwenye Maeneo Mbalimbali ya Mipakani, Bandarini na Viwandani**

**288. Mheshimiwa Spika**, Wakala imeendelea kuongeza nguvu katika kukagua bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya viwanda; vituo vya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mwanza pamoja na mipaka ya Horohoro, Holili, Mtukula, Namanga, Kasumulu, Tunduma na Sirari. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2017- Januari 2018, aina za bidhaa 2,272 zilikaguliwa ikilinganishwa na aina 1,985 zilizokaguliwa kwa kipindi hicho kwa mwaka uliopita.

**3.4.15 Tume ya Ushindani**

**a) Kudhibiti na Kupambana na Uingizaji na Uzalishaji wa Bidhaa Bandia**

**289. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Ushindani (FCC) ilifanya kaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na bandari kavu (ICDs) ambako jumla ya makasha (makontena) 4,004 yalিকaguliwa na kati ya hayo makasha 415 yalibainika kuwa na bidhaa mbalimbali zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 kama ilivyorekebishwa. Tume pia ilifanya kaguzi za kushtukiza zipatazo 13 kwenye maduka na maghala jijini Dar es Salaam. Katika kaguzi hizo, watuhumiwa wapatao 56 walikamatwa na bidhaa bandia zikiwemo vilainishi vya magari, vifaa vya mabomba na kofia ngumu za pikipiki. Pia, Tume ilifanya operesheni saba (7) na kukamata bidhaa zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma, Iringa, Morogoro, Mtwara, Shinyanga, Songwe na Tanga. Katika operesheni hizo, watuhumiwa wapatao 94 walikamatwa na bidhaa bandia zikiwemo dawa za meno na miswaki, wino (toner), mvinyo, vifaa vya ujenzi, vifaa vya mabomba, mabati ya kuelekea, viatu na sabuni. Bidhaa zingine zilizokamatwa ni mafuta ya maji ya kupaka, pampu za kumwagilia maji, maji ya tindikali, na pikipiki. Vilevile, Tume iliendesha operesheni tano (5) za uteketezaji na kugawa bidhaa bandia zilizo thibitika kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa.



**290. Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea na mapambano dhidi ya bidhaa bandia kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali vikiwemo TBS, TFDA na Jeshi la Polisi nchini na Mtandao wa Polisi wa Kimataifa INTERPOL. Kupitia ushirikiano huo, Tume imefanikiwa kutekeleza operesheni nne (4).

**b) Uchunguzi na Usikilizaji wa Mashauri Ushindani;**

**291. Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kuchunguza makubaliano ya siri ambayo yanakiuka Sheria ya Ushindani katika maeneo mbalimbali yakiwemo; Sekta Ndogo ya Mafuta, Uuzaji na Ununuzi wa Vifaa Tiba na Haki za Utangazaji wa Michuano ya Mpira wa Miguu.

**c) Kuchunguza Mashauri yanayohusu Miungano ya Makampuni**

**292. Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kuchunguza miunganiko ya siri ambayo inakiuka Sheria ya Ushindani (Un-notified mergers) katika maeneo mbalimbali yakiwemo; Sekta ya Nishati na Madini, Sekta Ndogo ya Saruji, Mabenki, Utalii na Vinywaji baridi. Pia, Tume imepitisha maombi 28 ya muungano wa makampuni yaliyowasilishwa mbele ya Tume. Katika maombi hayo yaliyopitishwa, 17 yalipitishwa bila masharti na 11 yalipitishwa kwa masharti.

**d) Utekelezaji wa Sheria juu ya Mashauri yahasuyo Matumizi Mabaya ya Nguvu katika Soko (Abuse of Market Power)**

**293. Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kuchunguza mashauri yanayohusisha matumizi mabaya ya nguvu ya soko yanayofanywa na baadhi ya washindani. Mashauri hayo yalijitokeza katika maeneo mbalimbali yakiwemo; sekta ndogo za tumbaku, filamu, benki na vinywaji.

**e) Utafiti wa Masoko ili Kubaini Mienendo Inayofisha Ushindani katika Masoko**

**294. Mheshimiwa Spika**, Tume imeendelea kukamilisha tafiti mbili (2) katika miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara nchini na sekta ndogo ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea. Tafiti katika miradi ya ujenzi wa barabara inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2017/2018 wakati tafiti katika soko la mbolea nchini upo katika hatua za awali za uandaaji wa *concept paper* na unategemewa kukamilishwa ifikapo robo ya kwanza ya mwaka ujao wa fedha. Aidha, Tume itaendelea na mpango wake wa kufanya utafiti katika Sekta ya Afya kwa lengo la kubaini matatizo ya kiushindani katika soko hilo.

**f) Kumlinda na Kumuelimisha Mlaji**

**295. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018 malalamiko 39 ya walaji yaliwasilishwa ambapo malalamiko 21 yalipatiwa ufumbuzi, malalamiko mawili (2) yanafanyiwa uchunguzi, malalamiko tisa (9) yapo katika hatua ya usuluhishi na malalamiko 7 yanaendelea kufuatiliwa. Aidha, asilimia 80 ya malalamiko yalihusiana na bidhaa za kielektroniki na asilimia 20 yalihusiana na vitendo hadaifu na danganyifu sokoni. Tume ilitoa elimu kwa umma katika maonesho ya wakulima ya Nane Nane yaliyofanyika kitaifa mkoani Lindi na DITF yaliyofanyika Jijini Dar-es Salaam. Maonesho hayo ni fursa nzuri ya kuwaeleza wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu shughuli za Tume, kugawa vitini na kufanya vipindi mubashara vya radio. Aidha, Tume imeendesha vipindi 11 vya radio na kwenye luninga kwa madhumuni ya kuelimisha umma kuhusu haki na wajibu wa mlaji na jinsi ya kuzitambua bidhaa bandia nchini.

**296. Mheshimiwa Spika**, pia, Tume iliendesha semina kwa ajili ya wahariri wa vyombo vya habari kwa lengo la kuhakikisha wadau hao wanapata uelewa wa kuweza kuelimisha jamii kuhusu masuala ya utetezi wa mlaji na udhibiti wa bidhaa bandia nchini. Makala tisa (9) zimetolewa katika magazeti mbalimbali yanayosomwa sana

zikielimisha umma kuhusu masuala ya utetezi wa mlaji, madhara ya bidhaa bandia na udhibiti wa bidhaa hizo. Tume imeandaa utaratibu wa kuanzisha vilabu (clubs) katika shule za msingi Mkoani Dodoma ili kujenga uelewa wa masuala ya utetezi wa mlaji kwa watoto ili kuwa na kizazi kinachoelewa haki na wajibu wao wangali wadogo ili waweze kujisimamia vizuri katika uchumi wa soko.

**g) Kufanya Mapitio na Usajili wa Mikataba ya Walaji**

**297. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, mikataba 196 ya walaji ilipokelewa kwa ajili ya kupitiwa na kusajiliwa. Aidha, mikataba 24 ya walaji ilipitiwa na kusajiliwa na Tume baada ya kukidhi vigezo kulingana na kanuni zinazo simamia mikataba ya walaji.

**3.4.16 Baraza la Ushindani**

**a) Kusikiliza na Kutoa Maamuzi ya Kesi za Rufaa**

**298. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Baraza lilipokea kesi 46, kati ya hizo, rufaa ni 24 na maombi ni 22. Vilevile, kulikuwa na kesi 33 zilizokuwa hazijaamuliwa katika kipindi cha 2016/2017 na hivyo kufanya kesi zinazopaswa kusikilizwa na kuamuliwa kwa mwaka 2017/2018 kuwa 79. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Baraza liliweza kusikiliza na kuamua kesi 25 na kesi 54 zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

**b) Kuongeza Uwezo wa Baraza Kushughulikia Kesi zinazohusu Masuala ya Ushindani wa Kibiashara.**

**299. Mheshimiwa Spika**, Baraza limewezesha wajumbe na watumishi wa Baraza kushiriki mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na taaluma katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, mafunzo hayo yamejumuishia *induction course* kwa Wajumbe wa Baraza, mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wawili (2) na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 13. Mafunzo hayo yamejikita katika nyanja za utawala, uhasibu, manunuzi, huduma kwa wateja, sheria na kazi za Baraza.

c) **Kuelimisha Umma kuhusu Kazi za Baraza**

**300. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Baraza limetoa elimu katika masuala yanayohusu ushindani wa kibiashara kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya DITF yaliyofanyika katika viwanja vya Mwl. Julius K. Nyerere vilivyopo katika Jiji la Dar es Salaam, Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Ngongo mkoani Lindi, Maonesho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika Viwaja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam na Maadhimisho ya Siku ya Haki za Mlaji Duniani yaliyofanyika Mkoani Kagera.

**301. Mheshimiwa Spika**, Baraza pia limetoa elimu ya uelewa juu ya utendaji kazi wa Baraza na masuala yanayohusu ushindani wa kibiashara kwa wadau wa Baraza katika Mkoa wa Morogoro ambapo wadau wa Baraza wakiwemo mahakimu, mawakili, waandishi wa habari pamoja na wawakilishi kutoka asasi za kidini na zisizo za kiserikali.

### **3.4.17 Chuo cha Elimu ya Biashara**

a) **Ujenzi ya Maktaba Mpya, Madarasa, Kumbi za Mihadhara katika Kampasi ya Dar es Salaam**

**302. Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika Kampasi ya Dar es Salaam umeanza na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2018/2019. Kazi zinazofanywa ni kuongeza ghorofa nne katika jengo la zamani la Kafeteria ili kuweza kuongeza kumbi za mihadhara, ofisi za walimu pamoja na maktaba kubwa na ya kisasa. Gharama ya utekelezaji wa mradi huo ni Shilingi 3,180,000,000 na tayari Chuo kimefanya upembuzi yakinifu (Feasibility study) ya mradi huo.

b) **Ujenzi na Ukarabati wa Majengo Kampasi ya Mwanza**

**303. Mheshimiwa Spika**, Chuo kimenunua eneo lenye ukubwa wa ekari 10.9 huko Nyasaka Mwanza ambalo awali lilikuwa ni Shule ya Sekondari *Crest Hill*. Eneo hilo lina majengo ambayo yalikuwa yakitumika kama ofisi na

madarasa. Chuo kimekarabati majengo ya madarasa, ofisi za walimu, hosteli pamoja na kafeteria. Kazi zinazofanywa ni kuweka vigae sakafuni, kupaka rangi, kuweka madirisha na milango mipya kutandaza mfumo mpya wa mabomba ya maji safi na maji taka, ukarabati wa vyoo na kubadilisha masinki. Gharama iliyotumika kufanya ukarabati huo ni Shilingi Milioni 800.

c) **Kuboresha Mifumo ya TEHAMA**

**304. Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeboresha mifumo yake ya TEHAMA katika kampasi zote nne. Mifumo hiyo inajumuisha kufunga mifumo ya kihisibu (PASTEL), na usajili wa wanafunzi uliunganishwa na wa kihisibu (SARIS).

d) **Kuimarisha Uwezo wa Watumishi (Capacity Building)**

**305. Mheshimiwa Spika**, watumishi 78 wapo katika mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za shahada ya uzamivu (PhD), shahada ya uzamili (Masters degree), shahada ya kwanza (bachelor degree) na stahhada (Diploma). Kati ya wafanyakazi 40 wanaochukua shahada ya uzamivu, 29 ni wanaume na 11 wanawake; 28 wanasoma ndani ya nchi (21 wanaume, na 7 wanawake) na 12 wanasoma nje ya nje (8 wanaume, na 4 wanawake). Kati ya watumishi 32 wanaochukua shahada ya uzamili, 28 ni wanaume na wanne (4) wanawake; kati yao 22 wanasoma ndani ya nchi (18 wanaume, 4 wanawake) na 6 wanasoma nje ya nchi (wote wanaume). Kati ya watumishi wane (4) wanaochukua shahada ya awali, wawili (2) ni wanaume na wawili (2) ni wanawake. Kwa upande wa stahahaha, watumishi ni wawili (2) ambao wote ni wanaume.

**4.0 MWELEKEO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

**306. Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya viwanda iliyotolewa ni taswira kuwa ujenzi wa uchumi wa viwanda unatazamwa kuwa kiini cha mageuzi yenye kuleta mafanikio na mwelekeo wa maisha bora na yenye furaha kwa kizazi cha sasa na

kijacho. Kwa maneno mengine, ujenzi wa uchumi wa viwanda ni suala jumishi, unganishi na shirikishi. Muunganiko (forward and backward linkage) wa uzalishaji katika Sekta ya Viwanda na sekta nyingine ni muhimu katika uchumi wa nchi (economic complementarity). Tanzania inatambua umuhimu huo na msingi mkuu wa ujenzi wa uchumi wa viwanda umewekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo imelenga kufikia uchumi wa kati wa viwanda wenye muunganiko ifikapo mwaka 2025.

**307. Mheshimiwa Spika**, dhamira ya ujenzi wa uchumi wa viwanda imefafanuliwa zaidi na kuwekewa mikakati katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017– 2020/2021. Msisitizo mkuu ni maendeleo ya viwanda vinavyotumia malighafi zinazozalishwa nchini hususan mazao ya kilimo (mafuta ya kula, sukari, vyakula na vinywaji), madini (chuma) na kemikali. Aidha, Serikali imeahidi kusimamia na kutekeleza mipango hiyo kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Vilevile, viongozi wa ngazi ya juu wa Serikali wametoa msisitizo juu ya dhamira ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kupitia hotuba katika Bunge na mikutano mbalimbali. Miongozo hiyo ndiyo nguzo ya Sheria, Sera, Mikakati na Mipango yote ya kisketa katika uwekezaji na ujenzi wa uchumi wa viwanda na kufanya biashara nchini.

**308. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Mwaka Mmoja wa Maendeleo wa Mwaka 2018/2019 unaweka msisitizo katika kushirikisha zaidi Sekta Binafsi kutumia fursa zilizopo na vivutio vinavyotolewa na Serikali kujenga viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati ili kuchochea ujenzi wa viwanda vipya na kuendeleza vilivyopo. Aidha, miradi mikubwa ya viwanda vya kimkakati na vya kielelezo itaendelea kutiliwa mkazo.

**309. Mheshimiwa Spika**, kwa misingi hiyo, mwelekeo wa kisketa ni kuhakikisha kuwa, nyaraka zote za kisketa zinazoongoza uwekezaji, uzalishaji na ufanyaji biashara nchini zinaboreshwa kwa kuzingatia mazingira na matakwa ya nyakati hususan ushindani wenye haki na

kuwezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika kuzalisha na kutumia mali, huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa, mchango wa sekta katika Pato la Taifa unakua, ajira kwa Watanzania zinazalishwa na kulindwa, bidhaa zinazalishwa kwa wingi hususan zile zinazotumika na wananchi walio wengi, uzalishaji wenye tija unahimizwa, kipaumbele kikiwa kutumia rasilimali zilizopo nchini, viwanda vya ndani vinapata ulinzi wenye tija na shindani, viwanda vipya vinajengwa na kuendelezwa, viwanda vilivyopo vinaendelea kuzalisha kwa malengo yaliyokusudiwa na vile vyenye changamoto kupata tiba stahiki.

**310. Mheshimiwa Spika,** katika ujenzi wa viwanda, uendelezaji na ulinzi wa viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati litakuwa jukumu letu la kipaumbele na kuhakikisha kuwa Taasisi zinazohusika kuendeleza viwanda hivyo zinajengewa uwezo unaotakiwa kumudu majukumu na matakwa ya wadau katika maeneo yote nchini. Kuweka mifumo muhimu ikiwemo miundombinu ya msingi na saidizi pamoja na ujenzi wa soko la ndani vitapewa msukumo wa kipekee ili kuleta tija kwa gharama nafuu kwa wawekezaji wa ndani ya nchi yetu. Mipango ya kuboresha na kurahisisha mazingira ya uwekezaji na biashara itaendelea kuwa ajenda ya kudumu ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi yenye mvuto kwa uwekezaji na kufanya biashara.

**311. Mheshimiwa Spika,** msukumo mkubwa kwa sasa ni kuendeleza viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati kutokana na mchango wake katika uchumi ulio shirikishi. Msingi wa msukumo huo ni kuwa viwanda vidogo vinasambaa kirahisi katika kila kona ya nchi na pia viwanda hivyo humilikiwa na wananchi wenyewe na hivyo inakuwa rahisi kviendeleza na kupanua wigo wa makusanyo ya kodi. Ndio maana hata sasa nchi zilizoendelea kiviwanda duniani kwa kiasi kikubwa uchumi wao unachangiwa na sekta hiyo. Mathalani, katika nchi ya Ujerumani sekta hiyo inachukua asilimia 99 ya Sekta ya Viwanda, Marekani asilimia 99.7, Ufaransa asilimia 98, Australia asilimia 97 na Italia asilimia 98.

Kwa Bara la Afrika, nchi zilizopiga hatua kama vile Afrika Kusini, sekta hiyo inachukua asilimia 91 na Ghana asilimia 92 ya viwanda vyote. Hivyo, ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda, hatuna budi kuelekeza nguvu kubwa katika kubuni mikakati ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati. Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi pamoja na kubuni mikakati mbalimbali ili kuziwezesha shughuli za ujasiriamali mdogo na wa kati kukua na kuongeza tija.

**312. Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yana lenga kukumbusha dhamira ya Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda na nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano kutekeleza ajenda ya viwanda ili kuleta maendeleo endelevu kwa kasi na maisha bora kwa Watanzania. Hivyo, vipaumbele na mipango kwa mwaka 2018/2019 inatokana na mipango ya kitaifa ambayo imeanishwa hapo juu.

**313. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nielezee vipaumbele na malengo ya sekta kwa mwaka 2018/2019.

## **5.0 VIPAUMBELE NA MALENGO YA MWAKA 2018/2019**

### **5.1 VIPAUMBELE KWA MWAKA 2018/2019**

**314. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2018/2019, vipaumbele vya Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake ni kutunisha mtaji wa NEDF; kuendeleza miradi ya kielelezo ya: Mchuchuma na Liganga, Magadi Soda Engaruka, na Kiwanda cha Matairi Arusha; Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO Kibaha, Mradi wa kuunganisha Matrika ya URSUS, uendelezaji wa Mitaa/maeneo ya viwanda vya SIDO; Kuendeleza Kanda Kuu za Uchumi (Ruvuma, Tanga, Kigoma na Manyoni); Bagamoyo SEZ & BMSEZ ; Kurasini Logistic Centre and Kigamboni Industrial Park; Kuendeleza utafiti katika taasisi za TIRDO, CAMARTEC na TEMDO; *Dodoma Leather and Dodoma SEZ*; na ujenzi wa *industrial parks*.

**315. Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo, Wizara itaweka msukumo wa pekee katika



kuhamasisha ujenzi wa Sekta Binafsi ya Kitanzania iliyo imara ili iweze kushiriki na kuchangia ipasavyo katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

## 5.2 MALENGO

### 5.2.1 Sekta ya Viwanda

**316. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Sekta ya Viwanda ina malengo yafuatayo:-

(a) Kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji viwandani pamoja na mahitaji ya bidhaa za viwanda kwa:-

- i) Kufanya tathmini ya sekta ya sukari;
- ii) Kufanya tathmini ya sekta ya mafuta ya kula;
- iii) Kufanya tathmini ya sekta ya vifaa vya ujenzi; iv) Kufanya tathmini ya sekta ya chuma;
- v) Kufanya tathmini ya sekta ya mbao na bidhaa za mbao;
- vi) Kufanya tathmini ya sekta ya ngozi na bidhaa za ngozi;
- vii) Kufanya tathmini ya sekta ya nguo na mavazi;
- viii) Kufanya tathmini ya sekta ya usindikaji vyakula (mchele, unga, mbaazi na vyakula vingine);
- ix) Kufanya tathmini ya usindikaji wa vyakula vya binadamu na wanyama; na
- x) Kufanya tathmini ya dawa za binadamu na vifaa tiba na vifungashio.

(b) Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996 – 2020 (Sustainable Industrial Development Policy - SIDP) na kuandaa Mkakati wa Utekelezaji;

(c) Kujenga uwezo wa taasisi za utafiti za wizara kwa:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i) kuimarisha uwezo wa maabara za utafiti;
- ii) kuhamasisha usambazaji wa teknolojia zinazobuniwa na taasisi; na
- iii) kuhamasisha Sekta Binafsi kutumia teknolojia husika.

(d) Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya viwanda mama na Miradi ya Kimkakati kwa:-

- i) Kukamilisha uchambuzi wa mikataba ya Mradi kwa kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017;
- ii) Kutafuta wawekezaji wa mradi magadi soda wa Engaruka na mradi wa kiwanda cha matairi cha Arusha; na
- iii) Kukamilisha taratibu za kumpata mwekezaji na kuanza utekelezaji wa mradi wa Kurasini SEZ.

(e) Kuendelea na utekelezaji wa mikakati mikuu ya kuendeleza sekta za alizeti, ngozi na bidhaa za ngozi, pamba mpaka mavazi, na viwanda vya dawa;

(f) Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini kwa:-

- i) kuendelea kutenga maeneo ya uwekezaji kwa kuzingatia msambao wa viwanda nchi nzima;
- ii) kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika sekta za kipaumbele na kuendeleza maeneo ya uwekezaji; na

iii) kushiriki makongamano ya uwekezaji yatakayofanyika mikoa mbalimbali nchini.

**5.2.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

**317. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo na biashara ndogo nchini kwa:-

i) Kushirikiana na Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda na biashara kwa kulenga mahitaji ya sasa na baadae;

ii) Kutengeneza kanzidata ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati;

iii) Kuhamasisha wajasiriamali kuchangamkia masoko ya ndani na nje ya nchi;

iv) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda kupitia mwongozo wa ujenzi wa viwanda kwa Mamlaka za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

v) Kuhamasisha na kuelimisha wajasiriamali namna ya kuanzisha na kuendeleza biashara. Kitabu chenye taarifa muhimu za namna ya kuanzisha biashara nchini hasa kwa wajasiriamali wadogo kitatumika.

(b) Kuwezesha uanzishwaji wa kongano la karanga kwa:-

i) Kuhamasisha wajasiriamali kulima zao la karanga kwa lengo la kutumia nafasi ya kongano litakaloanzishwa la kuongeza thamani zao hilo; na

ii) Kutafuta rasilimali za kuendeleza kongano la karanga.

(c) Kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- i) Kufanya tafiti za kina katika maeneoyaliyoanishwa;
  - ii) Kukamilisha mfumo wa uratibu wa sekta; na
  - iii) Kukamilisha mfumo wa kuwezesha sekta kifiedha.
- (d) Kuendelea kusimamia Mfuko wa NEDF kwa:-
- i) Kuongeza mtaji wa Mfuko; na
  - ii) Kufuatilia maendeleo ya mfuko huo;
- (e) Kutumia SIDO kama nyezo ya kujenga viwanda vidogo na vya kati kwa:-
- i) Kuendelea kulifanyia maboresho Shirika la SIDO; na
  - ii) Kuhamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia na viitamizi.

### **5.2.3 Sekta ya Uwekezaji**

**318. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Uwekezaji itatekeleza malengo yafuatayo:

- (a) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996 kwa:-
  - i) Kuratibu uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji;na
  - ii) Kuendelea kuchochea uwekezaji nchini kupitia ushiriki kwenye mikutano, makongamano na warsha za uwekezaji zinazofanyika ndani na nje ya nchi;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(b) Kukamilisha mapitio ya Sera, Mkakati na Sheria ya Uwekezaji kwa:-

i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996;

ii) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uwekezaji ya 1997; na

iii) Kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji.

(c) Kufuatilia miradi ya uwekezaji nchini kwa:-

i) Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji nchini; na

ii) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya miradi iliyosajiliwa na TIC.

(d) Kuratibu kwa karibu uwekezaji katika sekta maalum kwa:-

i) Kuhamasisha uwekezaji katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari;

ii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu (deep sea fishing) na viwanda vya samaki; na

iii) Kuboresha vivutio vya uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi.

**5.2.4 Sekta ya Biashara**

**319. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Biashara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini kwa:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

i) Kuendeleza majadiliano ya biashara kwenye nchi za China, Urusi, Mauritius, Uturuki, Misri, Israel, DRC Congo, Sudani ya Kusini, Vietnam na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuingia nazo makubaliano ya biashara kwa kushirikiana na sekta binafsi;

ii) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Continental Free Trade Area – CFTA);

iii) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;

iv) Kukamilisha majadiliano ya biashara ya huduma kwa sekta sita za kipaumbele katika nchi wanachama wa SADC;

v) Kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya biashara ya bidhaa na huduma; na

vi) Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo (WTO, UNCTAD, CFC na ITC).

(b) Kuhamasisha jumuiya ya wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatakonayo na majadiliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa;

(c) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measures*;

() Kutekeleza Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) unaohusu uwezeshaji wa Biashara;

(e) Kuendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara 2003;

(f) Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini ambazo ni; Kamati ya kusimamia Uondoaji wa Vikwazo vya Kibishara visivyokua vya kiushuru (NTBs); Kamati ya Urahisishaji Biashara (National Trade Facilitation Committee); Kamati ya usimamizi wa masuala ya Afya za Binadamu, Wanyama na Mimea (National SPS Committee); na Kamati ya Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (National TBT Committee); na

(g) Kuandaa miradi na program mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wataalamu na sekta binafsi katika majadiliano ya kikanda na kimataifa.

### **5.2.5 Sekta ya Masoko**

**320. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Masoko itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa:-

i) Kuondoa tozo kero, ada zinazojirudia na kurazinisha majukumu ya taasisi za udhibiti;

ii) Kuondoa mwingiliano wa majukumu ya taasisi za umma ili kupunguza gharama za uanzishaji na uendeshaji wa biashara;

iii) Kuhakikisha huduma za usajili wa biashara zinafanyika kupitia mitandao ya kompyuta (online registration) na usajili wa makampuni ufanyike kwa muda mfupi kadiri iwezekanavyo; na

iv) Kuhamisha jukumu la utoaji wa leseni za biashara toka Wizarani (Daraja A) kwenda BRELA na kutolewa katika kanda za Arusha, Dar, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza.

(b) Kuwaunganisha wazalishaji na masoko kwa:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

i) Kuwahamasisha wakulima kuzalisha na kuwaunganisha na viwanda vya usindikaji; na

ii) Kushirikiana na viwanda kutafuta masoko ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini;

(c) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa:-

i) Kuhamasisha sekta binafsi kujenga maghala;

ii) Kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa maeneo yote yanayozalisha zao la korosho;

iii) Kuanzisha matumizi ya Mfumo kwa mazao ya ufuta, mbaazi, mahindi na nafaka; na

iv) Kuunganisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na soko la mazao na bidhaa (commodity exchange).

(d) Kutafiti na kutafuta masoko mapya ndani na nje ya nchi hususan katika nchi za Afrika Mashariki, DRC, China, Mashariki ya Kati, Mashariki ya mbali, Ulaya, na nchi nyingine kwa:-

i) Kuanisha mahitaji ya soko kwa kila zao na kuwaunganisha wazalishaji wa mazao husika na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi;

ii) Kuimarisha na kuboresha taarifa za uzalishaji, masoko na kusambaza taarifa kwa wadau katika mnyororo wa thamani kupitia tovuti na aina nyingine za mawasiliano;

iii) Kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa na mazao yanayozalishwa ndani ya nchi; na



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

iv) Kuimarisha matumizi ya fursa za masoko nje ya nchi kupitia mikataba ya ushirikiano kati ya nchi na nchi, Kanda na Kimataifa.

(e) Kuhamasisha matumizi ya Vituo maalum vya kuuzia mazao kwa:-

i) Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo maalum vya kuuzia mazao;

ii) Kusimamia matumizi ya vituo hivyo ili vitumike kwa uuzaji na ununuzi wa mazao;

iii) Kuhamasisha ushindani katika ununuzi na uuzaji wa mazao ili mkulima apate bei nzuri; na

iv) Kusimamia na kuhimiza matumizi ya vipimo rasmi kwa nia ya kumlinda mlaji.

(f) Kuimarisha biashara na masoko ya mipakani kwa:-

i) Kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujenga Vituo vya Pamoja Mipakani-OSBP;

ii) Kutoa elimu kwa jamii ya wafanyabiashara kuhusu fursa na taratibu za kufanya biashara ya mipakani (cross border trade); na

iii) Kuwezesha wafanyabiashara hususan wafanyabiashara wadogo kufanya biashara ya mipakani kwa urahisi kwa kuboresha mazingira ya biashara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine mpakani.

(g) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania kwa:-

i) Kuwapatia mabanda wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na makundi maalum kutangaza bidhaa kupitia maonesho;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ii) Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali na wafanyabiashara wa Tanzania katika maonesho ya ndani na nje ya nchi; na

iii) Kuratibu ushiriki wa sekta binafsi na wataalam wa Serikali katika safari maalum za kutafuta fursa za masoko nje ya nchi.

(h) Kuimarisha na kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko kwa:-

i) Kupanua wigo wa vyanzo na aina ya taarifa za masoko; na

ii) Kutoa vitendea kazi vya kisasa kwa vyanzo vya taarifa na kukuza matumizi ya TEHAMA kukusanya na kusambaza taarifa muhimu za masoko.

(i) Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali kwa:-

i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy);

ii) Kuandaa Sera ya Ubora ya Taifa (National Quality Policy);

iii) Kukamilisha Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu;

iv) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 na Kanuni zake;

v) Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999;

vi) Kuandaa kanuni za utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Vipimo ya 2016;

vii) Kushirikiana na OR-TAMISEMI kuandaa sheria ndogo ya kusimamia matumizi ya vipimo rasmi katika biashara ngazi ya vitongoji, vijiji na wilaya; na

viii) Kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje.

(j) Kukamiliasha taratibu za kuridhia itifaki ya Marakhesh kwa:-

i) Kukusanya maoni ya wadau kuhusu mkataba huo,

ii) Kuchambua maoni ya wadau, na

iii) Kuandaa andiko kuhusu umuhimu wa kuridhia itifaki hiyo

### 5.3 MALENGO YA TAASISI CHINI YA WIZARA

#### 5.3.1 Shirika la Maendeleo la Taifa

**321. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) litatekeleza malengo yafuatayo,

(a) Kuendeleza mradi unganishi wa makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga kwa:-

i) kurejea tathmini ya mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi na kulipa fidia;

ii) Kupitia upya vivutio kwa ajili ya uwekezaji,

iii) Kutangaza mradi kwa wawekezaji,

iv) kuelimisha wananchi kuhusu faida za mradi katika Mkoa wa Njombe; na

v) kuratibu na kufuatilia kazi za miradi

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(b) Kuendeleza mradi wa kuzalisha Magadi wa Engaruka kwa:-

- i) Kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi;
- ii) kusimamia ujenzi wa miundombinu wezeshi;
- iii) kulipa tozo ya ardhi;
- iv) kufanya utafiti wa faida za kiuchumi za mradi; na
- v) Kutangaza mradi kwa wawekezaji

(c) Kuendeleza mradi wa ufufuaji wa Kiwanda cha Matairi Arusha kwa:-

- i) kuandaa taarifa ya kina ya upembuzi yakinifu ambayo inaweza kuvutia taasisi za fedha;
- ii) kuratibu ununuzi wa mitambo na mashine za kiwanda;
- iii) Kutangaza mradi kwa ajili ya kupata wawekezaji na kulipa tozo ya ardhi.

(d) Kuendeleza mradi wa mashamba ya mpira Morogoro na Tanga;

(e) Kuendeleza mradi wa kujenga miundombinu katika eneo la viwanda la TAMCO Kibaha kwa:-

- i) kuratibu ujenzi wa mtandao wa barabara za ndani ya eneo la mradi;
- ii) Kujenga uzio kuzunguka eneo la mradi;
- iii) kusanifu na kujenga bwawa la maji taka (oxidation pond) na kusimamia shughuli za ujenzi.

(f) Kuendelea kutekeleza Mradi wa Kuunganisha Matrika aina ya URSUS katika eneo la TAMCO Kibaha kwa:-

- i) Kugharamia uingizaji wa vifaa bandarini na kuvipeleka kwenye eneo la mradi;
- ii) Kuratibu uunganishaji wa matrika mapya,
- iii) Kuratibu ujenzi wa kiwanda kipya,
- iv) Kuratibu mauzo,
- v) kusimamia uanzishwaji wa maeneo mengine nane ya kufanya matengenezo ya matrika yaliyounganisha nchini; na
- vi) kulipa tozo ya ardhi;

### **5.3.2 Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa Kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi**

**322. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kukamilisha majadiliano na kuendelea kutekeleza miradi ya maeneo huru ya Bagamoyo SEZ na Benjamin Mkapa SEZ kwa:-

i) Kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya ndani (Detail design of onsite infrastructure-Roads) katika eneo la kituo cha Teknolojia Bagamoyo (Bagamoyo Technological Park);

ii) Kuandaa nyaraka za kisheria kwa ajili ya mradi wa Bagamoyo SEZ;

iii) Kukamilisha hatua zote za utwaaji wa Ardhi na kufanya upimaji wa eneo ili kupata hati miliki ya eneo lililokwishalipiwa fidia katika eneo la Bagamoyo SEZ;

iv) Kuratibu uendelezaji wa mradi wa Bagamoyo SEZ; na

v) Kukarabati miundombinu ya ndani ya eneo la Benjamin William Mkapa SEZ ikiwa ni pamoja na kukarabati mifumo ya uhifadhi na upitishaji wa maji na kujenga upya ukuta ulioanguka na kuweka kamera za ulinzi katika eneo la Benjamin Mkapa SEZ.

b) Kutekeleza mradi wa Kurasini Trade and Logistic Centre (Kurasini SEZ) kwa:-

i) Kukamilisha malipo ya fidia kwa wakazi watatu (3) ambao nyumba zao hazikuthaminiwa awali baada ya kurukwa na Mthamini Mkuu wa Serikali wakati wa zoezi la Uthamini; na

ii) Kuwezesha kuanza utelekezaji wa mradi. c) Kuendeleza Maeneo ya SEZ kwa:-

i) Kumaliza malipo ya fidia katika maeneo ya SEZ yaliyokwisha fanyiwa uthamini ya Tanga; Kigoma, Ruvuma na Manyoni;

ii) Kufanya utafiti wa faida za kiuchumi za mradi katika eneo maalum la uwekezaji Dodoma;

iii) Kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya ndani (*Detail design of on site infrastructure (Roads, Water, Power and Telecommunication)*) katika eneo la Kigamboni *Industrial Pack*; na

iv) Kuratibu ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha maeneo ya miradi.

### **5.3.3 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania**

**323. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) limepanga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira na zinazolenga matumizi bora ya nishati;

b) Kuanzisha na kuhakiki maabara ya makaa ya mawe, na maabara ya mafuta na gesi itakayokuwa na viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

c) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards';

d) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya chakula, mazingira, kemia, na maabara ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

e) Kuanzisha na kuhakiki (Accreditation) maabara ya vipimo vya chuma kigumu (Iron and Steel metallurgy laboratory);

f) Kufanya matengenezo ya vifaa vya maabara ya mazingira, chakula na kemia;

g) Kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuleta teknolojia mpya za uzalishaji, na

h) Kuhuhisha teknolojia ya kutumia *sensor* kufuatilia uzalishaji viwandani kwa wajasiriamali (sensor industrial process monitoring).

### **5.3.4 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini**

**324. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) kitatekeleza ufuatayo:-

- a) Kuendelea kufanya utafiti na kuunda teknolojia zinazolenga kuongeza tija na kupunguza kazi za sulubu na zenye kuchosha katika shughuli za kilimo vijijini;
- b) Kuendelea kuhamasisha utengenezaji wa mashine za kilimo, zana za kilimo na teknolojia nyingine za ufundi vijijini;
- c) Kusimamia utekelezaji wa kanuni za majaribio na ukaguzi wa zana za kilimo na teknolojia za ufundi vijijini; na
- d) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya utafiti ya Kituo.

### **5.3.5 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo**

**325. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) kitatekeleza yafuatayo:-

- a) Kujenga miundombinu ya kiatamizi cha teknolojia na biashara pamoja na kuwajengea uwezo wajasiriamali wa kati na wadogo kuanzisha viwanda vya kuunda na kutengeneza mashine na mitambo;
- b) Kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi kwa ujumla;
- c) Kupitia upya sheria iliyoanzisha Taasisi ya TEMDO, kutengeneza kanuni zake, na kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Taasisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu;
- d) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo ili kuongeza thamani;
- e) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kusindika chai;



f) Kubuni na kuendeleza utengenezaji wa mtambo wa kuweka baridi (cold room) ili kuhifadhi bidhaa mbalimbali kama vile mboga mboga, mazao ya mifugo, bidhaa za hotelini, machinjio;

g) Kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kutengeneza brikwiti kutokana na vumbi la makaa ya mawe;

h) Kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa teknolojia za kuzalisha bidhaa za marumaru kama vile vigae vya marumaru (ceramic tiles) kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini;

i) Kufanya utafiti ili kubainisha mahitaji ya soko katika teknolojia na huduma za kitaalamu pamoja na kutangaza shughuli za Taasisi kupitia vyombo vya habari na kushiriki kwenye maonesho ya kibiashara (DITF, Nane Nane, Maonesho ya kanda ya SIDO) ili kutangaza teknolojia zinazobuniwa na Taasisi; na

j) Kuanzisha na kuwezesha mpango wa kusambaza viwanda nchini kwa utaratibu wa kiwanda kimoja kila wilaya (One District One Factory - ODOF).

### **5.3.6 Kampuni ya Mbolea Tanzania**

**326. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kusambaza mbolea tani 95,000 za aina ya DAP (tani 30,000), UREA (tani 30,000), SA (tani 5,000), CAN (tani 5,000), NPK (tani 10,000), SULPHUR (tani 15,000) nchi nzima;

b) Kukamilisha majadiliano na kusaini mkataba wa ushirikiano baina ya Kampuni ya TFC kwa upande wa Serikali ya Tanzania na: OCP-SA kwa upande wa Serikali ya Morocco kuhusu mbolea aina ya DAP; na Kampuni ya Sirius PLC ya Uingereza utakaohusu mbolea za aina ya NPKs; na

c) Kufanikisha uagizaji wa tani 15,000 za *Sulphur* ya unga.

### 5.3.7 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo

**327. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) litatekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO na kutengeneza Mfumo Unganishi wa shughuli za TEHAMA za Shirika kwa:-

i) Kujenga miundombinu ya viwanda (barabara mifumo ya maji, umeme, mitaro, ya maji taka na uzio) katika mikoa ya Morogoro, Mara, Shinyanga, Lindi, Songea, Sumbawanga na Singida;

ii) Kujenga majengo (industrial sheds) ya viwanda katika mikoa ya Morogoro, Katavi, Simiyu na Njombe;

iii) Kujenga ofisi tatu (3) za kutolea huduma katika Mikoa ya Morogoro, Songwe na Katavi;

iv) Kuhamasisha matumizi ya majengo ya shughuli za viwanda *industrial sheds*; na

v) Kutengeneza mfumo unganishi wa shughuli za TEHAMA za Shirika.

b) Kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na kati chini ya Mkakati wa Bidhaa Moja Wilaya Moja (ODOP) kwa:-

i) Kuboresha karakana za kutengenezea mashine na mitambo mbalimbali katika mikoa ya Arusha, Mbeya na Shinyanga; na

ii) Kuwezesha upatikanaji teknolojia za kutengeneza vifungashio.

c) Kuwezesha uhawilishaji wa teknolojia kwa:-

i) Kuimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) vilivyopo Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya na Shinyanga; na

ii) Kuanzisha vituo vya kiatamizi kwa ajili ya kuendeleza teknolojia na ubunifu katika Mikoa ya Singida, Arusha, Lindi na Mwanza.

d) Kuendesha Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF) kwa:-

i) Kutoa mikopo kwa wajasiriamali;

ii) Kutoa elimu ya uendeshaji miradi inayohusika na mikopo; na

iii) Kufuatilia urejeshwaji wa mikopo.

### **5.3.8 Kituo cha Uwekezaji Tanzania**

**328. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kitatekeleza yafuatayo:-

a) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za TIC;

b) Kuhamasisha, kuvutia na kuwezesha uwekezaji kwa kushiriki na kuandaa makongamano ya biashara na uwekezaji ndani na nje ya nchi;

c) Kuendelea kusajili miradi ya uwekezaji nchini;

d) Kuendelea kuboresha huduma za mahala pamoja kwa wawekezaji kwa kuongeza taasisi zinazohusika kutoa huduma kwa wawekezaji na kuongeza maofisa katika taasisi zilizopo;

e) Kuweka taarifa zote zinazohusiana na utaratibu wa usajili miradi na utoaji wa vibali na leseni za taasisi

mbalimbali kwa mfumo wa huduma za mahala pamoja (One Stop Shop) kwenye jarida moja;

f) Kupitia mkataba wa huduma kwa wawekezaji ili kuuboresha na kusimamia utekelezaji wake;

g) Kushirikiana na mamlaka za Serikali kutafuta maeneo yanye ardhi inayofaa kuwekeza kwa ajili ya wawekezaji na pia kushirikisha Sekta Binafsi kujenga miundombinu ya uwekezaji wa viwanda (Industrial Parks);

h) Kutoa huduma ya haraka kwa wawekezaji waliosajiliwa ili kutatua changamoto zinazokwamisha kuanza utekelezaji wa miradi;

i) Kutekeleza mkakati wa kuperemba miradi iliyosajiliwa kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kujua faida halisi kiuchumi zinazotokana na miradi hiyo kama kiasi cha ajira, mitaji na matumizi ya vivutio vinavyotolewa na Serikali; na

j) Kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuishauri Serikali jinsi ya kuboresha sera ya uwekezaji nchini.

### **5.3.9 Shirika la Viwango Tanzania**

**329. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) litatekeleza yafuatayo:-

a) Kutayarisha viwango 400 vya kitaifa katika sekta ndogo ndogo, ambavyo kati ya hivyo 180 ni vya uhandisi (*Engineering*) na 220 ni vya usindikaji (*Process Technology*);

b) Kutoa leseni za ubora kwa bidhaa 300 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);

c) Kukagua ubora wa bidhaa 36,000 zitokazo nchi za nje kabla ya kuingia nchini [Pre-shipment Verification of Conformity to Standards - PVoC (CoCs)];

d) Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 40,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;

e) Kutoa hati 40 chini ya mpango wa msaada wa kiufundi kwa wauzaji wa bidhaa za nje (Technical Assistance to Expoters - TAE);

f) Kutoa mafunzo na semina 32 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;

g) Kupima sampuli 21,000 za bidhaa mbalimbali;

h) Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 9 ,000;

i) Kuanzisha ofisi mpya 3 za mipakani;

j) Kuendelea na ujenzi wa maabara mpya ya Kisasa (New TBS Test House); na

k) Kuendelea kusimamia ubora wa bidhaa hasa zinazotoka nje ya nchi ili kulinda viwanda vya ndani kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma.

### **5.3.10 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni**

**330. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kuendelea kuboresha mifumo na taratibu za utoaji huduma kwa kutumia njia za kiteknolojia ili kutoa huduma bora na kwa wakati kwa:-

i) Kuendeleza mfumo wa kutoa huduma kwa njia ya Mtandao (ORS) ;

ii) Kuunganisha mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (ORS) na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali; na

iii) Kuingiza taarifa za Makampuni na Majina ya Biashara yaliyosajiliwa nje ya Mfumo wa ORS katika kanzidata ya mfumo mpya.

b) Kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kushirikiana na ofisi za maafisa biashara katika ngazi za mikoa na wilaya kwa kuanzisha vituo elimishi na saidizi katika ofisi za maafisa Biashara katika ngazi za Mkoa na Wilaya.

c) Kupitia sheria zote zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati na kuwezesha utoaji wa huduma zetu kwa njia ya mtandao;

d) Kutoa elimu na kuendeleza uhamasishaji wa usajili na urasimishaji wa biashara kwa,

i) Kuendelea kutoa elimu na uhamasishaji wa usajili na urasimishaji wa biashara kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na maafisa biashara kote nchini; na

ii) Kuendesha mafunzo na warsha mbalimbali kwa maafisa biashara mikoani na wilayani ili waweze kujua majukumu ya wakala na namna ya kutumia mifumo yake kwa lengo la kuwasaidia wananchi katika utoaji huduma za wakala mikoani na wilayani.

### **5.3.11 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala**

**331. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kuainisha na kufanya ukaguzi wa ghala zinazotumika chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

b) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo husika;

c) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa wadau wote ili wapate uelewa wa jinsi mfumo unavyofanya kazi;

d) Kupanua wigo wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mazao ya nafaka na mbegu za mafuta; na

e) Kuanzisha mfumo wa mawasiliano wa wadau kutoa maoni kwa njia ya mtandao kuhusu utekelezaji wa mfumo;

### 5.3.12 Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania

**332. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania (COSOTA) kitatekeleza yafuatayo:-

a) Kuhakikisha wabunifu wa kazi za sanaa wananufaika kwa kupata mirabaha stahiki ili:-

i) Kuongeza makusanyo ya mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki na kugawa kwa wabunifu husika;

ii) Kuendelea kusajili wanachama wabunifu na kazi zao;

b) Kutoa elimu kwa Umma na wabunifu kuhusiana na masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki;

c) Kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (anti piracy raids);

d) Kusimamia na kuhamasisha mashirika ya Utangazaji kulipa mirabaha ya kazi za wasanii; na

e) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki.

### **5.3.13 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania**

**333. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kutafuta masoko ya bidhaa za viwandani, mazao na bidhaa za mazao ndani na nje ya nchi;

b) Kutangaza bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini katika masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia maonesho ya kimataifa ya biashara;

c) Kuratibu na kudhibiti uendeshaji wa maonesho ya kimataifa nchini;

d) Kuimarisha Sekta Ndogo ya Biashara (SMEs) kwa kutoa mafunzo na taarifa za biashara na masoko; na

e) Kuendeleza Fursa za Biashara na Masoko ya Ndani;

### **5.3.14 Wakala wa Vipimo**

**334. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wakala wa Vipimo (WMA) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo na viingiavyo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji;

b) Kuendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipakani, bandarini, na viwandani kwa lengo la kuhakiki usahihi wa kiasi/ Idadi iliyotamkwa (decrealed quantity);

c) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari 10 na vitendea kazi vya kitaalam (Gas Mobile Prover, Electricity Meter Test Bench na Optical Scanner for Verification of fuel Tanks);



d) Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo;

e) Kuongeza idadi ya watumishi (Maafisa Vipimo 100 na Maafisa vipimo wasaidizi 50); na

f) Kujenga ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo Mkoani Dodoma na Kuboresha ofisi za Wakala za Mikoa.

### **5.3.15 Tume ya Ushindani**

**335. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:-

a) Kuboresha hali ya ushindani katika soko (Competition Protection and Promotion improved) kwa:-

i) Kuharakisha uchunguzi na kufanya maamuzi kwenye mashauri 15 yaliyoko mbele ya Tume;

ii) Kufanya tafiti tatu (3) katika sekta mbalimbali zenye lengo la kubaini mienendo inayokinzana na Sheria ya Ushindani; na

iii) Kutoa elimu na ushawishi juu ya uelewa wa Sheria ya Ushindani katika soko.

b) Kumlinda mlaji dhidi ya mienendo hadaifu (Consumer Protection Enhanced) kwa:-

i) Kufanya uchunguzi wa malalamiko ya walaji juu ya vitendo hadaifu vya wafanyabiashara nchi nzima na kuyatatua;

ii) Kuelimisha umma juu ya haki na wajibu wa mlaji kupitia semina na vipindi vya vyombo vya habari kwa nchi nzima; na

iii) Kuongeza mapambano dhidi ya bidhaa bandia na pia kuhakikisha kiwango cha bidhaa hizo kinapungua katika soko.

c) Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma (Service delivery capacity improved) kwa:-

i) Kuboresha vitendea kazi kwa kununua magari 13 mapya na kuyaondoa magari chakavu na kuweka mifumo ya kielektronikia ndani ya Tume;

ii) Kuongeza wafanyakazi mpaka kufikia 85 ukilinganisha na idadi ya sasa ya wafanyakazi ambao ni 53; na

iii) Kuanzisha ofisi Dodoma na ofisi za kanda katika mikoa ya Mwanza, Tanga na Mbeya.

### **5.3.16 Baraza la Ushindani**

**336. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Baraza la Ushindani (FCT) litatekeleza yafuatayo:-

a) Kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi 35 za rufaa zinazotokana na mchakato wa udhibiti wa ushindani wa kibiashara nchini;

b) Kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi wa Baraza na Wajumbe wa Baraza kwa lengo la kuwaongezea uwezo; na

c) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya Baraza na namna ya kuwasilisha rufaa katika Baraza.

### **5.3.17 Chuo Cha Elimu ya Biashara**

**337. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:-

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- a) Kuendeleza na kumaliza ujenzi wa ghorofa nne (4) katika jengo la 'Cafeteria' (Vertical Extension of Cafeteria Building) Kampasi ya Dar es Salaam;
- b) Ununuzi wa shule na majengo katika eneo la Nyasaka kwa ajili ya upanuzi na matumizi ya Kampasi ya Mwanza;
- c) Ujenzi wa Kampasi ya Mbeya katika eneo la Iganzo;
- d) Kuandaa Mpango Kamambe (Master Plan) katika Kampasi ya Zanzibar;
- e) Kuboresha Maktaba pamoja na mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha *Computer Labs 2* ili kuongeza ufanisi wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- f) Kuendeleza rasilimali watu kupitia mafunzo ya muda mrefu (Human Resources Development);
- g) Kufanya upembuzi yakinifu wa kuanzisha kampasi katika ukanda wa Kaskazini wa nchi;
- h) Kufanya upembuzi yakinifu katika ujenzi wa miundombinu kupitia ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (Public Private Partnership – PPP); na
- i) Kuimarisha miundombinu na kufanya ukarabati wa majengo wa kuimarisha uzio wa makazi ya watumishi wake Oysterbay, kuezeka upya hema la mihadhara Kampasi ya Dar es Salaam na ukarabati wa madarasa na ofisi.

### 5.4 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA UTOAJI HUDUMA

**338. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/2019, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- a) Kuhamisha watumishi 70 waliobaki katika awamu ya tatu kuja Dodoma;

b) Kuajiri watumishi wapya 25 wa kada mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya Wizara;

c) Kupandisha vyeo watumishi 183 wa kada mbalimbali;

d) Kujenga uwezo kwa rasilimali watu kwa kuwapeleka watumishi kumi na wanane (18) mafunzo ya muda mrefu na watumishi arobaini (40) katika mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi;

e) Kutathmini utendaji kazi watumishi (236) kwa kipindi cha mwaka mzima 2018/2019 kwa kutumia Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA au OPRAS);

f) Kujenga na kulinda afya za watumishi kwa kuandaa programu mbalimbali za michezo yakiwemo bonanza;

g) Kuendelea kuratibu shughuli za utoaji huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Taratibu, Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma; na

h) Kuhakikisha watumishi watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

## 5.5 MASUALA MTAMBUKA

### a) **Kupambana na Rushwa**

**339. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara itaongeza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kuweka na kutekeleza mikakati mbalimbali pamoja na kutoa mafunzo ya sheria, miongozo, kanuni na maadili ya utumishi wa Umma. Wizara itahakikisha, watumishi wanazingatia kanuni na taratibu zinazotoa miongozo katika kutoa huduma bora na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Aidha, Wizara haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote ambao itabainika kuwa

wanajihusisha na vitendo vya rushwa. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja katika utoaji huduma bora kwa wateja wa ndani na nje ya Wizara.

**b) UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza**

**340. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) mahala pa kazi pamoja na kutoa huduma bora kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuandaa semina za kuelimisha na kuwahamasisha watumishi kujikinga na VVU pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) na kuzingatia upimaji wa afya kwa hiari ili kuendeleza kampeni ya ujenzi wa afya bora kwa watumishi jambo ambalo ni muhimu kwa uchumi wa viwanda.

**c) Mazingira**

**341. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha uelewa wa athari za mazingira kwa wenye viwanda na wafanyabiashara sambamba na kuwashauri kutumia teknolojia rafiki (cleaner production technologies) kwa mazingira.

**d) Masuala ya Jinsia**

**342. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2018/2019, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuhuisha masuala ya jinsia katika sera, mipango na mikakati ya kisékta; kushiriki katika mikutano ya kitaifa na kimataifa katika masuala ya kijinsia; na kuwajengea uwezo waratibu wa masuala ya jinsia Wizarani na katika taasisi zilizo chini ya Wizara juu ya uratibu wa masuala ya jinsia, ufuatiliaji na tathmini.

**5.6 UDHIBITI WA MATUMIZI**

**343. Mheshimiwa Spika**, Wizara itahakikisha matumizi yanafanyika kwa kuzingatia Kanuni, Taratibu na Sheria za

fedha za Serikali. Wizara itaendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili waweze kuhakikisha taratibu zote za fedha zinafuatwa na malipo yanafanyika kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwenye bajeti ya Wizara.

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2018/2019

### 6.1 MAPATO YA SERIKALI

**344. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 20,006,300,000 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni, ada za leseni na marejesho ya mshahara endapo mtumishi ataacha kazi.

#### Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa Mwaka 2018/2019

<b>(a) Fungu 44</b>	
Maelezo	Kiasi (Shs).
Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni na Marejesho ya Mishahara.	5,300,000
<b>JUMLA FUNGU 44</b>	<b>5,300,000</b>

<b>(b) Fungu 60</b>	
Uuzaji wa Leseni za Biashara, Faini kutokana na kukiuka Mashariti ya Leseni na Marejesho ya Mishahara.	20,001,000,000
<b>JUMLA FUNGU 60</b>	<b>20,001,000,000</b>
<b>JUMLA KUU (FUNGU 44 NA FUNGU 60)</b>	<b>20,006,300,000</b>

6.2 MAOMBI YA FEDHA

345. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inaomba kutengewa **Shilingi 143,334,153,648**, kati ya hizo, **Shilingi 43,309,628,648** ni za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 100,024,525,000** ni za Matumizi ya Maendeleo.

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Fedha kwa Mwaka 2018/2019**

		Fedha zilizotengwa 2018/2019 (Tshs.)
<b>(a) Fungu 44</b>		
Matumizi ya Kawaida	Mishahara	19,193,110,000
	Matumizi Mengineyo	5,069,373,000
<b>Jumla Ndogo</b>		<b>24,262,483,000</b>
Matumizi ya Maendeleo	Fedha za Ndani	90,500,000,000
	Fedha za Nje	2,524,525,000
<b>Jumla Ndogo</b>		<b>93,024,525,000</b>
<b>Jumla Fungu 44:</b>		<b>117,287,008,000</b>
<b>(b) Fungu 60</b>		
Matumizi Kawaida ya	Mishahara	17,077,055,000
	Matumizi Mengineyo	1,970,090,648
<b>Jumla Ndogo</b>		<b>19,047,145,648</b>
Matumizi ya Maendeleo	Fedha za Ndani	7,000,000,000
	Fedha za Nje	0
<b>Jumla Ndogo</b>		<b>7,000,000,000</b>
<b>Jumla Fungu 60</b>		<b>26,047,145,648</b>
<b>Jumla Kuu (Fungu 44 na 60)</b>		<b>143,334,153,648</b>

**Jedwali Na. 4: Mgawanyo wa Fedha za OC (Mishahara na Matumizi Mengineyo) kwa Mwaka 2018/2019**

FUNGU	Jina la Fungu	Mishahara	Matumizi Mengineyo	Jumla
44	Vivanda	2,940,928,000	5,069,373,000	8,010,301,000
44	Mashirika chini ya Fungu 44	16,252,182,000	0	16,252,182,000
60	Biashara na Uwekezaji	1,164,224,000	1,887,909,000	3,052,133,000
60	Mashirika chini ya Fungu 60	15,912,831,000	82,181,648	15,995,012,648
<b>JUMLA KUU</b>		<b>36,270,165,000</b>	<b>7,039,463,648</b>	<b>43,309,628,648</b>

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha za Maendeleo katika Fungu 44 na Fungu 60 kwa Mwaka 2018/2019**

FUNGU	AINA YA MATUMIZI	KIASI (Tshs)
44	Fedha za Maendeleo za ndani	90,500,000,000
44	Fedha za Maendeleo za nje.	2,524,525,000
	<b>Jumla Fungu 44</b>	<b>93,024,522,000</b>
60	Fedha za Maendeleo za ndani	7,000,000,000
<b>Jumla Kuu Fungu 60</b>		<b>7,000,000,000</b>
<b>Jumla Kuu fungu 44 na 60</b>		<b>100,024,525,000</b>



### 6.3 MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO

#### 6.3.1 Fungu 44

**346. Mheshimiwa Spika,** katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo, fedha za ndani, zimeelekezwa katika Miradi Mikubwa ya Kielelezo; Miradi ya Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO Kibaha; Kuendeleza Kongano za Viwanda; Kuendeleza Tafiti za Maendeleo ya Viwanda; Kuendeleza Viwanda Vidogo, Biashara Ndogo, Ujasiriamali na Kuongeza mtaji kwenye mfuko wa NEDF. Miradi hiyo ni ifuatayo:-

**a) Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga** imetengewa Shilingi 10,000,000,000.00 ili kurejea tathmini ya mali za wananchi watakaopisha eneo la mradi, kuratibu na kufuatilia kazi za miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga, na kuelimisha wananchi kuhusu faida za mradi katika Mkoa wa Njombe;

**b) Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka** umetengewa Shilingi 2,000,000,000.00 kwa ajili ya kufanya utafiti wa faida za kiuchumi, mazingira na kujenga miundombinu ya maji safi;

**c) Kiwanda cha Matairi Arusha** kimetengewa Shilingi 200,000,000.00 kwa ajili ya kutafuta wawekezaji na kuratibu mradi huo;

**d) Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi** umetengewa Shilingi 22,715,918,000 inajumuisha kanda za Bagamoyo (Technological Park), Tanga, Kigoma, Ruvuma, Dodoma na Manyoni ikiwa ni pamoja na Uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini; na Kigamboni *Industrial Park*.

**e) Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO** umetengewa Shilingi 13,000,000,000.00, kati ya hizo Shilingi 11,000,000,000.00 ni kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya Eneo la Viwanda TAMCO na Shilingi

2,000,000,000 ni za kuendeleza viwanda vya nguo na Mradi wa kuunganisha matrekta ya URSUS;

**f) Uendelezaji wa Kongano za Viwanda** umetengewa Shilingi 1,000,000,000.00 kwa ajili ya Kongano la Ngozi na bidhaa za ngozi Dodoma;

**g) Uendelezaji wa Tafiti za Maendeleo ya Viwanda** umetengewa Shilingi 10,000,000,000.00 kwa ajili ya kuendeleza tafiti za maendeleo ya viwanda katika Taasisi za TIRDO, TEMDO na CAMARTEC;

**h) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo, Biashara Ndogo na Ujasiriamali** umetengewa Shilingi 26,834,082,000.00, ambapo Shilingi 11,834,082,000 ni kwa ajili ya kujenga maeneo ya viwanda katika mikoa ya Manyara, Mtwara, Dodoma, Kagera, Njombe, Katavi, Geita na Simiyu; Shilingi 5,000,000,000.00 kwa ajili ya kutekeleza Mkakati wa Bidhaa Moja kwa kila Wilaya – ODOP; na Shilingi 10,000,000,000.00 ni kwa ajili ya kuongeza mtaji Mfuko wa NEDF;

**i) Chuo cha Elimu ya Biashara –CBE** kimetengewa Shilingi 700,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali katika kuboresha miundombinu inayojumuisha ujenzi wa kumbi za mihadhara, ofisi za walimu pamoja na maktaba katika kampasi ya Mwanza;

**j) Mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II)** umetengewa Shilingi 2,500,000,000.00 ni kwa ajili ya kuchochea uongezaji thamani wa bidhaa za ngozi (Shilingi 620,000,000); kuboresha na kuanzisha viwanda vinavyosindika mazao ya kilimo ikiwemo mihogo, alizeti na pamba (Shilingi 380,000,000,00); kubainisha miundombinu ya uchakataji wa mazao ya kilimo kwenye mnyororo wa thamani uliopo (Shilingi.220,000,000); kufanya upembuzi yakinifu katika kuanzisha kongano la karanga Mpwapwa (Shilingi. 240,000,000); kujenga miundombinu muhimu kwenye kongano la karanga mpwapwa (Shilingi 540,000,000); na kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini utekelezaji wa Mradi wa ASDP (Shilingi 500,000,000); na

**k) Mchango wa Serikali katika Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo (CounterPart Fund)** umetengewa Shilingi 1,550,000,000 inayojumuisha miradi ya UNIDO, (*Programme for Country Partnership- CPC*) Shilingi 1,000,000,000; miradi ya KAIZEN Shilingi 200,000,000; Trade Mainstreaming Shilingi 250,000,000 na Gender Shilingi 100,000,000.

### **6.3.2 Fungu 60**

**347. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu la 60 (Biashara na Uwekezaji) imetenga Shilingi 2,000,000,000 ni kwa ajili ya TBS kuendeleza ujenzi wa maabara ya kisasa ikiwemo maabara ya kisasa ya kemia; Shilingi 900,000,000 ni kwa jili ya COSOTA kuboresha mfumo wa usajili wa kazi na wanachama wanaojishughulisha na kazi za ubunifu kwa njia ya mtandao; na Shilingi 1,400,000,000 ni kwa ajili ya Bodi ya Stakabadhi ya Maghala (WRRB) kugharamia ujenzi wa ghala la kimkakati mkoani Dodoma lenye uwezo wa kutunza tani 30,000 kwa wakati mmoja, pamoja na miundombinu ya ukaushaji kwa ajili ya kuhifadhia mahindi, Karanga na Alizeti. Pia Shilingi 1,300,000,000 ni kwa Wakala wa Vipimo, kati yake Shilingi 500,000,000 ni kwa ajili ya kununua *optical scanner* ya uhakiki wa matenki makubwa ya mafuta, Shilingi 450,000,000 ni kwa ajili ya ununuzi wa gari la uhakiki wa vipimo (Verification Truck with Crane) kwa ajili ya kupima mizani mikubwa inayotumika kwenye udhibiti wa matumizi ya Barabara na Biashara ikiwemo ya mazao ya Korosho, Pamba na Shilingi 100,000,000 za ununuzi wa vipimo vya uhakiki wa vifaa vya kupima kasi ya Magari (Speed Detectors Standards) na Shilingi 250,000,000 kwa ajili ya kununua mizani na mawe ya upimaji wa madini (*weighing instrument class II capacity 1200 g na inspection kit*).

**348. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa ASDP umetengewa Shilingi 1,400,000,000. Kati ya hizo Shilingi 63,700,000 zitatumika kuimarisha mnyororo wa thamani na kuwezesha wakulima kuunganishwa na masoko; Shilingi 184,000,000 kuendeleza mpango wa kukuza masoko ya bidhaa za kilimo zinazozalishwa nchini; Shilingi 162,750,000 za kuimarisha

mifumo ya taarifa za masoko ya mifugo, mazao na bidhaa nyingine; Shilingi 380,531,173 za kufanya sensa ya mazao ya kilimo na mifugo na kufanya tafiti za mwenendo wa masoko ya mazao makuu ya biashara na mifugo; shilingi 58,000,000 kupitia na kukamilisha Mkakati wa Sera ya Masoko; Shilingi 123,368,827 kuendeleza na kukuza matumizi ya mifumo ya kuzuia majanga ya masoko kwa mazao na bidhaa zinazo zaliswa nchini, kuperemba na kufuatilia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa zao la korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani na katika maeneo mapya yatakayo anza kutekeleza Mfumo huo; Shilingi 68,950,000 kuimarisha na kukuza soko la bidhaa (*operationalize of Agricultural Commodity Exchange*); Shilingi 70,875,000 kuimarisha na kukuza biashara na masoko ya mipakani kwa bidhaa za kilimo na zinazozalishwa nchini; shilingi 90,250,000 kuendeleza na kuunganisha Mfumo wa Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*) na Mfumo wa Stakabadhi Gghalani kwa mazao ya alizeti, mahindi, mchele, na ufuta pamoja na maeneo mapya ambayo hayajawahi kutumia Mfumo wa stakabadhi ghalani pamoja kupanua wigo wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala; shilingi 84,950,000 kuendeleza miundombinu ya masoko katika mkakati kwa kuimarisha na kukamilisha ujenzi wa vituo vya biashara mipakani Sirari, Murongo, Nkendwa, Kabanga na Kahama; na Shilingi 112,625,000 kuwezesha ujenzi wa maghala matano (5) ya kimkakati kwa mazao yaliyopo kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani.

## 7.0 HITIMISHO

**349. Mheshimiwa Spika**, maamuzi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ni msimamo makini wa Serikali yetu unaozingatia uzoefu uliopo ambao umeinua uchumi wa nchi nyingi ulimwenguni na kuleta mafanikio na maendeleo katika nchi hizo. Kuthubutu, kutambua ushindani, kutumia fursa, kufanya kazi kwa ushirikiano na kutumia rasilimali kwa nidhamu ni masuala muhimu ya kuzingatiwa ili kufikia malengo. Ni dhahiri kuwa changamoto za uwekezaji huambatana na fursa ambazo hatuna budi kufungamana nazo. Wakati Serikali inaendelea na jitihada za kuweka mazingira rafiki na wezeshi, sekta binafsi ina jukumu la

kuzitumia fursa zilizopo na zinazojitokeza ndani na nje ya nchi kwa kuwekeza na kufanya biashara. Matokeo ya jitihada hizo yameanza kuzaa matunda. Hata hivyo, tunahitaji kuendelea kuunganisha nguvu kwa dhamira njema bila kuchoka kukabili vita dhidi ya uchumi wa viwanda ulimwenguni kwa kuhakikisha kuwa ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali unaendelezwa. Inawezekana, tukiweka nguvu ya pamoja katika kuendeleza sekta hii muhimu.

**349. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, ahsante sana kwa hotuba yako ambayo imetupatia mwanga mkubwa. Mheshimiwa Waziri kuna bidhaa zipo mezani kwako hujasema chochote sasa sijui, lakini basi haina neno labda baadaye kidogo.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, samahani nilipitiwa, nilijiandaa siku nyingi kusoma hotuba hii. Naibu Waziri wangu niliyepewa na Mheshimiwa Rais, nguo aliyovaa imeshonwa na mwana mama mjasiriamali aliyepo Mbeya kwa kutumia nyuzi. Naibu Waziri viatu alivyoshika vimetengenezwa na Kiwanda cha *Karanga Prison* Arusha na mimi suti niliyovaa imeshonwa na Khimji wa Dar es Salaam. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Huo ndio umaliziaji wa hotuba niliokuwa nautazamia. Pia kwa wale ambao hawakusikia lile *book* alilolibeba lile ndiyo lina orodha ya viwanda, maana wengi mlikuwa mnasema ooh viwanda, orodha iko wapi, lile *book* lile ndiyo orodha yote, hajaweka mezani bado msidai, ahsante sana. (*Kicheko*)

Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji baada ya hapo tutakuwa na uchangiaji, mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Zitto Kabwe (*ACT*), wa pili atakuwa CCM, Mheshimiwa Silvestry Koka mjiandae, mara baada ya Mwenyekiti kumaliza hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mweyekiti, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, karibu sana. Ni mara chache Mheshimiwa Suleiman Sadiq amewahi kupiga suti. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ – MWENYEKITI KAMATI YA BIASHARA, VIWANDA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo lakini naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunjalia salama siku ya leo na kunipa afya njema. Pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Kamati kufanya kazi hii hadi kuikamilisha siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wananchi wa Mvomero kwa kuendelea kuwa na imani na mimi na hatimaye Bunge nalo limenipa kazi kubwa na nzito na kunjenga imani kubwa. Nami naahidi kuifanya kazi hii kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. Sitakuangusha wewe na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, inaomba sasa itoe rasmi taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44 na Fungu 60 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi Fungu 44 na 60 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imedhamiria kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati na kupitia uchumi wa viwanda ifikapo 2025. Kamati imeona na kupongeza jitihada za Serikali katika kutekeleza hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia na kuipeleka nchi hii katika Tanzania ya Viwanda. Kamati inampongeza na inamuunga mkono katika juhudi zake zote hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake ambapo Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo na hatimaye wajumbe kuishauri Serikali ipasavyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (Fungu 44 na Fungu 60) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuchambua Mpango wa Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na hatimaye kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kwa lengo la kuliomba Bunge kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Aidha, taarifa hii itaainisha mapendekezo kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa malengo/majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ni pamoja na kutenga maeneo ya maalumu ya uwekezaji kwa kuzingatia msambao wa viwanda nchini.

Kamati ilipokea taarifa kuwa hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya ekari 622,030.65 zilikuwa zimeainishwa na kutengwa kwa ajili ya maeneo maalum ya uwekezaji. Kamati inapongeza jitihada hizi za Serikali katika kutekeleza lengo hili. Kamati ina maoni kwamba ili zoezi hili liwe na ufanisi, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia na kuendeleza maeneo haya kwa kuweka miundombinu stahiki ili kuyafanya maeneo haya kuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara inahimiza uanzishwaji wa viwanda nchi nzima katika mikoa na halmashauri zote. Kamati inaona ni jambo jema lakini inaishauri Serikali kuzingatia faida za kijiografia katika kutenga maeneo hayo. Katika kufanya hivyo itasaidia kupunguza gharama kwa wawekezaji wetu hasa usafirishaji wa malighafi au bidhaa na hatimaye kupunguza mzigo wa bei kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa mpango na bajeti wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ulizingatia makusanyo ya maduhuli na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Chanzo cha taarifa hizi ni zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati na majadiliano yalifanyika na hatimaye kupata taarifa hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizopo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Sh.28,000,000,000. Makadirio haya yalipangwa kukusanywa kutoka katika ada za leseni, mauzo ya nyaraka za zabuni na faini za kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuwa hadi kufikia Desemba, 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Sh.8.6 kiasi hiki ni sawa na asilimia 30.7 ya lengo lililokusudiwa. Kamati inaona fedha hizi ni ndogo sana, juhudi kubwa zinatakiwa ziendelee katika eneo hili.



Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa, Desemba, 2017, ilikuwa ni takribani miezi sita ya muda utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018 na kiasi kilichokusanywa ni kidogo ukilinganisha na makisio/malengo ya Sh.28,000,000,000, hivyo kuwepo uwezekano mdogo wa kufikia lengo lilowekwa mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha. Kamati inaendelea kusisitiza kwa Serikali kupanga makusanyo ya maduhuli kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato ili kuwa na uhakika wa kufikia malengo. Kamati inashauri Wizara iwe makini zaidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango na bajeti katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Fungu 44 na 60. Fedha zilizotengwa na kuidhinishwa kwa ajili Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni jumla ya shilingi bilioni 122, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 80 ikiwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 42 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yake yote mawili Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji).

Mheshimiwa Spika, Fungu 44 (Viwanda) lilitengewa shilingi bilioni 98 Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 73.8 zilikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 24 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji) lilitengewa shilingi bilioni 24.2 kati ya hizo shilingi 17.8 ni bajeti ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6.3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kamati ilipokea taarifa kuwa, hadi kufikia Machi, 2018, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 37.4 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 30.64 tu ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mafungu yote 44 na 60. Kamati ina maoni kwamba, kuchelewa kutolewa kwa wakati fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara imekuwa ni kikwanzo pia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na huku tukizingatia kwamba hii ni Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina shilingi bilioni 29.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 70 ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida. Mgawanyo wa fedha zilizopokelewa kutoka Hazina katika mafungu (44 na 60) ni kama ifuatavyo: Shilingi bilioni 17.3 kwa Fungu 44, kiasi hiki kinajumuisha mishahara, Shilingi bilioni 13.2 na shilingi bilioni 4.1 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Fungu 60 limepokea shilingi bilioni 12 kati ya hizi shilingi bilioni 10 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 1.12 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kiwango kikubwa unaonyesha kuwa Serikali inapanga matumizi makubwa yasiyoakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato vya ndani. Hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2018, kati ya shilingi shilingi 80 fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 8 tu ndizo zilikuwa zimepokelewa kwa mafungu yote mawili 44 na 60 kutoka bajeti ya fedha za ndani, kiasi hiki ni sawa na asilimia 9.97 ya fedha zote za miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni kidogo sana kwa uhalisia wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka fedha 2017/2018, Kamati ilibaini kwamba:-

(i) Kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha za maendeleo jambo linalokwamisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati na hatimaye kupanda kwa gharama hizo mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

(ii) Hakuna uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na fedha za miradi ya maendeleo.

(iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa mdogo ukilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Maelezo hayo yanaonyeshwa kwenye Jedwali lifuatalo ambalo linaonyesha fedha zilizoidhinishwa

na Bunge pamoja na kiasi kilichopokelewa. Jedwali lipo katika kitabu changu cha hotuba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi huu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa siyo wa kuridhisha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilifanikiwa kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo. Kamati ilifanya ziara katika maeneo ya *SIDO* na taarifa yangu ya ziara hiyo ipo katika ukurasa wa 8, 9 na 10 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo Serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii. Tunashauri Serikali iweke kipaumbele zaidi kwenye maoni na ushauri wa Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ipeleke fedha zilizosalia kwa ajili ya mradi wa *TAMCO* ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia miradi ya aina hii itekelezwe katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchini. Mara ya mwisho wakati Kamati inautembelea mradi huu ilipokea taarifa kuwa mradi ulikuwa unahitaji shilingi bilioni 16.9 kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wake. Maelezo yaliyotolewa na Wizara ni kuwa imetekeleza agizo hili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 12.9 ambazo hadi kufikia Machi, 2018 ni shilingi bilioni 2 tu ndizo ambazo zilikuwa zimepokelewa na kutumika katika ujenzi kiwanda cha

kuunganisha matrekta. Kamati bado inaendelea kuisitiza Serikali kupeleka fedha zilizosalia katika eneo hilo kwa mwaka huu wa fedha unaoishia wa 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie mazingira ya kufanya biashara hapa nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi. Maelezo ya Serikali ni kuwa yapo majadiliano yanayoendelea katika hatua mbalimbali za kutafuta ufumbuzi wa kudumu jambo hili. Kamati hairidhishwi jinsi Serikali inavyolishughulika suala hili kwani bado wawekezaji wengi wanalalamika kuhusu ugumu wa mazingira ya kufanya biashara Tanzania. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iongeze kasi katika mchakato wake wa kutafuta utatuzi wa kudumu na kupunguza urasimu katika taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ilipokea taarifa kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukushanya shilingi bilioni 20 kwa Fungu 44 na Fungu 60. Kiasi hiki ni pungufu kwa asililimia 28.5 ya shilingi bilioni 28 kiasi kilichokadiriwa katika ya mwaka wa fedha unaoishia.

Mheshimiwa Spika, Fungu 44 (Viwanda) linatarajia kukushanya jumla ya shilingi milioni 5.3 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi. Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji) linatarajia kukushanya jumla ya shilingi bilioni 20 kutokana na uuzaji wa leseni za biashara, faini kutokana na kukiuka masharti ya leseni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri wa Kamati uliokuwa ukitolewa kwa muda mrefu sasa wa kujikadiriwa kwa kuzingatia uwezo wao halisi wa makusanyo. Aidha, Kamati inaendelea kuisitiza Serikali kuangalia changamoto zilizopelekea kutofikia malengo hayo na kufanya jitihada za kukabiliana nazo ili kuhakikisha wanafikia malengo wanayojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Maombi ya fedha kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji mafungu yote mawili; 44 na 60, ni jumla ya shilingi bilioni 143.3. Kiasi hiki ni zaidi ya asilimia 17.28 ya shilingi bilioni 122.2 zilizo dhinishwa kwa bajeti inayotekelezwa sasa. Kati ya fedha zilizoombwa, kiasi cha shilingi bilioni 43.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 100 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 44 - Viwanda. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44, limetengewa jumla ya shilingi bilioni 117.2 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 81.8 ya shilingi bilioni 143.3. Fedha zote hizi zinaombwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 93, sawa na asilimia 79.3 ya bajeti ya Fungu lote la 44 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo; shilingi bilioni 24.2, sawa na asilimia 20.69 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 19.1 ni mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 5.1 ni matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo. Katika bajeti iliyoombwa kuna ongezeko la asilimia 17.28 ukilinganisha na bajeti inayotekelezwa kwa sasa. Kamati inapata mashaka kama kweli bajeti hii itaweza kutekelezwa kwa kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina si wa kuridhisha, hasa ikizingatiwa kwamba hadi kufikia Machi, 2018, ni asilimia 30 tu ya bajeti ya 2017/2018 ndiyo iliyopokelewa. Eneo hili kuna tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimekuwa zikiongezeka kila mwaka. Ongezeko la mwaka huu ni asilimia 24.7, changamoto ni upatikanaji wa fedha hizi kutoka Hazina, jambo linalosababisha kukwamishwa utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutoa fedha zote za miradi ya maendeleo kabla ya tarehe 30, Juni, 2018. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Baada ya kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi na uchambuzi wa taarifa mbalimbali ikiwemo taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara kwa Mwaka 2018/2019, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda. Ni matarajio ya Watanzania walio wengi kuona uanzishwaji wa viwanda unazingatia pia uanzishaji wa viwanda vikubwa na vya kati ambavyo vitachakata mazao ya kilimo, kwa mfano pamba, tumbaku, kahawa, alizeti, korosho na miwa. Kamati inaishauri Serikali kuwa na malengo maalum ya viwanda vikubwa na vya kati kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali na ajira. Kamati inakubaliana na utaratibu wa viwanda vidogo, viwanda vya vyerehani, lakini Kamati inasisitiza kuongeza malengo maalum kwa viwanda vikubwa na vya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi nchini bado wanalima kwa kutumia zana duni, hasa jembe la mkono. Kwa kuwa *SIDO, CAMARTEC, TEMDO* na *TIRDO* wana uwezo wa kutengeneza na kusambaza zana mbalimbali za kilimo kwa teknolojia rahisi na kuuza kwa bei nafuu kwa wakulima, Kamati inaishauri Serikali kuziwezesha taasisi hizi ili ziwe kichocheo kwa uanzishaji wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, lakini pia vitakavyotumia teknolojia rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vinavyochakata matunda na mbogamboga nchini vinalazimika kufanya uzalishaji kwa msimu kutokana na wakulima wengi kutegemea kilimo cha mvua. Hali hii imesababisha wenye viwanda vingi kuzalisha chini ya kiwango kwa kuwa na ajira za msimu, matokeo yake Serikali kukosa mapato. Kamati inaishauri Serikali kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima nchini kulima kilimo cha umwagiliaji ili kuwa na mavuno msimu wote. Kamati inaishauri Wizara inayohusika kuongeza fedha katika eneo hili la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea malalamiko ya wenye viwanda vya bidhaa ya karatasi wakilalamika kutopata kwa wakati malighafi za karatasi kutoka Kiwanda cha Mgololo, Iringa. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kupunguza kodi kwa malighafi ya karatasi kutoka nje ya nchi ili kuleta ushindani wa haki ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo kubwa sana ambalo Serikali inakosa mapato. Tofauti ya bei katika soko la bidhaa aina ya pombe na vinywaji vikali kumezua hofu. Pia kumekuwepo na stika bandia za *TRA* katika bidhaa za pombe na vinywaji vikali. Suala hili *TRA* wanalifahamu lakini hadi leo linaendelea na liko ndani ya nchi yetu. Aidha, kumekuwepo na viwanda vinavyotoa taarifa zisizo sahihi za uzalishaji, hali hii huisababishia Serikali kupoteza mapato mengi katika eneo hili. Kamati inashauri Serikali kutoza kodi katika *spirit* ambayo ndiyo malighafi inayoingia nchini wakati ambapo inaingia katika boda na bandari zetu ili kuondokana na udanganyifu unaofanywa na wenye viwanda. Eneo hili Serikali iwe makini sana, inapoteza mabilioni ya fedha katika stika bandia za *TRA* katika vinywaji vya pombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inaendelea kuhimiza uanzishaji wa viwanda nchini, wamiliki wengi wa viwanda nchini bado wanalalamikia nishati ya umeme kuwa siyo ya kutosheleza, wakati mwingine kusababisha hasara. Kamati inaunga mkono dhamira ya Serikali kujenga mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge* ili kupata ufumbuzi wa kudumu. Kamati inaendelea kusesitiza Serikali kuharakisha kupata suluhu ya kudumu kwa tatizo la umeme ili kufikia Tanzania ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara. Serikali katika kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini, hasa vinavyochakata mazao ya kilimo, inalenga kuwainua wakulima wadogo lakini hili litafanikiwa kama yatawekwa mazingira ya haki katika biashara kati ya wakulima na wenye viwanda. Eneo hili wakulima na wenye viwanda halijakaa vizuri, tunaomba Serikali iwatendee haki. Wakulima wengi wanalalamika kuwa viwanda hununua mazao yao kwa bei

ya chini, hasa kwa kuwa mengi yanazalishwa kwa msimu mmoja. Kamati inashauri Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa soko ambao utakuwa ni kwa manufaa ya pande zote mbili; wakulima na wenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kazi ya *TanTrade* katika kusogeza mbele gurudumu la uzalishaji na masoko kwa kuandaa maonesho makubwa ya biashara. *TanTrade* ina wajibu wa kuhakikisha bidhaa za Tanzania zinaingia katika masoko ya kimataifa. Kamati inashauri Serikali kuiwezesha *TanTrade* kuwekeza katika miundombinu ya masoko, maghala na viwanja vya maonesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapinduzi ya teknolojia yametoa mianya kwa wafanyabiashara ambao si waaminifu kuzalisha bidhaa bandia zinazoshabihiana kabisa na bidhaa halisi kwa kuzalisha na kuwafanya walaji kushindwa kutofautisha bidhaa hizo. Njia inayotumika sasa na Tume ya Ushindani kutambua bidhaa hizo kwa kuangalia usanifu, maandishi na rangi haiwezi kupata majibu sahihi. Kamati inashauri *FCC* itumie njia za kisasa zaidi, teknolojia bora ya kutofautisha kati ya bidhaa bandia na bidhaa halisi na Sheria ya *FCC* ifanyiwe marekebicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tofauti kubwa ya bei za bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi. Bidhaa nyingine za ndani ya nchi bei zake zimekuwa kubwa na bidhaa kutoka nje ya nchi bei zimekuwa ndogo, mfano bidhaa za sukari, mabomba ya maji, nguo na vifaa vya ujenzi. Kwa sababu hiyo, bidhaa za ndani zinakosa ushindani wa soko. Kamati inashauri Serikali kukaa na wazalishaji wa ndani kupitia gharama za uzalishaji na kuondoa mizigo mikubwa ambayo mwisho wake mtumiaji wa mwisho ndiyo anabeba mzigo wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wameitikia wito wa Serikali kwa kuanzisha viwanda vidogo kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali, mfano usindikaji wa asali, matunda na mbogamboga. Katika kutafuta masoko wamekuwa wanakumbana na vikwazo mbalimbali ikiwemo



kupata alama ya ubora kutoka *TBS*. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba *TBS* inawafikiwa wajasiriamali wote nchini ili waweze kujenga uwezo na bidhaa zao kuingia katika soko.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitambua nia njema ya Serikali katika kudhibiti uingizaji wa sukari ya viwandani. Bado kuna malalamiko kutoka kwa wenye viwanda wanaotumia malighafi hiyo kuwa kuna urasimu wa upatikanaji wa vibali kuingiza sukari hiyo ya viwandani kwa sababu viwanda hivyo vinazalisha chini ya kiwango, baadhi ya viwanda wameanza kupunguza wafanyakazi wao na kubwa zaidi ni kuikosha Serikali mapato. Kamati inaendelea kuisisitiza inaungana mkono na juhudi za Serikali lakini utaratibu mzuri zaidi uandaliwe ili viwanda viendeleo kuzalisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, wazalishaji wa ndani wa maziwa wanalalamikia Ongezeko la Kodi ya Thamani (*VAT*) inayotowza kwenye maziwa yanayozalishwa na viwanda vya ndani. Hatua hii inapunguza ushindani ukilinganisha na maziwa yanayoingizwa kutoka nchi jirani ambayo hayatozwi kodi hiyo katika nchi yao. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi hiyo ili kuvilinda viwanda vya ndani na pia kuongeza soko la maziwa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uwekezaji. Kumekuwa na uwekezaji katika Sekta ya Viwanda usiozingatia upatikanaji wa malighafi na faida za jiografia katika eneo husika. Kwa sababu hiyo kunakuwa na gharama kubwa ya usafirishaji wa malighafi kutoka eneo moja kwenda eneo lingine, lakini pia linawakosha fursa nyingine za kiuchumi zinazotokana na uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali kabla ya kuanzisha viwanda ufanyike utafiti wa kutosha ili kutambua aina ya kiwanda kutokana na faida ya jiografia ya eneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi nzuri zinazochukuliwa na Serikali, bado kuna malalamiko kwa wawekezaji wengi kwamba mazingira ya uwekezaji nchini si rafiki. Baadhi ya wawekezaji wanalalamikia uwepo wa

changamoto kama mamlaka nyingi za udhibiti, urasimu katika upatikanaji wa vibali vya uhamiaji na mlolongo wa kupata vibali vya uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iendelee kuboresha mazingira haya chini ya TIC ili uwekezaji wa kuvutia ufanyike nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka 20 sasa tangu wawekezaji wengi waliponunua viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali kwa njia ya ubinafsishaji. Kati ya mwezi Septemba na Desemba, 2017, Serikali ilifanya sensa ya viwanda hivyo katika mikoa 13 ikiwemo Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Mtwara, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Mwanza, Tabora, Shinyanga na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya sensa yameonesha kati ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa ni viwanda 62 tu ambavyo ndivyo vinafanya kazi, sawa na asilimia 39.7. Kwa takwimu hiyo inamaanisha kwamba asilimia 61.3 ya viwanda vyote havifanyi kazi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua kwa wawekezaji wote ambao hawajafufua viwanda hivyo kwa lengo lililokusudiwa. Sambamba na hilo, ipo haja ya Serikali kuunda Tume Maalum ili kufuatilia kwa karibu eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakupa dakika mbili ku-*wind up* Mheshimiwa Saddiq, soma mafungu tu yale.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba nikushukuru wewe sana na Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri. Nawashukuru pia Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu vyema shughuli za Bunge. Kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wangu wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu katika kupitia bajeti hii na kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yao leo mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba orodha ya majina yote yaingie kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya sasa naomba Bunge lako Tukufu likubwali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 60 na Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kiasi cha shilingi bilioni 143.3 ambapo shilingi bilioni 43.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 100 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI, FUNGU 44 NA FUNGU 60 KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 NA FUNGU 60 KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117 (11) ya Kanuni za Kudumu Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, **Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara na Uwekezaji** kwa Mwaka wa Fedha **2017/2018** na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara **Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara na Uwekezaji** kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019**.

**Mheshimiwa Spika**, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imedhamiria kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati na kupitia Uchumi wa Viwanda ifikapo 2025. Kamati imeona na kupongeza jitihada za Serikali katika kutekeleza hili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1), ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika

kutekeleza majukumu yake ambapo Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo na hatimaye wajumbe kuishauri Serikali ipasavyo.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kujadiri Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (**Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara na Uwekezaji**) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuchambua Mpango wa Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, ilipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na hatimaye kutoa maoni yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu kwa lengo la kuliomba kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Aidha, taarifa hii itaainisha mapendekezo kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

### 2.1 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa malengo/majukumu yaliyopangwa

kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo ni pamoja na:-

· ***Kutenga maeneo ya maalumu ya uwekezaji kwa kuzingatia msambao wa viwanda nchini.*** Kamati ilipokea taarifa kuwa hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya Ekari 622,030.65 zilikuwa zimeainishwa na kutengwa kwa ajili ya maeneo maalum ya uwekezaji. Kamati inapongeza jitihada hizi za Serikali katika kutekeleza lengo hili. Kamati ina maoni kwamba ili zoezi hili liwe na ufanisi, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia na kuendeleza maeneo haya kwa kuweka miundombinu stahiki ili kuyafanya maeneo haya kuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji.

· ***Serikali(Wizara) kuhimiza uanzishwaji wa viwanda nchi nzima katika Mikoa na Halmashauri zote.*** Kamati inaona ni jambo jema lakini inaishauri Serikali, kuzingatia faida za kijiografia katika kutenga maeneo hayo. Katika kufanya hivyo itasaidia kupunguza gharama kwa wawekezaji wetu hasa usafirishaji wa malighafi au bidhaa na hatimaye kupunguza bei kwa walaji.

## **2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulizingatia makusanyo ya maduhuli na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Chanzo cha taarifa hizi ni taarifa zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati na majadiliano yaliyofanyika na hatimaye kupata taarifa hizi muhimu.

### **2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizopo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **28,000,000,000**. Makadirio haya yalipangwa kukusanywa kutoka katika ada za leseni, mauzo ya nyaraka za zabuni na

faini ya kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara. Kamati ilipokea taarifa kuwa hadi kufikia Desemba, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **8,598,083,500.07** kiasi hiki ni sawa na asilimia **30.7** tu ya lengo lililo kusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa, Desemba, 2017, ilikuwa ni takribani miezi sita (6), ya muda utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018, na kiasi kilichokusanywa ni kidogo ikilinganishwa na makisio/lengo la Shilingi bilioni **28**, hivyo kuwepo uwezekano mdogo wa kufikia lengo lilowekwa mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha. Kamati inaendelea kusisitiza kwa Serikali kupanga bajeti makusanyo maduhuli kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vya mapato ilikuwa na uhakika wa kufikia malengo.

#### 2.2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Fungu 44 na 60

i) **Fedha zilizotengwa na kuidhinishwa kwa ajili Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwatika mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2017/2018**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa na kuidhinishwa jumla ya shilingi **122,215,109,750.00** kati ya fedha hizo Shilingi **80,190,377,000.00** ikiwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Shilingi **42,024,732,750.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yake yote mawili **Fungu 44** Viwanda na **Fungu 60** Biashara na Uwekezaji.

a) **Fungu 44 Viwanda**

**Mheshimiwa Spika**, Fungu **44** Viwanda lilitengewa shilingi **98,012,870,000.00** Kati ya fedha hizo Shilingi **73,840,377,000.00** zilikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **24,172,493,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

b) **Fungu 60** - Biashara na Uwekezaji  
**Mheshimiwa Spika**, Fungu **60** Biashara na Uwekezaji lilitengewa Shilingi **24,202,239,750.00**, kati ya hizo Shilingi **17,852,239,750.00** ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **6,350,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

ii) **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa kuwa, hadi kufikia Machi, 2018, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **37,447,911,373.33** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **30.64** tu ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mafungu yote **44** na **60**. Kamati ina maoni kwamba, kuchelewa kutolewa kwa wakati fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kumekuwa kikwanzo pia katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina Shilingi **29,447,911,373.33** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **70.07** ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida. Mgawanyo wa fedha zilizopokelewa kutoka Hazina katika mafungu (44 na 60) ni kama ifuatavyo; Shilingi **17,389,887,635.33** kwa fungu **44**. Kiasi hiki kinajumuisha Mishahara (PE) Shilingi **13,255,892,435.33** na Shilingi **4,133,995,200.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo(OC). Fungu **60** limepokea Shilingi **12,058,023,738.00** kati ya hizi Shilingi **10,929,162,438.00** kwa ajili ya Mishahara(PE) na Shilingi **1,128,861,300.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kiwango kikubwa unaonyesha kuwa Serikali inapanga matumizi makubwa yasiyoakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato. Hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2018, kati ya Shilingi **80,190,377,000.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi bilioni **8** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa

kwa mafungu yote mawili **44** na **60** kutoka bajeti ya Fedha za Ndani, kiasi hiki ni sawa na asilimia **9.97** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka fedha **2017/2018**, Kamati ilibaini kwamba:-

- i) Kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha za maendeleo jambo linalokwamisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati na hatimaye kupanda kwa gharama hizo mwaka hadi mwaka;
- ii) Hakuna uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na fedha za Miradi ya Maendeleo.
- iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa mdogo ukilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Maelezo hayo yanaonyeshwa kwenye Jedwali lifuatalo ambalo linaonyesha fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na kiasi kilichopokelewa kutoka Hazina kuanzia mwaka 2016/17 na 2017/18 hadi kufikia mwezi Aprili.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa uchambuzi huu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa siyo wakuridhisha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.



### 2.3 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2016, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inatekelezwa na Wizara hii. Lengo la kufanya ziara ya kutembelea miradi ya maendeleo ni kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

#### i) Ziara ya Kamati katika Mradi wa Institutional Support-SIDO Iringa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembela **Mradi Na. 6260** unaojulikana kama Institutional Support kwa upande wa Taasisi ya SIDO. Mradi huu unatekelezwa nchi nzima lakini Kamati ilipata fursa ya kutembelea karakana ya SIDO-Iringa (kituo cha uendelezaji wa Teknolojia Iringa) ili kujionea jinsi wanavyoendesha shughuli zao lakini pia kutoa maoni na ushauri.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza mradi huu Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na; Matumizi ya mitambo ya zamani (tangu miaka ya 1970) ambayo inasababisha

- Kuwepo matumizi makubwa ya umeme na kusababisha bidhaa wanazozalisha kuuzwa bei kubwa ikilinganishwa na washindani wao.
- Uchakavu wa mitambo unaosababisha kazi nyingi kufanywa kwa mikono hivyo kutumia muda mwingi kwa uzalishaji wa bidhaa chache.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ni upungufu mkubwa wa watumishi ambapo Karakana hii inawafanyakazi watatu (3) tu hivyo kusababisha fundi mmoja kufanya kazi zaidi ya moja kuliko uwezo wake.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto tajwa hapo juu bado karakana ya SIDO-Iringa imepata mafanikio ikiwa ni pamoja na kubuni na kutengeneza mitambo mbalimbali ikiwepo Mtambo wa kusafisha mafuta ya alizeti-Double refinery, Mtambo wa wa upepo na mvuke wa kukausha chai, Mtambo wa kusindika zao la Kakao.

Aidha, karakana inatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali vya ufundi, mafunzo na ushauri kwa wajasiriamali.

## ii) **Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Institutional Support-SIDO Iringa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitazama SIDO kama taasisi muhimu sana katika kutekeleza azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda kwa kutengeneza vipuri kwa ajili ya viwanda vingine. Kamati inaishauri Serikali kuwa, ni kwa kuzingatia umuhimu huu taasisi hii inapaswa kuwezesha kikamilifu ili kufufua karakana zake zote nchini pamoja kununua mitambo ya kisasa inayoendena na teknolojia ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, iliidhinishiwa shilingi **14,146,800,000** kwa ajili ya SIDO nchi nzima. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi **7,146,800,000.00** kwa ajili ya Mfuko NEDF ili kusaidia kukuza mitaji ya wajasiriamali. Kamati hairidhishwi na jinsi Serikali inavyotoa fedha kwa ajili ya Mfuko huu muhimu kwakuwa hadi kufikia Machi, 2018 hakuna fedha zilizokuwa zimetolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona niwakati muafaka sasa kwa Serikali kutoa nyenzo zote muhimu ili SIDO iweze kujiendesha kikamilifu. Aidha, Kamati ina maoni kwamba SIDO ikiwezesha vizuri inaweza kusaidia pia katika kubuni teknolojia rahisi ya kutengeneza majiko ya kupikia hatua ambayo itaisadia Serikali katika kupambana na uharibifu wa mazingira nchini.

### 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

i) ***Serikali ipeleke fedha zilizosalia kwa ajili ya mradi wa TAMCO ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia miradi ya aina hii itekelezwe katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchi.*** Mara ya mwishao wakati kamati inautembelea mradi huu ilipokea taarifa kuwa Mradi ulikuwa unahitaji shilingi bilioni 16.9 kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wake. Maelezo yaliyotolewa na Wizara ni kuwa imetekeleza agizo hili. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 mradi ulitengewa sh.12.9 ambazo hadi kufikia machi, 2018 ni shilingi bilioni 2 tu ambazo zilikuwa zimepokelewa na kutumika katika ujenzi kiwanda cha kuunganisha matrekta. Kamati bado inaendelea kusisitiza Serikali kupeleka fedha zilizosalia katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kazi zilizopangwa ziwezekufanyika. Aidha, suala la kutekeleza mradi huu katika maeneo mengine bado linasisitizwa na Kamati.

ii) ***Serikali iangalie mazingira ya kufanya biashara hapa nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi.*** Maelezo ya Serikali ni kuwa yapo majadiliano yanayoendelea katika hatua mbalimbali za kulitafutia ufumbuzi wa kudumu jambo hili. Kamati hairidhishwi jinsi Serikali inavyolishughulika suala hili kwani bado wawekezaji wengi wanalalamika kuhusu ugumu wa mazingira ya kufanya biashara hapa nchini. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iongeze kasi katika mchakato wake wa kutafuta utatuzi wa kudumu na kupunguza urasimu kupitia taasisi zake.

#### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

##### 4.1 Makisio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilipokea taarifa kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukusanya Shilingi **20,006,300,000.00** kwa **Fungu 44 na 60**. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **28.5** ya Shilingi **28,000,000,000.00** kiasi kilichokadiriwa katika ya Mwaka wa Fedha unaoishia.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu **44** - Viwanda linatarajia kukushanya jumla ya shilingi **5,300,000.00** kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi. Fungu **60** – Biashara na Uwekezaji linatarajia kukushanya jumla ya shilingi **20,001,000,000.00** kutokana na uuzaji wa leseni za biashara, faini kutokana na kukiuka masharti ya leseni na marejesho mishahara endapo mtumishi ataacha kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri wa Kamati uliokuwa ukitolewa kwa muda mrefu sasa wa kujikadiriwa kwa kuzingatia uwezo wao halisi wa Makusanyo. Aidha, Kamati inaendeela kuisisitiza Serikali kuangalia changamoto zilizopelekea kutofikia malengo hayo na kufanya jitihada za kukabiliana nazo ili kuhakikisha wanafikia malengo wanayojiwekea.

##### 4.2 Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019, maombi ya fedha kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mafungu yote Mawili (Fungu 44 na 60) ni Shilingi **143,334,153,648.00**. Kiasi hiki ni zaidi kwa asilimia **17.28** ya shilingi **122,215,109,750.00** zilizoidhinishwa kwa bajeti inayotekelezwa sasa. Kati ya fedha zinazoombwa Shilingi **43,309,628,648.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **100,024,525,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

a) **FUNGU 44 – Viwanda**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji **Fungu 44-Viwanda** limetengewa jumla ya shilingi **117,287,008,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **81.8** ya shilingi **143,334,153,648.00** fedha zote zinazoombwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha hizo shilingi **93,024,525,000.00** sawa na asilimia **79.31** ya bajeti yote ya Fungu **44** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo, shilingi **24,262,483,000.00** sawa na asilimia **20.69** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi **19,193,110,000.00** ni mishahara ya watumishi na Shilingi **5,069,373,000.00** ni Matumizi Mengineyo (OC).

b) **FUNGU 60- Biashara na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha **2018/2019**, Wizara Sehemu ya Biashara na Uwekezaji imetengewa Shilingi **26,047,145,648.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **18.17** ya bajeti yote ya Wizara, Shilingi **143,334,153,648.00**. Kati ya fedha zinazoombwa Shilingi **19,047,145,648.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kati ya hizo Shilingi **17,077,055,000.00** sawa na asilimia **65.56** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, kiasi kinachosalia Shilingi **1,979,090,648.00** sawa na asilimia **7.56** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Bajeti ya Maendeleo ni shilingi **7,000,000,000.00** sawa na asilimia **26.87** ya fedha zote zinazoomba kwa ajili ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuayo:-

Katika bajeti inayoombwa kunaongezeko la asilimia **17.28** ukilinganisha na bajeti inayotekelezwa kwa sasa. Kamati inapata mashaka kama kweli bajeti hii itatekelezeka, kwakuwa upatikanaji wa fedha kutoka hazina si wa kuridhisha hasa ikizingatiwa kwamba, hadi kufikia Machi, 2018

ni asilimia **30.64** tu ya bajeti ya 2017/2018 ndiyo ilikuwa imepokelewa.

Fedha zinazotengwa kwa ajili za Miradi ya Maendeleo zimekuwa zikiongezeka kila mwaka (ongezeko la mwaka huu ni asilimia **24.7**) changamoto ni upatikanaji wa fedha hizo kutoka Hazina jambo linalopelekea kukwamisha utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inaendelea kususitiza Serikali kutoa fedha zote za miradi ya maendeleo kabla ya tarehe 30 Juni,2018.

## 5.0 **MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya ziara za ukaguzi wa miradi, uchambuzi wa taarifa mbalimbali ikiwemo taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

### 5.1 **Sekta ya Viwanda**

**Mheshimiwa Spika**, ni matarajio ya watanzania walio wengi kuona uanzishwaji wa viwanda unazingatia pia uanzishaji wa viwanda vikubwa na vyakati ambavyo vitachakata mazao ya kilimo mfano pamba, tumbaku, kahawa, alizeti na korosho. Kamati inaishauri Serikali kuwa na malengo maalumu ya viwanda vikubwa na vya kati kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali na ajira.

**Mheshimiwa Spika**, wakulima wengi nchini bado wanalima kwa kutumia zana duni sana hasa jembe la mkono, kwakuwa SIDO, CARMATEC, TEMDO na TIRDO wanaouwezo wa kutengeneza na kusambaza Zana mbalimbali za kilimo kwa teknolojia rahisi na kuuza kwa bei nafuu kwa wakulima. Kamati inaishauri Serikali, kuziwezesha taasisi hizi ili ziwe kuchocheo katika uanzishwaji wa viwanda vidogo lakini pia vitakavyotumia teknolojia rahisi.

**Mheshimiwa Spika**, viwanda vinavyochakata matunda na mbogamboga nchini vinalazimika kufanya uzalishaji kwa msimu kutokana na wakulima walio wengi kutegemea kilimo cha mvua. Hali hii imesababisha wenye viwanda kuzalisha chini ya kiwango na kuwa na ajira za msimu matokeo yake ni Serikali kukosa mapato. Kamati inaishauri Serikali kuwahamasisha na kuwawezesha wakulima nchini kulima kilimo cha umwagiliaji ili kuwa na mavuno misimu yote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea malalamiko ya wenye viwanda vya bidhaa za karatasi zikilalamikiwa kutopata kwa wakati malighafi za karatasi kutoka kiwanda cha Mgololo. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kupunguza kodi kwa malingafi ya karatasi kutoka nje ya nchi ili kuleta ushindani wa haki.

**Mheshimiwa Spika**, tofauti ya bei katika soko la bidhaa za aina ya pombe na vinywaji vikali kumezua hofu, pia kumekuwepo na stika bandia za TRA katika bidhaa za pombe na vinywaji vikali. Aidha, kumekuwepo na viwanda vinavyotoa taarifa zisizo sahihi za uzalishaji. Hali hii huisababishia Serikali kupoteza mapato mengi katika eneo hili. Kamati inaishauri Serikali kuitoza kodi *spirit* ambayo ndiyo malighafi ya kutengeneza pombe ili kuondokana na udanganyifu wa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali inaendelea kuhimiza uanzishwaji wa viwanda nchini, wamiliki wengi wa viwanda nchini bado wanalalamikia Nishati ya Umeme kuwa siyo ya kutosheleza na wakati mwingine kuwasababishia hasara. Kamati inaunga mkono dhamira ya Serikali kujenge mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge* ili kupata ufumbuzi wa kudumu. Kamati inaendelea kuisitiza kwa Serikali kuharakisha kupata suluhu ya kudumu ya tatizo hili.

## 5.2 Sekta ya Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Serikali katika kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini hasa vinavyochakata mazao ya kilimo

inalenga kuwainua wakulima wadogo, lakini hili litafanikiwa kama yatawekwa mazingira ya haki katika biashara kati ya wakulima na wenyeviwanda. Wakulima wengi wanawalalamikia wenye viwanda kwa kununua mazao yao kwa bei za chini sana hasa kwakuwa mengi yanazalishwa kwa msimu mmoja. Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa soko ambao utakuwa na manufaa kwa pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati za inatambua kazi ya TANTRADE katika kusogeza mbele gurudumu la uzalishaji na masoko kwa kuandaa maonyesho makubwa ya biashara. TANTRADE ina wajibu wa kuhakikisha bidhaa za Tanzania zinaingia katika masoko ya kimataifa. Kamati inashauri Serikali kuiwezesha TANTRADE kuwekeza katika miundombinu ya masoko, maghala na viwanja vya maonyesho.

**Mheshimiwa Spika**, mapinduzi ya Teknolojia yametoa mianya kwa wafanyabiashara ambao siyo waaminifu na kuzalisha bidhaa bandia zinazo shabihiana kabisa na bidhaa halisi hivyo kuwafanya walaji kushindwa kutofautisha bidhaa hizo. Njia inayotumika sasa na Tume ya Ushindani kutambua bidhaa ni kwa kuangalia usanifu, maandishi, kuffia kwa rangi ambazo haziwezi kupata majibu sahihi. Aidha, sheria ya FCC imeonekana kukizana na mazingira halisi ya kufanya biashara. Kamati inaishauri Serikali kuwa na teknolojia bora ya kutofautisha kati ya bidhaa bandia na bidhaa halisi na sheria ya FCC ifanyiwe marekesho.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na tofauti kubwa ya bei za bidhaa zinazozalisha nchini na zile zinazolingia kutoka nje, mfano bidhaa za sukari, mabomba ya maji, nguo na vifaa vya ujenzi n.k. Kwasababu hiyo bidhaa za ndani zinanakosa ushindani katika soko. Kamati inaishauri Serikali kukaa na wazalishaji wa ndani na kupitia gharama za uzalishaji ili kuondoa mizigo mikubwa kwa watumiaji wa bidhaa za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, watanzania wengi wameitikia wito wa Serikali kwa kuanzisha viwanda vidogo kwa ajili ya



kuzalisha bidhaa mbalimbali mfano usindikaji wa asali, matunda na mbogamboga. Katika kutafuta masoko wamekuwa wanakumbana na vikwazo mbalimbali ikiwemo kupata alama ya ubora inayotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha TBS inawafikia wajasiriamali wengi nchini ili iwe rahisi kwa bidhaa hizo kuuzwa katika bei za ushindani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaitambua nia njema ya Serikali katika kudhibiti uingizaji holela wa sukari ya viwandani. Bado kuna malalamiko kutoka kwa wenye viwanda vinavyotumia malighafi hiyo kuhusu urasimu katika upatikanaji wa vibali vya kuingiza sukari hiyo. Kwa sababu hiyo viwanda hivyo vinazalisha chini ya kiwango, baadhi ya viwanda kupunguza watumishi na kubwa zaidi ni kuikoshesha mapato Serikali kwa njia ya kodi. Kamati inaendelea kuisisitiza kwa Serikali kuwa utaratibu utakaowekwa uzingatie maslahi mapana ya pande zote wawekezaji na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, wazalishaji wa ndani wa maziwa wanalalamikia kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) inayotozwa kwenye maziwa yanayozalishwa hapa nchini. Hatua hii inayapunguzia ushindani ikilinganishwa na maziwa yanayoingizwa kutoka nchi jirani ambazo hazitozi kodi hiyo. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi hiyo ili kuvilinda viwanda vya ndani.

### 5.3 Sekta ya Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na uwekezaji katika Sekta ya viwanda usiozingatia upatikanaji wa malighafi na faida za kijiografia za eneo husika. Kwa sababu hiyo kunakuwa na gharama kubwa za usafirishaji wa malighafi kutoka eneo moja kwenda jingine, lakini pia inawakosesha fursa nyingine za kiuchumi zinazotokana na uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali kabla ya kuanzisha viwanda ufanyike utafiti wa kutosha ili kutambua aina ya kiwanda cha kuanzisha kutokana na faida za kijiografia za eneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri zinazochukuliwa na Serikali, bado kuna malalamiko kutoka kwa wawekezaji kuhusu Mazingira ya Uwekezaji nchini kuwa siyo rafiki. Baadhi ya wawekezaji wanalaamikia uwepo wa changamoto kama, mamlaka nyingi za udhibiti; urasimu katika upatikanaji wa vibali vya uhamiaji; na mlolongo wa kupata vibali vya uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iendelee kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ili kuvutia wawekezaji wengi.

**Mheshimiwa Spika**, ni takribani miaka Ishirini (20) sasa tangu wawekezaji wengi waliponunua viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali kwa njia ya ubinafishaji. Kati ya mwezi Septemba na Desemba, 2017, Serikali ilifanya sense ya viwanda hivyo katika mikoa kumi na tatu (13) (Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Mtwara, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Mwanza, Tabora, Shinyanga na Dodoma). Matokeo ya sense hiyo ni kwamba kati ya viwanda 156 vilivyobinafishwa ni viwanda 62 tu sawa na asilimia 39.7 vinavyofanya kazi vizuri. Kwa takwimu hizo inamaanisha ni asilimia 61.3 ya viwanda hivyo havifanyi kazi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua kwa wawekezaji ambao bado hawajafufua viwanda hivyo ili lengo lilokusudiwa lifikiwe. Sambamba na hili ipo haja ya Serikali kuunda tume maalumu itakayofuatilia kwa karibu eneo hili ili kujua ukweli wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua uwepo wa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya mafuta ya Kula nchini. Hata hivyo bado wapo baadhi wafanyabiashara ambao siyo waadirifu kwa nia ya kulitawala Soko kwa maslahi binafsi. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhamasisha uwekezaji mkubwa katika Sekta ya hii ili kulinda maslahi ya mlaji.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe na Mhe. Naibu Spika kwa uongozi wenu mahiri.

Niwashukuru pia Wenyevidi wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Stella Manyanya (Mb) Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Wizara kwa jinsi walivyoshiriki katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha **2017/2018**, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha **2018/2019**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti hii mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa rukhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

i)	Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb	Mwenyekiti
ii)	Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	M/Mwenyekiti
iii)	Mhe. David Cecil Mwambe, Mb	Mjumbe
iv)	Mhe. Balozi Dkt. Diodorus B. Kamala, Mb	Mjumbe
v)	Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb	Mjumbe
vi)	Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
vii)	Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
viii)	Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb	Mjumbe
ix)	Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
x)	Mhe. Munde Tabwe Abdalah, Mb	Mjumbe
xi)	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
xii)	Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb	Mjumbe
xiii)	Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
xiv)	Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xv)	Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xvi)	Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

xvii)	Mhe. Zainab Mdolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xviii)	Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	Mjumbe
xix)	Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb	Mjumbe
xx)	Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xxi)	Mhe. Mansoor Hirani Sharif, Mb	Mjumbe
xxii)	Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xxiii)	Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb	Mjumbe
xxiv)	Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xxv)	Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xxvi)	Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu **44** na **60**, kwa mwaka wa fedha **2018/2019** kiasi cha shilingi **143,334,153,648.00** ambapo shilingi **43,309,628,648.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **100,024,525,000.00** ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Suleiman Ahmad Sadiq, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA  
MAZINGIRA**

10 Mei, 2018

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, kwa maoni hayo mazuri sana ya Kamati yanayotusaidia wachangiaji wote katika kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaanza sasa zoezi la uchangiaji, kama nilivyosema, ataanza Mheshimiwa Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Silvestry Koka na Mheshimiwa Andrew Chenge ajiandae. Mheshimiwa Zitto Kabwe, tafadhali.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii kwa mara ya tatu sasa, toka mwaka 2016, ni Wizara ambayo sijaacha kuichangia.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 mchango wangu ulijikita kwenye kufungamanisha sekta ya kilimo na sekta ya viwanda. Moja ya jambo kubwa ambalo tulikuwa nalo wakati ule ilikuwa ni mgogoro wa sukari ambao sasa unazungumzwa na tulikuwa pia na mgogoro wa kuhusu mafuta ya kula ambao bado tunazungumza.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Mikoa ya Dodoma, Manyara na Kigoma ni Wabunge ambao tukipambana vilivyo tunaweza kabisa kuiondoa nchi yetu na aibu ya kuagiza mawese kutoa nje. Migogoro ambayo tunaizungumza kila siku hapa na mijadala ambayo tunayo na wewe mwenyewe juzi ulikuwa mkali sana ni kwa sababu ya mawese kutoka nje. Tuna uwezo wa kuzalisha mawese lakini Serikali haijaweka mkakati wowote ule wa kuhakikisha kwamba tunajitosheleza na tunaweza tukauza nje. Haijaweka mkakati wowote ule wa kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji wa alizeti, tuweze kuchakata hapa na tuondokane kabisa na hii aibu ya kuagiza mawese kutoka Malaysia, watu ambao walikuja kuchukua mbegu Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa tatu sijaona katika mpango wowote wa Serikali kuhusiana na jambo hili

na bado tunabishana na kulumbana na kushutumiana kwa uagizaji wa mawese. Hili ni jambo ambalo linapaswa liwe ni aibu hata kulizungumza katika Bunge hili kwa sababu tuna alizeti, tuna mawese Kigoma na maeneo mengine kama Kyela yangeweza kabisa kumaliza matatizo kama haya.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilizungumza fungamanisho kuhusu miradi mikubwa inayoendelea nchini na viwanda na hasa hasa niliangalia suala la ujenzi wa reli na jinsi ambavyo tunaagiza malighafi za ujenzi wa reli kutoka nje. Leo umemsikia Waziri hapa anazungumza, bado tunalipa fidia Mchuchuma na Liganga. Leo umemsikia Waziri anazungumza kwamba wamekwenda wamefungua kiwanda cha nondo wapi, kiwanda cha nondo sehemu nyingine, nondo zote hizi malighafi zake ni kutoka nje na sisi tuna chuma Mchuchuma na Liganga miaka yote tunazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mbunge tangu mwaka 2000 unakumbuka, tangu mwaka 2000 tunazungumza Mchuchuma na Liganga, leo Waziri anazungumza kulipa fidia Mchuchuma na Liganga. Sisi ni watu wa namna gani? Kuna takwimu moja inaonesha kwamba *40 percent* ya Watanzania ni *stunted*, inawezekana humu *40 percent of us* ni *stunted*, kwa sababu tunaongea vitu vilevile, miaka yote tunakumbushana, *nothing happens*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii kweli inaingia akilini, tuna chuma na makaa ya mawe yamejaa pale Ludewa tunampa mkandarasi kazi ya kujenga reli, vyuma vinatoka Uturuki, India, China, kweli? Wenzetu Kenya wanajenga reli na wenyewe wanaagiza hukohuko wakati tungeweza kuwauzia. Zambia wanajenga reli kuunganisha Angola na Zambia, tungeweza kuwauzia chuma, kwa kweli mimi sioni *what we are doing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 Serikali ilikuja hapa na mpango unaitwa *C2C, Cotton-to-Clothing*, nimeangalia hotuba ya Waziri hapa, hata kulizungumza neno hilo ameona aibu. Unaondoaje umaskini bila viwanda vya nguo?

Niambie nchi gani? Uingereza ambayo ni moja ya nchi kubwa umasikini wake umeondolewa na viwanda vya nguo na hawakuwa na pamba walikuwa wanaagiza pamba kutoka kwenye makoloni yao. Hata kuzungumza Mheshimiwa Mwijage *Cotton-to-Clothing*, agenda yenu wenyewe na ulikuja hapa ukatamba na vitabu kama ulivyovileta leo, *where is it? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo kubwa ambalo napenda kuliongelea, nimalizie dakika zangu za mwisho ni biashara ya nje. Tunazungumza viwanda lakini kwa miezi 24 iliyopita Serikali hii ya Awamu ya Tano imesababisha hasara ya nchi yetu ya mauzo nje ya thamani ya dola bilioni moja na siyo takwimu zangu, ni takwimu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, angalia ukurasa unaozungumzia China, ukurasa wa 51, mauzo yetu nje China yameporomoka. Nasoma takwimu, China mauzo nje yameporomoka kutoka dola milioni 356 mwaka 2016 mpaka dola milioni 217 mwaka 2017, kutoka takwimu za Serikali. Japan, mauzo yetu nje yameporomoka toka dola milioni 140 mpaka dola milioni 75.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi tumeshindwa hata kuuza mbaazi India. Waziri alikwenda India amesema amezungumza, mimi sina hakika kama Waziri kweli alikwenda kuzungumza na Waziri mwenzake lakini biashara ni diplomasia. Mwigaje huwezi wewe unazunguka kuna viwanda, Naibu wako anazunguka na viwanda, *international trade* ni *Foreign Affairs*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi *Vice President* alikuwa London, Modi alikuwa London, mmeshindwa kuseti *appointment* ya *Vice President* na Modi wakazungumza tukatatua tatizo la mbaazi? Mbaazi bei imeporomoka kutoka Sh.3,000 mpaka Sh.150 kwa kilo. Mwezi Machi nimezunguka kwenye kata 16 nchi hii nimekuta watu wanalia mbaazi zimo ndani. Waziri Mstaafu Nape alizungumza hapa, alimuuliza Naibu Waziri, Naibu Waziri akasema kwamba tutakula, *no it is foreign trade! It is about forex!* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii tunaagiza nje vitu tunahitaji fedha za kigeni, mbaazi, choroko, gilgilani, zilikuwa zinatupa dola milioni 224 kuuza India mwaka 2016, mwaka 2017 ikaporomoka dola milioni 131, mwaka 2018 sasa hivi dola milioni 75, *what are you doing?* Unapopoteza hizi *forex* utanunua mafuta na nini kwa sababu inabidi uagize. *What will you buy mafuta with?*

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kuelewa *what are we doing*. Wizara ya Viwanda na Biashara *that part* ya biashara *especially foreign trade* hamna, tumepoteza *one billion dollars in the span of 24 months*, ni sawasawa na kupoteza kila siku shilingi za Kitanzania bilioni tatu *in the last 24 months, you are still here* Mwigaje, *why don't you just quit?* Umeshindwa kazi. *You can't run* Wizara ya Viwanda na Biashara *as if you are running TAMISEMI, it is diplomacy, it is about going out getting markets.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo Malaysia kule *a friend of Tanzania has been elected as a new Prime Minister*, Mzee Mahathir, *a very close friend of Mwalimu Nyerere, go there immediately, get the markets*. Hamuwezi mkajidanganya na viwanda vya cherehani mkadhani kwamba *you save this country! Foreign trade is power.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani sisi tukakosa soko India. *The majority* ya Wahindi ambao unawaona hapa Tanzania *they are from Gujarat, Modi is from Gujarat, use that, talk to them!* Hebu tuwaokoe hawa wakulima wa mbaazi, wakulima wa gilgilani, gilgilani imeshuka bei, mbaazi imeshuka bei, choroko imeshuka bei na dengi imeshuka bei, *what are you doing?*

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa mchango wako uliotuanzishia. Baadhi ya mambo tunakubaliana na wewe kwa kweli, Mawaziri inabidi msafiri kweli. Waziri wa Biashara hawezi kukaa na sisi hapa, lazima aende. Tumuombe popote pale kwenye mamlaka lazima



aondoke, asafiri. Maana bidhaa zetu sasa tutauza wapi? Tutauza Kongwa, kuna soko? Waziri wa Maliasili lazima aondoke, lazima asafiri, Waziri wa Utalii lazima apige mawingu huko na Mawaziri wengine, kabisa ndiyo ukweli wenyewe jamani, sisi Wabunge ndiyo tuwasemee. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mhishimwa Silvestry Koka, halafu atafuatia Mheshimiwa Komu.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya. Wizara ya Viwanda imekuwa ikijitahidi kwa hali mali ili kuhakikisha Sera yetu ya Viwanda inakua. Nichukue kweli nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kujitoa na kujitolea kwa ajili ya wananchi wa Tanzania kuhakikisha Watanzania wenyewe tunajenga viwanda na tunakwenda kushika hatamu za uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nitoe pongezi kwa kazi kubwa ya kujenga miundombinu mbalimbali kwa sababu kupitia miundombinu hii ndiyo tunaweza kujenga uchumi wa kati na hata uchumi mkubwa. Mifano iko wazi, ujenzi wa reli, ujenzi wa miundombinu ya umeme kama *Stiegler's Gorge* ni jambo ambalo tunahitaji tumuunge Mheshimiwa Rais mkono kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mojawapo ya changamoto tuliyonayo katika uanzishaji wa viwanda ni pamoja na nguvu za kusukuma au kuendesha viwanda kwa maana ya umeme. Ndugu zangu wote tunafahamu kwamba umeme unaozalishwa kwa maji ni rahisi kuliko umeme mwingine wote. Kwa hiyo, tutakapopata umeme mkubwa unaozalishwa na maji kutoka *Stiegler's Gorge* maana yake ni kwamba hata gharama za uzalishaji zitapungua, tutaweza kuzalisha kwa gharama nafuu na hatimaye kufikisha bidhaa kwa wananchi kwa gharama iliyo nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu wafanyabiashara wa Tanzania na Watanzania wote tumuunge mkono Rais, tujitokeze tujenge viwanda, tuunge mkono miradi ambayo ipo mbele yetu ili siku ya mwisho jihitada za kwenda kwenye uchumi wa kati ziweze kukamilika bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ina sababu hasa ya kutazama sasa *balance* ya biashara ya ndani nje. Tuangalie na tuweze kuona ni namna gani tunapoanza sasa kulea viwanda vyetu tuna *balance* pamoja *importation* ya bidhaa muhimu kwa ajili wananchi. Kwa sababu lengo la biashara pamoja na kupata faida na kulipa kodi lakini ni kuwafikishia wananchi bidhaa kwa bei iliyo nzuri, nafuu na ubora. Sasa kama hatutarudi tukaangalia bado kuna watu wachache wata-*take advantage* na wananchi wataendelea kununua bidhaa kwa gharama kubwa na wao kujilimbikizia faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuwepo na *balance* kati ya bidhaa zinazoletwa kutoka nje na zinazozalishwa ili yale mabadiliko ya bei ya uzalishaji na malighafi yaweze kumnufaisha vilevile mwananchi ambaye ndiye mtuamijaji. Nina imani kwa kufanya hivi tutatimiza azma ya Serikali ya kumhudumia na kumsaidia mwananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, kujenga viwanda ni jambo moja lakini kuviendesha ni jambo lingine ambalo ni gumu zaidi. Nitoe mfano wa kiwanda kinachozalisha viuadudu pale Kibaha. Kiwanda hiki kilianza kujengwa mwaka 2010 kikakamilika 2015 na kikaanza uzalishaji 2016. Kiwanda hiki ni cha pekee Afrika na kina uwezo wa kuzalisha viuadudu au viatilifu vinavyoua viluilui vya mbu kiasi cha tani milioni sita kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini navyoongea na wewe kuanzia kilipoanza kufanya kazi mwaka 2016 hadi leo kimezalisha tani laki nne tu na hakuna wanunuzi. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba tarehe 22 Juni, 2017

Mheshimiwa Rais alipotembelea viwanda Kibaha alikitembelea kiwanda hiki na alifurahishwa sana na kiwanda hiki kwa sababu ndiyo njia pekee ya kumaliza malaria nchini. Alitoa maagizo kwamba kila halmashauri inunue dawa hii iweze kutumika kuuwa viluilui vya mbu na tuangamize malaria hapa nchini. Tangu kipindi kile katika ya halmashauri 81 ambazo walichukua dawa hii ni halmashauri 25 tu ndizo ambazo zimelipa, nyingine hawajalipa kiwanda kinaendelea kudorora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dawa hii ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kama hamuifahamu kazi yake inashambulia viluilui vya mbu katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo maji yamesimama na kuhakikisha kwamba mbu hawawezi kuzaliwa. Nafikiri hii ndiyo njia pekee ya kumaliza malaria badala ya kutumia fedha nyingi kununua dawa kwa ajili ya malaria. Dawa hii ni nzuri sana, kwanza kabisa ni *environmental friendly*, yaani siyo kama dawa nyingine mfano DDT na nyingine tunazotumia kiasi kwamba unaweza hata ukainywa. Watengenezaji wali-*demonstrate* mbele ya Mheshimiwa Rais kwa kunywa ile dawa, haina hata madhara hata ukiinywa lakini ni sumu kwa viluilui vya mbu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa makusudi kabisa imetenga fedha nyingi kwa ajili ya huduma ya dawa na afya za Watanzania kutoka bajeti ya shilingi bilioni 30 mpaka shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba malaria inapigwa vita nchini. Sasa tunachoangalia ni watu tumeangukia, ndiyo tunahangaika kutibu malaria hatutaki kuangalia ni wapi tumejikwaa na tutapojikwaa ni kung'atwa na mbu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama kweli tunataka kusaidia viwanda vyetu vya ndani kiwanda ambacho kimejengwa kwa ushirikiano au kwa msaada kati ya Cuba na Tanzania ambacho hadi sasa tayari wenzetu wa Angola, Nigeria wameshaanza kupata hamu na kuleta *order* kwa ajili ya dawa hii, tusaidie kiwanda hiki kizalishe dawa na bajeti ya Wizara ya Afya itengwe kwa

ajii ya kulipia dawa hizi kwa sababu lengo letu ni kuangamiza mbu si kuendelea kila siku Watanzania wanaugua tunahangaika kuwatibu kwa gharama kubwa. Niombe sana Wizara ya Viwanda na Biashara ishirikiane na Wizara ya Afya ili waweze kununua dawa hizi, Watanzania wapewe elimu ya kuzitumia na hatimaye tuangamize mbu na Tanzania iwe *free from* malaria. Inawezekana, kiwanda tunacho, tutachekwa kama tutaendelea kuugua malaria na wakati tulishajipanga hadi kuweza kujenga hiki kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki hakijasimamiwa vizuri, kiko chini ya *NDC*, lakini hadi sasa hakina hata Bodi ya Wakurugenzi sasa kinajitendeshaje? Kina wafanyakazi, uzalishaji ni duni na hakuna anayekiangalia ipasavyo matokeo yake tunakwenda kwenye hasara na tunatoka sasa nje ya azma na sababu ya Tanzania ya viwanda. Ni wazi kama kitasimamiwa kina uwezo mkubwa sana wa kuuza bidhaa hii ndani na hata nje ya nchi yetu na kikaitetea Serikali mapato makubwa ya kigeni kwa sababu kiko pekee Afrika na dawa inayotengeneza ni pekee ambayo inakwenda kulenga mbu na kumwangamiza na kuhakiksha kwamba malaria haitaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na kuhimiza ujenzi wa viwanda vilevile tushiriki katika kuhakisha viwanda hivi tunavisimamia, tunavisaidia ili viweze kuleta tija na hatimaye tuweze kufikia malengo makubwa ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwaasa wafanyabiashara wenzangu Tanzania, kama nilivyosema lengo kubwa la biashara mbali ya kulipa kodi na kupata faida ni kumhudumia Mtanzania. Tuna wajibu wa kuhakikisha tunapopeleka bidhaa katika masoko ya Mtanzania tunamlenga Mtanzania apate nafuu katika bidhaa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameshanyoosha mkono kwa wafanyabiashara, ameamua kutuunga mkono

na kutusaidia na hata amekuwa akitoa maamuzi ya papo kwa papo kusaidia wafanyabiashara wa Tanzania. Ametaka wafanyabiashara wa Tanzania tufanye biashara, tuzalishe, tujenge viwanda na tutumie soko la ndani na fedha za ndani kuboresha viwanda vyetu. Sasa kutokupeleka azma hiyo kwa wananchi na kuwafanya wananchi wakawa wanatapatapa wapate wapi mahitaji ni sawasawa na kuiudhi Serikali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kuomba tujitahidi twende sambamba na azma ya Mheshimiwa Rais na Serikali yetu. Naunga mkono hoja tuendeleo kujenga nchi yetu ya viwanda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Silvestry Koka. Nilishakutaja Mheshimiwa Antony Komu, atafuatiwa na upande wa CUF Mheshimiwa Zainabu Mndolwa.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Wizara ambayo kimsingi ndiyo inayobeba kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. Joseph Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais lakini uhalisia kwa maana ya bajeti haupo. Kwa sababu 2015/2016 bajeti ya kwanza ya Mheshimiwa Rais, utekelezaji kwenye bajeti ya maendeleo kwenye Wizara hii ilikuwa ni asilimia 5 tu, 2017/2018 ikawa asilimia 9.47. Katika hali ya namna hii ukiunganisha hiyo kaulimbiu na majigambo yote yaliyokuwepo na dhamira ya kutaka kuona kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ripoti ya CAG ambayo inaangalia ufanisi kwenye viwanda vidogo vidogo

na vya kati ambavyo mahali popote duniani ndiyo moyo wa mapinduzi ya uchumi wa viwanda, anasema hali si nzuri, bajeti kwenye sekta hiyo imeendelea kushuka katika ngazi zote maana yake mpaka kule kwenye halmashauri zetu, si zaidi ya asilimia 16, kwa hiyo, bado uhalisia unaendelea kuonekana kwamba haupo. Mafunzo kwenye viwanda hivi vidogo vidogo kwenye sekta hii bado yameendelea kushuka, CAG anasema yako kwenye wastani wa asilimia 7 tu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye Vituo vya Maendeleo ya Teknolojia ambavyo vilianzishwa na Mwalimu Nyerere mashine ambazo zinatumiwa mpaka leo zina umri wa miaka 40, amesema Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, siyo sisi tunaosema. Sasa *seriousness* iko wapi? Ukiangalia CAG anasema, sekta ya viwanda vidogo vidogo na kati inaporomoka kwa asilimia 30 ikilinganishwa na kukua kwake kwa asilimia 5.6. Kwa hiyo, kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Tanzania ya Magufuli ya Viwanda haina uhalisia wowote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kamati alivyokuwa anazunguza hapa amezungumzia mazingira ya kufanya biashara Tanzania. Mpaka tunavyoongea hapa sasa hivi sisi ni wa 137 duniani kati ya mataifa 190 kwa mazingira rahisi ya kufanya biashara. Kinachokwenda kupeleka huo ugumu ni nini? Ni matamko ya viongozi wetu wa siasa wa upande huu wa CCM ambayo yanafanya mazingira yetu yawe si ya kutabirika na kwa sababu hiyo uwekezaji unakuwa ni mgumu katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukitaka kupata kupata kibali cha kuanzisha kiwanda hapa pamoja na mbwembwe zote anazosema Mheshimiwa Waziri hapa unaweza ukatumia miezi kadhaa. Kuna marufuku zinatolewa tu kila siku na hata wafanyabiashara waliomo humu ndani wamekuwa wakilalamika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, *ni-declare interest* nilikuwa kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, tulikutana na tatizo hili ambalo Mwenyekiti amelizungumza hapa vilevile la vibali

vya sukari ya viwandani. Vipo viwanda ambavyo tunapozungumza sasa hivi vimefungwa kama Kiwanda cha SAYONA kule Dar es Salaam kutokana na sukari yao kuzuliwa bandarini tangu mwezi wa nane eti uhakiki unafanyika na ukimuuliza Mheshimiwa Waziri anasema hili liko kwa tajiri mwenyewe. Kwa hiyo, masuala kama haya yanaleta shida. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya hizi mamlaka zetu za udhibiti, TRA, ubabe mtupu na urasimu ambao hausaidiaa nchi hii. Nimeona kwenye magazeti ya leo TRA sasa wanawaomba wafanyabiashara walifunga biashara zao warudi. Hizi kauli za kukinzanakinzana zinatupa shida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jana Waziri wa Fedha alikiri kwamba hali ni mbaya na ndiyo maana bajeti hazitekelezeki. Hawawezi kukusanya mapato kwa sababu ya hii mikanganyiko ambayo ipo kwenye uendeshaji wa Serikali yetu. Kwa hiyo, tunawataka waache hayo mambo ambayo wanafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kushikashika vitu vingi bila ya kuwa na jambo moja ambalo tumeamua kulifanya kwa sababu ya tafiti ambazo tumefanya na tukalikamilisha. Mheshimiwa Zitto hapa amezungumzia Mchuchuma na Liganga. Hivi kweli kama tuna akili sawasawa, tumefanya tafiti zetu na tumedhamiria kweli kuleta mapinduzi na kukomboa watu wetu ni kwa nini hatuutekelezi mradi huu? Tuna mradi wa Bwawa la Kidunda pale Morogoro ambalo linahitaji Dola za Marekani milioni 251 ili tupate umeme, ajira, kusaidia kilimo chetu, ku-stabilize Mto Ruvu na maji kwa ajili ya viwanda lakini jambo hili linaendelea kuwa ni hadithi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo nilisema hapa juzi, nchi hii inaagiza chakula kwa mwaka kulingana na takwimu za Benki Kuu ya kwetu sisi bilioni 888.5. Hivi jamani hii Serikali haina uchungu na nchi hii? Hivi hawaoni kwamba tungechukua hizo Dola bilioni 251 tukawekeza pale Kidunda

tungeweza tukaokoa hizo bilioni 888.5 na baada ya hapo tukaenda sasa kuwekeza katika mambo mengine ambayo kwa kweli mimi naita ni mambo ya kishamba tu, ya kujionyesha. Eti na sisi tuwe na ndege kwa kuwekeza trilioni moja tena sisi kwa sera ya nchi yetu tumeshakubaliana kwamba twende kwenye *Private Public Partnership (PPP)* hatufanyi. Tungeweza tukaweka hayo masuala ya ndege kwenye hiyo *PPP*, sasa hivi tunajenga reli ya *standard gauge* ambayo ni kitu cha maana na muhimu sana lakini tukaenda kwenye utaratibu huo. Tunachukua pesa za Watanzania, badala ya kuwekeza kwenye mambo ya msingi ambayo yatawapa matokeo ya haraka na yatakayosaidia kupiga hatua kwa haraka...

### TAARIFA

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Kaka yangu Mheshimiwa Komu, namna ya uwekezaji kwenye ndege ni moja ya eneo la biashara ambapo litaingiza mapato. Mapato yako ya aina nyingi, mojawapo ni *corporate tax, Pay As You Earn, SDL*, tutaimarisha utalii, kwa hiyo, itaendelea kusaidia sekta zingine ambazo zinaingiza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu hamna haja, muda umekwisha, huu ubishi wa mambo ya ndege sitaki kuuendeleza tena, imeshasemwa vya kutosha.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona upande wa *CUF* hamjajiandaa. Tuendeleo na Mheshimiwa Joseph Mhagama.



**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo ya kuchangia sekta muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Kwanza kabisa, niwapongeze Wizara na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kusimamia vizuri sana sekta hii ya viwanda na biashara kiasi kwamba wadau tunapata matumaini kwamba tunaweza kuifikia Tanzania ya viwanda ndani ya kipindi chake cha miaka 10 ya uongozi wake mahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kupata Tanzania ya viwanda kama tutaendelea kupuuza mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma, nataka nitumie nafasi hii nieleze vizuri, ulianza kuzungumziwa na Mbunge mtangulizi wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, lakini imekuja kuongelewa kwa zaidi ya miaka 10 na Mheshimiwa Jenista Mhagama (Waziri) na mimi ni Mbunge wa tatu kulizungumza hili lakini mpaka leo *commitment* ya Serikali imekuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Liganga kuna chuma, tathmini inaonesha chuma iliyopo Liganga inaweza kuchimbwa kwa kiwango cha tani milioni moja kwa mwaka, hiyo ni tani ya chuma. Chuma hii pamoja na kuzalisha chuma, inazalisha mazao mengine yanayoambatana na chuma. Kuna madini ya *vanadium pentoxide* na kuna *titanium dioxide*, haya nayo ni madini yanayoambatana na chuma. Watanzania wote tunajua chuma ni malighafi ya msingi ya viwanda. Ujenzi wa viwanda unatumia sehemu kubwa chuma, mashine zote za viwandani kwa asilimia kubwa zinahitaji chuma, unaipataje Tanzania ya viwanda bila kuchimba chuma ya Liganga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda jikoni utakuta kijiko, kisu, na uma, hivi vyote vinatengenezwa na chuma. Ukienda shambani utakuta jembe, panga, nyundo, vinatengenezwa na chuma. Ukipanda gari, asilimia 80 ya gari ni chuma, ni utajiri mkubwa sana Watanzania tumeauacha pale Liganga. Ipo mifano mingi, tukienda kwenye nyumba zetu

tunazozijenga, bati ni *product* ya chuma, madirisha yetu, nondo na *grill* zote hizi ni *product* ya chuma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni viwanda vingapi vinaweza kuanzishwa kutokana na chuma ya Liganga? Tunaweza kutengeneza viwanda vya bati, viwanda vya nondo, viwanda vya magari na kila aina ya kiwanda tunachokitaka tutatengeneza na sisi wenyewe tutakuwa wateja namba moja wa hivyo viwanda. Hatuwezi kuipata Tanzania ya viwanda kama hatuweki makusudi kwenda kuchimba chuma ya Liganga.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1864, nchi ya Marekani iliahirisha ujenzi wa reli kwa sababu walitaka watumie chuma yao kujenga reli kwa sababu waliamini kiwango cha chuma ambacho kitahitajika kujenga reli iwapo kitachimbwa ndani ya nchi husika, kwanza kitaokoa pesa kubwa ya Serikali lakini kitachangia sana kwenye pato la Taifa. Mwaka ule 1864 wakati Marekani wanajenga reli chuma cha ndani kilikuwa na bei mara mbili ya chuma kilichokuwa kinatoka nje ya nchi ya Marekani, hata hivi kwa sababu ya uzalendo waliamua kutumia chuma iliyozalishwa ndani. Kwenye hili niombe sana Wizara iamue sasa kwenda kuchimba chuma cha Liganga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, chuma cha Liganga pamoja na kutoa malighafi ya tani milioni moja ya chuma kwa mwaka itatoa ajira takriban 4,000. Ajira 4,000 ni mchango mkubwa sana kwenye idadi ya ajira. Tumesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ni nzuri. Hata hivyo, ukifanya uchambuzi, ajira zilizozalishwa kati ya mwaka 2015 mpaka 2017 ni 26,113, ajira 4,000 zina mchango gani katika hiyo maana yake ni zaidi ya robo ya ajira zilizozalishwa katika kipindi hicho.

## TAARIFA

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Hizi taarifa tungeomba ziwe za maana. Ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mjumbe anayezungumza kwamba ajira zitakazotolewa na Mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Liganga ni ajira zaidi ya 32,000 na siyo 4,000. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakubaliana na wewe, ajira 4,000 zinaweza zikawa za moja kwa moja lakini baada ya hapo ajira ni nyingi sana. Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa Mhagama. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili taarifa hii. Nikibaki hapo, ajira zitakazozalishwa kwenye mgodi huu wa chuma pamoja na *spillover effect*, maana yake ni zaidi ya ajira zilizozalishwa katika kipindi hiki chote cha utawala huu, kwa hiyo, si jambo la kulifanyia dhahaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nabaki hapo hapo kwenye Liganga na Mchuchuma, mradi wa Mchuchuma utakaozalisha kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe, umeme ambao utazalishia chuma cha Liganga, mtambo huu utakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme *megawatts* 600, hiyo ni faida nyingine. Sasa *megawatts* 600 ni sawasawa na nusu ya umeme wote tuliokuwa nao mwaka 2015. Mheshimiwa Rais amekabidhiwa nchi hii ilikuwa na umeme wa *megawatts* 1,308 sasa Mchuchuma peke yake itazalisha umeme *megawatts* 600, si kitu kidogo wala siyo cha kukidharau. Umeme huu sawa na robo ya umeme wote utakaozalishwa kwenye *Stiegler's Gorge*. *Stiegler's Gorge* watazalisha umeme *megawatts* 2,100 na *megawatts* 600 ni robo ya huo umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisitize kwa kusema umeme huu wa *megawatts* 600 utakaozalishwa Mchuchuma ni asilimia 12.2 ya malengo tuliyojiwekea ya umeme tunaohitaji mpaka ifikapo mwaka 2020. Sasa unajua huwezi kuipata Tanzania ya viwanda bila umeme. Katika michango yangu

iliyotangulia nilisema, umeme tulionao Tanzania hauwezi kutupa Tanzania ya viwanda. Afrika Kusini mwaka 1970 walikuwa na *megawatts* 14,000, sisi leo tuna *megawatts* 1,500 mpaka 2,500, tunahitaji uzalishaji mkubwa wa umeme. Mradi wa *Stiegler's Gorge* ni mradi muhimu sana kwa Taifa letu, lazima tuupe nguvu, lazima tuunge mkono lakini lazima tuongeze vyanzo, chanzo kingine ni huu wa Mchuchuma, *megawatts* 600, kwa kutumia makaa ya mawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeongea kwa msisitizo mkubwa kwa sababu ninaamini hatuwezi kuipata Tanzania ya viwanda bila umeme wa kutosha na hatuwezi kuipata Tanzania ya viwanda bila kwenda Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, niongezee tu hapo, kwenye hili suala la umeme. Wenzetu nchi nyingine wanaongea *megawatts* 84,000 sisi tunaitafuta Tanzania ya viwanda bila kwenda kuchimba chuma, bila kwenda kushughulika na Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nichangie tu kwamba, Tanzania tuna bahati, tumeendelea kuvutia wawekezaji na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri amefanya sana kazi tumeona wawekezaji toka nchi mbalimbali wanakuja kutoka Ujerumani, Ufaransa, ni *initiative* kubwa sana hii, watu wamebeza lakini wanabeza kwa sababu hawajui misingi ya uchumi. Hawa wanapokuja watatuongezea teknolojia na mtaji, tutahakikisha kwa kuwatumia hao tunavuka, tunafikia haya malengo yetu lakini eneo muhimu ni kulinda viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu muda haujanitoshia, nichukue nafasi hii kukushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mhagama kwa mchango wako. Ni kweli haya mambo ya Mchuchuma na Liganga kwa kweli yamesemwa kwa miaka, ni vizuri wakati fulani Mheshimiwa Waziri utakapokuwa kesho una-*wind up* ukatupa kidogo picha na Mwenyekiti wa Bodi ya

*NDC*, Dkt. Samuel Nyantahe yuko hapa, tulimtambulisha. Ninyi *NDC* mnatuangusha sana, kuna siku tutawaita hapa, inaelekea ndiyo mnaomwangusha Mheshimiwa Waziri ninyi *NDC*. Hiki kitu kimeongelewa sana kwa nini kiwe kinakwenda *slow-slow*. (*Kicheko/Makofi*)

Twende *CUF*, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya nzuri na leo hii kuweza kusimama katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mwenyekiti wangu wa Chama-Taifa, *full bright*, Profesa Ibrahim Lipumba kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya ujenzi wa Chama changu. Pia napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya ujenzi wa Chama changu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niingie katika mada. Wakati Tanzania tunaelekea katika uchumi wa viwanda, ni lazima tuwe na umeme wa uhakika na hakuna mwekezaji atakayekubali kujenga kiwanda ili apate hasara kwa sababu umeme unapokosekana kwa saa nne tu ni hasara kubwa kwa mwekezaji. Kwa mfano, itabidi apunguze wafanyakazi lakini pia wafanyakazi wataliobaki wanahitaji mishahara. Pia uzalishaji utakuwa chini ya kiwango, kwa mfano, kiwanda kilichopo kule kwetu Mtwara, Kiwanda cha Saruji cha Dangote kama kilikuwa kinazalisha kwa siku tani 100, umeme unapokatika uzalishaji utapungua, kiwanda kitazalisha tani 60 badala ya tani 100. Hii ni hasara kubwa kwa Taifa na mwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije katika masuala ya ajira. Umeme unapokuwa wa mgao au unapokatika mwekezaji itabidi apunguze wafanyakazi. Akifanya hivyo atakuwa amepunguza ajira na familia nyingi zitaishi maisha ya dhiki kwa kuwa kipato cha familia kitakuwa kimepungua.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi sasa wameamua kujajiri kwenye viwanda vidogo vidogo kama viwanda vya kuchomelea (*welding*), viwanda vya kuwekea samaki, viwanda vya kutengeneza barafu, viwanda vya *salon* za kike na za kiume, vyote vitakuwa hazifanyikazi kwa kukosa umeme wa uhakika. Hii ni hasara kubwa kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije upande wa kodi za Serikali. Uzalishaji wa viwandani ukipungua hata kodi za Serikali nazo zitapungua. Serikali itashindwa kutimiza majukumu yake ya kupeleka miradi ya maendeleo kwa wananchi wake. Ushauri wangu kwa Serikali iwekeze nguvu kubwa katika uzalishaji wa gesi iliyoko kule Msimbati, gesi ya Mnazi Bay ili iweze kutimiza majukumu yake ya kusambaza umeme wa majumbani na viwandani.

Mheshimiwa Spika, niongelee masuala ya kibiashara. Akina mama wengi tumepata mwamko wa kufanya biashara lakini kikwazo kikubwa tunachokumbana nacho ni kodi kubwa tunazotozwa na Maafisa wa *TRA*, tunafanyiwa makadirio makubwa mno. Naiomba Serikali yetu Tukufu ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli itupunguzie kodi hizi kwa sisi wajasiriamali, kama maduka ya nguo, vifaa vya ujenzi, mahoteli, biashara ya magari ya abiria yaendayo mikoani na daladala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Jitu Soni na atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi siku ya leo kuchangia. Awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kunijalia kufika hapa leo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya pamoja na watendaji wake wote. Muhimu ni kuelewa dhana nzima na mahali ambapo wanataka nchi yetu ielekee. Mimi nashukuru kwa hii dhana nzima ya kuwa na Sera ya Viwanda ambapo naamini kabisa tukienda vizuri na wote tukachangia vizuri na kila mmoja akaweka mawazo yake pale na tukaangalia changamoto zilizopo na namna ya kukabiliana nazo, mafanikio yapo na uchumi wetu utaendelea kukua.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi uchumi wetu ni mzuri na unaendelea kukua, kuna changamoto ndogo ndogo ambazo naamini Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya Mheshimiwa Mwijage na Naibu Waziri pamoja na timu nzima ikiongozwa na Katibu Mkuu na wote wanafanya kazi nzuri na kubwa. Changamoto bado zipo na tunahitaji kuwapa msaada, kuwapa mawazo mbadala na maeneo ambayo wanafanya vizuri tuwapongeze lakini maeneo ambayo wanatakiwa kuyafanyia kazi wafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu ni kuangalia namna ya kuunganisha Serikali yaani *coordination* bado haipo. Waziri unafanya kazi peke yako na kila Wizara inajitegemea. Mngefanya kazi kwa kuunganisha Wizara zote ili tupate mafanikio makubwa. Tanzania bado *easy of doing business* haipo. Bado kuna ukiritimba mkubwa na ukiangalia kila mmoja anajitahidi kuhakikisha kwamba anafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, muhimu ni kuangalia namna ya kulinda viwanda vya ndani. Namna ya kulinda viwanda vya ndani ni lazima muwekeze kufanya utafiti wa uhakika

kuhakikisha kwamba bei ya uzalishaji wa viwanda vyetu vya ndani inakuwa ndogo ili ishindane na bidhaa zinazotoka nje, hilo ndilo jambo kubwa kuliko yote. Leo hii wote wanaowekeza kwenye viwanda gharama yao ikiwa ni kubwa kuliko zile bidhaa zinazotoka nje watashindwa kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sisi watu binafsi tukifanya utafiti tunakuta bado tuna changamoto kwenye *regulatory bodies* zetu. Tunaendelea kushauri mziunganishe, ziwe moja na watu wasiwe analipa kwenye hizi *regulatory bodies*, ingekuwa ukishalipa kwenye leseni ya biashara basi huko huko kila kitu kiwe kimelipiwa ili tusipate usumbufu. Wanapokuja kukagua wakague wakati wowote lakini wasisumbuliwe kwa maana kwamba kila mmoja anataka alipwe tozo yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ni kuwekeza kwenye utafiti. Kwa sababu bila kufanya utafiti wa uhakika, kwenye *TIRDO*, *SIDO* na *COSTECH* ipatiwe fedha bado suala hili la namna ya sisi kuendelea itakuwa ni ngumu. Kwa mfano, ukiangalia viwanda vya ndani bei ya kuzalisha sukari, mafuta lakini pia bidhaa zote zinazoweza kuzalishwa ndani ya nchi, leo tuangalie kwenye pamba (*Cotton to Clothing*) ni ngumu. Kamati yetu ilitembelea kule *MWATEX* na viwanda vingine, bado unakuta gharama zao ni kubwa sana ukilinganisha na bidhaa inayotoka nje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa usiangalie tu pale kwenye kiwanda anaajiri watu wangapi na analipa nini, angalia *spillover effect* kwamba kuanzia mkulima mpaka hapo inapofika kwenye kiwanda na bado ile nguo itakayozalishwa wale washonaji na wengine ni kiasi gani itaweza kuzalisha. Bei ya bidhaa inayotoka nje Serikali ilituahidi kwamba nchi ambazo tunaagiza kutoka kwao kwa wingi mtaangalia bei zao, wengi wana-*under declare*. Wakisha-*under declare* kwa mfano kwenye *hii Cotton to Clothing* mtu wa ndani hawezi kushindana na huyu wa nje.



Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukapata uhakika wa bei ya uzalishaji na ni vizuri mkakaa na wafanyabiashara wakawaeleza bei ya uzalishaji wa viwanda vya ndani. Sehemu nyingine, kwa mfano, kwenye pombe kali, ni mahali ambapo Serikali inapoteza pesa nyingi sana kwa sababu gharama yake ya uzalishaji haijulikani. Wengine wanauza kwa bei ya kodi tu, sasa ile pombe anauzaje? Ina maana kuna mahali ambapo tunapoteza mapato mengi ni vizuri kuangalia. Pia tukiangalia viwanda vyetu kwa mfano vya mbolea, yeye kwa upande wa kodi anatozwa kodi zote hawezi ku-*claim* kwa sababu *end product* yake bado haina VAT lakini ile inayotoka nje haitozwi, unakuta gharama yake ya uzalishaji inakuwa kubwa hawezi kushindana na ile mbolea ambayo imetoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni viwanda na biashara mngeangalia pia kwa nini *informal sector* inazidi kukua? Leo hii asilimia 80 ya watu wako kwenye *informal sector* (sekta isiyokuwa rasmi), ni kutokana na hizi tozo, kodi na ushuru mbalimbali ambapo mtu anaona ni kero anaona ni bora aendelee kuwa *informal* na maisha yanaenda. Kama tuki-*formalize* na tukiangalia namna ya kwenda haraka Serikali itapata mapato mengi zaidi kwa sababu *tax base* yetu tukiitania nina uhakika kabisa kwamba unaweza ukapunguza hizo kodi nyingine ili wengi walipe kodi ziteremke na *compliance* itakuwa ni kubwa. Kwa hiyo, hilo ni jambo muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama mngekuwa mnafanya kazi na viwanda vingine, niwape mfano, Manyara tuna Kiwanda cha Kuchambua Pamba, ambapo kwenye sekta nzima ya kilimo wanatumia umeme kwa muda mdogo, ni viwanda kabisa vikubwa vinatumia kwa muda wa mwezi au miezi miwili halafu wanafunga mpaka msimu ujao. Unakuta wanalipishwa *capacity charges* ya miezi mitatu asilimia 70 ya ile gharama, *cost of production* lazima iwe juu. Kwa mwendo huo viwanda vingi vitaendelea kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukija kwenye maziwa na viwanda karibu vyote msipoangalia, msipokaa na Wizara nyingine ambazo zote ziko kwenye sekta hiyo ya viwanda, kuanzia *production* mpaka wakati wa kuuza, bado hamtakuwa mmevilinda viwanda vya ndani. Ni muhimu kuangalia namna ya kupata *cost of production*, faida na kodi. Ni muhimu Serikali iendelee kupata kodi yake sahihi maana isipopata kodi yake sahihi hizi ndoto zetu za kuwekeza kwenye huduma nyingine hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, pia tuangalie viwanda ambavyo vitalenga wakulima, wafugaji, wavuvi, vitu wanavyozalisha vinawezekana kupatikana ndani ya nchi. Kwa nini tunaendelea kuagiza vitu vyote kutoka nje? Bahati nzuri Mheshimiwa Rais pia amelizungumzia mara nyingi, tunaomba sasa muendeleo kushirikiana kama Serikali moja, kuwe na uratibu baina ya Wizara zote ili ndoto yetu iweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna jambo lingine ambalo ni muhimu tujue kwamba viwanda haviwezi kujitegemea bila kujua *raw material* yatakuwa yanatoka wapi. Kwa nchi yetu *raw material* kwa sehemu kubwa ni sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Tukiwekeza kwenye hizo sehemu tatu na mkaweka mkakati kwamba mwaka huu tunafanya *kwenye product* mbili au tatu, tukawekeza *value chain* nzima, yaani mnyororo wa thamani kutokea kwenye uzalishaji, viwandani mpaka kwenye kuuza, nina uhakika kabisa kwamba ndani ya miaka miwili, mitatu, tutaona mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi yetu kuagiza bidhaa ambazo tungeweza kuzalisha ndani ya nchi hii. Mifano ipo mingi, kwanza tuangalie kwenye matunda na mbogamboga, samaki, vitu vyote hivi tunaweza kuzalisha ndani ya nchi. Ni vizuri kama Serikali kwa pamoja tuwekeze kwa ajili ya upatikanaji wa bidhaa hizo. *Juice* zote tunazokunywa hakuna hata tone moja linalozalishwa hapa nchini zote ni *concentrates* kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye biashara, kwa mfano kwenye pombe kali, bei ya kodi baina ya pombe inayozalishwa ndani ya nchi na nje ya nchi ni ndogo, hivyo hivyo kwenye *juice*. Sasa tuangalie, inayozalishwa ndani ya nchi ama tufute kabisa au ipungue kabisa lakini ile inayotoka nje tuipandishe ili watu wawe na *incentive* ya kuwekeza hapa nchini, waone kwamba ni bora kuwekeza hapa nchini kuliko kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine bado zina mamlaka ya kusamehe kodi kwenye bidhaa zao za *export* lakini sisi hatuna. Kama Kenya au Zambia wanazalisha wao wanapewa kuingiza nchini bila kodi unakuta bidhaa zao ndio ziko kwenye soko letu badala ya sisi bidhaa zetu kuingia sokoni, kwa sababu sisi hatuna msahama wa aina yoyote. Nchi za *SADC* tayari tuna ile *SADC Protocol* ambapo bidhaa zao zinapouzwa kwenye nchi hizi kodi yake ni ndogo, kwa hiyo, ushindani unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kama Serikali muangalie mambo haya na Wizara hii ya Viwanda na Biashara ndiyo mnatakiwa kufanya utafiti wa uhakika, mshauri Wizara nyingine zote kwa pamoja mfanye nini. Pia tuhakikishe kuna miundombinu muhimu kama barabara na umeme kwa wale wanaohitaji kuwekeza kwenye viwanda. Vilevile tuwaondolee changamoto nyingine, kwa mfano, watu wanaanzisha viwanda halafu unasema barabara hii mwisho tani kumi hatuwezi kufika. Ni muhimu Wizara hii iendelee kushauriana na wengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba leo nianze kwa kutoa tafsiri fupi ya nini maana ya viwanda. Kiwanda ni mahali ambapo malighafi inachakatwa kuwa bidhaa iliyokamilika kwa ajili ya mtuamaji au bidhaa kwa ajili ya viwanda vingine viweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa tafsiri hiyo fupi ya viwanda, sasa tutaona Tanzania tutaweza kuelekea katika nchi ya viwanda. Historia ya viwanda duniani kote ukiangalia kwa mfano Britain, America, India, France, China walianza kwa kuwa na viwanda vya nguo na ndipo wakaweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zitto ameeleza kwa kifupi mimi nitaenda kwa undani zaidi. Inasikitisha sana ni kwa namna gani sisi kama Tanzania tunaweza kuwa ni nchi ya viwanda kama hatutaongelea viwanda vya nguo. Leo katika kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri sijaona ni namna gani ameongelea viwanda vya nguo nchini Tanzania. Hii inasikitisha sana kwa sababu inaonesha ni kwa namna gani hatuwezi kuwa na nchi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na nchi ya viwanda nchini Tanzania halijaanza leo, lilianzishwa na Mheshimiwa Rais wetu Mtukufu, Hayati Julius Kambarage Nyerere mwaka 1970 hadi mwaka 1992 viwanda vikabinafsishwa. Inasikitisha Serikali haijaweza kuvichukulia hatua yoyote viwanda 156 vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niko katika Kamati ya Viwanda na biashara. Kamati ilitisha *list* ya viwanda 156 ambavyo vilibinafsishwa mwaka 1992. Taarifa ambayo ililetwa mbele ya Kamati na ninayo hapa, Serikali inajaribu kueleza ni kwa namna gani inachukua hatua lakini ukiangalia maelezo yanayotolewa ni kwamba ushauri wa Mwanasheria

Mkuu wa Serikali unachukuliwa na wanasema mashauri mengi yako mahakamani.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii kusema ukweli hata Kamati ilisoma na ikaona na haikuweza kuridhika na majibu ya Serikali. Nilitegemea leo hii katika kitabu hiki ambacho ni cha Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Waziri angeweza kuelezea na kufafanua ni kwa namna gani Serikali imejipanga kuwachukulia hatua watu ambao walibinafishiwa viwanda 156. Watu hawa ni wezi, ingekuwa ni nchi nyingine kama China wanguyongwa kwa sababu ndiyo wametufikisha hapa sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umasikini tulio nao Tanzania leo ni kwa sababu ya viwanda vilivyobinafishwa. Viwanda hivyo 156 vingi ambavyo ni vikubwa vilikuwa ni vya nguo. Sasa ukiangalia kama nilivyoanza kusema viwanda vya nguo vilisababisha nchi za Marekani, Britain, France na China kuweza kufanikiwa kuwa nchi za viwanda lakini leo hii sasa sisi Tanzania tuko wapi, tunaenda wapi? Naitaka Serikali kuchukua hatua kwa hivi viwanda ambavyo vilibinafsishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huyo anaitwa Mheshimiwa Kiteto Koshuma. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kutangulia kusema hayo, naomba sasa tuangalie katika Mkoa wa Mwanza. Mwanza tuna Kiwanda cha *MWATEX*. Kiwanda cha *MWATEX* kilikuwa kina wafanyakazi zaidi ya 3,500 miaka ya nyuma kikashusha wafanyakazi hadi kufikia 1,500. Leo hii tunaongelea wafanyakazi si zaidi ya 150 katika Kiwanda cha *MWATEX*. Suala hili linasikitisha sana. Siku moja nilisikia Mheshimiwa Rais akisifia kwamba Kiwanda cha *MWATEX* kinafanya vizuri, yawezekana Mheshimiwa Rais hajapata ukweli kutoka kwa watendaji juu ya Kiwanda cha *MWATEX*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana sana, watendaji wa Wizara hii ya Viwanda wamsaidie Mheshimiwa Rais, kwa kumueleza ukweli na si kwa kuja hapa kwa kujitamba kwamba tuna viwanda vingi, viwanda vingi wakati *impact* kwa Watanzania haionekani? Mtu anakuja hapa anaongelea suala la viwanda vya cherehani, hivi unataka kusema leo hii mimi nikimuita Waziri wa Viwanda na Biashara kwamba twende naye Mwanza tukazindue viwanda watu wana vyerehani vinne, atakuja kweli? Je, inaleta *impact*? Mimi hainiingii akilini, sahamahi sana kwa kusema hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna Kiwanda cha *MUTEX* ambacho kiko Musoma kimekufa. Pamoja na viwanda vingine ambavyo vimekufa Kiwanda hiki cha *MUTEX* kinanisikitisha kwani kilikuwa kinatoa vitenge na kanga nzuri, vitenge vilikuwa vinauzwa mpaka nje ya nchi Swaziland. Leo hii kiwanda kimekufa lakini katika kitabu kiwanda hiki hakionekani kuongelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali kuangalia ni kwa namna gani inachukua hatua madhubuti za mikakati kuweza kuviinua viwanda ambavyo vilikuwa vimekufa ambavyo ni viwanda vya nguo ili nasi tuweze kuitumia pamba yetu. Katika Mkoa wa Mwanza na mikoa mingine kama Simiyu na Shinyanga wanalima pamba kwa wingi lakini unapoangalia kwenye taarifa ya Waziri ni asilimia 30 tu ya pamba ndiyo ambayo inatumika, pamba nyingine yote inaenda nje.

## TAARIFA

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto, jamani hizi taarifa kama nilivyosema ziwe za maana.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Ndiyo Mheshimiwa.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa mchangiaji kwamba aliyewa viwanda katika nchi hii si Mheshimiwa Mwaijage aliyekuja jana, viwanda vimeuawa na Sera ya Ubinafishaji ya Chama cha Mapinduzi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Kweli ni usumbufu tu, ungemuacha Mheshimiwa aendelee kusema. Hizo *blame game* mnazofanya ndizo zinaleta migawanyiko ambayo haina maana. Hapa tunataka tujenge *direction* ya viwanda katika nchi yetu, mwacheni Mheshimiwa aendelee. (*Makofi*)

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunisaidia kujibu taarifa ile isiyokuwa na maana yoyote. Kwa sababu mimi sijasema viwanda amevuia Mheshimiwa Mwaijage ndiyo maana naona kwamba taarifa ya kaka yangu pale haijakaa vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niendelee kwa kusema kwamba viwanda hivi vinapaswa kufufuliwa kwa ari kubwa sana ili pamba iweze kutumika kwa asilimia walau 70 ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Urafiki kinasikitisha. Leo hii ukienda kwenye kiwanda kile kuna *show room* ya magari ya Wachina iko pale. Ni kwa sababu gani Kiwanda hiki cha Urafiki hakifanyi kazi? Tunakuomba Mheshimiwa Mwaijage pamoja na watendaji wote katika Wizara hii muangalie viwanda hivi ambavyo ndivyo vinaweza kutusaidia Watanzania kujivunia na kuwa nchi ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii ukiangalia Kiwanda cha Kiltex, Mbeya Textile, Sungura Textile, Tabora Textile vyote havipo. Katika taarifa tunaambiwa kuna viwanda 11 vya nguo, sijui ni viwanda gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo niliyoyaongea, naomba nitumie dakika mbili kutoa ushauri kwa Serikali. Hatuwezi kuwa na viwanda vya uhakika kama

hatuwezi kusaidia upatikanaji wa uhakika wa umeme katika viwanda vyetu. Mashine nyingi zinakufa katika viwanda kwa sababu umeme upatikanaji wake siyo *effective*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iweze kujitahidi kuangalia viwanda vyetu vinapata umeme wa uhakika lakini pia vinapata maji ya uhakika na pia barabara za kutoa malighafi sehemu moja kupeleka katika viwanda na kutoa bidhaa viwandani kwenda sehemu za masoko ili kuweza kusaidia viwanda vyetu kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia naomba kutoa ushauri, kama inawezekana Serikali ichukue ushauri huu, kwamba viwanda vya nguo vitolewe ile asilimia 18 ya kodi ili kuweza kuvi-*motivate* kuweza kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja lakini yale niliyoyasema yaweze kuzingatiwa na Serikali na hatimaye yaweze kufanyiwa kazi. Nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Huyo ni Mheshimiwa Kiteto Koshuma, nilikuwa simfahamu. Amechangia vizuri sana, huo ndiyo ukweli, sana kabisa na hii ndiyo michango ya Wabunge inayotarajiwa. (Makofi)

Maana Mheshimiwa Rais ameshaweka *direction* kwamba safari hii ni viwanda. Sasa tunakwendaje kwenye viwanda lazima tumsaidie Waziri hapa na timu yake. Leo ametuletea bodi zote, wataalam wamejaa hapa, watu wa viwanda wako hapa wanaangalia Bunge linasemaje kuhusu viwanda? Kwa hiyo, nia ni njema, sisi wote tusaidie kujenga nyumba hii inayoitwa viwanda. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaendelea na uchangiaji, wale wote ambao majina yenu yamo humu, mtaendelea kupata nafasi kadri tunavyoendelea. Nawashukuru sana, mjadala wetu unaendelea jioni. Kwa jinsi hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)



(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu baadaye Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye sekta hii ambayo ni kipaumbele cha Taifa na vilevile ni Dira ya Taifa kupitia Mpango wa II wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile niipongeze sana Wizara kupita kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa sababu kwa kweli utaona wanafanya kazi na kama walivyoeleza kwamba viwanda vinaongezeka, niwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kuonyesha dhamira yake ya dhati ya kujenga Sekta ya Viwanda katika Taifa letu. Ukikuta Rais ameonyesha dhamira yake nina hakika Watanzania wote watajielekeza huko na naomba tufanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ndani ya Bunge hili, alisisitiza kuwa sekta ya viwanda ina jukumu kubwa la kuipeleka Tanzania kwenye uchumi wa kati ifikapo 2025. Toka alipozindua Bunge hili, dhamira ya Rais inatupa uhakika wa kufikia azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nilimuona Mheshimiwa Waziri wa Fedha, akizindua kitabu kilichoandikwa na Watendaji Wakuu wa Serikali kilichoelezea changamoto ambazo zinaikabili azma yetu hii, kama ifuatavyo:-

(i) Ukosefu wa vipaumbele madhubuti;

- (ii) Sera thabiti;
- (iii) Ukosefu wa umeme wa uhakika;
- (iv) Ukosefu wa mitaji;
- (v) Ukosefu wa uzalendo wa kiuchumi; na
- (vi) Ukosefu wa mfumo mzuri wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na viwanda hayo yote ni muhimu. Nimefurahi sana katika ukurasa wa 140, Waziri wa Viwanda mwenyewe amesema kwamba watajaribu kuangalia Sera ya Viwanda endelevu na ndiyo ilikuwa changamoto ya pili kwamba sera zikipitwa na wakati azma yetu inaweza isifikiwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri fanyeni haraka ili tusishindwe kufika kwenye azma yetu ifikapo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nizungumzie mradi wa Liganga na Mchuchuma wa chuma na mkaa. Kama Waheshimiwa Wabunge wengine walivyosema, kwanza niipongeze sanasana Serikali kwa kuuweka mradi huu kuwa mradi wa kielelezo. Wamefanya hivyo, umeanzia Awamu ya Nne na awamu hii imeweka umuhimu mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa uhakika uchimbaji wa chuma ni nguzo muhimu na ni sekta mama kwa kweli, ni viwanda mama au ni viwanda vya msingi. Liangalieni jengo hili thamani yake robo tatu ni chuma uone chuma inavyohitajika nchi hii. Kwa hiyo, tutakavyoharakisha utekelezaji wa mradi huu utasaidia sana nchi hii. Angalieni hata maendeleo ya nchi za Ulaya yametokana na chuma wakati wa Oliver Twist. Angalieni maendeleo ya India, Mahalanaumis alifungwa lakini chimbuko la uchumi wa India leo ni mradi wa chuma kule India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuone hilo, fikirieni kama reli hii ya kati inayojengwa sasa hivi chuma chake kingekuwa kinatoka Liganga ni kiasi gani cha ajira kingebaki Tanzania? Ni kiasi gani cha manufaa makubwa ya uchumi yangebaki Tanzania? Kwa hiyo, naomba sana tuangalie mradi huu ambao unaelezwa toka nikiwa shuleni hata kabla, naomba utekelezaji wake uende kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana miradi kama hiyo *incentive* zinazombwa mziangalie, tunaweza tusipate faida lakini baadaye maendeleo ya kiuchumi na ya viwanda yatakuwa ni ya upesi zaidi, *iron and steel industry* ni chimbuko la maendeleo yote duniani. Angalieni chuma tutakachoagiza nje na kitakavyojenga ajira na uchumi wa nchi ambazo zinatuletea, hayo tunawanyima Watanzania. Nikimwangualia Waziri na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano, sina wasiwasi na nina hakika tunataka bati na misumari itoke hapa, kila kitu ambacho kinataka chuma kitoke hapa, tuna uwezo. Chuma kina *multiplier effect*, sina neno la Kiswahili, kinanufaisha sana sekta zingine kwa haraka. Naomba Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kuongelea masuala ya biashara, naomba Serikali ijitahidi sana kuweka mazingira bora ya kufanya biashara nchini. Tumejitahidi toka miaka iliyopita lakini sasa tuendelee na jitihada hizo. Jambo kubwa ambalo linafanya sasa biashara iwe ya shida, Waziri wa Fedha yupo hapa ni mzunguko mdogo wa fedha. Mzunguko wa fedha uongezeke lakini ziwe fedha ambazo zinakubalika zisiwe ni fedha chafu. Kama *cash* haipo biashara haitakuwepo. Kwa hiyo, Serikali iangalie ni namna gani mzunguko wa fedha utaongezeka ili biashara iende na nchi yetu iendelee kupata faida kutokana na biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mazingira ya uwekezaji, nami ni-*declare interest* hapa nilikuwa Waziri wa Uwekezaji. Mazingira ya uwekezaji yakiwekwa sawa ujenzi wa viwanda hivi utaenda kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nitalishauri hapa na ambalo limeanza na najua Wizara nayo na Serikali kwa ujumla inafanyia kazi, ni kuwa na *One Stop Center*. Hatuwezi kuwa na taasisi mbalimbali zinazohusika na ambazo zimetawanyika tukafikiri kwamba mwekezaji atakuwa na uvumilivu awaze kuona kwamba atabaki hapo na hela zake zinabaki benki halafu hazimletei faida hatakubali. Kwa hivyo, naomba tuharakishe hii *One Stop Center* ianze kufanya kazi. Ukimkamua ng'ombe kama humlishi hutapata maziwa. Kwa hiyo, wawekezaji tuwawezeshe ili waweze kuwekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee juu ya viwanda Hanang. Hanang ni eneo la kilimo, kwa hiyo, viwanda ambavyo vinatakiwa pale ni vya kilimo. Sisi tuna *limestone* nyingi sana kwenye ukuta wa bonde la ufa na hakuna mahali patakuwa na bei na gharama nafuu kutengeneza *cement* kama Hanang. Kuna mwekezaji amekuwa anaomba kuwekeza pale mpaka anakata tamaa kwenda Singida lakini hatapata mazingira mazuri kama ya Hanang, ukuta ule wote una *limestone*. Itigi kuna *gypsum* ambayo inatakiwa umbali wake ni chini ya kilomita 100. Fikiria Dar es Salaam na Mtwara wanapata *gypsum* wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kiwanda hiki kiweze kuanzishwa na tumfanye yule mwekezaji awe na matumaini na kwa hivyo tusimzungushe. Napenda kusema kwamba *bureaucracy* au urasimu unapaswa utumike kuwezesha viwanda vianzishwe na kurahisha uwekezaji. Naomba tusitumie urasimu kuzuia wawekezaji kuwekeza vinginevyo nchi yetu haitapiga hatua. Nataka niseme kwamba Tanzania ni ya pili Afrika katika ukuaji wa uchumi na naipongeza Serikali kwa hili. Ili maendeleo ya nchi yawe *sustainable* lazima yapitie kwenye uwekezaji.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara, naunga mkono hotuba ya Waziri na tukizingatia ushauri huu, kazi yangu ni ushauri siyo kupinga. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary. Tunaendelea na Mheshimiwa Elibariki Kingu, ajiandae Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Kingu hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku hii ya leo kusimama hapa mbele na kuweza kuchangia katika Wizara hii. Pia niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba tunapata Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahia kuona hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaeleza wazi kwamba nchi yetu imekuwa na jumla ya viwanda 53,876 lakini katika hivyo viwanda vikubwa ni 251, viwanda vya kati ni 173, viwanda vidogo 6,957 na vile viwanda vidogovidogo sana ni 46,495, sio kazi ndogo. Mara nyingi huwa tunatoa mfano kujenga nyumba ni kazi ngumu lakini kusema nyumba hii mbaya ni kazi rahisi sana, unatumia maneno sita tu. Leo hii Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa sana ya kuielekeza Tanzania yetu katika uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema peke yake hata kule kupiga debe ni kazi. Wananchi wa Tanzania sasa wameelekea katika kuileta Tanzania ya viwanda. Wawekezaji wote sasa wamebadilika na kutaka kuwekeza kwenye

viwanda. Si jambo dogo lililofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, John Magufuli kwa kazi kubwa anayofanya ya kuelezea na kutia nia yake ya dhati kabisa katika moyo wake kwamba anataka kuleta Tanzania katika uchumi wa viwanda. Lengo la viwanda si kwamba anavileta viwanda vile anataka kukuza ajira kwa vijana. Tumekuwa na vijana wetu wengi hawana ajira viwanda hivi vitakavyojengwa vijana wengi watapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mazuri yapo lakini changamoto kwa kila binadamu ipo na kwa jambo lolote utakalolifanya utakutana na vikwazo. Vikwazo hivyo vinaweza vikatatuliwa polepole lakini azma ya nchi yetu ni kuipata Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayofanya sasa naomba nirudi katika mchango wangu na nitachangia kuhusu leseni za biashara. Nimeona wazi kuna eneo wamesema wameweza kutoza faini za kukiuka sheria za biashara takribani shilingi bilioni 9.7. Kitendo hiki cha watu kukiuka kukata leseni na kuingiza pesa kiasi hiki tunaweza kuona ni kizuri lakini ndani yake kuna ubaya, lazima tujulize kwa nini wananchi wanakiuka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya leseni na hasa katika Jiji langu la Dar es Salaam imekuwa mtihani. Mama lishe akikaa barabarani hana leseni, mama lishe akijiongeza akasema nikachukue tu kakibanda kadogo niweke hapa sufuria yangu ya wali, vikombe vyangu na meza yangu moja imekuwa shida katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mama lishe huyo ataambiwa aende kwanza Manispaa kuomba leseni, ataambiwa nenda TRA ukapate *clearance*, ukifika TRA hakuachi hivihivi akakupa ile *clearance tax clearance* ya hivihivi kwamba unakwenda kwanza biashara lazima uanze

kulipia si chini ya Sh.300,000. Unawenda halmashauri wanakwambia ulipe leseni hiyohiyo Sh.100,000, unarudi Sh.500,000 imeshaondoka mama lishe huyu biashara hajaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akija kuanza biashara miezi mitatu anaambiwa ulipe kodi. Hivi huyu anayejitahidi kuboresha mazingira yake ndiyo sisi tunatumia kuliko yule aliyekaa pale anauza bila ya kitu chochote wala usafi. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri uliangalie hili akina mama wa Dar es Salaam kweli wanaendesha kwa kutumia biashara ndogondogo. Sisi katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam hatuna mashamba ya kulima kwamba tunaweza kupitisha mazao yetu kwenye ki-*carry* kidogokidogo kukwepa kodi, sisi tunayo biashara. Biashara zetu ndiyo hizi akina mama kukaanga mihogo, kuuza *ice cream* lakini yule anayepata mtaji kidogo anahamisha mtaji wake, anauboresha, anaangalia ananunua viti vyake vya *plastic* sita, anaweka, anafanya biashara. Niiombe Serikali iangalie biashara za namna hii, waangalie jinsi gani watawaelekeza akina mama hawa waweze kulipa leseni vizuri si kwa uonevu, wala kukandamizwa na kodi lakini pia waweze na wao wenyewe kujiendesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije *TBS*. *TBS* si rafiki wa mfanyabiashara mdogo ni rafiki wa mfanyabiashara mkubwa. Nasema hivyo kwa sababu akina mama wa mkoa wangu wanatengeneza bidhaa mbalimbali zikiwemo sabuni, mafuta ya nazi, majani, mdalasini, wanajitahidi kwa kadri ya uwezo wao lakini wanavyokwenda *TBS* hawapati ushirikiano wa kuangalia ule ubora wa zile biashara zao hali ambayo inawafanya akina mama hao wakate tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefuatwa na mabinti, nina deni la kulipa hapa Kinondoni, vijana wa filamu badala ya kuonyesha filamu wamejiongeza wakasema wao wawe wajasiriamali, wanatengeneza vitu vyao lakini *TBS* haiwapi ushirikiano kabisa. Nawaona wanatenga fedha za

semina, semina hizo mnawapa akina nani wakati akina mama bado wanahangaika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie eneo la *TANTRADE* ambayo sisi tunaita Sabasaba. Niwapongeze sana hawa *TANTRADE* wanawezesha kuonyesha maonesho mazuri, watu wanajaa, wanapata fedha, lakini sisi kama akina mama wa Dar es Salaam tunafaidika na nini wakati hatuna hata banda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai kabisa na niwapongeze wanachukua akina mama Tanzania nzima. Sisi Dar es Salaam hatuna mgodi, ardhi ile ndiyo rasilimali iliyoko kwetu na uwanja ule ndiyo tunaategemea angalau na sisi Serikali ituwezeshe kupitia Uwanja ule wa Sabasaba. Leo hii akina mama wa Dar es Salaam wanahenyahenyha tu mitaani inafika Sabasaba anaingia kwa tiketi anaenda kuangalia kazi za wenzie yeye kazi yake haipo. Niiombe Serikali, nikuombe Mheshimiwa Waziri utakaposimama unieleze kwamba Mkoa wa Dar es Salaam mwaka huu *TANTRADE* wako tayari kuwatengea banda angalau *tent* tu pembezoni na wao waweze kuonyesha bidhaa zao ili na sisi tuweze kufaidika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lingine kuhusu watoto. Watoto wa Temeke hawana sehemu ya kuchezea. Inapofika Sikukuu ya Iddi na Christmas wanazagaazagaa maeneo yale ya Uwanja wa Sabasaba, hawana pa kuchezea. Hivi Serikali inashindwa nini kuwafungulia watoto wale kucheza mle ndani ya uwanja siku ya Sikukuu ya Iddi na Christmas angalau na wao wafaidike na mradi ule wa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kuingiza watoto wale wakiletwa wajasiriamali wakaleta bembea na michezo mbalimbali ya kitoto, itaisaidia Serikali pia kuingiza mapato. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu wafanye jitihada ili watoto wetu nao wakafurahie uwanja ule. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kuhusu masoko. Ni ukweli kabisa kuna tatizo kubwa la masoko. Pamoja na kuhangaika kote na viwanda, bado bidhaa zetu zinakosa masoko. Mimi nashindwa kuelewa, bidhaa za Watanzania tunafika sehemu tunahamasisha lakini baada ya kutengeneza kile kitu unakuta gharama yake imekuwa kubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa kumpongeza Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii. Kazeni mwendo, mwendo huo huo, Mwenyezi Mungu atawasaidia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Kisangi. Tunaendelea na Mheshimiwa Andrew Chenge, baadaye Mheshimiwa Jaku Hashim na Mheshimiwa Jumanne Kishimba wajandae.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na wataalam wa taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ni pana, ni nzuri na inatoa mwelekeo. Sote tumekubaliana kwamba Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni mojawapo ya sekta za kipaumbele katika Mpango wetu wa Maendeleo katika kuipeleka nchi yetu kufikia uchumi wa kati na nguzo kubwa ni viwanda. Tunaliona hili, wamelisemea vizuri, changamoto zilizopo na jinsi wanavyokabiliana nazo, nawapongeza sana, endeleeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasumbuliwa sana na suala zima la gharama za uwekezaji nchini, bado ziko juu sana. Hili limesemwa vizuri tu kwenye hotuba unaona hali ya upatikanaji wa umeme, maji na miundombinu mingine yote ya kiuchumi ambayo inaendana na kufanikisha uwekezaji gharama gharama ziko juu. Sasa, kuanzia leo mniite Bwana Reli, kwa sababu nitakuwa naizungumzia katika kila Wizara hata kama haihusiki nayo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo na tutakapokamilisha reli hii tutaona uchumi wa Tanzania utaibuka kama uyoga, ikumbukeni tarehe ya leo, Bwana Reli anasema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, narudia kama nilivyosema juzi wakati nachangia kwenye Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Pamoja na jitihada nzuri za sasa, napenda Serikali iendelee kutafuta mikopo ya masharti nafuu ili tuweze kushambulia ujenzi wa reli hii tuikamilishe. Hii ni kwa maana ya reli ya kati pamoja na matawi yake yote ya msingi, tufanye kazi hiyo na tutaona uchumi wa nchi utakavyokua kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishuke kwenye upande wa mradi huu wa siku nyingi sana wa Liganga kwa chuma na Mchuchuma kwa upande wa makaa ya mawe. Kusema ukweli kwa nchi hii kama mpaka leo tunaendelea kuongea kwa lugha hiyo ni tatizo. Hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nadhani ukurasa wa 13, hiyo Kamati ya wataalam, kinachosemwa pale ni kwamba timu hiyo imekamilisha taarifa ya awali wala hatuambiwi ni nini. Maana Waheshimiwa Wabunge, hizi sheria mbili tulizopitisha mwaka jana, mimi nasema Bunge lipo, kama kuna vifungu ambavyo tunaamini kwamba vinakwamisha kwenda mbele, Serikali ndiyo ileile iliyoleta Miswada hiyo Bungeni sasa Serikali hiyohiyo haiwezi ikaogopa kurejea Bungeni na kueleza kwa nini hatuendi mbele. Bunge lipo ndiyo kazi hiyo, watajenga hoja, tutawasikiliza na tutafanya marekebisho twende mbele. Haiwezekani tunaenda mbele tunarudi. Tangu mwaka 2011 Septemba waliposaini mkataba, *NDC* pamoja na ile kampuni ya China, *what is wrong with us Tanzanians?* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tuna vivutio lakini hatuendi mble, jenga hoja, unamwambia mwekezaji bwana, haya hatuyakubali, mwambie ili afunge virago aende lakini hatuwezi kila mwaka tunaenda mbele na kurudi nyuma. Mimi nasema tuufikishe mradi huu mwisho. Mheshimiwa Waziri, tueleze *exactly* changamoto ni nini kwa sababu navyokumbuka mimi mkataba ule unatoa 20% ya *free carried interest* kwa Serikali bila kulipa kwa sababu madini hayo ni *National patrimony* yetu. Pia inaiwezesha Serikali kupitia *NDC* kupata *an additional 49%*. Tuliweka wazi kabisa kwamba mikopo yote ya uwekezaji itakayochukuliwa ambayo wana-*estimate* kuwa *three billion US dollars*, ni lazima ikubalike na pande zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa nasema tufike mahali mradi huu utekelezwe. Tulikuwa tumepanga *by now*, mwaka huu wa fedha, kwa upande wa umeme tungekuwa tumefikia hizo *megawatt 600* na chuma kingekuwa kimeanza kuzalishwa mwaka 2015. Kwa hiyo, reli hii tungekuwa tunaanza kutumia vyuma vyetu lakini *what is wrong with us?* Tusimuangushe Rais Magufuli kwa nia yake njema ya kuleta maendeleo ya haraka kwa nchi yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ukurasa wa 69 wa hotuba kuhusu hili suala la tozo na ada zenye kero zinazojirudiarudia, tumelisema, bado tunaelezwa ooh, tunakaribia kumaliza. Mheshimiwa Waziri nadhani unapohitimisha, hebu mtueleze *exactly*, najua kuna *vested interest* za Mawaziri, wanataka kuendelea taasisi ambazo ziko chini ya Wizara zao, wanategemea sana mapato yanayotokana na tozo na ada hizi lakini sisi tunataka kujenga mazingira mazuri ya kuwekeza na kufanyia biashara Tanzania. Kama tozo basi ziwe na mtiririko mmoja, tunasema *One Stop Centre*. Tumeona Benjamin Mkapa wameweka wote pale, tungependa hata *Export Processing Zones* za maeneo ya mikoani utaratibu huohuo utumike maana humkwazi mwekezaji. Nadhani tuyafanyie kazi haraka haya maana tumeyasema sana mpaka unafika mahali unachoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa jambo la jumla tu. Kusema kweli tunafanya kazi nzuri, amelisema vizuri sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na nilimsikiliza Mheshimiwa Rais kwenye *National Business Council* siku ile lakini hayo ambayo yameamuliwa pale napenda visiwe vikao hivi ambavyo havina *record*, havina yatokanayo ili kikao kinachokuja haya mengi haya yawe yameshatanzuliwa, siyo tena wanakumbushana kulikuwa na kikwazo gani, tumalize tunaenda mbele. Mheshimiwa Waziri, wewe ndiyo sekta yako hii, hayo ambayo unadhani yanakukwamisha lazima uwe mwepesi kuyasema na ndiyo maana taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hiyo zina wataalam wengi tu. Angalia hayo ambayo wameyafanya, nadhani tukifanya kwa haraka tutayafanikisha lakini sio ya watu wazima tunaongea kila mwaka yale yale hatuendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimeona *project* za kielelezo ni hii reli yetu ya kutoka Tanga – Arusha - Engaruka. Sasa najuliza, nimesoma *speech* ya Waziri wa Ujenzi juzi, ninyi mnachotuambia ni nini hapa maana inaonekana hamuongeti pamoja. Mnachosema kwenda kutekeleza, mtatekeleza nini maana kule kwenye ujenzi hatukuona chochote ambacho kinaongelewa kuhusu ujenzi wa reli mpya ya kutoka Arusha - *Lake Natron* na mwaka kesho mtakuja na lugha hizi hizi, kwa hiyo tunabaki hapo hapo. *Let's walk the talk* tumalize, yale ambayo hatuwezi kuyafanya tuseme haya hatuwezi kuyafanya sekta binafsi itakuja tu kama tutaijengea mazingira wezeshi na rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nikupongeze sana Waziri na timu yako, endeleeni. Mazingira ndiyo hayo lakini tusibebe mambo mengi kwa wakati mmoja. Tuchukue vipaumbele vichache tuweze kuvisimamia ili twende mbele. Ahsanteni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Andrew Chenge. Tunaendelea na Mheshimiwa Jaku Hashim, baadaye Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Ibrahim Raza. *(Makofi)*

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nikushukuru kwa kunipa fursa hii, jioni hii kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Hata Mheshimiwa Rais wetu amekuwa akihimiza sana viwanda na kasi yake. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, maneno mazuri sisi Waislam tunasema ni sadaka au maneno mazuri humtoa nyoka pangoni. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, uongozi ni dhamana, ni jambo la kupita, leo lipo kesho halipo na baada ya siasa kuna maisha nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, biashara ni nini? Biashara haifanywi na mtu mmoja, biashara lazima iwe na *monopoly*. Biashara haiwezi kufanywa na mtu mmoja hata kidogo. Uzuri wa Wizara ya Biashara haiwezi kwenda bila ya fedha. Fedha ndiyo biashara, biashara ndiyo fedha, kwa hiyo, hivi vitu kidogo vinaoana. Hapa kidogo Mheshimiwa Waziri nataka unisikilize kwa makini, hasa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango, nikuombe sana, kuomba siyo kosa, kuiba ndiyo kosa, kama kuna watu wanateseka, Benki ya *FBME* watu wanateseka, nimepiga kelele, nitaendelea kupiga kelele mpaka pumzi yangu ya mwisho. Watu wanaweka haki zao kule, wananyanyasika, wengine wameshaanza kutangulia mbele ya haki, hakuna harufu yoyote na Benki Kuu ndiyo dhamana na kama nilivyosema cheo ni dhamana na tutaenda kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu au mbele ya haki, tumetumia vipi dhamana zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanataka kusomesha, fedha zao zimekwama benki. Mnawaambia nini? Benki Kuu iko chini ya Wizara ya Fedha, *Bureau de Change* zote mna-*control* ninyi. Tumeona *Greenland Bank* imefungwa na wakati huohuo mnasema fedha za wateja ziko salama, salama iko wapi? Au Salama jina la mtu? Maana kuna jina la mtu Salama. Kuna wawekezaji Zanzibar pesa zao zimekwama, wafanyakazi wa benki pesa zao zimekwama, mishahara yao haipatikani.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa huruma na unyenyekevu, sijawahi kukuambia hivi Mheshimiwa Dkt. Mpango. Wewe binadamu na mimi binadamu, tuwe na jicho la huruma. Je, ungefanyiwa wewe au mimi tungekubali? Tuwaonee huruma wananchi. Wananchi ndiyo walioweka Serikali hii madarakani. Mtu ana shilingi milioni 200, unampa milioni moja na laki tano ni sawasawa na kumpa peremende baadaye ukamnyang'anya, haifai hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika kero za Muungano, biashara ndogondogo bandarini. Hii tuliambiwa moja kati ya kero ya Muungano. Msijali mtu wa mbali, jirani yako ndiyo mtu wa karibu. Tumetimiza miaka 54 ya Muungano huu na tuombe uendelee kudumu. Wafanyabiashara bandarini Mheshimiwa Mwijage wanateseka na hesabu inaanza moja ndipo ije mbili na tatu. Hawa wote wafanyabiashara wameanzia biashara ndogondogo wakafika kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa Zanzibar amechukua TV moja, amechukua mashati yake matatu, amechukua kilo zake sita za sukari akafika pale ananyanyaswa. Imefika wakati watu wakathubutu kuvunja TVzao, huu siyo ubinadamu wala siyo uungwana. Nikuombe Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Waziri wa Biashara mliangalie hili suala. Leo imekuwa mali inayotoka Zambia, Uganda, Burundi na Kenya inaingia hapa iko salama, inayotoka kwa ndugu zetu upande wa pili utafikiri umeleta bangi au unga, kwa nini tunafanya hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema na nitaendelea kusema, baada ya siasa kuna maisha nje, haya mambo ni ya kupita na cheo ni dhamana lakini hatuwatendei haki. Zanzibar inategemea zao la karafuu, uchumi wake wa pili ni biashara. Leo bandari imezuiwa usajili wa meli, kuna matatizo hatujui kinachoendelea, lakini tusiwanyanyase wafanyabiashara. Mtu ana TV moja, mbili, atakula nini? Anakuja na boti yake asubuhi, jioni apate kuuza aondoke lakini anakuja mzigo unaoza ndani mle, ndiyo lengo hilo?

Katika moja ya kero kubwa ya Muungano hili ni moja, tuwe wakweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, hapa nisikilizeni vizuri. Kiwanda hiki kipo Tanzania, Tanzania hii imeitwa na Zanzibar ikiwemo. Tunalinda viwanda vya Tanzania, je, Zanzibar haipo Tanzania? *That is my question.* Tunalinda viwanda vya Tanzania, Zanzibar haiko Tanzania? *This is my question* au hailindwi Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalinda viwanda vya Tanzania Bara kwa hiyo Zanzibar haipo? Pombe, nondo, saruji, unga wa ngano unaingia Zanzibar lakini bidhaa kutoka kule kuleta huku imekuwa mtihani, tuwe wakweli. Ndiyo yale nimemwambia Mheshimiwa Keissy, moja iwe moja, mbili iwe mbili, mbichi iwe mbichi, kavu iwe kavu. Kama tunalinda tuseme tunalinda viwanda vya Tanzania Bara siyo Tanzania, tuwe na vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. au Prof. Mwijage maana cheo chao kikubwa, juzi ulijibu swali la 205. Mheshimiwa Spika aliona udhaifu wa swali hili, ningesema mimi ingekuwa mtihani, huku unakataa Tanzania hakuna uhaba wa sukari, huku unasema baada ya miaka mitano sukari itakuwa ya kutosha, tukamate wapi? Huku unakataa, uhaba wa sukari haupo, baada ya miaka mitano unasema uhaba wa sukari utakuwa umekwisha. Sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Waziri toka kaangalie bandarini, hiyo sukari imeshafika usije ukauziwa mbuzi kwenye gunia. Uende ukapate ushahidi, usije ukapata ushahidi wa Kinyamwezi. Nenda kaangalie hii sukari uliyowapa vibali imefika? Isije kufika Ramadhan hapa tukawasumbua au kuwatesa wananchi. Narudia tena, Serikali hii isingekuwa madarakani bila wananchi. Hata Uwaziri wako huu, Mheshimiwa Waziri ungekuwa mtihani tungetawala nini, miti au barabara? Wananchi ni kitu muhimu. Hata Mheshimiwa Rais mwenyewe anawajali wananchi, tumpongeze kwa dhati kabisa hasa wananchi wa chini, *credit* yake kubwa iko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isiogope kula hasara kwa mambo madogo madogo kama haya na wewe mshauri Mheshimiwa Rais usiogope kuwa hiki kiko hivi, hiki kiko hivi, mueleze tuna upungufu huu. Tuliwapa vibali vya sukari, mimi na ninyi, twende mguu kwa mguu kama sukari mliyotumbia imeshaingia tani 135,000, twende tukaiangalie.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza lakini itabidi nishukuru hivyo hivyo kwa muda ulionipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, baadaye Mheshimiwa Ibrahim Raza na Mheshimiwa Zainabu Mndolwa.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Nitaanza upande wa viwanda na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala ambalo linaendelea sasa hivi kwa Kiswahili linasema kuongeza thamani au kwa Kingereza ku-*add value*. Suala hili kama hatukulifanyia utafiti wa dhati litatuletea mtafaruku mkubwa. Maana yangu kusema hivyo ni kwamba, kila mwenye kiwanda sasa hivi anapigania kuzuia wananchi wasiuze mali zao akiwa anasema yeye yupo tayari kununua mali yote na kui-*add value*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Hapa tunakatazwa kuuza mahindi nchi za nje tunaambiwa tuuze



sembe lakini watu wa Kongo sembe wanachanganya na muhogo, sasa utawauziaje sembe na wenyewe wakachanganye muhogo, wanakwambia wanataka mahindi ili wakasage waweke muhogo. Kwa kuwa Waziri yuko hapa aliangalie kwa makini sana suala hili, kama mtu anasema anataka ku-*add value* ni lazima aoneshe uwezo wa kiwanda chake ataweza kweli kununua mali za Watanzania ili watu wasikae na mali zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kwenye ngozi. Sasa hivi karibu ngozi zote zinatupwa, zimezuiwa na zimewekewa *export levy* ya 80% na *indication price* iliyowekwa na TRA ni senti 58 ya Dola ambayo ni Sh.1,300 lakini bei ya ngozi leo duniani ni senti 35 ambayo ni Sh.800. Itawezekana vipi sasa mtu alipie Sh.1,300 auze Sh.800? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumesaini mkataba na Uganda na Kenya kwenye hilo suala la ngozi. Wenzetu Waganda na Wakenya wana-*under value invoice*, wanalipia kwa bei chini na kununua mali zetu, ni kwa nini na sisi wananchi wetu wasiruhusiwa kuuza mali zao ili kuondoa huu mtafaruku ambao unaendelea? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaungana na Wabunge wenzangu kwenye suala hili la Liganga na Mchuchuma ingawaje mimi mtizamo wangu uko tofauti kidogo. Mtizamo wangu mimi ni kwamba, madini haya kwa utafiti wa wataalam wetu wanavyosema yako mengi kiasi cha kutosha miaka 100 lakini miaka 100 kwa dunia inavyokwenda haraka ni kweli teknolojia hiyo au chuma hicho kitakuwa kinatakiwa duniani. Kwa nini tusiwe na *option* mbili, tukawa na *option* ya kuuza udongo wa chuma kama ulivyo na tukawa na *option* ya kuyeyusha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya *analysis* ya madini yaliyomo mle ndani nchi nyingi duniani wakati bei ya chuma au madini fulani yanapanda wanauza kwa ajili ya

kupata pesa muda ule na kujikimu. Sasa hivi hapa kwetu tunalia kwamba, hatuna pesa ya maji lakini tuna mlima zaidi ya miaka 50, kuna ubaya gani kufanya *analysis* na baadhi ya mawe yale yakaendelea kuuzwa ili tupate pesa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Jimbo letu la Kahama au Wilaya yetu ya Kahama na Mkoa wa Shinyanga mwaka huu tuna mavuno mazuri sana ya mpunga. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri hili neno la *add value* aliangalie. Sisi tunataka kuuza mpunga au mchele kwa Waganda lakini tunabanwa na sheria inayosema huwezi kuuza mpunga lazima ukoboe mchele, lakini wakati unasubiri kukoboa mchele hilo soko litakuwa linakusubiri kweli kule Uganda? Haiwezekani. Ni lazima Mawaziri wafikirie sana suala hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye suala la biashara. Kwenye mkutano wa Mheshimiwa Rais ni kweli mambo mengi sana yalijitokeza pale. Ukiangalia maswali mengi ya wafanyabiashara ilikuwa ni kwenye tatizo la Sheria ya *Importation* na Sheria ya Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Importation* inatusumbua, sisi tunatumia *tarrif* ambayo haisumbui sana ukienda kwenye vitu kama mafuta ta dizeli, sukari, simenti na vinywaji kwa kuwa hawa wanatumia ujazo au kilo lakini unapokwenda kwenye *item* ndogondogo, nitatoa mfano wa *item* moja, kwa mfano wewe ume-*import glass*, *glass* kwenye *tarrif* inaitwa *glassware*, lakini kuna *glass* ya Sh.10,000 na ya Sh.1,000 lakini *TRA* ata-*pick glass* ya Sh.10,000 kuku-charge wewe wa *glass* ya Sh.1,000/=. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwa yuko hapa ni miongoni mwa kero nyingi sana ambazo wafanyabiashara wamezionesha wakati wa kufanya *importation*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna tatizo kubwa sisi tunaotoka mikoa ya mpakani. Kuna hii sheria mpya ya ku-*declare* pesa. Wananchi walioko Kongo, Burundi, Uganda wanataka kuja kununua mali kwetu Mikoa ya Mwanza,

Shinyanga na Geita. Haiwezekani mtu atoke Uganda au atoke Kongo afike Mutukula aoneshe Dola zake 50,000 apande basi, ni kitu ambacho hakiwezekani hata iweje. Tumeshuhudia wote hapa mtu anatoka kuchukua pesa pale *Mlimani City* anavamiwa anauawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Fedha kwa kuwa yuko hapa alifikirie, hili neno tume-*copy*kwa Wazungu, kwao ni sawa, London uki-*declare* hakuna mtu atakuvamia lakini ku-*declare* kilometa 300 upite porini ambako mpaka mabasi yanafanyiwa *escort* na wewe ulionesha dola, tumekwama kabisa watu wa nje wamekataa kuja kununua mali kwetu kwa sababu hiyo, hawawezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi hizo ni zile ambazo hazina mfumo wa kibenki, Kongo hakuna benki, Burundi kuna vita, watu hao wote wanatembea na *cash*. Nafikiri Waziri wa Fedha kwa kuwa yuko hapa ajaribu sana kulifikiria suala hili ambalo linatusumbua sana. Sisi Mwanza tunauza samaki, mchele na vitu vingi lakini mpaka sasa tumekwama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza kwa kuwa na Waziri wa Nishati yuko hapa tungeomba sana wenzetu wa *TANESCO* waruhusu, kama walivyoruhusu kwenye *transformer*, kwa wafanyabiashara hasa wanaotaka kuanzisha viwanda kama wanaweza kuvuta umeme kwa gharama yao halafu wakawarudishia wakati wa bili inapoanza. Kwa kuwa, yeye sasa hivi analalamika kwamba hana pesa ya kununua nguzo au vifaa vya umeme itasaidia watu wanaotaka kuanzisha viwanda waweze kufanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ibrahim Raza, baadaye Mheshimiwa Zainabu Mndolwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu vilevile kwa kunipa uzima wa afya nikiwa nimesimama hapa kwa nguvu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kaka yangu Waziri wa Biashara na Viwanda, Mheshimiwa Mwijage. Kwa kweli, hiki kitabu nimekipitia leo mchana vizuri kabisa, nakiona kipo vizuri sana. Nimpongeze yeye na timu yake nzima kwa jinsi walivyoandaa bajeti hii na ripoti ya Wizara ya Biashara na Viwanda, Mheshimiwa Mwijage na timu yako hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mambo aliyoyaweka jana vizuri sana. Amewatoa wananchi wasiwasi, maneno yalikuwa mengi kwamba katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan kutakuwa hakuna mafuta na sukari. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Mwijage kwa kutuhakikishia kwamba, hakutakuwa na suala hilo wala matatizo hayo ya mafuta wala sukari. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mwijage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyohangaika kufufua viwanda ambavyo vilikuwa vimekufa. Naweze kusema kwamba jitihada ya Mheshimiwa Rais imetuletea faraja kubwa sana na naamini kwa Waziri aliyekuwa naye ni Waziri jembe kabisa, Mheshimiwa Mwijage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage nimefanya naye kazi wakati nilipokuwa kwenye Kamati ya Biashara na Viwanda miaka miwili iliyopita. Namjua kazi yake, ni mtu ambaye yuko *straight* kabisa na makini kabisa, hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa na ushauri kwa Wizara ya Biashara na Viwanda. Mheshimiwa Mwijage

nataka utusaidie au uwasaidie wafanyabiashara ambao wanapakia mizigo yao Dubai kuja Dar-es-Salaam wanalipia SGS kule Dubai na kila *item* wanatozwa kwa Dola 20 mpaka Dola 30. Baada ya ku-*register* SGS Dubai wanatakiwa baada ya mali kufika hapa TBS inawa-*charge* tena katika kuchunguza vile vitu walivyoleta. Kwa hiyo, wanakuwa wanalipa SGS kule Dubai wakija huku wanachajiwa tena na TBS. Sasa utakuta mfanyabiashara analipa mara mbili ya kile kitu ambacho amekinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa SGS kule Dubai wamekuwa *very slow* yaani ukiwapelekea sampuli, huchukua *more than four or five weeks*, sasa utakuta mfanyabiashara anaumia na kule ameweka mzungo kwenye *godown* za watu analipa zile gharama kwa sababu Dubai hakuna mtu ambaye atakuwezesha kukuwekea mali kwa mwezi mmoja, mwezi mmoja na nusu. Kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri labda ukae na hawa wenzetu wa SGS Dubai na TBS, kwa nini wanakuwa wana-*charge* mara mbili mzungo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa sababu, tukiwasaidia wafanyabiashara naamini watapata nguvu ya kutuletea mali kwa wingi na Wizara ya Fedha itapata kodi. Kwa hiyo, hapa tunampa motisha mfanyabiashara *at the same time* Wizara ya Fedha na TRA wanapata pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna tatizo moja kubwa la wenzetu hawa wa TFDA. Naweza kusema kwamba TFDA sio wote, sitaki kuwakaanga wote, baadhi yao hupelekewa sampuli ikiwa ya maziwa, *juice* au kitu chochote wanakwambia kwamba utapata ripoti *after 60 or 70 days*. Mheshimiwa Mwijage wenzetu hawa TFDA hivi kweli wanatutakia mema Tanzania hii? Wakati wewe unapigania wafanyabiashara walete mali wauze nchi ipate pesa tupate kodi, wanaambiwa warudi *after 70 days*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi navyozungumza haya huwa nina ushahidi, sizungumzi tu kwa kuwaelemea TFDA. Kwa hiyo, naomba TFDA kama kuna upungufu wa watu basi waajiriwe watu wengine lakini huwezi kumuweka mtu *60 or*

70 days ndiyo unampa *report*, inarejesha nyuma maendeleo yetu na sisi tunataka kusonga mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hata hizo ada ambazo wana-charge *TFDA* ni kubwa sana Mheshimiwa Waziri. Ningeomba kidogo hizo ada ziteremshwe ili watu wawe na hamu ya kuleta mali nchini. Kiwango kinachotozwa sasa hivi ni kubwa sana. Hata hivyo vitu ambavyo *SGS* wana-charge kule Dubai kwa kila *item* ni Dola 30 nyingi Mheshimiwa Mwijage. Wewe ni msikivu naamini utachukua hatua. Haya ndio yalikuwa ni kero na nilikuwa natoa ushauri kupitia Wizara yako ifuatilie kwa karibu sana hili suala ili tufike hapo tunapotaka kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana watu wanapoiponda Serikali hii, mimi siwafahamu. Kwa sababu, hiki kitabu kimeeleza kuna wawekezaji 99 wamesajili kuanzisha viwanda Tanzania hii. Ina maana hao wawekezaji ambao wanakuja kuwekeza hapa si wendawazimu, wameshajua Tanzania ni nchi ya amani, Tanzania kuna kuna moja, mbili, tatu. Sasa wanapoiponda kwamba hakuna viwanda au hakuna chochote wasome hiki kitabu ambacho kimeandikwa kwenye ukurasa wa 186, miradi mipya ya viwanda vilivyosajiliwa na *TIC* mwaka 2017/2018. Hii ni ushahidi tosha kwamba watu wana imani na Serikali ya Mheshimiwa Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna wengine wanakuwa na choyo na binadamu sisi tunakuwa na choyo. Mheshimiwa Mwijage ukivaa suti nzuri kama mtu hakupendi atakwambia unaringa lakini kwa sababu umevaa suti nzuri. Kwa hiyo, nasema tupunguze uchoyo, tumpe haki yake Mheshimiwa Rais Magufuli anavyofanya hii kazi kwa sababu, kuileta Tanzania katika amani ni kitu kikubwa sana ndio maana hawa wawekezaji 99 wamekuja kuwekeza Tanzania *billions of Dollars, it is billions of Dollars*. Leo kwa nini tunakaa tunaiponda hii Serikali? *Why?* Badala ya kuipa nguvu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini katika miaka michache ijayo tutakwenda kwenye uchumi wa kati, hapa tulipo tutasonga mbele. Ni juhudi zetu sisi Watanzania, Wabunge waliokuwa humu ndani tumpe nguvu na ushirikiano Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri wake wote walikuwa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaposema kwamba labda kiwanda kiwe na ekari tano, ekari sita, kule China unaweza kukuta kichumba kidogo sana wanazalisha mambo ambayo huwezi kuyaamini Mheshimiwa Mwijage. Wana vyerehani 10, 15 lakini *the production* ambayo wana-*make* ni kubwa sana. Kwa hiyo, kiwanda si lazima kiwe na ekari 10 ndiyo ukaita kiwanda. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ibrahim Raza.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na naipongeza sana Wizara hii na naiunga mkono asilimia 100 Wizara ya Biashara na Viwanda. *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia na tumuombe Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainabu Mndolwa baadaye Mheshimiwa Frank Mwakajoka na Mheshimiwa Gimbi Masaba.

**MHE. ZAINABU M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba sisi kuwa wanadamu kisha akatupa akili na ufahamu ili kuweza kujadili mambo mbalimbali kuhusu Taifa letu. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni kitovu cha biashara katika nchi yetu na wafanyabiashara wa Dar es Salaam huchangia pato kubwa katika Taifa hili lakini wanakabiliwa na changamoto nyingi sana. Ili uanzishe biashara kuna taratibu za kufuata hadi biashara yako ifunguliwe, kwanza lazima upate leseni, lakini kinachotokea kwa wafanyabiashara hao wanaanza kulipa mapato kabla ya kufanya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawaumiza sana wafanyabiashara. TRA wanakadiri watu mapato kulingana na eneo analilopo na siyo biashara wanayoifanya. Wanapoenda kudai leseni wanaambiwa kwanza waende TRA wakakadiriwe mapato, nauliza inawezekanaje mtu hajaanza kufanya biashara anakadiriwa mapato, kauza nini huyu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali Taasisi ya Mamlaka ya TRA itoe *grace period* kwa wafanyabiashara. Wakati wanataka kuanzisha biashara zao kwanza wapewe leseni, pia wapewe muda wa kufanya biashara hiyo angalau miezi mitatu wakati wanatumia mashine za EFD kisha ndiyo wakadiriwe. Kitendo kinachofanywa na TRA kuwakadiriwa watu mapato kabla ya biashara kwa kweli, kinawaumiza sana wafanyabiashara, hususan wa Jiji hili la Dar-es-Salaam. Naomba sana Serikali ilichukue hili na ilifanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naishauri Serikali wale ndugu zetu wafanyabiashara ndogondogo Wamachinga ni wafanyabiashara pia lakini watengewe maeneo maalum. Sasa hivi ukifika katikati ya Kariakoo maeneo ya Narung'ombe, Kongo, Mchikichi, wafanyabiashara ndogondogo wameweka bidhaa zao mbele ya maduka ya wafanyabiashara ambao wanalipa kodi kihalali. Kutokana na *buyer behavior* ya watu wetu wa Tanzania wenye kipato cha chini kuona kwamba biashara zilizokuwa barabarani ni rahisi kuliko za ndani hupelekea watu wenye maduka kushindwa kufanya biashara zao vizuri na Taifa kukosa mapato kutokana na kwamba wafanyabiashara wale wanaosambaza barabarani kutolipa mapato ya aina yoyote.



Kwa hiyo, naishauri Serikali itenge maeneo maalum kwa ajili ya Wamachinga ili nao waweze kufanya biashara pia walipe kodi kwa Taifa letu. Najua kwamba Machinga ni wapiga kura pia wafanyabiashara wa madukani ni wapiga kura wa Taifa hili, kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine sasa hivi kumetokea mtindo kwa Kikosi cha Zimamoto kupita katika maduka ya wafanyabiashara Kariakoo kuwalazimisha waweke *fire extinguisher* ndani ya maduka. *Fire extinguisher* ina kilo 5 na kila mtungi mmoja ni Sh.200,000 na kila mwisho wa mwaka ulipe Sh.40,000 unaweka ndani ya duka, je, moto ukitokea saa 8.00 za usiku wakati mfanyabiashara huyo yuko nyumbani kwake ile *fire extinguisher* itamsaidia nini kuokoa mali zake? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhahiri kwamba Kikosi cha Zimamoto kimeanzisha mradi mwingine kwa wafanyabiashara ili kuwakandamiza. Naishauri Serikali ikutane na Kikosi cha Zimamoto, iwashauri wale wamiliki wa majengo waweke *fire extinguisher* kwenye *corridors* za nyumba na siyo ndani ya maduka ya wafanyabiashara, kwa sababu huwezi kujua moto utatokea wakati gani. Ni bora *fire extinguisher* ziwekwe kwenye *corridor* kuliko ndani ya maduka ya wafanyabiashara, hii itasaidia moto ukitokea wakati wowote aidha, asubuhi, mchana hata usiku kuweza kutumia *fire extinguisher* kuzima moto ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelekea Tanzania ya Viwanda kuna viwanda vingi ambavyo vimepewa wawekezaji. Nitatolea mfano Kiwanda cha Nguo cha Karibu *Textiles Mills* ambacho kiko Wilaya ya Temeke. Kwa sasa hivi kiwanda kile kimefungwa na kimegeuzwa kuwa ghala la kuhifadhia soda. Nimetembelea mwezi uliopita pale wameweka soda na kiwanda kile kilikuwa kinazalisha nguo, vitenge, khanga pia mashuka na kilikuwa kinaleta ajira kwa zaidi ya watu 1,000. Kwa sasa hivi Mheshimiwa Waziri kimegeuka kuwa ghala la kuhifadhia soda na hakuna kiwanda tena pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali, wakati tunaelekea Tanzania ya Viwanda badala ya kutafuta maeneo ya kuanzisha viwanda vingine ni bora kwanza tuvifufue vile viwanda ambavyo vimepewa wawekezaji. Maeneo mengi yalikuwa na viwanda, nitakutolea mfano Mkoa wa Morogoro, mwaka wa 1980 ulikuwa ukifika Morogoro unaweza kupata ajira mapema kuliko kupata chumba cha kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna Kiwanda cha *Canvas Mill, Ceramics, Polyester, Moro Shoe, Tanneries, Magunia*, Kiwanda cha Tumbaku, Kiwanda cha Sukari Mtibwa, Kiwanda cha Sukari Kilombero, vyote hivi vilikuwa Mkoa wa Morogoro, lakini kwa sasa hivi viwanda vile wamepewa wawekezaji na haviendelezwi. Morogoro ni katikati ya Dar es Salaam na Dodoma, viwanda vile vifufuliwe na kupewa wawekezaji na kusimamiwa vizuri, iwe ni *sampling area*. Sasa hivi tunajenga treni ya mwendokasi ambayo itarahisha watu kufika kwa urahisi Morogoro, italeta ajira kwa watu wa Morogoro, Mkoa wa Pwani pia wa Dodoma wanaweza kupata ajira katika Mkoa wa Morogoro. Badala ya kutafuta maeneo ya kwenda kuanzisha viwanda vingine ni bora tuvifufue viwanda vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona viwanda vingi pia Mkoa wa Tanga. Kilikuwepo Kiwanda cha Mbolea, Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha Amboni, Kiwanda cha Gardenia na Mbuni, viwanda vile vyote vifufuliwe kuliko kwenda kuanzisha maeneo mengine mapya, ili viweze kutoa ajira kwa watu wetu. Mkoa wa Tanga unazalisha matunda mbalimbali lakini katika hotuba ya Mheshimiwa tunashauri, kuanzishwe Kiwanda cha Juice ambapo itasaidia wakulima kwenda kuuza matunda yao katika kiwanda kile, kuliko sasa hivi matunda ikifika msimu yanaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushauri Mheshimiwa sana wakati unaelekea kuanzisha viwanda vipya vile vya zamani visimamiwe kwa uhakika ili kuleta ajira na pato la Taifa letu. Naomba haya yazingatiwe kwani yatasaidia sana kuliendeleza Taifa letu kuliko kuanza kukata misitu huko na

kutafuta mashine za kufunga, tuboreshe mashine katika viwanda vya zamani ambavyo vitasaidia kuleta ajira kwa kwa wananchi wetu na pia kuchangia katika pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naomba maoni ya Kamati yazingatiwe ili kuelekea Tanzania ya Viwanda. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Mndolwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii. Kwanza nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbilinyi (Mheshimiwa Sugu) kwa kutoka siku ya leo. Namshukuru sana Mungu aliyemwezesha kukaa gerezani kwa muda wote bila kutetereka na sasa ametoka anakuja kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia hotuba hii na nataka kumaanisha ili ushauri wetu ambao tumekuwa tukiutoa kila wakati katika Bunge Serikali iweze kuufanyia kazi Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkumbuka sana Mheshimiwa Mbilinyi alijaribu kuzungumzia sana kuhusiana na jambo ambalo lilikuwa linafanywa na Serikali ya kuikusanyia nchi ya Kongo mapato. Baada ya ushauri ule nafikiri Serikali ilikubali na sasa ilishaondoa na sasa hivi naona Wakongo wanatumia Bandari ya Dar es Salaam vizuri na mambo yanakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kwamba siasa safi ni uchumi. Tusije tukajidanganya hata siku moja tukafikiri siasa za kibabe, siasa za kutenganatengana zinaweza zikasababisha nchi ikawa na uchumi bora. Siasa ni uchumi lakini pia uchumi ni sayansi. Kwa hiyo, sisi ni lazima

tujue kabisa kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, bila kujua hili tukaendeleza ubabe tunakoelekea siko kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusiana na wafanyabiashara wengi Tanzania wanaohama nchi. Liko kundi kubwa sana la wafanyabiashara ambao wanahama katika nchi yetu na wanakwenda kufanya biashara kwenye nchi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo liko wazi na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara wajibu wake mkubwa ni kuhakikisha kwamba ustawi wa wafanyabiashara na biashara zao katika nchi hii ya Tanzania ni kipaumbele kikubwa kabisa. Huwezi kuamini wafanyabiashara wengi sasa hivi, ukienda Malawi wengi wamehamia kule. Ukienda Zambia maeneo yote kuna wafanyabiashara wametoka Tanzania wamehamia Zambia. Pia ukienda Kongo ambako hali kwa kweli ya usalama si nzuri lakini wafanyabiashara wako tayari kuondoka Tanzania waende wakafanye biashara Kongo, kwa sababu ya mazingira mabaya ambayo yapo kwa wafanyabiashara wetu ambao wanajitahidi kuwekeza kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu jambo moja kwamba leo Mtanzania akitoka na mzigo wake Dubai, akifika kwenye Bandari ya Dar es Salaam amekuja na *invoice* yake ya kiwandani kabisa alikonunua mzigo kinachotokea watu wa *TRA* wanamwambia kwamba hii wamekukadiria vibaya umetengeneza *invoice*, anaanza kukadiriwa upya akiwa bandarini Dar es Salaam. Amenunua mzigo wa Dola milioni 10 anaambiwa huu mzigo bwana ni milioni 20, mfanyabiashara anakimbia, anaacha mzigo, mizigo inakaa pale kwa muda mrefu na biashara baadaye zinakufa na huyo mfanyabiashara anapoteza fedha zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nakumbuka wakati tunajadili hapa, juzi nilikuwa nasikiliza *Radio Clouds* wanasema tumeshangaa sana Wabunge wetu, wanasema wakati Mbunge anaomba mwongozo watu walishangilia

sana, wakati Mwijage anajibu watu wakashangilia sana lakini wakati Mheshimiwa Spika anatoa ufafanuzi na kutoa maelekezo kwa Serikali watu wakashangilia tena. Sasa wanasema Wabunge wetu hawa tatizo ni nini hapa yaani kipi ambacho walikuwa wakikishangilia, ni ule mwongozo uliotolewa na yale majibu ya Waziri au kilichokuwa kinashangiliwa ni yale maamuzi ambayo Mheshimiwa Spika aliigiza Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumesikia hapa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akitoa maelekezo kuhusiana na tatizo la mafuta ambayo yako bandarini. Ametoa maelezo hapa na akasema kwamba anatoa siku tatu. Tunaomba sana uchumi hauhitaji nguvu, unahitaji kukaa na kuzungumza. Hawa wafanyabiashara ambao wamekaa kule na mizigo yao nia yao kubwa ni kuja kuuza na kuhakikisha kwamba wanalipa kodi kwenye Taifa hili lakini kitendo cha kuendelea kutumia nguvu kwa kuwalazimisha haitaweza kutusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ikubali kukaa na wafanyabiashara. Hata mwanzo tuliwaambia kukaa na wafanyabiashara na kuzungumza nao ni jambo kubwa katika nchi hii. Hawa ndiyo watu wanaoweza kulipa kodi na ndiyo ambao wanaweza wakaendesha Taifa hili, lakini bila wafanyabiashara kukubali kufanya biashara katika nchi hii na kuwekewa mazingira mazuri nchi hii haitakusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekiri hapa ndani, amesema tatizo kubwa kwa nini mnasema fedha hazijaenda huku, kwa sababu makusanyo yamekuwa madogo, fedha hakuna. Tafsihi yake ni kwamba wafanyabiashara hawalipi kodi kwa sababu biashara zao zimeshadhoofi lakini wengine wamefunga biashara, wengine wamehama na biashara zao, sasa anataka kodi kutoka kwa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kuangalia ni namna gani wanaweza wakatengeneza

mazingira mazuri kwa ajili ya wafanyabiashara wetu ili waweze kufanya biashara vizuri. Ukienda Tunduma pale mpakani tumepakana na eneo la Nakonde Zambia. Sasa hivi nyumba ambazo walikuwa wanaishi Wazambia zimeshafumuliwa Watanzania wameingia mikataba wameamua kuhamisha biashara zao na sasa wamefungua maduka makubwa upande wa Zambia kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza sana, nimesema ndani ya Bunge lakini pia nimewashauri Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya hawawezi kusikiliza wanaendelea kukomaa wanasema hapana tunataka tufunge barabara. Wamefunga njia ambazo watu walikuwa wanapita, wafanyabiashara wa Zambia na Kongo wakitoka wamenunua mizigo wanapita katika njia ambazo walikuwa wanazipita siku zote. Wamefunga wameweka mataruma wafanyabiashara wa Kongo na wa Zambia wamesema hatuji tena Tanzania tunakwenda kununua maeneo mengine. Kwa hiyo, walichokifanya wafanyabiashara wameamua kutumia akili zao za haraka haraka na kwenda kuhamia upande wa Zambia na leo Zambia maduka ni mengi. Wafanyabiashara walioko pale sasa hivi ni karibuni wafanyabiashara 3,000 waliohama kutoka Tunduma wanafanya biashara Zambia lakini wanalala Tanzania. Kwa hiyo, tunachokizungumza hapa tunakuwa tunamaanisha katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni lazima pia afike mahali aangalie kodi kwenye Taifa hili limekuwa ni tatizo. Kila mwaka wanaleta taarifa hapa kwamba wanakwenda kuzifanyia kazi hizi kero za kodi ili wafanyabiashara wetu waweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini, wafanyabiashara wengi sasa hivi wanakadiriwa kodi, mtu anakadiriwa shilingi milioni 300, shilingi milioni 400, mwingine anakadiriwa shilingi bilioni 1, shilingi bilioni 2 bila sababu za msingi na kuelezwa kwa nini anatakiwa kulipa kodi hiyo. Wafanyabiashara sasa hivi wamekuwa kama wakimbizi, Serikali haiwaamini wafanyabiashara wa Tanzania. Serikali inawaona ni wezi wafanyabiashara wa Tanzania na Serikali

inawaona wafanyabiashara wa Tanzania ni watu ambao wanakwepa kodi wakati si kweli. Kazi ya Serikali ni kuweka mazingira bora na safi ya kufanyia biashara na siyo kuwayumbisha wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema ni lazima tukubaliane ukienda TRA sasa hivi wanakukadiria fedha wanayotaka na ukiwaambia sina fedha wanakwambia nenda halafu baadaye wanakwambia bwana ili tukufanyie vizuri tunaomba utupe labda shilingi milioni 10 au shilingi milioni 5 au shilingi milioni 6 na kwa sababu Serikali imewatia woga wafanyabiashara wanakwenda kutoa rushwa badala ya kuingizia mapato Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wanatumia msemommoja wanasema wewe hujui kama ni Serikali ya Awamu ya Tano ya Magufuli hii, ni hapa kazi tu, hakuna namna yoyote utatoa na usipotoa tunakufilisi. Ndicho wanachowaambia wafanyabiashara, imefika mahala wafanyabiashara wameamua kusema sasa ngoja na sisi tuache. Wengine wanafunga biashara wanaona afadhali waende maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nirudi kwenye vitabu vya bajeti vya Waziri. Nakumbuka kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 fedha iliyokuwa imetengwa kwenye viwanda ilikuwa shilingi bilioni 45 lakini fedha iliyokwenda kwenye viwanda kutekeleza majukumu ya maendeleo ni shilingi bilioni 6.7 ambayo ni sawa na asilimia 8 ya bajeti yote. Hii inaonyesha ni jinsi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi inazungumza ndani ya Bunge lakini haijajiandaa kutengeneza viwanda na kuleta viwanda katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ni jinsi gani ambavyo utekelezaji wa bajeti umeendelea kuwa chini mwaka hadi mwaka na hatujui tatizo ni nini. Leo mnasema viwanda, viwanda haviji kwa maneno, viwanda haviji kama alivyokuja Mwijage na Kitabu kikubwa hapa. Viwanda vinakuja kwa kutenga fedha na fedha hizo kuzipeleka katika

maeneo husika ili zikafanye kazi. Kwa hiyo, yote haya ni lazima yaeleweke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya 2017/2018 walikuwa wamepangilia kukusanya shilingi bilioni 28 kwenye Wizara lakini wamekusanya shilingi bilioni 6.6 peke yake. Hii inaonyesha hata uwezo wa kukusanya mapato kwenye Wizara yenyewe imekuwa ni chini kabisa. Yote haya yanafanyika kwa sababu ya kutokuwa na maandalizi ambayo yako sawasawa.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakajoka. Tunaendelea na Mheshimiwa Gimbi Masaba na Mheshimiwa Sabreena Sungura kwa dakika tano tano.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na nimpe hongera kwa kuongeza CV ya siasa katika Taifa hili. Tunamwambia karibu tuendelee na kulijenga Taifa hili, mapambano yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi ya kuzungumza kutokana na kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, yapo mengi nayofahamu na Waziri wa Viwanda anafahamu nini ambacho nimekuwa nikikidai katika Kamati hiyo. Kwa leo



nataka nibebe angalau hoja moja au mbili kutokana na muda na naomba nizungumzie kuhusu uhaba wa sukari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitaji la sukari kwa mwaka ni tani 440,000, uwezo wa viwanda vyetu ni kuzalisha tani 3,000 pekee. Hivi navyozungumza bei ya sukari kwa mfuko wa kilo 50 ni Sh.110,000 lakini kila mwaka tunakuwa na upungufu wa sukari karibia tani 140,000 sawa na asilimia 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa vibali kwa ajili ya kuagiza sukari kwa wafanyabiashara kwa lengo la kukidhi mahitaji ya Taifa letu au kwa maana nyingine kwa walaji. Nikizungumzia suala la bei ya Brazil, sukari kwa bei ya Brazil ni sawa na dola 3,090 sawa na Sh.860,000 na hiyo ni pamoja na kodi asilimia 25 na VAT asilimia 18. Kwa bei hii sukari ilipaswa kuuzwa Sh.65,000 na siyo Sh.110,000 au ingeweza kuuzwa Sh.80,000 maana wao kule wananunua kilo 50 Sh.65,000 maana yake wangeweza kuuza hapa Sh.80,000 na isiwe Sh.110,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa masikitiko kwa sababu kila kukicha tunaisikia Serikali inasema ni Serikali ya wanyonge. Kama Serikali ni ya wanyonge ni kwa nini Serikali inawauzia wananchi sukari kwa bei ya juu kiasi hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ina maana ukigawanya hapa ni kama wanauza kwa kilo Sh.3,000. Kama Serikali ni ya wanyonge, kwa nini basi Watanzania wasipate sukari kwa Sh.1,500 kwa kilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa vibali watu waagize sukari kwa lengo la kuleta ushindani wa soko. Cha kushangaza ni kwamba sukari ile ile ya ndani na nje inauzwa bei moja. Sukari kwa bei ya ndani inauzwa Sh.110,000 na sukari ya nje inauzwa bei ileile. Sasa najiuliza, ni kwa nini Serikali ilitoa vibali kwa walewale wenye viwanda badala ya wafanyabiashara wengine ili kuleta ushindani wa soko na kuleta tija kwa walaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja anipe majibu, kwa nini Serikali haikutoa vibali kwa wafanyabiashara wengine na ni kwa nini imetoa kwa wafanyabiashara walewale ambao sisi tunasema sukari ambayo wanazalisha wao haikidhi na ndiyo maana Serikali iliamua kutoa vibali ili tukidhi hitaji la Watanzania? Kwa hiyo, naomba majibu atakapokuja Mheshimiwa Waziri wa Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili, nataka nizingumzie suala la uhaba wa...

*(Hapa kengele ilitika kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Gimbi, muda wako wa dakika tano umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Sabreena Sungura, dakika tano na baadaye Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimewahi kuhoji kwenye Bunge hili kwamba ni nani kati yetu atapewa mtaji wa shilingi milioni 250 a-raise mpaka shilingi bilioni 2 ndani ya miaka mitano? Hoja yangu ni kwamba mabenki mengi yamefungiwa baada ya kukosa vigezo vya kutimiza mtaji wa shilingi bilioni 2. Athari yake ni nini kwa uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi walikuwa wamewekeza pesa kwenye mabenki hayo na wakati wakisubiri *process za insolvency* maana yake watachukua muda mrefu sana ili waweze kuletewa fedha zao. Waliahidiwa kwamba kwa awali watalipwa Sh.1,500,000 kila mmoja halafu watasubiri *process* ya mfilisi mpaka itakapofikia mwishoni ndiyo waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi iweze kuhakikisha kwamba inashusha riba ili watu wetu waweze kuwa na uwezo wa kurudisha mikopo katika mabenki yetu. Ukiangalia ripoti ya

CAG inaonesha mikopo isiyolipika ilipanda kutoka shilingi bilioni 9.1 mpaka shilingi bilioni 2.5. Watu wengi kushindwa kulipa mikopo kwa sababu mbalimbali. Wapo ambao wanashindwa kulipa mikopo kwa sababu kodi za *TRA* zimezidi lakini wapo ambao wanashindwa kulipa mikopo kwa sababu sekta ya biashara na uchumi imezidi kudorora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka napenda nizungumzie *Special Economic Zone*. Kuna suala zima la fidia ambalo limezungumziwa katika Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia hata kwenye sheria zetu, mfano Sheria ya *Land Acquisition Act, section 15* inaelezea kwamba maeneo ambayo yamefanyiwa tathmini kwa ajili ya kulipwa fidia ya *Special Economic Zone (SEZ)* na *Export Processing Zone (EPZ)* yaweze kulipwa takriban shilingi bilioni 60 kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi fidia zile zimefikia shilingi bilioni 190. Hiyo ni kwa sababu kila mwaka kwa mtu ambaye alithaminiwa na alitakiwa alipwe fidia ukipita mwaka mmoja kuna 6% kama nyongeza ambayo anatakiwa aongezewe. Kwa hiyo, kwa wananchi wote wa maeneo ya Tanga, Bagamoyo, Kigoma, Kigamboni kwa maana ya Kurasini (*Tanzania-China Logistic Center*), Mara, Ruvuma na maeneo mengine yote, fidia imeongezeka kwa kiwango kikubwa kwa sababu Serikali imeshindwa kulipa fidia kwa wakati na hivyo kuliingizia Taifa hasara na mzigo mkubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka napenda kuitaka Wizara iwasaidie wawekezaji wetu kutoka nje. Kuna *Tanzania Diaspora*, tumeona hapa wenzetu Wachina na India, juzi hapa wallitishwa Wahindi wote waliopo duniani warudi India kwa ajili ya kwenda kufanya uwekezaji ambao utakaokuwa na tija. Wahindi waliopo Tanzania na wengine walitoka kwenye Bunge letu hili walienda India kuwekeza. Kwa nini *Diaspora* wetu ambao wapo nje ya nchi wenye uwezo mzuri, ambao wangeweza kuchangia uchumi wa nchi

hii, hawawi *included* katika kuendeleza uchumi wa nchi hii?  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne iliweka *Desk la Diaspora* pale na walikuwa wameshaanza *process* hizi lakini mpaka sasa bado kimya. Ukiangalia katika Katiba pendekezwa ya Ndugu Warioba, Ibara ya 72, iliweka kipengele kwamba Watanzania ambao walibadlil uraia kwa ajili ya kutafuta maisha wapewe *special priority* au hadhi maalum ili waweze kutambulika katika uchumi wa nchi yetu, waweze kumiliki ardhi, kuwekeza katika hisa na waweze kumiliki mali katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba tuweke *desk* maalum kwa ajili ya *Diaspora* ili waweze kujiunga vikundi kwa vikundi, waweze kuwekeza kwenye sekta za maji, kilimo, viwanda na kadhalika kwa sababu kuna Watanzania wenye fedha na wenye uwezo mzuri katika nchi za Arabuni, America na Ulaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni kabisa napenda nimalizie kwa kuzungumzia hali ya uchumi katika Mkoa wa Kigoma. Ukitaka kuhakikisha kwamba hali ya uchumi imekuwa mbaya, mwaka uliopita Mkoa wa Kigoma takriban miezi sita au mpaka saba wafanyakazi na wafanyabiashara wa maduka mbalimbali katika Mji wa Kigoma waligoma kufungua maduka kwa sababu walipandikiziwa tozo kutoka Sh.15,000 mpaka Sh.50,000 na Chama cha *ACT* Wazalendo. Hiyo inaonesha kabisa kwamba uchumi unayumba ndiyo maana watu waliamua kufunga maduka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Chama cha *ACT* Wazalendo walilikoroga akaja Ndugu Polepole akalinywa, alipoingia pale aliambia wananchi wanatakiwa wafungue maduka na kodi ile inashushwa. Kupandisha kodi ni mchakato wa sheria na ulifanywa kwa mujibu wa sheria na Baraza la Madiwani ndiyo lililopandisha na ikaenda Mkoani, TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri akaweka saini ikashuka, inakuwaje anakuja Mwenezi na kukataza kodi ile isilipwe?  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sabreena. Tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge na baadaye Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kabla sijachangia, naomba nimtangulize Mungu mbele kwa kumshukuru sana kwa kunipa afya na hekima. Kwa kuwa natambua kwamba maandiko yanasema katika mambo yote tutangulize dua na sala na Bunge lako huwa tunaanza na dua na sala na mahali popote unapomtaja Mungu tunasema lazima umtaje katika roho na kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mbunge unapotoa mchango wako ni lazima umtangulize Mungu ili akupe hekima uweze kuchangia vitu ambavyo vitatupeleka mbele. Kwa hiyo, naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa namna walivyoleta hoja hii. Hoja imeandikwa vizuri sana, inatoa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuamua kwamba ili tuweze kufikia uchumi wa kati lazima tuweke nguvu yote kwenye uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, ni jambo moja zuri, lazima tumuunge sana mkono Rais wetu ili tufikie azma hiyo ya uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme tu kwamba katika viwanda ambavyo tunavizungumza, kweli vipo vingi; nimejaribu kuangalia karibu nusu ya kitabu ina orodha ya viwanda lakini unaweza ukaona uhalisia wa uchumi wa viwanda na uchumi wa kipato cha mtu mmoja mmoja. Tanzania wananchi walio wengi ni wakulima na tunaweza tukawasogeza mbele kama tutawekeza viwanda ambavyo vitasaidia sana wao kuuza mazao yao ili waweze kuwaongeza kipato walichonacho. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Mwijage katika orodha kubwa aliyokuwa nayo

hapa, ajaribu kuangalia na kuweza kulea viwanda vile ambavyo vinasaidia sana wakulima wetu kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Wanging'ombe asilimia 90 ni wakulima wa mahindi na viazi mviringo. Wakulima hawa hawana soko la kuuza mazao haya ya viazi. Katika viazi kuna tatizo sana la vipimo. Kuna Wakala wa Vipimo, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wanasema wanashughulikia namna ya kusimamia vifungashio. Wakati wa mwanzo walikuwa na vifungashio vikubwa ambavyo wanajaza vile viroba vikubwa vya lumbesa ambapo ukipima kwenye kilo ni zaidi ya kilo 100 ambayo ipo kwenye sheria. Hata hivyo, usimamizi wake ni mgumu sana kwa sababu wafanyabiashara wanatanguliza mawakala ambao wanakwenda kuwarubuni wakulima kule mashambani. Naomba hii Wakala itafute mbinu za kusimamia jambo hili, kusiwepo na kurubuni wakulima katika kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchezo mwingine ambao wanafanya wanasema wewe Wanging'ombe usipouza viazi wanakwenda kununua Mporoto au Arusha ambapo wanaweza kuuza kwa vipimo hivi vya lumbesa. Nafikiri kwa sababu huu Wakala upo basi uwajibike ili wakulima wetu wauze viazi kwa kilo siyo kwa vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wameleta viroba vidogo ambavyo vinaweza kujaza debe tano. Sasa ili gunia litimie unajaza viroba viwili na lumbesa yake. Kwa hiyo, unakuta kwa wastani kunakuwa na debe kumi ambazo wanasema hizi sasa ndiyo kilo 100 kwa vipimo. Kwa hiyo, tukiweza kwenda kwa kipimo cha kilo, tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingine ambavyo nafikiri navyo tungevivanyia kazi ni viwanda vya mazao ya pamba, korosho, chai, kahawa, pareto, mahindi, mpunga na alizeti. Kwenye Jimbo langu tuna viwanda viwili; kimoja kinazalisha sembe, kinaitwa *Mbomole Investment Company*. Kile kiwanda hakizalishi kwa kiwango kikubwa kwa sababu

tu TANESCO wameshindwa kutoa *transformerya* KVA 200 kwa zaidi ya mwaka mmoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda kingine kimewekezwa pale cha kukamua mafuta ya alizeti kinaitwa *Wende Investment Company*. Hiki nacho kimeisha mwaka mzima lakini TANESCO wameshindwa kutoa *transformer* ya KVA 200. Sasa inawezekana mifano ya namna hii iko maeneo mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri kama anavyokimbia hivi, nilifikiri ni vizuri viwanda hivi ambavyo vimeshaanzishwa visaidiwe. Wananchi wetu tumewahasisha wananchi wetu walime sana alizeti kwa sababu kiwanda kipo, najua watapata mahali pa kuuza lakini kama kinakuwa *white elephant* kwa sababu ya *transformer* tu, basi Serikali ni moja, uweze kuona namna ya kuwasiliana na Mheshimiwa Dkt. Kalemani tupate *transformer*, wananchi wangu wapate mahali pa kuuza hiyo alizeti na *transformer* nyingine kwa ajili ya wananchi wangu kuuza mahindi ili waweze kuinua kipato chao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzaji wa mahindi imeoneka ni ngumu sana kwa sababu kipindi fulani Serikali ilikuwa imefunga mipaka lakini nashukuru sasa mmefungua. Hata hivyo, kuna urasimu sana katika kuuza mahindi nje ya nchi au maeneo mengine. Tuwasaidie kwa viwanda hivi ambavyo vinaanza kuibuka kwa kuwezesha mambo kama ya umeme na vitu vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nichangie pia suala la kuinua uchumi. Nchi nyingi ambazo zimeendelea zilianza na viwanda vinavyohusiana na chuma. Tanzania tumezungumza habari ya Liganga na Mchuchuma kwa karne, kuanzia awamu ya kwanza ya Serikali zetu hizi lakini hakuna kinachoendelea. Unajua ukisema umtegemee Mchina, naye anataka kuinua uchumi wa nchi yake hataweza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka uamuzi wa Rais uje kama wa *Stiegler's Gorge* kwamba sasa tunaamua kujenga *Stiegler's Gorge*, basi tuamue na kujenga Mchuchuma kwa namna yoyote inavyowezekana. Nina uhakika tutakuwa hatulii umaskini kwamba hatuna maji na vitu vingine, tunaweza kujitegemea wenyewe kama tulivyoanza kujenga reli. Nilifikiri kwamba nishauri na ndiyo maana naunga mkono hoja hii ili unisikie vizuri na ukalifanyie kazi kusudi Tanzania kwell ifike azma ya kuwa na uchumi wa kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambalo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba hapa Dodoma kuna mwekezaji mmoja alianzisha kiwanda cha kutengeneza hizi *ceiling boards* kwa kutumia *gypsum* na malighafi yake inatoka Dodoma hapa hapa, kipo hapo Kizota na Mheshimiwa Waziri nilishawahi kumwambia. Mwekezaji yule ameshindwa kukiendeleza kile kiwanda kwa sababu ya ushindani wa soko. Tatizo lipo kwa wafanyabiashara ambao wanaleta *semi-finished goods*, wanasema hii ni *gypsum* ghafi lakini kumbe ni *finished goods* ambazo sasa wao hawalipii kodi. Sasa hiki kiwanda kimefungwa na huyu mtu ameamua kuondoka. Aliwekeza fedha na wananchi wa Dodoma walikuwa wamepata ajira na Serikali inakosa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili ili kusudi mwekezaji yule akifungue hiki kiwanda cha Dodoma na kama kuna kodi ambazo zipo kwa mujibu sheria, basi yeye anasema hana tatizo kulipa kodi, lakini kwa nini watu wengine wanasamehewa kodi kwa *finished products*, wanadanganya kwamba wanaleta malighafi ya *gypsum*? Tutakuwa tumeendeleza sana Mkoa wetu wa Dodoma ambao sasa ni makao mapya ya Serikali. Kwa hiyo, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri walifanyie kazi jambo hili kiwanda kile kifufuliwe ili kiweze kuleta ajira kwa wananchi wetu na Serikali pia itapata kodi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, nashukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)



**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Lwenge. Tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Mгимwa baadaye Mheshimiwa Deogratias Ngalawa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Naendelea kumpongeza sana kwa sababu mwaka 2011/2012 na 2012/2013 Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda. Kwa hiyo, yupo kwenye nafasi sahihi kabisa. Miongoni mwa hoja nyingi ambazo zimezungumziwa hapa, *Engineer* anazifahamu. Kwa hiyo, atakuwa kwenye nafasi nzuri sana kumwelekeza Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni Mchuchuma na Liganga. Mwaka 2012 pale *Mlimani City*, Dkt. Cyril Chami akiwa Waziri, Tanzania kupitia *NDC* tulisaini mkataba wa Liganga na Mchuchuma, mimi nikiwepo na Naibu Waziri alikuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninapozungumza ni takriban miaka sita. Mambo yote ya msingi kwenye mkataba ule tulikubaliana na naamini kwa kiasi kikubwa yametokelezwa. Inasikitisha sana miaka sita imeshapita toka sasa hakuna kitu chochote kilichofanyika kwenye Mchuchuma na Liganga. Kama kweli tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda, miongoni mwa maeneo ambayo tutatakiwa tuyaenzi kwa nguvu zetu kubwa ni eneo la Mchuchuma na Liganga ambapo malighafi za uhakika za umeme na chuma zinapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makaa ya mawe ya Mchuchuma na makaa ya mawe ya Ngaka yanaweza kuzalisha umeme wa *megawatt* 120. Tulikuwa tuna tatizo kubwa la *transmission line*, lakini kwa bahati nzuri tumepata hela kwa wafadhili na *transmission line* ile inajengwa. Kwa

hiyo, umeme umeshapatikana, sasa kigugumizi kinatoka wapi cha kutoanzisha mradi wa Mchuchuma? Naamini kabisa Mheshimiwa Waziri akija hapa atatuambia ni sababu zipi zinapelekea leo mpaka miaka sita imefika hatujafanya chochote kwenye mradi mkubwa huu wa Liganga? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tano, tumejielekeza kwenye uchumi wa viwanda. Tunapotaka kuzungumzia habari ya viwanda kuna baadhi ya mambo tunatakiwa tuyaangalie kwa karibu zaidi. Malighafi kubwa ambayo inatakiwa ipatikane kwenye eneo hili inatakiwa itoke kwenye kilimo. Tumejipanga vipi ku-*invest* kwenye kilimo kusudi tuwe na uhakika wa kupata *raw materials* za kutosha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda unakwenda *simultaneously* na uchumi wa kilimo. Tunaweza tukajenga viwanda vikubwa hapa nchini lakini kama malighafi hakuna, tutakuwa tuna hadithi, tutakuwa na viwanda ambavyo haviwezi kufanya uzalishaji. Kwa hiyo, tujiangalie, tunapotaka kujenga viwanda, tujiulize, hiyo malighafi inatoka wapi? Kwa hiyo, nashauri, tunapojiangalia kwenye uchumi wa viwanda, tujiangalie na namna ya kuandaa malighafi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kulichangia na kumwomba Mheshimiwa Waziri aje kuniambia ni suala la *Kurasini Logistic Center*. Tumelipa fidia zaidi ya shilingi bilioni 90 kwenye *Kurasini Logistic Center* na tulisaini mkataba wa mwaka 2013 na Wachina kwa ajili ya kujenga *logistic* ile lakini leo ni miaka mitano hatujafanya chochote na shilingi bilioni 90 imeshakwenda pale. Kwa hiyo, tusije kuwa tuna matumizi ambayo siyo sahihi. Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja, aje atueleze kwa nini mpaka leo *logistic center* haijaanza? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwa kazi na juhudi kubwa anayoifanya katika eneo lake, lakini pamoja na kazi kubwa anayoifanya, tunatakiwa sisi kama Tanzania tujipange namna

ya kuvi-*protect* viwanda vyetu vya ndani. Kwa mfano, tuna viwanda vikubwa tu vya maziwa hapa nchini na maziwa mengi tunayotumia hapa nchini yanakuwa-*imported* kutoka nje, matokeo yake tunashindwa kuvisaidia viwanda vya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye taasisi nyingi za Serikali utakuta maziwa yanayotumika ni ya nchi za nje. Ukiuliza sababu zipi zimesababisha kutumia hizo *Lactogen* na maziwa mengine kutoka nchi za nje, hupati majibu. Kwa hiyo, kama tulivyofanya kuzuia *importation* ya *furniture* za nje, ifike wakati na Serikali izuie *importation* ya maziwa kutoka nchi za nje. Sisi kama Watanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na ng'ombe wengi katika Afrika. Kwa hiyo, tutumie utamaduni huo na rasilimali tuliyonayo kuhakikisha tunafanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pamba huwa linaajiri watu wengi sana. Ukienda Cambodia pamoja na kwamba hawalimi pamba lakini watu wengi wameajiriwa katika *industry* ya *textile*. Kwa hiyo, ifike wakati sasa tuanzishe viwanda vingi hapa nchini vya nguo, naamini vitaajiri watu wengi kuliko kujielekeza kwenye kuuza rasilimali yetu ya pamba tutakuwa hatuitendei haki. Tuko tayari kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa kuhakikisha *raw material* zinazopatikana kwenye maeneo ya pamba, nyingi zinatumika ndani ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo wenzetu wa viwanda wamefanya vizuri sana. Kwa mfano, eneo la *BRELA* (Msajili wa Makampuni), siku za nyuma palikuwa na shida sana, lakini sasa hivi wamefanya vizuri sana. Usajili unafanyikia *online* na unafanyika kwa kipindi kifupi. Kwa namna ya kipekee, tumpongeze Mheshimiwa Waziri na Mtendaji Mkuu wa *BRELA* kwa kazi nzuri anayoifanya katika maeneo yake. Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, kama anafanya vizuri, naomba tumpongeze sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mahmoud Mгимwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza kwa kunipa fursa ya kuweza kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa napenda tu kuzungumzia suala la Mchuchuma na Liganga. Suala hili limekuwa likizungumzwa muda mrefu sana. Huu mfupa umekuwa mkubwa na mgumu. Liganga na Mchuchuma imeanza kuzungumzwa toka mwaka 1929 kipindi cha Mkoloni. Mkoloni alishindwa na hizi Serikali nyingine zote zimekuwa zinaweka mipango lakini ni mipango ambayo kwa kweli haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kitu kinachoitwa mradi ni lazima uwe na mwanzo na mwisho. Lazima kuwepo na *activities* au *programs* za kuhakikisha kwamba tunaanza hivi, tunapita hapa mpaka mwisho wa safari inakuwaje. Kitu kinachoshangaza katika Mradi wa Liganga na Mchuchuma ni kwamba hatuoni ile mipango ambayo inawekwa, kwamba sasa Liganga na Mchuchuma imewekwa kwenye Programu ya Miaka Mitano ya Serikali; Liganga na Mchuchuma imezungumzwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi; Liganga na Mchuchuma inawekwa kwenye kila bajeti ya mwaka ambazo tunazipitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ule Mpango wa Miaka Mitano sasa tunaingia mwaka wa tatu lakini bado hatujaona Liganga na Mchuchuma hasa ina tatizo gani. Tuliambiwa kwamba tatizo ni *incentives*, tunajaribu kujiuliza hizi *incentives* Serikali inashindwa kuchukua hatua ili tuweze kuona namna gani tunazi-*accommodate* na baada ya hapo hii miradi iweze kuanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia kitabu cha bajeti, nimeona Liganga imewekewa shilingi bilioni 5 na Mchuchuma imewekewa shilingi bilioni 5, lakini sasa haifafanui *activity* ya hizi shilingi bilioni 5 zilizowekwa kwenye Liganga na Mchuchuma ni kwa ajili ya nini hasa? Kwa hiyo, naamini kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake basi atatuzeleza hizi shilingi bilioni 5 ni kwa ajili ya nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya fidia pale, mpaka leo imekuwa ni kizungumkuti. Alipita Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 26 Januari, 2017, tulilizungumzia kwa kiasi kikubwa suala la fidia na ikaonekana kama fidia imekuwa *exaggerated* na ikasemekana kwamba itaweza kuundwa Tume au tukafanya *review* ya ile fidia ili wale watu waliopisha ile miradi iweze kufanyika pale walipwe kwa sababu sasa hivi wala hawajui nini cha kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *incentives* kule tunaona kuna suala la *Power Purchase Agreement*. Mara ya kwanza ilikuwa ungetumia ule mfumo wa *Build, Own and Transfer* lakini baadaye kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2017, wakaja tena na mfumo ule mwingine kwa maana ya kubadilisha kwamba itakuwa ni *Build, Own and Transfer*. Sasa hatujajua ni *incentives* zipi ambazo zinasababisha ule mradi usianze? Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri atakapokuja basi atatuambia wamefikia wapi. Hizo *incentives* ambazo zinasemwa kwamba zinashindikana kufanya ule mradi uanze ni zipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwamba kuna miundombinu wezeshi ambayo inafanya sasa ule mradi unaweza ukaanza, lakini pia inahitaji maamuzi magumu. Naona upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ambazo zinakwenda kwenye ile miradi, kwa maana kuna barabara inayotoka Mchuchuma kwenda Liganga na pia kuna barabara ambayo inatoka Mkiu kupitia Liganga kwenda Madaba. Naona zoezi lile linakwenda vizuri na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina safari hii utaisha mwezi Oktoba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona umeme wa Gridi ya Taifa ambao vilevile utashushwa pale eneo la Liganga na pia moja kwa moja utaelekea kule Mchuchuma. Jitihada hizi za Serikali tunazona, miundombinu wezesi hii ya Serikali tunaiona. Napenda kuiomba Serikali, suala la fidia basi mwaka huu iwe mwisho. Wale watu wamesubiri kwa muda mrefu, tuondokane nalo hilo. Kama itashindikana mwekezaji kulipa basi Serikali ichukue jukumu hilo na kuhakikisha kwamba hii adha ya fidia kwa wananchi wetu wa Mkomang'ombe na kule Mundindi inaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchuchuma na Liganga tumekuwa tukiongelea muda mrefu sana. Mimi na watangulizi wangu wote nane wamekuwa wakiongelea Mchuchuma na Liganga katika Bunge lako hili. Mwaka 2017 zaidi ya asilimia 80 ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiongelea Mchuchuma na Liganga. Tukijaribu kuangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mchuchuma na Liganga haijapewa ile *weight* yake yaani ni maneno ya mistari 11 tu, basi Liganga na Mchuchuma imeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe tunasema kwamba Liganga na Mchuchuma ni miradi kielelezo. Miradi kielelezo ya nchi sikutegemea kwamba ingeweza kupewa *weight* ndogo kiasi hiki. Tungeweka *weight* kubwa na tujue tatizo ni nini? Angedadavua kiasi cha kutosha ili Waheshimiwa Wabunge tujengewe uelewa ili mwisho wa siku tuweze kuishauri Serikali vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nanukuu maelezo ya Mheshimiwa Waziri ya masuala ya viwanda mama na miradi kielelezo ya nchi, Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Anasema, katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga, Serikali iliunda Timu ya Wataalam wa Serikali ikiwa na jukumu la kuchambua vivutio vilivyooombwa na wawekezaji. Vilevile uchambuzi ulifanyika kwa kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Madini, 2010; Sheria ya *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act, 2017*; na *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms), 2017*

na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na Serikali. Timu hiyo imekamilisha taarifa ya awali ambayo inasubiri kutolewa maamuzi na mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya ni ya kila siku na kwenye kila bajeti huwa yanakuja haya haya, kwamba tunaendelea na mchakato. Sasa ifike wakati Serikali ije na maamuzi magumu kuhusu mradi huu. Kwa hiyo, bado Taifa linasimama na naamini kwamba unapozungumzia viwanda ndani ya nchi hii, unazungumzia Liganga na Mchuchuma kwa sababu *multiplier effect* yake inaenda mbali. Kwa hiyo, ifike mahali sasa tuchukue maamuzi magumu. Nami naamini kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ina uwezo wa kuchukua maamuzi magumu na kuhakikisha kwamba miradi hii ina-*take-off*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye upande wa biashara, mimi huwa najiuliza, tunawajua wafanyabiashara wetu? Tunayo *database* ya wafanyabiashara wetu? Kwa sababu tunaweza tukawa tunazungumza biashara na inaweza ikaleta *impact* gani wakati hatuwafahamu wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlivyo-*categorize*, kuna wafanyabiashara wa kati, wadogo na wakubwa. Je, tunayo hiyo *database* ya hao watu kiasi ambacho tunaweza tukawa na uhakika kabisa kwamba tunapozungumzia suala la biashara *impact* yake ni hii na *revenue* tutakayoipata kwa wafanyabiashara ni hii hapa ili mwisho wa siku sasa tutengeneze *platform* kwenye kila maeneo, tunaweza tukaweka semina kwa wafanyabiashara wa kati, wadogo na wakubwa. *Otherwise* tutatakuwa tunatwanga maji kwenye kinu kama hatuwajui wafanyabiashara wetu ni nani na tunatarajia nini kutoka kwao na *impact* kwa wananchi wetu kiuchumi kuanzia mtu mmojammoja, vikundi na mpaka Taifa inakuaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ifike mahali sasa hawa Maafisa Biashara wetu kwenye Halmashauri, kwenye mikoa, ni lazima watengeneze *database* za wafanyabiashara

wetu. Kwa sababu *database* hiyo inaweza ikatumika kama *role model* kwa watu ambao wanataka kuingia kwenye biashara ili waweze kujua kwenye biashara *playground* yao ikoje? *Sometimes* tukiwa na *role models* wana uwezo wa kushawishi watu wengine kuja kuingia kwenye mfumo wa kibiashara. Tusipotengeneza semina hizi wezeshi hatutaweza...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Lulida na baadaye Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nami kuchangia katika hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mahali Waheshimiwa Wabunge wanaliongelea eneo hilo basi Serikali ilifanyie kazi. Waheshimiwa Wabunge wengi wanaongelea *TRA*. Sasa hivi *TRA* ni eneo ambalo haliko rafiki na wafanyabiashara wadogo wadogo. Wameweka urasimu wa makusudi, siwezi nikasema ni wote, lakini maeneo mengi ya *TRA* sasa hivi ni eneo ambalo linawakwamisha wafanyabiashara wadogo wadogo, hivyo, siyo eneo rafiki kwao. Hili eneo litawakatisha tamaa wafanyabiashara hawa ili wasiweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosikia, unatakiwa kwanza wakutoze ushuru hata kazi hujafanya. Mama Ntilie anapika wali, hajajua kama anaweza akauza wali wake, umeshamwekea tayari, lipa shilingi milioni moja, anaipata



wapi? Huu ni unyanyasaji wa kibiashara kwa wazawa.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kwenda katika Tanzania ya viwanda. Tanzania ya viwanda inahitaji mazingira wezeshi kwa viwanda. Enzi za Mwalimu Nyerere alianzisha maeneo ya viwanda na maeneo yale aliweka mazingira mazuri ya maji, umeme na barabara. Kwa mfano, alianzisha viwanda 14 vya korosho, hili nalirudia tena karibu mara ya tatu, viwanda vile vilikuwa na umeme, maji na ajira ya kutosha. Vilevile walikuwa wana uwezo wa kupata malighafi ya korosho palepale katika mikoa inayozalisha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametaja mikoa yote ambayo imepewa kipaumbele cha viwanda; Lindi, Mtwara na Ruvuma sijaona hapa. Kwa maana moja, hata hivi viwanda vya korosho vilivyopo, mategemeo ya kuvifufua hayapo. Ni aibu kiasi gani korosho inalimwa Tanzania inanunuliwa inapelekwa India, wanakwenda ku-*process* tunaletewa korosho ile iliyobanguliwa kuja kula tena Tanzania. Huu siyo mfumo mzuri wa kibiashara. Tunavyo viwanda vya korosho Tanzania lakini unavikuta vinapeleka korosho nje ya nchi *as a raw material*. Huu ni uharibifu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda katika semina ya korosho, tunaambiwa Tanzania haionekani kabisa kama ni mzalishaji wa korosho, kwa vile tunaipeleka nje wale ndio wanaonekana wanazalisha na kusafirisha korosho. Je, tutapata lini ajira kama korosho yote tunaipeleka nje? Viwanda vyote vimefungwa. Cha kusikitisha zaidi, Mkoa wa Lindi hatuna kiwanda hata kimoja. Hivyo viwanda vya korosho vilivyokuwepo; vya Mtama na Lindi, vyote vimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama Mheshimiwa Waziri ameikutia tu hii *issue*, ni makosa makubwa yalifanyika ya ubinafsishwaji na uwezeshaji. Uwekezaji wa nchi hii haukuweka mazingira mazuri katika mikataba, haukuweka

mazingira mazuri kwa kujua nini tufanye katika kubinafsisha. Tumewabinafsishia watu, wamevifunga viwanda, watu walewale ndiyo wanapeleka korosho nje. Haiwezekani kabisa. Nataka utupe taarifa, ni nani wamechukua viwanda? Bado walewale waliochukua viwanda wanapeleka korosho nje, huu ni uhujumu wa uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na viwanda Tanzania ambavyo vinakamua mafuta. Mwanza tulikuwa tunapata Mafuta ya OKI, SUPA-GHEE, TanBond ya Tanzania ambayo hata Kenya walikuwa wanaipeleka, viwanda vile vyote vimefungwa, kwa nini vimefungwa na nani amevifunga? Kama ni mkataba, mkataba wake ulikuwa wa muda gani? Palikuwa na mikataba mibovu ambayo haikuwa na *timeframe*. Hivyo mtu amechukua kiwanda, amekifunga, anaagizia mafuta machafu kutoka nje wakati tunaweza kutengeneza mafuta masafi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni nini? Nafika mahali sielewi kama najielewa au pengine mimi niko nyuma ya wakati. Viwanda vya mafuta tunavyo. Nachingwea tulikuwa na viwanda vya mafuta, Mafuta Ilulu, ufuta wetu wote ulikuwa unakamuliwa Nachingwea. Leo ufuta wote wa Tanzania tunaupoleka nje, halafu hapa tunalalamika tuna uhaba wa mafuta wakati mafuta yetu mnapeleka mbegu nje, mnapeleka ajira nje na *raw material* inabakia kule na makapi yanatengeneza *feed cake* za wanyama. Huu ni uhuni wa kibiashara ambao umechezwa kwa muda mrefu, tunafanya biashara kwa mazoea, matokeo yake tunaiweka nchi katika *crisis*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila inapofika karibu na Ramadhani wafanyabiashara wanaanza uhuni wao; mara hakuna mafuta, sukari, hii ni *crisis* ya makusudi wanataka kupandisha bei ili wananchi wapate ghadhabu na Ramadhani. Mfanyabiashara kupata pepo ni ngumu sana. Wanaangalia ni eneo gani nitafanya fujo yangu halafu watu watahamasika ili angalau hili litakuwa ni chachu kwa wananchi kulalamika hakuna sukari na mafuta. Nina imani sukari ipo, mafuta yapo, yatafutwe na wananchi wapate

sukari na mafuta. Tumechoka kusikiliza uhuni wa kibiashara wa muda mrefu. Nchi haiendeshwi kwa uhuni wa kibiashara, nchi inaendeshwa kwa taratibu zilizopangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii alizeti inapelekwa nje, magazi kutoka Kigoma yanapelekwa nje, wanachuja wanatuletea tena, ooh, tuna mafuta yako nje yamenasanasa. Kwa nini mmefunga viwanda vyetu vya mafuta na mmevizia hamkamui mafuta, mnatuletea matatizo kibiashara? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kusema ubinafsishaji ndiyo donda ndugu la nchi hii. Tumefunga viwanda vyote. Tulikuwa na viwanda vya kusokota nyuzi. Kamati ya PIC tulikwenda Ubungo, eti hata nyuzi tunaagiza kutoka China. Tulikuwa na viwanda vya kusokota nyuzi Tanzania, pamba inatoka Mwanza na Shinyanga. Wenzetu, ndugu zetu, watani zangu Wasukuma wanalima pamba, ile pamba inabidi ipelekwe nje ikatengenezwe nyuzi tuletewe Tanzania wakati tulikuwa na viwanda vya nyuzi, tulikuwa na Kiwanda cha *Mwatex* na Kiwanda cha *Kilitex*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, yeye ni mbuzi wa kafara, haya mambo ameyakuta. Naomba timu nzima ya Mawaziri irudi ikakae ituambie viwanda hivi viko wapi, vinafanya nini? Tupate *database*, nani wamechukua na kwa nini wanatuletea *crisis* ya mambo ya viwanda? Haiwezekani kila siku tunachukua khanga mbovu kutoka nje, madira mbovu kutoka nje, wakati Tanzania tulikuwa tunatoa khanga nzuri; Kenya na Uganda soko kubwa lilikuwa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema sana lakini najjuliza, kulikoni Tanzania? Tumekuwa katika zigizaga, nenda mbele rudi nyuma, nenda mbele rudi nyuma. Viwanda hivi kwanza vingefanya kazi, basi hivyo vingine vingekuwa vya ziada kwa vile tayari ajira na uchumi ungekuwa mkubwa, lakini vile viwanda vikubwa vyote vimefungwa, kwa nini? Nani amevifunga, ni hao hao wafanyabiashara. Nataka utakapokuja kesho, uniorodheshee majina yote ya

waliochukua viwanda na mpaka leo wamevifungia. Kwa nini wamevifungia na kwa nini nguo hazitengenezwi Tanzania? Kwa nini nyuzi hatuosokoti Tanzania? Kwa nini korosho tunapeleka nje, tunaletewa tena zile zile hapa Tanzania? Kwa nini ufuta mnapeleka nje na tunakosa mafuta Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengine ya kusema, nataka jibu hilo kesho. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Tunaendelea na Mheshimiwa Salome Makamba baadaye Mheshimiwa Munira Mustafa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa najiuliza swali moja, hivi hii Serikali ya Awamu ya Tano ndiyo Tanzania ya Viwanda au ilikuwa ni Serikali ya Awamu ya Nne? Kwa sababu kinachofanyika sasa hivi, mwaka 2014/2015 katika bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzetu walikuwepo humu waliipitisha, asilimia 82 ya bajeti ilipelekwa kwenye viwanda na vikaboreshwa. Leo 2015/2016 bajeti ya shilingi bilioni 35.3 tumepeleka shilingi bilioni 1.6 sawa na asilimia 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hiyo, mwaka 2016/2017 tumepeleka 8% ya bajeti nzima. Mwaka 2018 mpaka Machi, taarifa tuliyopewa kwenye Kamati tumepeleka asilimia 9.4 tu yaani hakuna mwaka ambao tumepeleka angalau asilimia 50 ya bajeti ya viwanda halafu tunajinasibu kwamba tunaenda kwenye Serikali ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili swala linanipa wasiwasi na ndiyo maana ukiona mtu anajitetea sana, ujue kuna maovu nyuma yake. Ndiyo maana ukiangalia viongozi mbalimbali wa Serikali wana matamko tofauti tofauti juu ya ni viwanda vingapi vimeanzishwa Tanzania mpaka leo hii?

Mkuu wa nchi anasema tumeanzisha viwanda zaidi ya 3,060, Waziri kwenye hotuba yake anasema kwamba ameanzisha viwanda 1,287, kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wanasema viwanda viko 50. Kila mtu anaongea *statement* yake, Serikali moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima ujichanganye kwa sababu Watanzania tumewaaminisha tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda. Laiti kama Watanzania wangegundua kwamba viwanda wanavyoahidiwa kwenye kampeni ni vya kutengeza juisi, zile *blender*, ni viwanda vya cherehani, sijui kama leo tungekuwa tunaongea haya maneno. Leo tumebadilishiliwa *story* tunaambia kwamba viwanda ni aina yoyote, vya kati na vidogo. Sawa, basi hivyo viwanda vidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye ripoti ya *CAG, SIDO* wanaweza kutoa mikopo kwa asilimia 40 tu ya pesa ambazo walikuwa wame-*propose* kwamba wanatoa mikopo. Watu wanaoahidiwa watapewa mikopo kwa *SIDO* ndio hao wenye viwanda vya kati na viwanda vidogo lakini pesa hawapelekewi. Mheshimiwa Waziri anajitapa hapa ameanzisha viwanda vipya. Jamani, wengi hapa sisi ni wazazi. Hivi kweli mtoto wako hata kama una watoto wengi kiasi gani, mtoto wako mmoja akifa kwa kifo ambacho umesababisha wewe mwenyewe mzazi utajisikiaje? Viwanda vinakufa vidogo na vya kati, pesa hatupeleki halafu tunajinasibu kwamba tunatengeneza Serikali ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika bajeti ya mwaka 2018, hiyo 8% ninayosema imepeleka siyo fedha za ndani, ni fedha za wafadhili, fedha ambazo tunapewa na watu wengine. Uangalie *seriousness* ya Serikali katika kukuza uchumi wa viwanda, wewe mwenyewe utaona kuna changamoto kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, ili viwanda viweze kukua, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba lazima tukuze malighafi, lazima tuhakikishe tunaboresha pamba, tumbaku na barabara. Shinyanga ni

wakulima wakubwa wa pamba. Sisi mpaka sasa hivi tuna-*export* pamba tani 700,000. Yes, tunauza marobota 700,000 lakini tuna-*import* marobota ya nguo 2,000,000 kuleta Tanzania. Mbona tunafanya biashara kichaa? Kwa nini Serikali isiwekeze kwenye malighafi ili kukuza viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namweleza Mheshimiwa Waziri, hivyo viwanda anavyovitaja kwenye kitabu chake wanampigia makofi, anapiga nao picha, anatuma kwenye mitandao, hao watu wanamwangualia waone yeye ana *commitment* gani kukuza viwanda? Wale watu wamewekeza Tanzania lakini Waziri unathubutu kukaa na Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Kilimo kuangalia utarahisisha vipi uzalishaji kwenye hivi viwanda? Au tunafanya majaribio ya kusema tumeleta viwanda na baada ya miaka mitano viwanda vimeshindwa kufanya kazi au viwanda vyote vimefungwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi viwanda anavyotuaminisha leo Mheshimiwa Waziri, hebu jilulize swali, vinaajiri Watanzania wangapi? Juzi nimesikia Mheshimiwa Waziri anasema kwamba cherehani tano ni kiwanda. Mheshimiwa Waziri tusifanye mchezo na Watanzania, wanatutegemea sisi Wabunge na Serikali kuamua hatima ya maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwangu Kahama, Shinyanga na Mikoa ambayo kimsingi ilikuwa imekaa *strategic* kibiashara, nikikueleza tangu Serikali yenu imeingia madarakani, zaidi ya asilimia 70 ya wafanyabiashara waliokuwa wanamiliki maduka na biashara wameshapokonywa mali zao na Serikali. Watu wana mikopo Mheshimiwa Waziri. Wewe unachekelea kuleta viwanda vipya, una mkakati gani kuhakikisha viwanda ambavyo vilikuwepo ambavyo kimsingi vilikuwa vinalipa kodi na vinaendesha Serikali unavi-*maintain*? Una mkakati gani wa kuhakikisha hawa watu pamoja na kutusaidia kuendesha Serikali, wanaendelea kuwepo kwenye *circular* ya uchumi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nakaa namfikiria Mheshimiwa Waziri, sijui anaposema kwamba tuna viwanda 3,000 anakuwa ana-*project* nini? Kwa sababu kama mwisho wa siku Shinyanga pale kuna Kiwanda cha Nyama hakina uwezo wa kuajiri hata watu 2,000. Shinyanga leo maji na barabara ni changamoto, ng'ombe ndiyo kwanza mmekazana kupiga chapa mnakusanya ushuru wa Sh.5,000, umeme ndiyo kabisa, labda wanunue na *power bank* pale kwenye kile kiwanda, hali ni mbaya, lakini Mheshimiwa Waziri anajinasibu anasema viwanda vinaendelea, tunafanya vizuri, tunafanya vizuri wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *commitment* ya Serikali, tutafanyaje kuhakikisha wawekezaji wa kati na wadogo ambao ni wafanyabiashara kwa Tanzania hii na ndiyo walezi wa Tanzania hii, wanarudi kwenye hali yao ya kiuchumi kuweza kuendesha nchi hii? Nataka *commitment* ya Serikali juu ya huu utaratibu wenu, mtu akiamka asubuhi, *TRA* inapanga leo tunatoza kodi kiasi hiki, kesho asubuhi wanasema kiasi hiki, nini *commitment* ya Serikali? Watu wanafunga biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa leo, huyo huyo ambaye ni sehemu ya Serikali, anasema mnaofunga maduka, fungueni, njooni mezani tuzungumze, tunaweza tuka-*negotiate* bei ya kulipa kodi *TRA*.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Salome Makamba, kwa bahati njema amegusa sekta ya mifugo na amekitaja Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilitaarifu Bunge tu kwamba Kiwanda cha Shinyanga Serikali imeshachukua hatua, tena hatua nzuri sana. Kiwanda hicho kilikuwa kinamilikiwa na *Triple S* tumesharudisha na hivi sasa mchakato wa kuhakikisha kwamba kiwanda kinatangazwa ili kiweze kupata mbia wa kuhakikisha kwamba kinafanya kazi na kuleta tija katika sekta ya mifugo unaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nalotaka kumwambia ni kwamba hakuna ng'ombe aliyepigwa chapa kwa bei ya Sh.5,000 katika nchi hii. Mwongozo ni Sh.500 na *almost* nchi nzima ng'ombe wote wamepigwa chapa kwa Sh.500 kwa ajili ya kuleta tija katika sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome, taarifa hiyo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, halafu naomba kitu kimoja, tukiwa tunawashauri muwe mnatusikiliza kwa sababu Tanzania nzima haiwezi kuja hapa kuongea, sisi ni Wawakilishi wa wananchi. Tena kwa taarifa yako, kule kijijini njoo kwangu watu wanapiga chapa ng'ombe mpaka Sh.7,000 siyo Sh.5,000, ninyi mmekaa hapa sisi tunatoka kwa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu suala la kiwanda, mimi kwa uelewa wangu, kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania, anapokuja kuwekeza Tanzania anapewa kitu kina *tax incentive*. Akipewa *incentive*, maana yake kwa kipindi cha muda fulani yule mwekezaji hatalipa kodi mpaka ambapo ule muda wa *incentive* uwe umeisha. Kama hiyo haitoshi, kuna kitu kinaitwa *operational cost*, yule mwekezaji yuko pale hana miaka miwili, amekuwa anafanya *operation* pale na halipi kodi kwa sababu anasema *costs* zake za uzalishaji hazijalipwa. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali wanatujia hapa na mazingaombwe eti wanatafuta mbia mpya, *what about the incentive?* Vipi kuhusu ile *tax holiday* mliowapa wale wawekezaji? Jamani nyie si mnajisema kwamba ninyi ni Wataalam, ni wataalam wa nini basi? Tusifanye siasa kwenye maisha ya Watanzania. Siasa hizi zitakuja kutuadhibu, makaburi yetu yatapigwa fimbo na wajukuu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijifiche nyuma kwa kusema kwamba Serikali inatafuta mbia. Mheshimiwa Waziri hata *standard gauge* miujiza hii hii ilifanyika. Tumeacha mkopo wenye riba ya asilimia 1.2 tumeenda kuchukua mkopo wenye asilimia 4. Unakaa unasema umekaa na wataalam wanakokotoa mimi sijui mahesabu au biashara, lakini kwa uelewa wangu tu wa kawaida, siwezi kufanya biashara ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iwasaidie Watanzania, itengeneze miradi. Wakae pamoja, naamini Balaza la Mawaziri ni moja, wamsaidie Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara tutengeneze miundombinu kwa ajili kusafirisha malighafi na tuboreshe zao la pamba. Zaidi ya Watanzania milioni 16 wa *Lake Zone* wanalima pamba. Mheshimiwa Rais anasema hao ndiyo wapiga kura wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kilimo chetu tunategemea pamba. Hebu tuboreshe zao la pamba ili tuweze kufungua viwanda vya nguo na kufungua viwanda vya mafuta. Leo kelele za mafuta zisingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikitembea tu kidogo kilometa moja kutoka nyumbani, naona maua ya pamba yametanda kila mahali, leo tuko *busy* tunanunua ndege, tunajenga *flyover*, Tanzania siyo Dar es Salaam, Tanzania ina Mikoa zaidi ya ishirini na kitu. Tanzania siyo Dar es Salaam. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Munira Mustafa na Mheshimiwa Joseph Musukuma ajjandae. *(Makofi)*

**MHE. MUNIRA M. KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata nafasi kuchangia jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na timu yake yote, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kauli yake ya kusema sasa suala la mafuta ndani ya nchi yetu siyo tatizo. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuwa katika ufunguzi wa Kiwanda cha Singida alisema kuwa viwanda vya kuzalisha mafuta anaondoa VAT kwa asilimia 18. Naomba Serikali iniambie, imetekeleza vipi agizo hili la Mheshimiwa Rais kwa kuondoa VAT katika mafuta ya alizeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka tufikie katika uchumi wa viwanda basi la kwanza ni kuvilinda viwanda vyetu vya ndani. Siyo viwanda vya mafuta tu, hata viwanda vyetu vya maziwa, tunaiomba Serikali iweze kuangalia suala hili ya VAT ya asilimia 18. Tutapoondoa asilimia hii 18, kwanza tutaweza kuongeza uzalishaji ndani ya nchi yetu, tutaweza kupunguza kuagiza mafuta ndani ya nchi yetu, tutaweza kuwasaidia wakulima wetu kimaisha ndani ya nchi yetu, hata pia tutaweza kuondoa tatizo la wafugaji kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu SIDO. Katika taarifa ya CAG, SIDO inaonekana iko katika hali mbaya. SIDO inafanya vibaya ndani ya mikoa yetu na Tanzania kwa ujumla. Mwaka 2017/2018 imepangiwa shilingi bilioni 6 lakini ndani ya pesa hii haijapatikana hata asilimia 1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira nyingi za vijana zinapatikana katika viwanda vidogo vidogo. Kama tungeisaidia vizuri *SIDO* basi tungeweza kuzalisha ajira nyingi kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea *SIDO* ya Iringa ina wafanyakazi watatu tu ambao wameajiriwa na Serikali. Hivi tutafikiaje uchumi wa viwanda na tunawasaidiaje vijana? Naiomba Serikali iangalie namna ya kuajiri watumishi wa *SIDO* ndani ya mikoa yetu na wazisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ina wafanyakazi watatu, waliobakia wote wanajitolea mpaka Mnuuzi Mkuu na Mhasibu ndani ya *SIDO* wanajitolea, hizi kazi zinaendeshwaje? Naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri uko hapo, uisaidie *SIDO* ili kuweza kufikia katika uchumi wa viwanda. Kama hatuwezi kuzisaidia *SIDO* zetu, basi hatutaweza kusaidia uchumi wa viwanda. Ndani ya *SIDO* kuna mashine za miaka 70 kabla mimi sijazaliwa ndizo zinatumiwa mpaka leo. Naomba hizi pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya *SIDO*, zifike na zitolewe kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii *FCC* imekuwa tatizo sana kwa wafanyabiashara. Wamekaa kwa ajili kupiga *penalty* tu. Naiomba Serikali wangekaa na hizi taasisi wakawapa wafanyabiashara elimu. Wakienda sehemu za kuchukua bidhaa wajue ni bidhaa gani ambazo zinatakiwa ziingie ndani ya nchi yetu ili wasiwe wanachukua mzigo ambapo kisa tu haukuandikwa *Samsung* au haukuandikwa *iPhone* ukifika ndani ya Tanzania mzigo ule ikawa ni kuharibiana biashara kwa kuchomeana moto. Tungekaa tukafikiria, kuna wafanyabiashara mpaka wanaumwa, wengine wanakufa kwa sababu ya hii *FCC*. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri akae basi aangalie Watendaji wake aweze kuwasaidia wafanyabiashara wengi. Juzi kontena nzima ya chupi imechomwa moto na *FCC*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vimebinafishwa ambavyo vilikuwa haviwezi kufanya kazi.

Naiomba basi Serikali viwanda vile virudi katika mikono ya Serikali. Viko ambavyo havijabinafsishwa lakini vinamilikiwa na sekta binafsi na zipo *share* za Serikali. Naiomba basi Serikali ikaangalie viwanda hivi ili viweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niliuliza swali hapa kuhusu Kiwanda cha Nguo cha Urafiki lakini sikupata majibu ya kutosha na ndani ya kitabu cha Mheshimiwa Waziri sikuona maelezo yoyote kuhusu kiwanda hiki. Naomba basi wakati anahitimisha aniambie suala hili la Kiwanda cha Urafiki limefikia wapi kuhusu zile *shares* ambazo tunazo na wenzetu wa China? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kiwanda cha Nyama Dar es Salaam, naomba Mheshimiwa Waziri akiwa anahitimisha pia aje aniambie. Pia kuna Kiwanda cha ZK Mbeya, kilikuwa kinatengeneza vifaa vya kilimo. Naomba Mheshimiwa Waziri akija aniambie, kwa sababu mpaka sasa hivi wakulima wetu kutumia majembe ya mkono wakati sisi wenyewe tulikuwa tuna kiwanda kikubwa tu na hakifanyi kazi, itakuwa ni aibu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie kuhusu viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la vinywaji vikali ambapo Serikali inapoteza kodi nyingi. Vinywaji hivi vikali vinakosa kodi kwa kubandika *sticker* bandia na hili suala kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameliongea na ushahidi upo. Naomba basi Serikali iangalie inapoteza mapato kiasi gani katika suala hili la kubandika hizi *sticker* bandia katika vinywaji vikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vinywaji vikali Serikali ingekuwa ina-*charge* ile *spirit* wakati inaingia hapa nchini badala ya *spirit* ikiwa imeshatumika ndani ya vinywaji vikali ndiyo inakuja kuchajiwa. Hizi *spirit* zinapoingia tu nchini zichajiwe. Kwa sababu hizi *spirit* zinachajiwa kwa kiwango kidogo tu zinazokwenda kwenye hospitalini na sehemu nyingine lakini kiwango kikubwa kinatumika katika vinywaji vikali. Kwa hiyo, Serikali ingekaa ikaangalia vizuri kwa upande wa *spirit* inapoingia nchini. Tusi-*charge* ndani ya

vinywaji, bali tu-charge inapoingia tu ndani ya nchi yetu.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munira. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Chegeni baadaye Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa Mwijage na Naibu wake wanafanya kazi nzuri sana. Naomba tukiri hilo kwamba wanafanya kazi nzuri isipokuwa tu ni kwamba uwezeshwaji wa kufanya kazi ndiyo kuna matatizo. Hii nadhani sisi kama Bunge tufikie mahali tutafute namna ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mtambuka, ina mambo mengi sana. Bila kusaidiwa na kuwezeshwa kufanya kazi, itakuwa ni hadithi. Ndiyo maana anajita ni Mzee wa *Sound*, ni kweli anapiga *sound* tu, anazunguka huku na huku, anapiga *sound*. Nadhani tafsiri halisi ya Mheshimiwa Mwijage mimi ninavyofikiri ilikuwa ni kwamba kauli ya Watanzania katika uchumi wa viwanda iweze kushamiri. Mheshimiwa Mwijage, umefanya kazi nzuri, lakini bado kuna wingu kubwa sana la tafsiri ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali kama nchi tuweze kuwa na tafsiri pana na iliyo sahihi. Unaposema viwanda, cherehani tano ni kiwanda, kwa baadhi ya watu tunashindwa kukuelewa vizuri zaidi, kuna vitu vinaitwa *factory* na *industry*, sasa ni lazima kuwe na utofauti wa namna hiyo. Tukitofautisha hivyo, tukisema kwamba tumekuwa na viwanda 3,000 na kitu Watanzania wataelewa ni kitu gani. Nadhani tamaa kubwa ya Watanzania ni kuona kwamba

mnapozungumzia viwanda ni vya kati na vile vikubwa zaidi ili viweze kuchochea zaidi katika kuleta uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii pamoja na yote inayofanya, kuna vitu ambavyo ni lazima mvisimamie kwa uhakika zaidi. Ni namna gani ya kumsaidia mwananchi huyu na hasa mkulima maana zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima kuongeza thamani ya mazao yao, tukishafaulu pale hiyo ndiyo Tanzania ya viwanda tunayoitaka. Bila hivyo, itakuwa tunaongea kama ngonjera tu. Haiwezekani leo hii tunazidi ku-*import* vitu kutoka nje ambavyo tunaweza kuzalisha hapa nchini na tukapunguza kutumia fedha zetu za kigeni kununua bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu mkulima wa pamba. Mkulima wa Pamba ana mateso makubwa sana. Mwaka 2017 alilima pamba na akapata bei nzuri ya Sh.1,200 ikamhamasisha kulima zaidi mwaka huu, lakini utaratibu uliopo mwaka huu unamvunja moyo mkulima wa pamba. Ni vema kuangalia namna ya kuweza kumsaidia, vivyo hivyo hata kwa wakulima wa mazao mengine, tuangalie namna ya kuweza kufufua vinu vya kuchambua pamba ambavyo vitaongeza thamani ya mazao ya mkulima. Namna ya kuanza kuwa na viwanda vya kuweza ku-*process* bidhaa ya mkulima kama ni pamba, tuweze kupata nguo hapa nchini. Bila ya kufanya hivyo, haiwezekani na lazima tuwe na sera ya kulinda viwanda vyetu. Bila kulinda viwanda haitawezekana. Haiwezekani tunaacha soko letu, tunaingiza tu bidhaa kutoka nje bila kuangalia viwanda vya ndani. Bila ya kuwa na hiyo sera, hatutafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba sana Mheshimiwa Mwijage pamoja na Wizara yako, hili jambo mliangalie kwa makini, linamgusa Waziri wa Fedha. Lazima tuwe na sera za fedha na za kodi za makusudi kabisa za kulinda viwanda vya ndani. Kama ni kodi, basi tutoze kodi kubwa kwa bidhaa kutoka nje na tufanye *zero rating* kwa bidhaa za ndani. Tukifanya hivyo itasaidia kuchochea mkulima huyu aweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mkulima wa korosho amepata bei nzuri, wamehamasika zaidi na korosho inaendelea vizuri lakini mazao mengine yanaanguka. Mazao kama chai, kahawa, mbaazi na kadhalika, sina haja ya kuyarudia sana, lakini leo hii Tanzania miaka 57 ya uhuru bado tuna-*import* mafuta ya kula kutoka nje, hii ni aibu. Tufike mahali tuangalie namna gani nzuri zaidi ya kuwezesha kuzalisha bidhaa hapa hapa nchini ambazo zitasaidia kwa kiwango kikubwa kuweza kupata uzalishaji wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Wizara hii, Mheshimiwa Waziri acha tu kutembea mikoani, toka nje kaone, fanya *economic diplomacy*. Zunguka, tembea, unganisha nchi hii na mataifa mengine ili biashara ziweze kwenda. Haiwezekani kuna maonyesho mbalimbali ya kidunia, sijaona Waziri wa Viwanda na Biashara au Naibu wake nao wanafunga safari kwenda kuiunganisha Tanzania na dunia nyingine. Bila kufanya hivyo hatutakwenda tunapotaka. Mheshimiwa Waziri, wewe sio Waziri wa kwenda kijijini kwangu, kwenye kata, wewe Wizara yako ni muhimu sana. Tumwache Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI azunguke na kata na vijiji lakini wewe zunguka nje, tafutia Tanzania masoko na namna ya kuiunganisha kibiashara. Kama huwezi kushona suti, tukusaidie kutafuta suti nzuri uweze kuzunguka. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Mwijage kwa sababu anafahamu na upeo wake ni mkubwa sana na toka amekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, tunaona anavyohangaika, sasa hiyo *sound* ipige mpaka nje, isiishie hapa peke yake. Msaidie Mheshimiwa Rais, kila siku anazungumza, ninyi wasaidizi wake msipomsaidia itakuwa ni mbio ya mtu mmoja. Hawezi kupiga ngoma mwenyewe akacheza mwenyewe, lazima Mawaziri mumsaidie Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ifike mahali Watanzania sasa tumsaidie Mheshimiwa Rais zaidi. Kila wakati unaona anavyolia, anavyohangaika, ninyi mnasema kama

mlivyoagizwa, sasa mjiungeze zaidi ya hapo. Nami naomba sana kupitia hotuba hii ya bajeti, kwa kweli ningependa sana fungu la bajeti ya Wizara hii tuliongeze. Tufanye kila namna na Mheshimiwa Mpango najua wewe ndiyo unajaribu kumgawa huyu sungura mdogo, lakini tuwe na *priority sectors na ministries* kwamba tukiweka hela hapa itazaa na kusaidia Watanzania zaidi. Tufike mahali tufikirie zaidi, *let's think big*, tusifikirie kidogo kidogo, tufikirie zaidi kwa mustakabali wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Fedha, najua kuna changamoto kubwa sana za kimapato, lakini tujaribu kugawa *resources* kulingana na mahitaji halisi ya kila Wizara. Wizara hii inatakiwa ipate fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya *Cotton to Cloth* lazima ndiyo iwe wimbo wa Mheshimiwa Mwijage wa siku zote. Naomba katika *sounds* zake tutamuelewa tu kama kweli atatimiza azma hii. Hii inakuwa *record* yake kama Waziri ambaye ameanzisha mbio za *Cotton to Cloth*. Naomba sana viwanda vyetu hapa ndani tuzidi kuvilinda na wanaowekeza hapa ndani tuwasaidie, tuondoe urasimu wa uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIC* iwasaidie. Siku hizi hakuna *tax holiday*, kuna *tax incentives*, lakini kuna *conflicts*. Mtu anakuwa na cheti cha *TIC* lakini watu wa *TRA* baadhi ya vitu hawavikubali, tufike mahali tu-*harmonize*. Haiwezekani mwekezaji anakuja hapa anazungushwa. Tunapata wawekezaji wanakuja hapa Tanzania kupata kibali tu hapa cha kujenga kiwanda au kufanya shughuli hapa, anazungushwa, wengine wanahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kuna watu walikuja hapa tukawazungusha wakaenda nchi jirani, wameanzisha viwanda vikubwa vya magari na vingine. Naomba tuache urasimu. Kama tunataka tuisaidie nchi hii Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na wadau wengine wanaohusika tuondoe urasimu kwa watu wanaokuja kuwekeza hapa Tanzania. Tukifanya



hivyo, tutakuwa tumeisaidia nchi yetu kuweza kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mikoa ya Kanda ya Ziwa inategemea sana kilimo, uvuvi na mifugo. Sasa wakulima wanalia, wavuvi wanalia na wafugaji wanalia. Sasa naomba tutoke kule, mtusaidie namna ya kufanya *coordination* na hasa viwanda hivi viweze kufanikiwa zaidi. Tukifufua viwanda itasaidia kuweka ajira hata kwa vijana. Vijana wengi wako mtaani hawana kazi, tuwasaidie kupitia viwanda. Naomba kuwe na sera mahsusi ya kuwawezesha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu South Africa walikuwa wana sera inayosema '*Black Economic Empowerment*' na sisi Watanzania tuwe na *Tanzania Economic Empowerment*, tuwawezeshe Watanzania. Leo hii Mtanzania ukienda hata kukopa hela unaonekana kama nyanya chungu au pilipili hoho, unaonekana kama mtu wa ajabu tu. Naomba Watanzania wapewe nafasi. Kama mtu anawekeza, apewe nafasi kadri anavyoweza kuwekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Watanzania tuachane na mawazo ambayo ni ya kizamani, tuangalie dunia inavyokwenda sasa hivi. Wawekezaji wanabembelezwa, akishaondoka kuja kumpata inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Mheshimiwa Mwijage kaza buti. Punguza maneno kidogo tuone kazi zaidi na vitendo. Maana yake tukikutana mtaani hapo, unauliza unataka kiwanda? Kama unacho mfukoni, Mheshimiwa Mwijage acha *style* za namna hiyo, hebu kuwa *serious* kidogo. Maneno yako yaakisi kile unakifanya, nina imani una wasaidizi wazuri kwenye Wizara yako, fanyeni kazi kama Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Chegeni. Tunaendelea nna Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ni Wizara muhimu sana hasa kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu ni Serikali ya viwanda na kwa ajili ya kukuza uchumi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote ya wataalam pamoja na watu wote wanaomsaidia, wanafanya kazi vizuri sana. Ni kweli pamoja na kwamba watu wanasema labda Mheshimiwa Mwijage anaongea kwa utani lakini kwa jinsi navyomwangalia nafikiri yupo *serious* ndiyo sababu hata Mheshimiwa Rais amemwamini kwa kipindi chote hicho amebaki kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho nataka nichangie kwenye Wizara hii, naona tumejikita mno kwenye viwanda, hatujaangalia biashara. Leo hii ukiniuliza hata mimi, masoko yako kwa nani? Yako kwa Wizara ya Viwanda au yako Kilimo au Mifugo au yako kwa nani, sijui. Wakulima wanahangaika na sehemu ya kuuza mazao yao. Ni nani mwenye jukumu hilo, hatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye kilimo, tumehangaika kuhusu mahindi hapa, aliyesulubiwa ni Waziri wa Kilimo. Nimezungumza kwa muda mrefu kuhusu pareto hapa. Nilikuwa naongelea kupitia kwa Waziri wa Kilimo lakini leo hii nilipoangalia hotuba hii, nikakuta kuna chombo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kinaitwa *TANTRADE*, kazi yake ni kutafuta masoko ya viwandani na mazao. Jiulize humu ndani kama kweli hawa watu hizo kazi wanazifanya zaidi ya Maonyesho ya Sabasaba. Inabidi tusifumbiane macho, tunapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu nalima pareto. Nimeongelea kuhusu pareto mpaka Wizara imeamua iifute pareto kwenye mazao manne ya kimkakati Tanzania wakati pareto tunayolima Tanzania tunaongoza Afrika na ni ya pili duniani. Sasa uangalie ni kwa kiasi gani wakati mwingine tunafanya vitu vya ajabu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pareto tunayozalisha leo hii haizidi tani 1,000 ndiyo tumejitahidi sana, lakini *potential* ni karibu tani zaidi ya 10,000, ndiyo inatakiwa duniani. Kwa nini hatufiki huko? Kwa sababu mnunuzi ni mmoja. Ni nani alitakiwa atutafutie wanunuzi? Ni huyu mtu anaitwa *TANTRADE* au Wizara ya Viwanda ba Biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachomwomba Mheshimiwa Waziri aje na mkakati ni namna gani atusaidie Tanzania kwa sababu *potential* tuliyonayo Tanzania ni kuwa wazalishaji wakubwa wa pareto duniani. Leo hii pareto tunaiuza mkulima anapata kwa bei kati ya Sh.2,300 mpaka Sh.2,700 lakini ukipeleka sokoni moja kwa moja, wale wanaonunua wanapata kati ya Sh.8,000 mpaka Sh.10,000 na hiyo ni kwa vile ni biashara wanaotuchezea. Anayenunua na anayezalisha Tanzania ndiyo huyo huyo anayenunua Marekani. Anapeleka Marekani kama *crude*, anakwenda kuichakata kule na sisi Tanzania hatuonyeshwi kama ndiyo tumezalisha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda kilianzishwa Inyala kikajaribu kupeleka pareto nje, wale waliponunua na kuingia mkataba, wakatishiwa kwamba kwa sababu mnanunua pareto kwa huyu mzalishaji mwingine kutoka Tanzania, nasi ndiyo tumekamata zao la pareto duniani, basi hatutawaletea tena pareto, kwa hiyo, wale watu wakaogopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna chombo chini ya Wizara hapa kinaitwa *FCC* kama sikosei na kazi zake, sijui kama haya wanayaona ya kwamba zao ambalo tunaongoza Afrika, hata *FCC* sijui kama wanajua ni kiasi gani wakulima wananyonywa? Mnunuzi ni mmoja, ame-*dominate*

soko la pareto ndiyo *giant* duniani. Tukiendelea namna hii tutakuwa tunamsaidia vipi mkulima wa Tanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nilitaka nichangie kidogo ni kuhusu kufufua viwanda. Watu wameongelea kuhusu kufufua viwanda na Mheshimiwa Waziri ametamka kuwa ana nia ya kufufua Kiwanda cha Nyama kwa kutafuta mnunuzi wa Kiwanda cha Nyama cha Tanganyika *Packers*kule Mbeya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Waziri, tuna kiwanda ambacho kimejengwa na Halmashauri. Ni kiwanda cha thamani ya shilingi bilioni 2, kimejengwa kwa asilimia 90. Vifaa ya *UNIDO*vimeshawekwa mle ndani na sasa hivi Halmashauri inaomba pesa kidogo tu kama shilingi milioni 900 ili waweze kumaliza. Kiwanda hiki ni cha kisasa na ni kizuri kuliko hicho ambacho wanataka kufufua sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanganyika Packers*ilijengwa kabla ya mwaka 1970, yale mashamba sasa hivi yamezungukwa na jiji, yako mjini. Kuna ekari pale karibu 5,000 ziko mjini na mjini huruhusiwi kufuga wala kulima zaidi ya ekari tatu. Sasa unakuta Mheshimiwa Waziri naye anasimama anasema tunatafuta mwekezaji kwa ajili ya *Tanganyika Packers*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muwe mna-*coordinate*. Halmashauri imeomba lile eneo wapewe na wao wametoa ekari 7,000 kwenye sehemu ambayo ndiyo kuna ng'ombe wengi iwe kama *holding ground*, lakini tubakize kiwanda, kutoka pale ni kilomita 30. Wizara ya Ardhi walishauja, Naibu Waziri wa Ardhi alikuja, Katibu Mkuu wa Ardhi alikuja, wote waka-*recommend* nami mwenyewe nimeongea na *Treasury Registrar* akaona hilo ni wazo zuri ili lile eneo sasa ambalo lilikuwa ni la *Tanganyika Packers* libadilishane na hili eneo, Halmashauri iliendeleze hili eneo kwa ajili ya kuupanga mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo ni karibu kabisa na *Songwe International Airport*. Sasa badala ya kutenga maeneo kwa ajili ya *EPZ* unataka wewe ukachungie ng'ombe, nafikiri hivyo ni vitu ambavyo katika dunia ya leo havikubaliki. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa makusudi kwa vile hiki kiwanda ni kwa ajili ya soko la ndani na nje. Kiwanja cha ndege sasa hivi kimetengenezwa ili kiwezeshe ndege kubwa kutua Mbeya ziende moja kwa moja Ulaya, tuweze kupeleka nyama kutoka Mbeya kwenda Ulaya na tupeleke maparachichi na kadhalika. Kwa hiyo, hatukatai Kiwanda cha Nyama ila tunachosema ni mfumo gani tuuchukue ambao unaendana na leo? Ile *spirit* ya 1970 huwezi ukaitumia hiyo hiyo mpaka leo ukawa unaimba humo Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda kuchangia kidogo ni hii taasisi mpya ya inaitwa *Tanzania Commodity Exchange Market*, ni nzuri mno na inaweza kuwa mkombozi. Sasa ndiyo hivyo ambavyo nachanganyikiwa kwamba, je, itakuwa chini ya nani; Wizara ya Viwanda, Wizara ya Fedha au labda Wizara ya Kilimo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa makusudi. Kilimo sasa hivi walikuwa wanahangaika jinsi ya kuuza kahawa. Unajaribu kuangalia, je, kuuza kahawa ni Wizara ya Kilimo, au ni Wizara ya Viwanda au ni *TANTRADE*? Sasa Wizara ya Kilimo badala ya kuboresha kilimo wanaanza kuhangaika na kutafuta masoko. Nafikiri tutapoteza mwelekeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hivi vitu tuvifanye kwa makini. Imarisha *Tanzania Commodity Exchange*, tuige Ethiopia, Nairobi wana soko la kuuza kahawa. Tanzania tunauza kahawa kwa kilo 50 dola 150 wakati Nairobi ni kati ya dola 350 mpaka 400 na Ethiopia ni zaidi hapo. Sasa angalia ni kiasi gani uchumi wa nchi hii tunavyoupoteza kwa kutokuwa na mipango mizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili wenzetu nao wakajipange vizuri. Zao la kahawa liingie moja kwa moja kwenye *Tanzania Commodity Market Exchange*. Kwa sababu gani *TCB* wao ni *regulator*, huwezi ukamfanya *regulator* vilevile akawa ni muuzaji. Sisi wengine ni wakulima wa kahawa, unaona kabisa kuna watu pale wanajifanya wana mnada lakini wanaangalia kahawa ya leo ya Tanzania tununue kwa shilingi ngapi? Tumenyonywa kiasi cha kutosha, naomba tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa Wakala wa Vipimo. Amezungumza Mheshimiwa Lwenge akafikiria labda viazi vya kutoka Mporoto ambako ndiyo Jimboni kwangu labda kuna nafuu, sisi ndiyo kuna usumbufu mkubwa, hatulali. Magari yanakuwa yamebeba viazi, wakulima maskini amekodi gari tani saba siyo ya mtu mmoja, hana hela, akiuza Dar es Salaam ndiyo apate nauli ya kumrudishia mwenye gari lakini...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza muda wetu umemalizika.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, muda wetu kwa siku ya leo na shughuli zetu zimefikia mwisho. Nawashukuru wote ambao mmeweza kutoa michango yenu kwa siku ya leo, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Kabla sijaahirisha shughuli za Bunge, nina tangazo la Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Olenasha, jana jioni aliacha simu yake aina ya *Samsung Note 4* nyeupe. Kwa hiyo,

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

anaomba yeyote ambaye ameikota aweze kumrudishia. Pia anaomba watu wa *camera* waweze kumsaidia ku-*trace*.

Baada ya tangazo hilo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 11 Mei, 2018 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, tarehe 11 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*